**6 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 6 Juni, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu.

Na. 335

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Namiungo

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 500 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Namiungo na shilingi milioni 200 ya Kituo cha Afya cha Nakayaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nakayaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata za kimkakati kwa awamu ikiwemo Kata ya Namiungo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**NDG. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Kituo cha Afya cha Namiungo, ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ni Hayati, alitoa ahadi Milioni 500 ili kuweze kukamilisha Kituo cha Afya cha Namiungo. Sasa je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kituo cha Afya cha Nakapanya, kilitengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 400 mwaka wa fedha 2021 na kilipokea shilingi milioni 200 na kujenga majengo ya upasuaji pamoja na maabara.

Je, ni lini Serikali itatupatia kiasi kilichobaki ili kuweza kujenga majengo mengine muhimu kama vile *mortuary* na mionzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Kungu kwa namna ambavyo anawakilisha kwa dhati wananchi wa Tunduru Kaskazini, na nimhakikishie kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele cha Serikali. Tunafahmu kwamba Namiungo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nasi tayari tumeshaweka mpango wa kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Namiungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Nakapanya, hiki ni kituo kati ya vituo 52 ambavyo katika mwaka wa fedha huu tumetenga Bilioni 15.6 kwa ajili ya umaliziaji wa vituo hivi kikiwemo kituo hiki cha afya cha Nakapanya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dokta. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Je, ni lini Serikali itapeleka Shilingi Milioni 200 katika  Kituo cha Afya cha Nyalioba, ikiwa ni ni utekelezaji wa ahadi ya Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samizi anawasemea sana wananchi wa Jimbo la Muhambwe, nakumbuka katika ziara ya Mheshimiwa Makamu wa Rais tulikuwa pamoja tuliahidi Milioni 200 Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi. Ninakuhakikishia kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI tayari imetenga fedha hizo na wakati wowote zitaingia kwenye Kituo cha Afya cha Nyalioba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli mwaka 2018 aliahidi kutoa Shilingi Milioni 100 kumalizia Kituo cha Afya cha Mchomoro, lakini mpaka leo fedha hizo hazijapatikana. Je, Serikali iko tayari kuzitoa fedha hizo ili kuendeleza Kituo cha Afya cha Mchomoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Kawawa kwa kazi kubwa anayofanya kuwasemea wananchi wa Namtumbo, na nimhakikishie kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele, tunafahamu milioni 100 inahitajika katika kituo hiki cha Namchomoro na tutaleta fedha hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwaka jana Wabunge wote tulitoa vipaumbele vya vituo vya afya kwenye Kata mbalimbali nchini. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha za Kituo cha Afya cha Kata ya Ruvu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakamo, amekuwa mchapakazi sana, mwakilishi mzuri wa wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, tunafahamu kwamba Kata ya Ruvu inahitaji kituo cha afya, kwa sasabu ya idadi ya wananchi waliopo na tayari tumeweka kwenye mpango mkakati kwa ajili ya ujenzi

wa kituo cha afya katika Kata ya Ruvu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John kwa niaba yake Mheshimiwa Lugangira.

Na. 336

**Ujenzi wa Jengo la Halmashauri Biharamulo**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA K.n.y. MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, mwezi Februari, 2022 iliwasilisha maombi maalum ya shilingi bilioni 3.475 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri. Maombi hayo yaliwasilishwa nje ya muda ambapo ukomo wa bajeti kwa mwaka

2022/2023 ulikuwa umeshatolewa hivyo kushindwa kutengwa kwa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 itatenga kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa kuwa ni kiasi ambacho kimewekwa na Wizara kwa ujenzi wa majengo ya Halmashauri. Ahsante.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ucheleweshaji sio la Biharamulo, kwa sababu Biharamulo walishawasilisha Mkoani na Mkoani wanaleta moja kwa moja TAMISEMI. Jengo la Halmashauri ya Biharamulo, liko kwenye miradi ya kimkakati ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa. Swali la kwanza, maombi yalikuwa ni bilioni 3.4 lakini Serikali imetenga bilioni 2.7 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 lakini kwa uchumi wa Biharamulo haitaweza kupata hiyo milioni 700 inayosalia.

Je, Serikali ina mpango gani waku-*top up* kiasi hicho cha fedha tukifika wakati huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali tayari imeshaweka *commitment* na ahadi kwamba itatenga hiyo bajeti ya bilioni 2.7; je, bado kuna haja tena ya kuandika maombi haya au hakuna haja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum ambayo ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi bila kujali vimechelewa wapi ni suala la kwamba jengo la utawala la Halmashauri litatengwa kwenye mwaka wa fedha 2023/2024. Lakini kiasi ambacho kimeombwa ni Bilioni 3.475 lakini mpango wa Serikali tumefanya *standardization* ya majengo yetu yote ya halmashauri ili kuepukana na *variation* ya majengo ambayo yamekuwa yanajengwa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sasa Halmashauri zote zitakuwa na mchoro mmoja na kila halmashauri itapata bilioni 2.7, kwa hiyo hatuna haja ya kuongeza fedha hiyo, hiyo ndiyo fedha kulingana na mchoro huo ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na *standardization*. Lakini pale ambapo tutalazimika kuwa na *variation* ya mchoro kulingana na mazingira, basi tutaona namna ya kufanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, wafanyakazi wake wanakaa sehemu tofauti tofauti, kutokana na uchakavu wa jengo, na jengo kuwa na

nafasi ndogo. Je, ni lini Serikali itatujengea jengo jipya na maombi tulishapeleka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharami, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kujenga majengo haya ya utawala, mpaka sasa takribani jumla ya Bilioni 224.5 zimetumika kwa majengo ya Halmashauri 95, tunafahamu Bagamoyo mlileta maombi hayo, nikuhakikishie kwamba tunaendelea kutafuta fedha na baada ya hapo tutaanza shughuli za ujenzi wa jengo la Halmashauri. Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Fakharia Shomar. Swali Na. 340 ni Wizara ya Elimu na Teknolojia?

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Wizara ya Katiba na Sheria.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni la Wizara ya Elimu, siyo Wizara ya Katiba na Sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu.

Na. 337

**Muswada wa Sheria utakaozuia watuhumiwa kukamatwa kabla ya kukamilika kwa upelelezi**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawasilisha Muswada wa Sheria unaozuia Polisi kukamata na kuwashikilia watuhumiwa kabla ya kukamilisha upelelezi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura Na. 20 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2022 mwezi Machi, 2022, ambapo kwa sasa Sheria imeweka masharti ya kutofungua mashtaka mpaka upelelezi utakapokamilika, isipokuwa kwa makosa makubwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, idadi kubwa ya mahabusu walioko kwenye magereza zetu wanaipa mzigo mkubwa sana Serikali yetu kuwahudumia. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta sheria ambayo itawezesha watuhumiwa wakapewa nafasi ya kujidhamini wenyewe ili kuipunguzia Serikali mzigo na kuwapunguzia adha wananchi wanaotekesaka kwenye magereza, kwa makosa mbalimbali ambayo kimsingi yanaweza kudhaminika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHSERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mtuhumiwa kujidhamini au kudhaminiwa ni kuhakikisha kwamba anarudi mahakamani kwa tarehe itakayotakiwa. Kwa hivi sasa Serikali imejikita katika mpango wa kuweka anwani za makazi pindi zoezi hili litakapokamilika tutakuwa na uwezo wa kujua kila mtu anaishi wapi, hivyo kutakuwa na uwezekano wa kujidhamini wenyewe. Kwa hiyo, kazi ambayo Mheshimiwa Nape anaifanya ikikamilika, pamoja na vitambulisho vya Taifa *NIDA*, itawawezesha Watanzania kujidhamini wenyewe, hivyo kupunguza msongamano wa mahabusu ambao watakuwa wako nje. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kero kubwa ya msongamano wa

mahabusu na wafungwa magerezani imekithiri. Je, Serikali inaonaje ikaleta utaratibu wa vifungo vya nje kwa makosa madogo madogo ili kupunguza msongamano huo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHSERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria mwaka huu, tulisema moja kati ya vipaumbele ni kwenda kuangalia upya, kuufumua na kuupanga upya mfumo wa jinai hapa nchini. Katika mpango huo moja kati ya jambo ni hili kuangalia adhabu mbadala ambazo zitasaidia kupunguza msongamano wa mahabusu magerezani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

Na. 338

**Kupitia sheria zinazokinzana na umiliki wa ardhi kwa wanawake**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia sheria zinazokinzana na Sheria Namba 4 na 5 juu ya umiliki wa ardhi kwa wanawake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inampatia kila mtu bila kujali jinsia yake, haki ya kumiliki mali ikiwemo ardhi na haki ya kuhifadhi kwa mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kama kuna Sheria inayokinzana na Katiba na Sheria za Ardhi Na. 4 na Na. 5 ya mwaka 1999 kuhusu umiliki wa ardhi kati ya mwanaume na mwanamke, Serikali itaanzisha mchakato wa kuzifanyia mabadiliko Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umiliki wa ardhi kwa watoto chini ya miaka 18 wanaweza kumiliki ardhi kwa kupitia waangalizi wao kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa mujibu wa takwimu za Serikali ya mwaka 2016 zinaonesha kwamba ni asilimia 19 tu ya wanawake ambao wanamiliki ardhi wakati wanachangia takribani asilimia 54 ya uzalishaji katika kilimo ambao ndiyo uti wa mgongo wa uchumi. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Je, Serikali imeweka kipaumbele gani kuhakikisha kwamba umiliki wa ardhi kwa wanawake unaongezeka kwa kuipa uhai na meno Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mila, tamaduni na desturi ni kati ya sababu kubwa ambazo zinachangia kutokumiliki ardhi kwa wanawake. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba sheria za kimila za umiliki ardhi, pamoja na sheria zingine ambazo zinakinzana na Sheria Na. 4 na 5 haziwi juu ya hii Sheria Mama ya Umiliki wa Ardhi wa Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, ni kweli idadi ya wanawake ambao wanamiliki ardhi hapa Tanzania bado ni ya chini na hiyo haisababishwi na sheria, inasababishwa na mtazamo wa jamii, inasababishwa na mila na desturi zetu ambazo ni lazima sasa tushirikiane kati ya Serikali na Asasi za Kiraia, kati ya Serikali na Wadau wote kutoa elimu kuhusu haki ya mwanamke kumiliki ardhi kwa mujibu wa Katiba kama ambavyo imeelezwa kwenye Ibara ya 24, lakini pia kama ambavyo imeelezwa katika Sheria ya Ardhi, Kifungu cha 3(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, Sheria hizi za kimila zimekuwepo toka zamani lakini ni wazi

kama ambavyo Mheshimiwa Neema amesema zinakinzana na haki za wanawake ambazo zimeelezwa kwenye Katiba na Mikataba mingine ya Kimataifa ambayo tumesaini. Hivyo basi, sisi kama Serikali tumejipanga kuzipitia upya sheria hizi ili kuweza kupendekeza mabadiliko na endapo Bunge lako litaridhia, basi kadhia hii itaweza kuondoka kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda. Mheshimiwa Mtanda kwa niaba.

Na. 339

**Hitaji la mabweni katika Chuo cha *VETA* Kitangali**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga mabweni pamoja na miundombinu mingine katika Chuo cha *VETA* Kitangali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Serikali inatambua mahitaji ya miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo

mabweni katika Chuo cha *VETA* Kitangali ambapo mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilitoa Sh.299,267,002.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, jengo la utawala na vyoo na ukarabati wa karakana ya ushonaji, umeme pamoja na uwekaji wa samani na vifaa.

Mheshimwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya miundombinu ikiwemo mabweni, bwalo, nyumba za Walimu na uzio katika Chuo cha *VETA* Kitangali.

Mheshimwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza; kwa kuwa changamoto ya miundombinu katika Chuo cha *VETA* cha Kitangali ni kubwa sana; na kwa kuwa wanafunzi wanaotoka sehemu hiyo wanatoka katika maeneo mbalimbali vijijini. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha mradi huo na kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka sehemu mbalimbali ikiwepo wanaotoka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Maimuma Mtanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa changamoto ya vijana wanaomaliza Sekondari na Shule za Msingi imekuwa ni kubwa, vijana wengi wanamaliza shule na wengi wanatarajia sasa kwenda kwenye vyuo hivi vya *VETA* kupata elimu. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha kwenye hivi Vyuo vya *VETA* vyote nchi nzima wanaweka miundombinu na mabweni ili watoto mbalimbali wanaomaliza shule kutoka vijijini

waweze kwenda kwenye Vyuo vya *VETA* na kupata mafunzo na ujuzi wa mbalimbali? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI YA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali iliweza kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa baadhi ya mbiundombinu katika chuo hiki; na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka wa fedha ujao, tutahakikisha kwamba maeneo haya ambayo ameyataja hasahasa katika hiki Chuo cha Kitangali kupitia mapato ya ndani ya *VETA* tutakwenda kuongeza miundombinu katika eneo hili ikiwemo pamoja na mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, ni kweli tukiri kwamba tunajenga *VETA* katika wilaya zote Tanzania, lakini *focus* yetu kwanza ilikuwa ni ujenzi wa miundombinu ya vyuo hivi na tumeweza sasa kukamilisha karibu katika Wilaya 77 nchini. Kuna wilaya chache ambazo bado hatujazifikia, tunaamini katika kipindi kijacho kwanza tutakwenda kukamilisha kwenye wilaya hizi ambazo hazina Vyuo vya *VETA*, lakini vilevile kuhakikisha kwamba haya maeneo ambayo yana upungufu wa mabweni nao vilevile tunaweza kuwafikia kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hii ili wanafunzi wetu, vijana wetu, waweze kupata mafunzo katika maeneo hayo.

Mheshimwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sera ya Serikali ni kuwa na *VETA* kila wilaya. Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilaya ya Maswa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi, kwamba Sera yetu kama Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na Chuo cha *VETA* katika kila wilaya nchini ikiwemo na Wilaya ya Maswa. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira katika hiki ambacho Serikali tunaendelea kutafuta fedha na tunaamini katika mwaka ujao wa fedha tutaweza kuzifikia baadhi ya wilaya lakini tutaipa kipaumbele vilevile Wilaya ya Maswa; kuhakikisha kwamba miongoni mwa vile vyuo vichache ambavyo vitapata fedha basi tuweze kutekeleza mradi huo katika Wilaya ya Maswa. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, wajiandae Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Londo.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze

kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Chuo cha Ufundi Stadi cha Mangaria kilicho kwenye Kata ya Mamba Kaskazini na kukipa vifaa vya kufundishia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza awali kwamba Serikali bado tunaendelea na mchakato wa utafutaji wa fedha; kwanza tuweze kufanya ujenzi kwenye wilaya ambazo hazina hivi vyuo. Hata hivyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Dkt. Kimei, kwa vile ametaja suala la ukarabati katika Chuo hicho cha Mamba, nitamwomba tu baada ya kikao hiki cha leo tuweze kuonana baadaye ili kwanza tuweze kutuma timu yetu ya wataalam kwenda kule Mamba, iende ikafanye tathmini ya kina, tuweze kujua gharama za ukarabati ukaohitajika pale ni kiasi gani ili tuweze kuingiza kwenye mipango yetu na tukipata tuweze kukipa kipaumbele cha ukarabati chuo hiki. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiku, ajiandae Mheshimiwa Londo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwaka 2014 tuliweza kubadilisha Sheria ya *Skill Development Levy* ambapo zilikuwa asilimia nne zote ziende *VETA* kwa ajili ya kuboresha ujuzi na miundombinu ya *VETA,* lakini 2014 tulibadilisha kwa sababu *by then* tulikuwa hatuna *VETA* nyingi na sasa hivi Serikali imejenga *VETA* nyingi sana.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka warudishe ile sheria tuibadilishe, hizi asilimia mbili ambazo zilipelekwa Bodi ya Mikopo kwa ajili kukopesha wanafunzi wa elimu ya juu ziweze kurudishwa *VETA*; zitumike kama ilivyokuwa imedhamiriwa awali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa swali lake la msingi na kuona umuhimu wa taaluma hii ya *VETA* katika nchi yetu. Hata hivyo, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Esther kwanza Serikali imekuwa ikipeleka ruzuku kwenye vyuo hivi, ruzuku zile za uendeshaji, ndiyo kwa maana unaona hata zile ada zake ziko chini sana kwa wanafunzi wa kutwa ni Sh.60,000 na kwa wale wa mabweni ni Sh.120,000. Kwa vile Mheshimiwa amezungumza habari ya sheria kwamba tuirejeshe hapa Bungeni ili tuweze kuirekebisha ili basi ile asilimia nne iweze kwenda kuongeza nguvu kwenye eneo lile la *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tubebe ushauri wake Mheshimiwa Matiko twende tukaufanyie kazi, tufanye tathmini ya kina, tukiona kuna haja ya kuleta hiyo sheria hapa ili tuweze kubadilisha, tuweze kufanya hivyo. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, imetosha kwa kuwa umeshapokea ushauri. Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Chuo cha *VETA* Mikumi ni chuo ambacho kilijengwa na *Irish people* kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na kwa nia njema kabisa Chuo kile tuliikabidhi Serikali. Tangu tumeikabidhi Serikali hakuna jitihada zozote za kujenga ama kukarabati miundombinu ya chuo kile hasa ukizingatia kwamba hali yake ni mbaya na hakina mabweni. Sasa nini kauli ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa miundombinu hasa mabweni katika Chuo cha *VETA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Londo kwa ufuatiliaji wa karibu wa chuo hiki, siyo mara moja wala mara mbili tumeshawahi kukutana.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Londo aridhie baada ya kikao hiki tuweze kukutana ili kuangalia kitu gani cha kufanya na vilevile tuweze kutuma timu kwenye eneo hili kwa ajili ya kufanya tathmini kama tutakavyofanya kwa Mheshimiwa Kimei, tuweze kufanya vilevile na kwake, kuangalia thamani ya ukarabati pamoja na uongezaji wa miundombinu kwenye eneo lile ili tuweze kutekeleza kwa wakati.

Mheshimwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 340

**Vijana waliopata nafasi za ufadhili nje ya nchi**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, ni vijana wangapi wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kwa mwaka 2015 - 2020 na kati yao ni wangapi wanatoka Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwa mwaka 2015 - 2021, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar iliratibu ufadhili wa masomo katika Nchi za Uingereza, Hangaria, China, Morocco, Misri, Algeria, Urusi, Ujerumani, Msumbiji, Thailand, Mauritius, Iran na Indonesia. Watanzania walionufaika na ufadhili huo ni 856 ambapo kati yao wanaume ni 609 sawa na 71.1% na wanawake 247 sawa na 28.9%.

Mheshimwa Naibu Spika, nafasi za ufadhili wa masomo nje ya nchi hutolewa pasipo kujali mwombaji anatoka upande upi wa Muungano.

Mheshimwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri na vijana wetu wanasikia kwamba vipi uteuzi huo unavyoelekea. Baada ya maelezo hayo ningeomba kujua, makubaliano yao yanakuwa baina ya SMT na SMZ na wanateua hao vijana. Je, huduma za vijana hao kutoka Zanzibar hadi kufika chuoni huwa zinafadhiliwa na nani SMT au SMZ? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; vijana ambao tayari huwa wanawateua *percentage* kubwa ni wanaume kuliko wanawake na wanawake kwa kipindi hiki wanachacharika katika kupata elimu. Je, mtazamo huo unakuwa uko namna gani hata vijana wanawake wanakuwa kidogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi; ufadhili kwa wanafunzi hawa

wanaokwenda nje unafadhiliwa na nchi zile ambazo wanafunzi hawa wanakwenda na siyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wala siyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo taratibu zote zile za kugharamia yale masomo huwa zinafanywa na zile nchi husika; ingawa sasa hivi sisi kama Serikali tumetoa fursa kwa Bodi yetu ya Mikopo kuweza kuwa na ile *partial scholarship*. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao wanafadhiliwa kupitia Bodi zetu ile Zanzibar pamoja na hii ya Tanzania Bara kwa kupata *partial scholarship*; kwa hiyo utaratibu wake unakuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili amezungumza habari ya wanaume kuwa wengi kuliko wanawake. Kwanza tukiri kwa sababu takwimu zinaonesha hapa wanaume ni asilimia 71 na wanawake ni asilimia hiyo 29. Hii inatokana na zile sifa kwa sababu hawa wanapochaguliwa kwenda kufanya masomo kwenye nchi hizi za nje kuna sifa ambazo zinaorodheshwa pale pamoja na ufaulu. Kwa hiyo, hii nadhani inatokana na ile namna gani wanaume wanafaulu kuliko wanawake.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa vile Mheshimiwa Mbunge amelileta jambo hili hapa, basi sasa labda katika ugawaji hata zile nchi tutaziambia angalau ziweze kufanya *fifty fifty* ili na wanawake wengi waweze kupata fursa hii. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri mwelekeo wa Serikali

kutafuta *scholarship* ni katika maeneo gani hususan ambayo inataka wanafunzi wetu waende kusoma. Vilevile ukiangalia idadi ya wanafunzi 400 kwa Taifa hili ni kidogo sana ambao wamepata *scholarship*. Je, mpango wa Serikali ni upi hasa wenyewe makusudi kutafuta *scholarship* nje ya nchi ili iweze kuongeza idadi ya Watanzania wengi waweze kwenda kusoma nje ya nchi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, ingawa amezungumzia maeneo mawili ambayo kipaumbele ni vipi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba nchi hizi zinapotoa ufadhili kwenye hizi *scholarship* ni nchi zenyewe ndizo ambazo zina-*detect*, zinazoamua kwamba kozi gani ziende zikasomewe; lakini maeneo mengi sana yamekuwa ni maeneo ya Udaktari pamoja na Uhandisi. Pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka ujao wa fedha, sisi kama Serikali kwanza tumeviagiza vyuo vyetu vikuu viweze kuandaa au kupendekeza maeneo ambayo wanafunzi wa Kitanzania watakwenda kufanya masomo yao nje ya nchi.

Mheshimwa Naibu Spika, vile vile kama nilivyoeleza katika swali la nyongeza ni kwamba, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo tumekuwa tukifadhili baadhi ya *scholarship* kwa kupata *partial* mikopo kwa ajili ya vijana wetu ambao wanakwenda kusoma nje. Kwa hiyo, huo ndiyo

mkakati wetu kama Serikali na tutaendelea kufanya hivyo wakati upatikanaji wa fedha utakapokuwa mzuri. Nakushukuru sana.

**NAIBI SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Shangazi kwa niaba ya Mheshimiwa Maige.

Na. 341

**Serikali kujenga viwanda vya mbolea nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Viwanda vya Mbolea nchini ili Wakulima waongeze tija?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA,** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na Mpango wa Kuratibu Uwekezaji wa Viwanda vya Mbolea Nchini. Matokeo ya uratibu huo ni pamoja na Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu na ujenzi unaoendelea wa

Kiwanda cha Mbolea cha *Itracom Fertilizer Limited*, Jijini Dodoma. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kuna maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa sasa tunakaribia kwenda kusaini mkataba mkubwa wa uchakataji wa gesi asilia wa *LNG* kule Kusini na sehemu ya uzalishaji wa malighafi za gesi kuwa pia inatengeneza mbolea.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kufungamanisha uchakataji wa gesi asilia na uanzishaji wa Kiwanda cha Mbolea katika eneo la Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Tanga ndiyo tutakaopokea hifadhi ya mafuta ghafi kutoka Uganda.

Je, Serikali haioni kwamba tunaweza tukatumia eneo la Chongoleani ikiwa ni sehemu pia ya usafishaji ghafi; kwa sababu mafuta haya pia ni malighafi kwa ajili kutengeneza mbolea tukapata Kiwanda kingine cha Mbolea katika Mkoa wa Tanga kama kile kilichokuwepo miaka ya nyuma? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya

Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Shangazi kwa kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa viwanda hasa vya mbolea katika nchi hii na hasa katika Mkoa wa Tanga. Serikali ina mpango wa matumizi ya gesi asilia ambao unatekelezwa kupita Shirika letu la Maendeleo la Petroli *(TPDC)* lakini pia kwa kushirikiana na Kituo chetu cha Uwekezaji cha *(TIC)*. Kwa hiyo, katika mpango huo tumeshaendelea kuvutia wawekezaji na zaidi ya kampuni tatu ambazo zimeonesha utayari wa kuweka katika kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi asilia kampuni hizo ni pamoja na *Helmik* na *Ferosta* kutoka Ujerumani lakini pia tunayo *Polyserve* kutoka Misri, lakini zaidi na wengine wanaendelea kufanya tathmini na namna ya kutumia gesi asilia ikiwemo Kampuni ya Dangote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mpango huo tumeshaendelea kuvutia wawekezaji, na zaidi ya kampuni tatu zimeonesha utayari wa kuwekeza katika uzalishaji wa mbolea kwa kutumia gesi asilia. Kampuni hizo ni pamoja na Helium na Feroster kutoka Ujerumani na pia tunayo Polysafe kutoka Misri. Vile vile na wengine wanaendelea kufanya tathmini ya namna ya kutumia gesi asilia ikiwemo Kampuni ya Dangote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni sahihi kabisa, ni mawazo mazuri kuona namna gani Tanzania inatumia fursa ya mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda ambayo yatakuja Tanzania, tuone namna gani ya kutumia mafuta hayo ghafi kuzalisha mbolea ili tukidhi mahitaji makubwa

ya nchi hii kutokana na upungu au nakisi ya mbolea kwa ajili ya sekta ya Kilimo. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa changamoto ya mbolea bado ni kubwa sana nchini; na kwa kuwa Tanga tulikuwa na Kiwanda cha Mbolea na sasa hivi hakifanyi kazi: Je, Serikali haioni haja sasa yakutafuta mwekezaji kwa ajili ya kwenda kuwekeza kwenye kiwanda kile ili kutatua changamoto kubwa ya mbolea tuliyonayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema tuna changamoto kubwa sana ya mbolea, zaidi ya tani 600,000 zinahitajika katika kukamilisha mahitaji ya tani 700,000 kwa mwaka ambazo zinatumika katika nchi hii. Kwa hiyo, Serikali ina mpango wa kuendelea kufufua viwanda ikiwemo na hiki ambacho anasema Mheshimiwa Mbunge kule Tanga. Tutaona namna ya kutafuta wawekezaji ili waweze kuwekeza katika kiwanda hicho ili kuendelea kuzalisha mbolea kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, ajiandae Mheshimiwa Mafuwe na Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kununua viuatilifu hasa vinavyotumika katika zao la korosho, na mnunuzi mkubwa ni maeneo yote ya Mtwara na Lindi: Je, Serikali haioni sasa ni wakati muhimu wa kujenga viwanda vya viuatilifu ambavyo vinaendana na *material* hii ya gesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna changamoto kama ilivyo kwenye mbolea, lakini pia kwenye viuatilifu ambavyo kwa kiasi kikubwa tunaingiza kutoka nje. Serikali imeshaanza mipango hiyo ikiwemo kuzalisha kupitia kile kiwanda chetu cha viuwadudu pale Kibaha, lakini tutaona pia namna ya kutumia gesi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ambapo nayo ikianza kuchakatwa inaweza kuzalisha viuatilifu mbalimbali ambavyo vinaweza kutumika katika sekta hii ya kilimo hasa kwenye mikorosho na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA,** Mheshimiwa Mafuwe, niandae Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kiwanda cha LOSAA, kiwanda ambacho ni cha ufundi wa ufumaji na Seremala; kilisimama kwenye ujenzi wake tangu mwaka 1973. Tukazungumza na Mheshimiwa Waziri akamtuma Katibu Mkuu wa Wizara yako, ametembelea pale na akaahidi kiwanda kile kitamaliziwa na kuanza kufanya kazi: Je, ni lini Serikali itaanza umaliziaji wa kiwanda hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali tuna mpango wa kufufua viwanda vyote ikiwemo kiwanda ambacho anakisema Mheshimiwa Mbunge. Kweli Serikali tumeshachukua jitihada ikiwemo kutuma wataalamu wetu na Katibu Mkuu alishaenda pale kuweka tathmini ya kuona mahitaji halisi ya gharama ya kukiendeleza kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali katika fedha za mwaka huu ambazo zimepitishwa hapa, mojawapo tutaangalia namna ya kuanza hatua za awali kukifufua kiwanda hicho ili kiweze kuendelea kufanya kazi na wananchi wa Jimbo la Hai weweze kunufaika na nchi nzima tuweze kutapa faida ya uwekezaji katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali ya nyongeza. Kwa kuwa tafiti zimeonesha kwamba Gypsam au jasi inatoa mbolea ikichakatwa na kwa kuwa Wilaya ya Same ina jasi nyingi katika Kata ya Bendera na Makanya: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka viwanda katika sehemu hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyoka, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika malighafi ambazo zinatumika katika kuzalisha mbolea, mojawapo ni Gypsam, na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amesema kuhusiana na Jimboni kwake, Mkoani huko, basi tutaona namna gani ya kuvutia pia wawekezaji waweze kuona namna ya kutumia malighafi zilizopo pale ili kuanzisha viwanda vya mbolea kama ambavyo tunavutia maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Anton Albert kwa niaba ya Mheshimiwa Ally Jumbe.

Na. 342

**Kukamilika kwa Mradi wa REA katika Jimbo la Rungwe**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa *REA II* wenye vijiji 25 na *REA III* wenye vijiji 33 utakamilika katika Jimbo la Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji takribani 25 vilivyokuwa vinatekelezwa chini ya Mradi wa *REA* II vimeshafanyiwa uhakiki ili kujua upungufu ambao haujafanyiwa kazi. Marekebisho ya upungufu uliobainika katika vijiji hivyo utarekebishwa ndani ya miezi mitatu kuanzia mwezi Julai, 2022. Kazi hizo zitatekelezwa na Mkandarasi *M/S ETDCO*.

Mheshimiwa Naibu S[pika, Mradi wa REA III Mzunguko wa II ambao unapeleka umeme katika vijiji 33 vya Wilaya ya Rungwe unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2022. Kwa sasa, Mkandarasi *M/S Electrical Transmission and Distribution Construction and Maintenance Co. LTD* anaendelea na kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa leo tumeambiwa tarehe ya utekelezaji wa mradi huo na kwa kuwa kabla ya hapo tuliahidiwa kwamba mwezi wa Tatu mradi huu ungekuwa tayari.

Je, wananchi wa Vijiji hivyo kwenye Wilaya ya Rungwe wategemee kauli gani ya Serikali ya kuhakikisha hili jambo linakamilika kwa uweli baada ya miezi mitatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; Kijiji cha Ikombe Wilayani Kyela kilishafanyiwa uhakiki na kuwekea *peg* lakini mpaka sasa hivi hakuna dalili zozote za kupelekewa umeme wa *REA*: Je, ni lini Serikali itapeleka umeme huko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Ally Jumbe kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza ni kweli kwamba tulitarajia kumaliza mradi huu mapema lakini kama mnavyofahamu kulitokea ongezeko na mabadiliko makubwa sana ya bei na hivyo hata baada ya ukamilishaji wa kuangalia upungufu uliokuwa umejitokeza, tumeingia katika *negotiation* ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha halisi ya kuweza kuongeza ili tumalize mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaahidi wananchi wa maeneo hayo kwamba baada ya kukamilisha mchakato wa kukubaliana bei halisi ya ongezeko la vifaa, sasa tupo tayari kwenda kupeleka umeme katika maeneo hayo kwa kurekebisha yale maeneo ambayo yalikuwa yamebakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili. Katika kijiji hicho ambacho kimesemwa na vijiji vingine vyote ambavyo vipo Tanzania bara kama tulivyosema, vitapelekewa umeme kufikia Desemba mwaka huu kama ahadi ya Mheshimiwa Rais kwenye Ilani ilivyotolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kutokana na matatizo mbalimbali wanayopata wananchi wanaotumia umeme nje ya Gridi ya Taifa, mwezi wa Pili mwaka huu Wizara iliunda timu ya wataalam ikiongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kuzungukia maeneo haya kusikiliza wananchi na baadaye kutoa uelekeo nini utatuzi wa changamoto zile, lakini tokea wakati huo mpaka sasa Wizara imekuwa kimya. Wananchi, wakiwemo wananchi wa Jimbo la Ukerewe Visiwa vya Gana na Ukara wanataka kusikia nini maelekezo na uelekeo wa Serikali juu ya changamoto hizi? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mimi mwenyewe nilifika Nansio, Ukerewe; nilifika Ukara, Gana, Kamasi, Irugwa katika visiwa vyote vya Ukerewe ili kuangalia changamoto ambayo wananchi wanaipata. Maeneo haya yapo mengi zaidi. Yalikuwepo mengine katika Mkoa wa Kagera na mengine katika maeneo ya Buchosa. Zoezi lile linaendelea na tunatarajia litakamilika mwishoni mwa mwezi huu. Litakapokuwa limekamilika, taarifa ya Serikali na maelekezo ya Serikali yatatolewa kwa maeneo yote ambayo yalikuwa na changamoto ya bei ya umeme na wananchi wataendelea kupata umeme kwa gharama ambazo ni nafuu ili Serikali iweze kuwahudumia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi. Jimbo la Lupembe katika Vijiji vya Lyalalo, Mfiriga, Itambo, Madeke na Kanikelele wamepata umeme wa *REA,* lakini tangu mwaka 2021 zimewekwa nguzo na hakuna ambacho kinaendelea. Wananchi hawa wangependa kujua nini mpango wa Serikali kufunga umeme hayo maeneo ambayo wananchi wangu wana nguzo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ufuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema hapo awali, kulitokea mabadiliko makubwa sana ya vifaa vya dukani hasa vinavyotengenezwa kwa kutumia chuma, *alminium* na *Copper.* Tumemaliza mazungumzo sasa ya

kuona gharama ambazo zimeongezeka na Serikali inayo fedha ya kuongeza katika utekelezaji wa mradi huu, kutoka ile Shilingi trilioni 1,250.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika muda mfupi ujao wakandarasi watarudi *site* wakiwa sasa wamepata fedha ya nyongeza ya kununua vile vifaa ambavyo gharama zake zilikuwa zimepanda na mradi utaendelea kama uvyoanza na *plan* ilivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa, jiandae Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kwenye mradi wa *scope* hii ya mwisho ya *round III* ya *REA* tuliongeza *proposal* ya kuongeza vijiji, *hamlets* na *institutions,* tukaipeleka *REA* na *TANESCO* kwa ajili ya utekelezaji, lakini tuliruka chanzo cha maji cha Kijiji cha Njomlole:-

Je,Serikali inaweza ikatuorodheshea Kijiji hicho pia ambacho kilirukwa kwa bajati mbaya ili kiingie katika mradi utakaokuja kwa vijiji tulivyoomba viongezwe na miradi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa Zaytun.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni eneo la kijiji, vijiji vyote vimechukuliwa na vipo kwenye mpango wetu wa *REA III round* II na umeme utafika katika eneo hilo. Ila nimesikia kwamba ni kwenye chanzo cha maji; upo mradi mahususi wa kupeleka umeme kwenye vyanzo vya maji, kwenye migodi na kwenye vituo vya afya. Tunazo *site* zaidi ya 560 ambazo zimechukuliwa katika bajeti inayokuja, tutaiweka eneo hilo kuwa mojawapo la kupelekewa umeme ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swai, jiandae Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha ina changamoto kubwa sana ya kukamilika kwa miradi ya *REA* hususan kwenye Kata za Bangata, Oltroto na Lengijave; na hii imetokana na kubadilishwa kwa wakandarasi:-

Je, Serikali itatatua vipi changamoto hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa tuna utaratibu wa kutekeleza mradi uliokuwa unaitwa *GOODS*. Tunampa makandarasi fedha, anakwenda ananunua vifaa; kwenye mkataba unakuta asilimia 80 ni vifaa,

asilimia 20 ndiyo *labour.* Akishanunua vifaa akapata faida yake, anaondoka, anatelekeza mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu tunaoutekeleza sasa, tumebadilisha utaratibu. Tunafanya kwa utaratibu unaoitwa *WORKS.* Tunamlipa mkandarasi kulingana na kazi aliyoifanya. Hatutarajii kuwepo na utelekezaji wa miradi wala kushindwa kukamilika kwa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hiyo ya nyuma, tumeongeza usimamizi. Kama mnavyofahamu, wasimamizi tangu ngazi ya Jimbo kuja kwenye Mikoa tunahakikisha kwamba miradi yote inakamilika kwa kadri tulivyojipangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, halafu Mheshimiwa Mama Salma jiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma tulichelewa kupata umeme wa awamu ya kwanza na ya pili: Je, katika awamu wa tatu mzunguko wa pili, Serikali ipo tayari kumsimamia mkandarasi ili umeme uweze kufika vijijini na katika vitongoji vyote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali na ahadi ya Serikali ni kusimamia wakandarasi bega kwa bega

kuhakikisha kwamba miradi yote inakamilika kwa wakati na kwa kadri tulivyojipangia. Usimamizi huu ni wa vitendo; wapo wasimamizi kwenye ngazi za Jimbo wanakuja, wapo wasimamizi kwenye Kanda, wapo wasimamizi ngazi ya Taifa, na watu wote wamewezeshwa kuhakikisha kwamba kazi hizi zinafanyika na kukamilika kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kujua tu kujua kuhusiana na suala la *REA* Awamu ya III ujazilizi. Kwenye Jimbo langu la Mchinga, nilibakiza vijiji 12. Naipongeza Serikali wamenipatia, lakini sambamba na hilo, kuna nguzo zimewekwa, sasa ni zaidi ya miezi sita hakuna kinachoendelea. Nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba tulipata changamoto kidogo ya miradi kutoendelea kwa kasi na *speed* tuliyoitarajia kwa sababu ya mabadiliko ya bidhaa za viwandani. Tunasema kwamba nguzo zilipatikana kirahisi, ni kwa sababu tulipolipa ile *advace payment* asilimia 20, Wakandarasi walitumia asilimia 15 kwenda kununua vifaa ambavyo vinapatikana hapa hapa nyumbani zikiwemo na nguzo. Kuja kuingia kwenye awamu ya pili ya kununua vifaa ambavyo vinatoka madukani, ndiyo sasa bei zimepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya mazungumzo na committment ya Serikali ya kuongeza fedha, matatizo yote haya ya nguzo zilizosimama bila kuwekewa nyaya na *transforma*, zinaenda kwisha na kazi itaendelea kwa kasi kubwa zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, halafu Mheshimiwa Flatei.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mpango wa *REA* kwa Mkoa wa Singida mpaka mwezi wa Saba wanatakiwa wawe wameunganisha vijiji 10 na umeme, lakini katika Wilaya ya Ikungi Majimbo ya Singida Magharibi na Mashariki vijiji saba vyote ni vya Jimbo la Singida Mashariki:-

Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaongeza idadi ya vijiji katika Jimbo la Singida Magharibi kutoka vitatu na kuendelea ili wananchi wapate huduma ya umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii tunayoitekeleza inalenga kupeleka huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, kama kijiji kimepata umeme kwenye mradi mmoja, kwa mfano vijiji alivyovisema saba vimepata umeme kutoka kwenye mradi wa *backborn* wa Mradi wa msongo wa *kilovolt* 400 kwenda Namanga, *then* vimeshapata umeme. Vile vijiji vingine vyote vilivyobaki ndiyo

vinaingizwa kwenye *REA III round II*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna kijiji hata kimoja kitakachobaki bila kupata umeme; kama hakipo kwenye *REA III* basi kitakuwa kipo kwenye mradi mwingine kwa ajili ya kpatiwa umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mbulu Vijijini kuna kata tatu ambazo hazina umeme na vijiji 15. Nakubali majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba *REA* wameondoka *site* kutokana kupanda umeme na kupanda gharama za umeme:

Je, ni lini mnamaliza huo utaratibu wa kukubaliana na hao wakandarasi ili warudi site wakakamilishe mradi huu wa *REA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe nilienda katika Jimbo lake kuzindua umeme katika *REA III round II* na kazi ilikuwa inaendelea. Kama alivyosema, ni kweli tulikuwa na changamoto hiyo, lakini tayari tumeshakamilisha taratibu za mazungumzo, na wakati wa maonesho hapa Mheshimiwa Waziri aliwaambia wakandarasi wote Serikali tayari imeshatoa fedha kwa ajili ya kuongeza ile nakisi iliyokuwepo. Kwa hiyo, wakandarasi wanarudi *site* kwa ajili ya kuendelea

kufanya kazi wakiwa na uhakika kwamba Serikali ya Awamu ya Sita itatoa fedha ili kazi iweze kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wilaya ya Kyerwa ina vijiji 29 ambavyo bado havijapatiwa umeme ikiwemo Kata ya Nkwenda Kijiji cha Kakerere, Kata ya Kakanja Kijiji cha Keshanda na Kata ya Lukolaijo Kijiji cha Mgorogoro. Navitaja hivi kwa sababu vipo mjini. Ni lini hivyo vijiji vitapatiwa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni *committment* na Serikali kwamba itakapofika Desemba mwaka huu vijiji vyote viwe vimepelekewa umeme mabadiliko na nyongeza kidogo itatokana na changamoto ambazo wakati tunawasilisha bajeti tulizisema. Ila Kyerwa ni eneo mojawapo ambalo mkandarasi yupo *site* na kazi zinaendelea na tunaamini kwamba kazi itakamilika kwa jinsi tulivyojipangia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa muda umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni

Wenyeviti wa Bodi, Watendaji na wadau wa maendeleo wa sekta ya michezo na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu, ahsante. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Saidi Yakubu – Naibu Katibu Mkuu; pia wapo wafadhali mbalimbali wa sekta za Wizara, ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge, wasimame kwa pamoja. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wote simameni kwa pamoja, ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 28 kutoka Chuo Kikuu cha Iringa, ahsanteni. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 100 na walimu kutoka Shule ya Sekondari Nzuguni ya Jijini Dodoma, ahsanteni. *(Makofi)*

Pia wapo wawakilishi 40 kutoka taasisi ya Sisi Tanzania ya Jijini Dodoma; wachezaji 47 wa timu zilizocheza fainali ya *Vunjo Cup* kutoka Vunjo Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii ikiongozwa na Waziri na Katibu Mkuu Dkt. Hassan na Naibu Katibu Mkuu Saidi Yakubu ndio iliyosimamia zoezi zima la *Royal Tour* ambayo sasa mnaona matunda yake, matunda makubwa sana yanaonekana, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu mmefanya kazi nzuri sana, tunakupongeza sana na wewe. *(Makofi)*

Sasa tunataka kuona *Post Royal Tour* kwa maana ya taasisi zote zishirikiane na ziwezeshe *Post Royal Tour*. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu ni ndefu kidogo, *summary* ina kurasa 96 na hotuba yenyewe ina kurasa karibu 140, nitaomba pale ambapo nitashindwa kulizungumza jambo fulani, basi eneo lote la hotuba yangu liingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii leo katika Bunge lako tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena hapa Bungeni tukiwa bukheri wa afya na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza kwa ufanisi mkubwa majukumu niliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu naomba nitumie fursa hii kwa heshima kubwa kuwapongeza wanawake na Watanzania wote nchini kufuatia ushindi mkubwa wa kishindo waliotuletea siku ya jana kupitia timu yetu ya Taifa ya Wananwake chini ya umri wa miaka 17 *Serengeti Girls,* baada ya kuicharaza timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 ya Cameroon jumla ya mabao matano kwa moja. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kwamba Mheshimiwa Spika amewaandalia siku maalum kwa maana ya siku ya kesho wataingia hapa Bunge ni kupata heshima ya ujasiri na uzalendo waliouonesha kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hiyo ndio maana ya *Post Royal Tour. (Makofi/Vigelegele)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huu umeipa heshima nchi yetu na kuiwezesha kufuzu kushiriki katika

mashindano ya michuano ya Kombe la Dunia kwa Wanawake wenye umri wa chini ya miaka 17 yatakayofanyika nchini India, hakika haikuwa kazi rahisi hata kidogo hasa ukizingatia kwamba nchi ya Cameroon ni nchi iliyobobea na yenye historia kubwa katika mchezo wa mpira wa miguu, jambo ambalo lingeweza kuwaogofya wachezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali chini ya uongozi na maelekezo thabiti ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha timu hiyo inapata ushindi na kufuzu tuliwajengea matumaini, tulitengeneza na kuzalisha chembechembe za uzalendo na utaifa mioyoni mwao ili kuwapa ari ya kushinda katika michuano yao ya kimataifa hususani katika mchezo yao miwili ya mwisho dhidi ya Cameroon. Hongereni sana *Serengeti Girls,* hongera sana Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, hongera sana wanawake wote wa Tanzania, hakika mmetuheshimisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza katika historia imeandikwa wanawake hawa chini ya umri wa miaka 17 kututoa Watanzania kimasomaso, kuwatoa kimasomaso Wana-Afrika Masharika kwa ujumla kwa kuipeleka nchi yetu kushiriki michuano ya Kombe la Dunia kwa mchezo wa soka la wanawake. Hivyo natoa rai kwa timu zetu zote za Taifa katika michezo mbalimbali kuiga mfano wa *Serengeti Girls* kwa kupambana kufa na kupona, kwa ari na uzalendo kw ajili ya maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya ulinzi na usalama kwa kutimiza mwaka mmoja hivi karibuni katika uongozi wa Taifa letu tangu alipoapishwa kushika nafasi hiyo mwezi Machi, 2021. Aidha, ninampongeza kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi chake kifupi cha uongozi katika sekta zetu yaliyo shahiri na dhahiri yaliyotokana na kuliongoza Taifa letu kwa umahiri, weledi, umakini na upeo mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. Sisi na wadau wetu wote wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo tunamuahidi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuendana na fikra, maono na falsafa yake ya kazi iendelee, lakini pia tunaendelea kumuombea dua njema kila uchao kwani Waswahili husema; dua njema ya msafiri ndilo tairi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kutawazwa kuwa Chifu wa Machifu Tanzania, Chifu Hangaya tarehe 8 Septemba, 2021. Pia tunampongeza kwa namna alivyo mstari wa mbele kuhimiza masuala ya utamaduni na sanaa pamoja na kusimamia na kuendeleza michezo nchini hususan michezo kwa wanawake kupitia maagizo na maelekezo yake aliyoyatoa kwa nyakati mbalimbali. Nasi tupo mstari wa mbele kutekeleza maagizo na maelekezo yote ya Mheshimiwa Rais anayotoa katika sekta ninazozisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaongeza ubunifu, tutafanya kazi kwa weledi, tutafanya kazi usiku na mchana kwa kuzingatia kuwa hii ni Wizara ya wananchi. Hivyo tutahakikisha kuwa tunaendelea kuutengeneza mwingi ili Mheshimiwa Rais aendelee kuupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais na ambayo yanaendelea kuwa dira kuu kwetu ni pamoja na kufanyika kwa matamasha ya utamaduni yatakayoshirikisha mikoa yote kwa kushindanishwa ili kumpata mshindi mmoja; kufufua mashindano ya *Taifa Cup,* michezo iliyositishwa kwa muda mrefu. Vilevile kuboresha michezo kwa wanawake ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wanawake kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo katika michezo, ikizingatiwa wanawake wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa kila wanapopata nafasi, kurejesha tuzo mbalimbali; kutoa mirabaha kwa wasanii; na kuhakikisha timu zetu za Taifa zinafanya vyema ndani na nje ya nchi yetu kwa kuandaa timu bora za Taifa zitakazoundwa na vijana watakaopatikana kupitia programu ya kusaka na kuibua vipaji vya vijana nchi nzima itakayoitwa Michezo Mtaa kwa Mtaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na pia katika kumsadia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita mambo mengi yamefanyika ikiwa ni pamoja na kuzindua matukio mbalimbali ya kimichezo, kiutamaduni na sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa juhudi zake za kuendeleza Kiswahili na hasa msisitizo

anaoutoa mara kwa mara katika mikutano yake kutumia Kiswahili fasaha na sanifu. Aidha, Serikali kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kuthamini mchango wake ilimtunuku tuzo ya heshima ambayo alikabidhiwa rasmi katika Kongamano la Idhaa za Kiswahili Duniani lililofanyika Jijini Arusha tarehe 14 hadi 18 Machi, 2022 na yeye alikuwa mgeni rasmi wa kuhitimisha kongamano hilo. Aidha, tunapongeza jitihada anazochukua katika kuleta ufanisi kwenye sekta za utamaduni, michezo na sanaa kwa upande wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi alitumia jukwaa la kongamano hilo kupongeza jitihada zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan zilizokiwezesha Kiswahili kutangazwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)* mwezi Novemba, 2021 kuwa na siku yake rasmi katika mwaka ambapo itaadhimishwa katika kila tarehe 7 Julai na pia Kiswahili kuwa lugha ya kazi ya Umoja wa Afrika, uamuzi uliopitishwa katika Mkutano wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Umoja huo tarehe 6 Februari, 2022. Aidha, Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi alielekeza Kongamano la Idhaa lifanyike kila mwaka na Kongamano hilo kwa mwaka 2023 litafanyika Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema; mwenda tezi na omo, marejeo ngamani; sasa nitambue na kumpongeza Mheshimiwa Spika binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa wabunge wote kuwa Spika wa Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwake

kumeendeleza historia katika nchi yetu kwani amekuwa mwanamke wa pili kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia ameshika madaraka hayo akiwa ni Spika kijana kabisa katika historia ya Bunge la Vyama Vingi. *(makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa na yeye kuwa Bunge letu litaendelea kutoa haki kwa Wabunge wote kama alivyotuthibitishia wakati wa kuapishwa kwake kushika nafasi hiyo. Hili tayari limedhihirika katika vikao ambavyo ameviongoza katika kipindi hiki. Jina jema hung'ara gizani. Hongera sana Mheshimiwa Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa uzoefu wako wa muda mrefu ukiwa Mwenyekiti wa Bunge, utawezesha kutekeleza majukumu yako kwa ufanisi mkubwa na kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuisimamia Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo, kwa hakika ya kale ni dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kujiunga na Bunge lako tukufu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi katika majimbo yao. Waheshimiwa hao ni pamoja na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani kutoka Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Mohamed Said Issa kutoka Jimbo la Konde. Waheshimiwa Wabunge wote hawa wamechaguliwa na wananchi

katika majimbo yao ili kuwa wawakilishi wao. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru tena kipekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kwa mara nyingine tena na kuniteua kusimamia Wizara hii kubwa yenye dhamana ya kuratibu na kuendeleza sekta za kimkakati za utamaduni, sanaa na michezo ambazo ndio nguvu shawishi ya Taifa letu *(soft power)*. Natoa shukrani hizo kwanza kwa kuteuliwa mara ya pili ndani ya kipindi kifupi cha mwaka mmoja nikitumikia nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na sasa ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na teuzi hizo, Mheshimiwa Rais ameniweka kwenye historia mpya inayonifanya niwe miongoni mwa Mawaziri hapa nchini waliopata bahati ya kulitumikia Taifa hili kwenye mihimili yote mitatu ya dola katika nafasi andamizi. Nimekuwa kwenye mhimili wa Mahakama nikitumikia nafasi mbalimbali andamizi za uongozi, nimekuwa kwenye Bunge nikitumikia nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria katika vipindi vitatu mfululizo, na sasa naitumikia Serikali katika chombo cha juu kabisa cha ushauri na maamuzi (Baraza la Mawaziri) nikiwa Waziri kamili ambapo nikihesabu utumishi wangu Serikalini sasa ni takribani miaka 20 katika utumishi wa umma. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa sana na muhimu kwani ina nguvu ya kujenga ushawishi *(soft power)* kwa nchi kwa sababu inakusanya watu wote na inagusa maisha ya Watanzania wengi wapenda michezo na burudani katika nchi hii kupitia sekta zetu za utamaduni, sanaa na michezo ambao wanakadiriwa kuwa takribani asilimia 90 ya Watanzania. Kila mtu katika nchi hii anaguswa ama kwa michezo, utamaduni au sanaa. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais utendaji bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu niliyokabidhiwa ili kutimiza adhima yake ya kuiunda upya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti mpambanaji Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao ya Kamati kwenye Wizara yetu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Aidha, ushauri, maoni na maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako tukufu.Wizara itaendelea kuzingatia ushauri, kupokea maoni, mapendekezo na maelekezo yanayotolewa na Kamati kwa maendeleo ya sekta za utamaduni, sanaa na michezo kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, chambilecho wahenga, mcheza kwao hutuzwa na mfukua lao halimchafui ukucha; nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Jimbo letu

kwa lengo la kuwaletea maendeleo Wana-Rufiji. Ninawaahidi utumishi uliotukuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jifya moja haliinjiki chungu; natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Pauline Gekul (Mbunge), Naibu Waziri wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu; Saidi Yakubu, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi wote Wakuu na Wasaidizi katika maeneo mbalimbali. Pia nawashukuru kwa dhati watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kumwelewa Mheshimiwa Rais na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma ili hatimaye kuleta tija na ufanisi kwa Wizara. Wadau wa maendeleo na wadau wengine kama mashirikisho ya vyama, vilabu na kila mdau mmoja mmoja wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo ninyi nyote mmekuwa msukumo mkubwa katika kuhakikisha hatukati tamaa, haturudi nyuma, mmetushamirisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko yetu tunapobaini kwamba katika kipindi hiki Bunge lako tukufu lilipatwa na misiba kwa kuwapoteza Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliokuwa wawakilishi wa wananchi katika majimbo yao. Wabunge hao ni Mheshimiwa Elias John Kwandikwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Ole Nasha wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatib Said Haji wa Jimbo la Konde; na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama

aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Nitoe pole kwako, Waheshimiwa Wabunge, familia za marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa majimbo ya Ushetu, Ngorongoro, Konde na Rukwa, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azipokee na kuzilaza mahala pema peponi roho za marehemu, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifanya dhukuru ya mwaka huu mmoja pia kwa masikitiko natambua kuwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Mei, 2022 Taifa letu limepoteza wadau wakiwemo wanamichezo na wasanii mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuwapoteza wapendwa wao, hakika sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2021/2022 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/2023 aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Aidha, hotuba hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, ukurasa wa 241 mpaka 245, Mpango wa Mkakati wa Wizara 2021/2022 - 2025/2026 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu nane. Sehemu ya kwanza ni utangulizi; sehemu ya pili ni majukumu,

misingi ya mwelekeo, na vipaumbele vya Wizara; sehemu ya tatu inaelezea mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2021/2022; na sehemu ya nne inaelezea changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023; sehemu ya sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2022/2023; sehemu ya saba ni maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2022/2023; na sehemu ya nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya msingi ya mwelekeo wa vipaumbele vya Wizara. Ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa, kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mipango, miradi na programu mbalimbali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na rasilimali watu ya Wizara na kusimamia utendaji wa kazi wa Taasisi zilizo chini yake ambazo ni BAKITA, BASATA, Bodi ya Filamu, TaSUBa, *COSOTA*, BMT na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, inasimamia na kunaratibu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu hayo na kuimarisha utendaji, Wizara inaongozwa na misingi mitano ambayo ni kuwafikia wadau, mageuzi ya taasisi, utawala bora, uendelezaji wa miundombinu na utafutaji wa rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo Saba

ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya utamaduni, sanaa na michezo nchini, ikiwemo viwanja na kumbi, kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya utamaduni, sanaa na michezo na kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha, ushiriki wa Timu za Taifa katika michezo na michuano mbalimbali. Vilevile, kuhamasisha wadau kusaidia timu, vilabu na wawakilishi mbalimbali wa kitaifa katika ushiriki wa michezo na michuano ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ni kukamilisha mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali za kisera na kisheria katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo, kujenga, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kitaasisi katika usimamizi na utekelezaji wa masuala ya sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususani zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, TAMISEMI, Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushiriano wa Afrika Mashariki na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika maendeleo ya Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliundwa kupitia tangazo la Serikali Na. 782 lililochapishwa na Gazeti la Serikali la tarehe 22 Novemba, 2021 kwa kutenganishwa iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuitoa Idara ya Habari - Maelezo na kuipeleka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Mei, 2022, Wizara hii imepata mafanikio mbalimbali, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kupitia sekta hizi tatu ni pamoja na kusaidia kutengeneza ajira kwa vijana wengi, watu wa rika mbalimbali, kuwezesha kujenga afya ya akili na mwili kwa wananchi kupitia michezo, kuendelea kuimarisha umoja na mshikamano baina ya wananchi na zaidi ni sehemu ya kimkakati ya kuitangaza nchi yetu kupitia utamaduni, mila na desturi na hata utalii wetu wa kihistoria na kiutamaduni ili mataifa mengine yatufahamu sisi ni akinanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujivunie ongezeko la furaha nchini limekuwa kubwa na halina kipimo. Ni lazima tujivunie ongezeko la uhuru na amani limezidi na halina kipimo. Kiwango cha matumaini kwa Watanzania hakina mfano, ni lazima tujivunie na hii ndiyo Wizara inayosimamia furaha na amani katika eneo la kuwafurahisha na kuwaletea faraja Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta za utamaduni, sanaa na michezo zina umuhimu mkubwa katika Taifa hili. Hii inadhihirishwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akianzisha Wizara ya Utamaduni na Vijana, wakati akihutubia Bunge Tarehe 10 Desemba, 1962 alisema na ninanukuu sehemu ya hotuba yake inayobaki pia kuwa ni dira katika kusimamia shughuli za Wizara hii. Alisema: "Mabadiliko makubwa niliyofanya ni kuunda Wizara mpya, Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana. Nimefanya mabadiliko haya kwa sababu ninaamini kuwa utamaduni ni kielelezo na roho ya Taifa letu. Nchi isiyokuwa na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa

watu pasipokuwa na roho inayowafanya kuwa Taifa". Mwisho wa kunukuu. Sekta hizi ndiyo uhai wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Mapato; Katika mwaka 2021/2022 Wizara awali ilikadiriwa kukusanya Shilingi Milioni 960, baada ya Idara ya Habari ambayo awali ilikuwa imekadiriwa kukusanya shilingi 177,798,000 wizara ilibaki na makadirio ya jumla ya shilingi 782,202,000. Hadi kufika mwezi Mei, 2022 shilingi 513,216,895 sawa na asilimia 65.6 ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni shilingi 5,788,121,000 ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2022 shilingi 2,982,766,206 sawa na asilimia 54.4 ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi; Katika mwaka 2021/2022 iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa shilingi 54,741,802,000. Kati ya fedha hizo mishahara ilikuwa shilingi 19,146,653,000, matumizi mengineyo yalikuwa ni shilingi 14,880,149,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi 20,715,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuundwa kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo bajeti iliyobaki ni shilingi 40,092,502,240, ambapo mishahara ni shilingi 12,598,353,240, matumizi mengineyo shilingi 12,780,149,000 na miradi ya maendeleo shilingi 14,714,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2022 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 34,349,718,436 sawa na asilimia 85.6 ya bajeti yote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, ambapo kati ya fedha hizo matumizi mengineyo ni shilingi 12,553,466,699, mishahara ni shilingi 11,973,173,503; na miradi ya maendeleo ni shilingi 9,823,078,234.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Idara ya Maendeleo ya Utamaduni. Katika kuhakikisha kuwa Wizara inakutana na kuweka mikakati madhubuti na wadau wake, iliratibu kikao kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya zote nchini kilichofanyika Jijini Dodoma Tarehe Nne hadi Tarehe Sita Aprili, 2022. Kikao hicho kililenga kuibua fursa zilizopo, changamoto na kupendekeza njia madhubuti za utatuzi wa changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mafanikio ya vikao hivyo ni kuitambua kada ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenye muundo wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambapo sasa kumeanzishwa Kitengo kipya kinachojitegemea kwa Utamaduni, Sanaa na Michezo badala ya kuwa chini ya Idara ya Elimu kama ilivyokuwa hapo awali. Muundo huo utachangia mafanikio mengi kiutendaji, tayari umesainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tayari umekwishaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na ni matarajio yangu kuwa huko tuendako sasa kutakuwa na utekelezaji wenye tija zaidi

wa majukumu ya Wizara katika ngazi ya Halmashauri na Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utamaduni, imeendelea kuratibu na kuandaa matamasha ya kiutamaduni kwa lengo la kudumisha urithi wa utamaduni. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Mei, 2022, miongoni mwa matamasha yaliyoratibiwa ni pamoja na tamasha la utamaduni la watu wa Mwanza, tamasha la utamaduni la Mkoa wa Kilimanjaro, tamasha la tambiko la kimila la jamii ya Waluguru, tamasha la kumbukizi ya Vita vya Majimaji, tamasha la siku ya utamaduni lililofanyika Tarehe 09 Oktoba, 2021 Jijini Dar es Salaam katika Shule ya Awali na Msingi ya Joseph na tamasha la mawasiliano, utalii na utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimataifa pia, Wizara ilishiriki katika maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya ya Nchi zilizo chini ya Mwambao wa Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Rim Association)*. Kutokana na uzoefu wa matamasha haya, kwa sasa Wizara inaratibu tamasha kubwa la utamaduni litakalofanyika kuanzia mwezi Julai, 2022 Jiji Dar es Salaam na kushirikisha Mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na suala la mmomonyoko wa maadili nchini, Wizara imekamilisha Kitabu cha Mwongozo cha Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Mwongozo huo umejumuisha maoni ya wadau yaliyokusanywa kupitia vikao mbalimbali na unatarajiwa kuzinduliwa wakati wa Tamasha la Kitaifa la Utamaduni linalotarajia kufanyika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Katika kipindi hiki, mafanikio lukuki yamepatikana kupitia BAKITA. Naweza kujinasibu kuwa matumizi ya Kiswahili yanazidi kukubalika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambapo jitihada hizo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 zimezaa matunda kwa Kiswahili kuvishwa joho jipya kuwa lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika. Kiswahili kilipitishwa kuwa Lugha ya Kazi ya Umoja wa Afrika katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Tarehe 05 mpaka Tarehe 06 Februari, 2022 Jijini Addis Ababa - Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni fursa muhimu kwa Wataalam wetu wafasiri na wakalimani nchini ambao katika muda mfupi tayari Watanzania 65 wamesajiliwa kupata fursa za ajira za muda na za kudumu katika Umoja wa Afrika na Kamisheni zake. Pia kutokana na nafasi ya Kiswahili kuendelea kushamiri, baadhi ya Vyuo Vikuu vya nje ya Tanzania ambavyo awali havikuwa na programu za Kiswahili vimeanza harakati ya kuingiza Kiswahili katika programu zao ambapo tayari kuna makubaliano ya awali kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ethiopia, Chuo Kikuu cha *Port Harcourt* - Nigeria na Chuo Kikuu cha *Joachim Chisano* – Msumbiji na ninaamini mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ya kihistoria yaliyopatikana kwa juhudi za Serikali pamoja na wadau wa Kiswahili ni kupitishwa kwa Tarehe 07 mwezi Julai kila mwaka, kuwa ni Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. Tarehe hii ilipitishwa rasmi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni -

*UNESCO* Tarehe 23 Novemba, mwaka 2021. Tarehe hii ilipendekezwa kutokana na ukweli kuwa tarehe 07 Julai, 1954 Mkutano Mkuu wa *TANU* chini ya Uenyekiti wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere uliamua kwa kauli moja kutumia Kiswahili kwa lengo la kuleta umoja kwa Watanganyika wote katika harakati zao za ukombozi. Hivyo, si kujinasibu bali ni kueleza ukweli wa dhahiri shahiri kwamba msingi wa uamuzi huu ni kutokana na mchango mkubwa wa Tanzania katika kukiasisi na kukiendeleza Kiswahili duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu ni wa kihistoria, kwani kwa mafanikio haya Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Kiafrika ambayo imepangiwa siku maalumu ya kusherehekewa na kuadhimishwa Kimataifa. "Chanda chema huvishwa pete". Licha ya kuwa lugha ya kwanza kutoka Bara la Afrika, pia ni lugha yenye wazungumzaji wengi, wanaozidi Milioni 200 duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa johari hii ya thamani na furaha yetu kwa mafanikio haya, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara hii inaendelea na mikakati ya kuiongoza dunia kuadhimisha Siku hii kwa mara ya kwanza Tarehe Saba Julai, 2022 katika Balozi zetu kote Duniani. Tayari Kamati ya Kitaifa ya kuratibu maadhimisho ya siku hii inaendelea na kazi. Ikumbukwe kwamba, kule Umoja wa Mataifa siku hii ya Tarehe Saba itasheherekewa palepale Umoja wa Mataifa - New York, pia kule *UNESCO* itasheherekewa kule nchini Ufaransa siku hii maalum ya Kiswahili. Waswahili husema "Hamadi ni ilio kibindoni na silaha ni iliyo mkononi" Kiswahili ndiyo silaha

yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lilianza na Kongamano la Waandishi la Watangazaji wa Idhaa ya Kiswahii Duniani Tarehe 14 mpaka 18 mwezi Machi, 2022 lililofanyika Jijini Arusha na kufunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na kufungwa na Rais wa Zanzibar, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi ambapo washiriki takribani 250 kutoka redio na televisheni za ndani ya nchi ya Tanzania walishiriki. Kongamano hili litaendelea kufanyika kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Sekta ya Utamaduni na Sanaa imekuwa muhimu si tu kwa kukuza na kuendeleza mila, desturi, lugha na sanaa zetu bali ni chanzo cha ajira na maendeleo ya uchumi kwa Taifa. Sekta hii imekuwa kimbilio la kundi kubwa la vijana kwa kuwapatia ajira kupitia shughuli za kiutamaduni na sanaa kama vile ususi, ufinyanzi, uchongaji, utengenezaji wa batiki, muziki na filamu. Hata hivyo, ili kuzalisha ajira, sekta hii imekuwa ikisuasua kutokana na kukosekana kwa mitaji na utaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huu, leo tunayo furaha kuliambia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imefanikiwa kufanya jambo jingine la kihistoria katika mageuzi ya kiutendaji kwa kuhuisha Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa uliokuwa umekwama kufanya kazi tangu mwaka 2013. Mfuko huu sasa utakuwa na chachu ya ukuaji wa Sekta

za Utamaduni na Sanaa kupitia utoaji wa mikopo, ruzuku na kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo waandaaji wa kazi za utamaduni na sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuanza mchakato wa utoaji mikopo, tayari Serikali imekwishakutoa kiasi cha fedha katika Mfuko huu kati ya bajeti iliyotengwa ya shilingi 1,500,000,000 katika Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Sanaa. Wizara imeendelea kuandaa matukio makubwa ya kimkakati ikiwemo Tamasha kubwa la Kitaifa la Muziki la Serengeti *(Serengeti Music Festival)*. Tamasha hili lilifanyika katika Jiji la Dodoma kwa siku mbili mfululizo tarehe 12 - 13 Machi, 2022 ambapo wasanii mbalimbali zaidi ya 250 walipata fursa ya kushiriki huku wananchi zaidi ya 12,000 walihudhuria tamasha hili na wengine wakinufaika kiuchumi kupitia malipo ya malazi katika hoteli na nyumba za wageni, shughuli za usafiri na huduma nyingine mbalimbali. Aidha, watu wengi zaidi walifuatilia mubashara kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya kwa ufanisi mkubwa maandalizi na ushiriki wa nchi katika maonesho ya Sanaa na Utamaduni duniani kwenye maonesho ya *Dubai Expo2020* tarehe 21 - 27 mwezi Februari, 2022. Katika maonesho hayo, makundi ya kimkakati yaliiwakilisha nchi katika ngoma za asili na za kisasa, muziki wa singeli, muziki wa kizazi kipya na sanaa za ufundi. Vilevile, kulikuwa na kikundi cha muziki wa taarab kutoka Zanzibar. Vikundi vyote hivi vilifanikiwa kuitangaza nchi katika hatua mbalimbali katika maonesho hayo ambapo msanii Mrisho Mpoto kupitia

maonesho ya *Dubai Expo2020* amepata mwaliko katika maonesho ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika nchini Ufaransa tarehe 1- 8 Julai, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Afrika, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Sanaa cha Utamaduni kwa Viziwi Tanzania (KISUVITA) iliratibu kwa mafanikio makubwa mashindano ya urembo na utanashati na mitindo kwa Viziwi tarehe 14 Agosti, 2021, Jijini Dar es Salaam, ambapo jumla ya warembo, watanashati na wanamitindo 74 kutoka Nchi 14 za Afrika walishiriki. Kati ya hao, Watanzania sita wakiongozwa na Mtanzania mrembo kiziwi namba mbili Afrika walifuzu kushiriki mashindano kama hayo ngazi ya dunia yaliyofanyika Nchini Brazil mwezi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninayofuraha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na ufanisi uliooneshwa na Tanzania katika maandalizi ya mashindano hayo ngazi ya Afrika, Bodi ya Wakurugenzi wa Mashindano hayo Duniani *(The Executive Board of Directors for Miss and Mr. Deaf Internaltional)* wameiteua rasmi Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano hayo na kukubaliana yafanyike mwezi Oktoba, 2022, hapa Tanzania Jijini Dar es Salaam. Hii ni heshima nyingine kubwa kwa nchi yetu na katika mashindano hayo yanayotarajiwa kuwa na zaidi ya washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali duniani na tayari yameanza na kuratibiwa kwa ubora wa kidunia kama ulivyosisitiza kuhusu *Royal Tour* kuendelea kuupiga mwingi kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa; baada ya kipindi kirefu cha kutokuwa na Tuzo za Muziki

nchini, tangu mwaka 2015, Wizara kupitia Baraza pamoja na wadau wengine wa Sekta ya Sanaa nchini tumezirejesha tuzo hizi. Serikali ya Awamu ya Sita imezisimamia na kuzigharamia tuzo hizi kwa lengo la kuhamasisha, kuchochea ushindani ili kuzalisha kazi bora na kuendeleza ubunifu kwenye Tasnia ya Muziki Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzo hizi zilizinduliwa tarehe 28 Januari, 2022 na kutolewa rasmi tarehe 2 Aprili, 2022, zilikuwa na jumla ya vipengele 19, ambapo tuzo zilizoshindaniwa zilikuwa 47, na tuzo za heshima zilikuwa nne na Tuzo Maalum moja, jumla ya kazi za muziki zilizopolewa zilikuwa jumla ya kazi za muziki zilizopokelewa zilikuwa 1,360 kutoka kwa wasanii wapatao 536 waliojisajili na kuwasilisha kazi zao ili kushindania tuzo hizi. Washindi wa tuzo hizo wote tunao hapa Bungeni ambao walifanikiwa kupata ushindi kwenye tuzo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu zipo changamoto kadhaa zilizojitokeza katika utoaji wa tuzo hizo, hali hii ilinisukuma kufanya tathmini ya mwenendo wa tuzo hizo katika vikao vya tathimini ya tuzo hizi zilizopita. Nimewaagiza watendaji wangu kuhakikisha kuwa michakato yote ya tuzo zitakazotolewa katika wizara yangu siku za usoni, inafuata misingi ya haki, misingi ya uwazi na uadilifu kwa kuzingatia misingi ya utoaji wa haki duniani inayosema haki ni lazima itendeke kwa uwazi, *justice must be done but not only to be done, it must be seen to be done*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa tuzo hizi zinaandaliwa na Serikali Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo alipohudhuria tamasha la muziki wa kufokafoka akiwa ni Rais wa kwanza mwanamke

kuhudhuria katika tamasha la muziki moja kwa moja la muziki wa kufokafoka tarehe 31 Mei, 2022 mahususi kwa ajili ya kuboresha tuzo zetu. Kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara yangu tutakwenda kujipanga pamoja na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango ili tuzo za mwakani ziwe na mvuto wa hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mageuzi mengine muhimu ni katika kuwaondolea adha wadau wa sanaa kwani kwa mara ya kwanza imeanzishwa mifumo ya kielektroniki kwa usajili na utoaji wa vibali mtandaoni. Kwa sasa baada ya kero ya muda mrefu ya wasanii kutoka mikoa yote nchini kulazimika kusafiri kwenda Ofisi za BASATA, Dar es Salaam, kwa mifumo hii, wasanii wanaweza kujisajili mitandaoni na kupata vyeti na vibali vyao ambavyo vinatumika kuwatambulisha katika mamlaka na taasisi mbalimbali ili wapate huduma wanazohitaji. Kutokana na Mfumo huu muda wa kutolewa vibali umepungua kutoka siku tatu hadi nusu saa. Mfumo huu unajulikana kwa jina la *Artists Management Information System (AMIS)* na unapatikana katika kiunganishi ambacho nimekitaja hapo chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokuwa kwa suala la kihistoria la kurejesha Tuzo za Muziki, kwa upande wa filamu, Serikali ya Awamu ya Sita, kwa upande wa filamu kupitia Bodi ya Filamu Tanzania imefanya mageuzi ya kukumbukwa kwa kuanzisha kwa mara ya kwanza tuzo za Kitaifa za filamu. Tuzo hizi zilizotolewa Jijini Mbeya mwezi Desemba, 2021, zilishuhudia hamasa kubwa ambapo jumla ya filamu 638 ziliwasilishwa na kupatikana washindi 30 waliopata tuzo na fedha taslimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile imeendelea kushirikiana na wadau kuratibu maandalizi na kufanyika kwa Tamasha la Tuzo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu *(UNI AWAS)* lililofanyika tarehe 3 Julai, 2021 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Jijini Dar es Salaam, ambapo tuzo 21 zilitolewa kutoka kwa washiriki 157.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa upande mwingine Wizara kwa mageuzi yanayoendelea, inazidi kuona umahiri wa wanatasnia ya filamu hapa nchini ukiongezeka katika uzalishaji wa filamu bora zinazopata nafasi katika majukwaa ya kimataifa. Mathalani, Filamu ya Vuta Nikuvute iliyoandaliwa mwaka 2021 na inayotoa uhalisia wa hadithi ya Vuta Nikuvute iliyoko kwenye riwaya ya Shaffi Adam Shaffi, ambaye leo tunaye hapa Bungeni imepata nafasi ya kuzinduliwa katika Tamasha la *Toronto International Film Festival (TIF)* Nchini Canada ambalo ni tamasha kubwa katika matamasha matano makubwa ulimwenguni, lakini filamu hii imeshinda mpaka sasa tuzo tatu za kimataifa; tuzo ya Bukinafaso ambayo ni tuzo mashuhuri zaidi Afrika na tuzo iliyotolewa kule Nchini Rwanda. Filamu hii imeendelea kuoneshwa kwenye matamasha mengi zaidi ya kimataifa na kuendelea kushinda tuzo kadhaa ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Filamu ya Binti ambayo tarehe 7 Januari, 2022 iliingia katika moja ya majukwaa maarufu zaidi ya usambazaji wa filamu ulimwenguni ijulikanalo kama *Netflix,* inakuza ari ya wadau wa filamu kutengeneza filamu zilizo bora na zenye viwango vya Kimataifa, inatangaza utamaduni wa nchi ikiwemo lugha ya Kiswahili, inaongeza kipato cha wadau wa filamu na Serikali na inafungua fursa ya washiriki wa

filamu wa Kitanzania kwa kampuni za nje na kuwapatia ajira zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, Bodi ya Filamu inaratibu programu mbalimbali za mafunzo. Moja ya mafunzo yanayoratibiwa ni mafunzo kwa njia ya Semina, ambapo Bodi kwa kushirikiana na Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais, iliratibu mafunzo ambayo ni mafanikio ya awali kabisa ya Filamu ya *Royal Tour*. Aidha, mafunzo yaliyoratibiwa ni kuwakutanisha wadau wa filamu na Bwana John Feist, mtayarishaji wa Filamu ya *Royal Tour*, kutoka *Hollywood,* Nchini Marekani, ambaye alitoa semina hiyo tarehe 29 Aprili, 2022 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam na wadau takribani 300 walishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ilitoa leseni 31 za uendeshaji wa shughuli na biashara za Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini. Leseni hizo zilitolewa ikiwa ni hatua za urasimishaji wa shughuli na biashara ya filamu nchini. Aidha, vitambulisho 125 vilitolewa kwa wadau wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza. Vilevile, kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022 filamu 1,751 zilipokelewa na kuhakikiwa na kupangiwa madaraja; kati ya filamu hizo za ndani zilikuwa 1,713 na za nje ni filamu 38.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Hakimiliki Tanzania *(COSOTA)*; katika kuhakikisha haki za wasanii zinapiganiwa, utendaji na usimamizi wa *COSOTA* uliimarishwa na kuweka rekodi ya ukusanyaji wa mirabaha ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2021 hadi 31 Desemba, 2021 jumla ya Sh.312,290,259 zilikusanywa na kugawanywa kwa wasanii wa muziki

ambapo jumla ya wanufaika 1,123 wenye kazi 5,924 walipata mirabaha. Gawio hilo lililotangazwa tarehe 28 Januari, 2022, ni kubwa zaidi kuwahi kukusanywa tangu Taasisi hiyo ilipoanza kutoa mirabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na agizo la Mheshimiwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan la kuelekeza vyombo vya Habari na Televisheni na Redio ambavyo ni wadau wakubwa wanaotumia kazi za muziki kulipia mirabaha. Mgao ambao ni ongezeko la asilimia 58 ukilinganisha na mgawo uliofanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nafahamu pia katika eneo hili yaliyojitokeza malalamiko mengi kutoka kwa wasanii na wadau mbalimbali juu ya mgawanyo wa mirabaha. Nimewaagiza watendaji wa Wizara wajipange ipasavyo kuhakikisha kuwa malalamiko yaliyojitokeza hayajirudii tena katika mgao unaofuata. Vilevile katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu juu ya malalamiko haya ya mgawanyo wa mirabaha, Wizara na *COSOTA* tuko kwenye hatua za kutafuta mwekezaji ambaye atawekeza katika mfumo wa kisasa kabisa utakaochakata na kutoa taarifa za jinsi ya kazi za muziki zitakavyotumika katika vyombo vya habari mbalimbali, burudani kwa ajili ya kubaini kiasi gani kinapaswa kukusanywa kutoka kwa wasanii kutoka kwa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Michezo; katika mwaka huu, kazi kubwa ya kupigiwa mfano iliyoanza kufanyika ni kuanza kushughulikia tatizo sugu la miundombinu ya michezo, ambayo kwa muda mrefu imekuwa na changamoto au kuanzisha

miundombinu mipya inayoendana na matakwa ya sasa. Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuja na mtazamo mpya katika eneo hili na imetekeleza miradi kadhaa ya kihistoria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tumeanza hatua za ujenzi wa Viwanja vya mazoezi na mapumziko *(Recreational and Leisure Centres)* vitatu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Geita ambapo hatua zote za usanifu zimekamilika na sasa ujenzi utaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uamuzi wa kimkakati wa kujenga viwanja changamani vya michezo na sanaa *(Sports and Arts Arena)* katika Mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, umefikia katika hatua muhimu ambapo usanifu wa michoro umekamilika na sasa Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wizara inazungumza na wadau wa sekta binafsi ili kutekeleza kwa pamoja ambapo sasa Tanzania inakwenda kuwa na *Arena* ya kwanza nchini itakayokuwa na uwezo wa kuchukua wastani wa watu 16,000 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ujenzi wa kiwanja kikubwa cha michezo Jijini Dodoma nao umeendelea katika hatua za kutafuta mkandarasi baada ya upembuzi na hatua zote za maandalizi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ujenzi wa shule 56 za michezo *(sports academy)* katika kila mkoa ambapo kila mkoa kutakuwa na shule mbili za kimkakati za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, ni ujenzi wa Kituo cha Umahiri katika michezo *(Center of Excellence)* katika Chuo cha maendeleo ya Michezo cha Malya; hosteli mpya ya wanafunzi ambapo kwa upande wa Kituo cha Umahiri, hatua zote za usanifu zimekamilika huku ujenzi wa hosteli ukifikia asilimia 40. Vituo hivi vitageuza kilichokuwa Chuo cha Kawaida cha Michezo Malya sasa kuwa na taswira mpya na kuwa Kituo cha Kimataifa kitakacholea watoto wetu wenye vipaji kutoka mitaani huku kikiendelea kutoa mafunzo kwa vijana waliotoka mashuleni. Mwelekeo huu utasaidia kuzalisha wasomi wa michezo lakini pia na wanamichezo mbalimbali watakaokuwa wamepikwa wakiwa wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi pia kuishiwa wingi na shukrani kwa baadhi ya Halmashauri kama Geita, Ruangwa; na majiji kama Arusha na Mwanza, Manispaa za Temeke na Kinondoni kwa viongozi wao kuona umuhimu wa michezo na kutumia fedha zao kufanya ukarabati wa viwanja vyao au kuanza miradi mipya ya ujenzi wa viwanja huku wataalam wa Wizara wakisaidia kutoa ushauri wa kiufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pia tutambue uwekezaji muhimu wa Jiji la Dodoma katika eneo la Chinangali lenye viwanja vingi vya michezo ikiwemo mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa mikono na michezo mingine. Nitumie fursa hii kuwaomba Wakurugenzi wengine nchini kufuata nyayo hizi kwani Sera ya Michezo inatupa hamasa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, mashirikisho mbalimbali ya michezo nchini nayo yamewekeza katika ujenzi na ukarabati wa miradi ikiwemo Shirikisho la Mpira

wa Miguu Tanzania *(TFF)* kwa msaada wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani *(FIFA)* wanaojenga vituo viwili vya michezo Jijini Dar es Salaam na Tanga ambavyo viko katika hatua za mwisho. Aidha, jitihada ya ujenzi wa vituo hivyo kwenye maeneo mengine zinaendelea kufanyika kutegemeana na jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha za ujenzi kutoka kwa wadau wa michezo wa *FIFA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Timu yetu ya Taifa ya Soka la Walemavu *Tembo Warriors*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nenda kwenye Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kwenye kitabu hiki ni ukurasa 103 sababu muda wako umekwisha, Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023...

**NAIBU SPIKA:** Ukurasa 103. Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Sh.900,000,000 kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo, pamoja na vyanzo vya mapato. Hayo ni pamoja na viingilio kutoka matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo kutika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokadiriwa kukusanywa ni shilingi 5,396,455,000 ambacho kimeelezewa katika Kiambatisho 8A na 8B ambao ni mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida; mwaka 2022/2023, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 35,425,991,000. Kati ya fedha hizo Mishahara ni shilingi 8,201,882,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 11,392,949,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni Sh.15,831,160,000 kama ambavyo imeelezewa kwenye Kiambatisho cha 10A, 10B na 10C kinachoonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa mwaka 2022/2023; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2022/2023, naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2022/2023, yenye jumla ya shilingi 35,425,991,000. Kati ya fedha hizo Mishahara ni shilingi 8,201,882,000. Matumizi Mengineyo ni shilingi 11,392,949,000; na Miradi ya Maendeleo ni shilingi 15,831,160,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika mwaka 2022/2023, Wizara yangu inakusudia kufanya mageuzi makubwa katika kuendeleza Sekta zake na kuimarisha mchango wake katika pato la Taifa, kuongeza ajira hususan kwa vijana na kuimarisha michezo nchini. Aidha, kama nilivyobainisha hapo awali, Wizara itawajengea uwezo wasanii wetu kimitaji na mafunzo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, hatua ambayo itaongeza tija, ubora na ushindani wa kazi za sanaa na ubunifu wetu kitaifa na kimataifa. Pia, Wizara inakamilisha uundwaji wa kuanza matumizi ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya kuwahudumia wasanii na wadau wengine wa sanaa ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma, kurahisisha urasimishaji wa Sekta ya Sanaa na shughuli za ubunifu ukubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kama nilivyosema awali hotuba yangu ni ndefu, naomba kila neno lilozungumzwa katika hotuba yangu liingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.michezo.go.tz na kupitia mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA**

## MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii leo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena hapa Bungeni tukiwa buheri wa afya, na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza kwa ufanisi mkubwa majukumu niliyokabidhiwa.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita (6) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi yote ya ulinzi na usalama kwa kutimiza mwaka mmoja hivi karibuni katika uongozi wa Taifa letu tangu alipoapishwa kushika nafasi hiyo mwezi Machi mwaka 2021. Aidha, nimpongeze kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi chake kifupi cha uongozi katika sekta zetu yaliyo shahir na dhahir yaliyotokana na kuliongoza Taifa letu kwa umahiri, weledi, umakini na upeo

mkubwa unaoendelea kulishamirisha Taifa letu ndani na nje ya nchi. Sisi na wadau wetu wote wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo tunamuahidi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuendana na fikra, maono, na falsafa yake ya kazi iendelee lakini pia tunaendelea kumuombea dua njema kila uchao kwani Waswahili husema: "Dua njema ya msafiri ndilo tairi salama".

**4. *Mheshimiwa Spika,*** sambamba na pongezi hizo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kutawazwa Septemba 8, 2021, kuwa Chifu wa Machifu Tanzania, Chifu "*Hangaya.*" Pia, tunampongeza kwa namna alivyo mstari wa mbele kuhimiza masuala ya Utamaduni na Sanaa pamoja na kusimamia na kuendeleza Michezo nchini hususan Michezo kwa Wanawake kupitia maagizo na maelekezo yake aliyoyatoa kwa nyakati mbalimbali. Nasi tupo mstari wa mbele kutekeleza maagizo na maelekezo yote ya Mheshimiwa Rais anayotoa katika Sekta ninazozisimamia. Tunamuahidi kuendelea kuutengeneza mwingi, ili aweze kuupiga mwingi.

**5. *Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais na ambayo yanaendelea kuwa Dira Kuu kwetu ni pamoja na: kufanyika kwa matamasha ya utamaduni yatakayoshirikisha mikoa yote kwa kushindanishwa ili kumpata mshindi mmoja; Kufufua mashindano ya Taifa Cup, michezo iliyositishwa kwa muda mrefu. Vilevile, kuboresha michezo kwa wanawake ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wanawake kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo katika michezo, ikizingatiwa wanawake wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya

Kimataifa kila wanapopata nafasi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** maelekezo mengine ya Mheshimiwa Rais ni kurejesha Tuzo mbalimbali; kutoa mirabaha kwa wasanii; na kuhakikisha Timu zetu za Taifa zinafanya vyema ndani na nje ya nchi yetu kwa kuandaa timu bora za Taifa zitakazoundwa na vijana watakaopatikana kupitia programu ya kusaka na kuibua vipaji vya vijana nchi nzima itakayoitwa michezo Mtaa kwa Mtaa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** Halikadhalika, nawapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kumsadia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Kipekee, viongozi hawa wasiochoka, wamekuwa wadau mahiri wa sekta zetu ambapo katika kipindi hiki viongozi hawa wabobezi hapa nchini wameshirikiana nasi kuzindua au kufunga matukio mbalimbali ya kimichezo, kiutamaduni na sanaa na kutupatia maelekezo ya kuboresha sekta hizi. Tunawashukuru sana.

**8.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba nitambue pia na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kiongozi mwingine galacha ambaye Taifa hili limebarikiwa kuwa naye, kwa juhudi zake thabiti za kuendeleza Kiswahili na hasa msisitizo anaoutoa mara kwa mara katika mikutano yake, kutumia Kiswahili fasaha na sanifu kwa kiasi cha kutambuliwa mchango

wake kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na kukabidhiwa Tuzo ya Heshima wakati wa Kongamano la Idhaa za Kiswahili Duniani lililofanyika Jijini Arusha tarehe 14 hadi 18 Machi, 2022. Dkt. Hussein Ali Mwinyi pia si mchache wa mengi katika maeneo na mawanda mengine nje ya Kiswahili; tunampongeza kwa jitihada kubwa, mahiri na za kimkakati anazochukua katika kuleta ufanisi kwenye sekta za utamaduni, sanaa na michezo kwa upande wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

**9. *Mheshimiwa Spika,*** Waswahili wanasema: "Mwenda tezi na omo, marejeo ngamani," sasa nitambue na kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa wabunge wote kuwa Spika wa Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwako kumeendeleza historia adhimu katika nchi yetu kwani umekuwa mwanamke wa pili kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia umeshika madaraka haya ukiwa ni Spika kijana kabisa katika historia ya Bunge la Vyama Vingi. Sisi tuna imani kubwa na wewe kuwa Bunge letu litaendelea kutekeleza wajibu wake kwa kasi na umakini mkubwa. Hili tayari limedhihirika katika vikao ambavyo umeviongoza kwa kipindi hiki. "Jina jema hung'ara gizani." Hongera sana!

**10. *Mheshimiwa Spika*,** pia nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa uzoefu wake wa muda mrefu akiwa Mwenyekiti wa Bunge, utamwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kwa mujibu wa

sheria ikiwa ni pamoja na kuisimamia Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo. "Kwa hakika ya kale ni dhahabu".

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kujiunga na Bunge lako Tukufu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi katika majimbo yao. Waheshimiwa hao ni pamoja na: Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani kutoka Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai wa Jimbo la Ngorongoro; na Mheshimiwa Mohamed Said Issa kutoka Jimbo la Konde. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru tena kipekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kwa mara nyingine tena na kuniteua kusimamia Wizara hii kubwa yenye dhamana ya kuratibu na kuendeleza Sekta za Kimkakati za Utamaduni, Sanaa na Michezo ambazo ndio Nguvu Shawishi ya Taifa (*Soft Power*). Natoa shukrani hizo kwanza kwa kuteuliwa mara ya pili ndani ya kipindi kifupi cha mwaka mmoja nikitumikia nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na sasa ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na teuzi hizo, Mheshimiwa Rais ameniweka kwenye historia mpya inayonifanya niwe miongoni mwa mawaziri wachache

hapa nchini waliopata bahati ya kulitumikia Taifa katika mihimili yote mitatu ya Dola katika nafasi andamizi. Nimekuwa kwenye mhimili wa Mahakama nikitumikia nafasi mbalimbali andamizi za uongozi kwa takribani miaka 20, nimekuwa kwenye Bunge nikitumikia nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa vipindi viwili mfululizo, na sasa naitumikia Serikali katika chombo cha juu kabisa cha ushauri na maamuzi (Baraza la Mawaziri) nikiwa Waziri kamili.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara hii ni kubwa na muhimu kwani ina nguvu ya kujenga ushawishi (*soft power*) kwa nchi kwa sababu inakusanya watu wote na inagusa maisha ya Watanzania wengi wapenda michezo na burudani katika nchi hii kupitia sekta zetu za Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao wanakadiriwa kuwa takribani asilimia 90 ya Watanzania. Kila mtu katika nchi hii anaguswa ama kwa michezo, utamaduni au sanaa. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais utendaji bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu niliyokabidhiwa ili kutimiza adhima yake ya kuiunda upya Wizara hii.

**15.** ***Mheshimiwa Spika*,** naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kwa maelekezo, ushauri, michango na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Aidha, ushauri, maoni na maelekezo hayo yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Wizara itaendelea kuzingatia ushauri, maoni,

mapendekezo na maelekezo yanayotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2022/23.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, chambilecho wahenga, "Mcheza kwao hutuzwa na mfukua lake halimchafui ukucha" nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Jimbo letu kwa lengo la kuwaletea maendeleo wana Rufiji. Ninawaahidi utumishi uliotukuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** "Jifya moja haliinjiki chungu"natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu wa Wizara wakati wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu na mageuzi makubwa tunayoendelea nayo wizarani na katika sekta zetu. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Pauline P. Gekul (Mb.), Naibu Waziri makini wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Dkt. Hassan S. Abbasi, Katibu Mkuu anayehakikisha mambo yanakwenda na mageuzi yanatokea; Saidi O. Yakubu, Naibu Katibu Mkuu anayehakikisha katika mageuzi haya hatukati tamaa wala kurudi nyuma; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wasiolala kuhakikisha mambo yanatokea na mipango inakua kweli.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, niwashukuru kwa dhati Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma ili

hatimaye kuleta tija na ufanisi kwa Wizara. Wadau wa maendeleo na wadau wengine kama mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau mmoja mmoja wa sekta za sanaa, utamaduni na michezo ninyi nyote mmekuwa msukumo mkubwa katika kuhakikisha hatukati tamaa, haturudi nyuma. Mmetushamirisha!.

**19. *Mheshimiwa Spika,*** ni masikitiko yetu tunapobaini kwamba katika kipindi hiki Bunge lako Tukufu lilipatwa na misiba kwa kuwapoteza Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliokuwa wawakilishi wa wananchi katika majimbo yao. Wabunge hao ni Mheshimiwa Elias John Kwandikwa wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Ole Nasha wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatib Said Haji wa Jimbo la Konde; na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa. Kwa niaba yangu binafsi, Wizara na wadau wetu, tunatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Familia za Marehemu, Ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa majimbo ya Ushetu, Ngorongoro, Konde na Rukwa. Nawaombea kwa Mungu azipokee na kuzilaza roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**20. *Mheshimiwa Spika,*** nikifanya dhukuru ya mwaka huu mmoja pia kwa masikitiko natambua kuwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Mei, 2022 Taifa letu pia limepoteza wadau mahiri na wa kutegemewa wakiwemo wanamichezo na wasanii mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia za marehemu wote, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuwapoteza wapendwa wao "Hakika sote tu wa Mwenyezi Mungu, na kwake tutarejea". Hapa pia natambua tunao

wadau wetu ambao wamepatwa na maradhi na wanaendelea kupigania afya zao akiwemo msanii mahiri kupata kutokea katika kizazi cha awali cha muziki wa kizazi kipya na Mbunge mwenzetu wa zamani Joseph Haule, Profesa Jay, ambaye anaendelea kupigania afya yake katika Hospitali ya Muhimbili Dar es Salaam kwa miezi kadhaa sasa. Wizara na wadau tunaendelea kumuombea lakini pia kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tunaendelea kusimamia kwa uthabiti ahadi ya Mhe Rais ya kuhakikisha Serikali inabeba matibabu yake kwa hatua zake zote na mpaka sasa hakuna lililokwama.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2021/22 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/23 aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Aidha, hotuba hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025; Mpango Mkakati wa Wizara 2021/22 - 2025/26; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2021/22 na Sehemu ya Nne inaelezea changamoto zilizojitokeza na hatua

zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/23; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2022/23; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2022/23; na mwisho Sehemu ya Nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

## 2.0 MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO, NA VIPAUMBELE VYA WIZARA

**23.** ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za utamaduni, sanaa na michezo na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimali watu Wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Taasisi ya Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania (COSOTA), Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Pia, Wizara inaratibu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa wenye jukumu la kuwajengea uwezo wadau wa utamaduni na sanaa nchini kwa kuwapatia mafunzo na mikopo yenye riba nafuu.

**24.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza na kuimarisha

utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Maboresho ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Uendelezaji wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali *(Resources Mobilization)*.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2022/23 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo saba ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiwemo viwanja na kumbi za kisasa za sanaa na michezo; kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kuimarisha, kuwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa katika michezo na michuano mbalimbali. Vilevile, kuhamasisha wadau kusaidia timu, vilabu na wawakilishi mbalimbali wa kitaifa katika ushiriki wa michezo na michuano ya kimataifa.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni kukamilisha mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali za kisera na kisheria katika kuimarisha usimamizi na utendaji katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha na kuongeza uwezo wa kitaasisi katika usimamizi na utekelezaji wa masuala ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo. Masuala mengine ni kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususani zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, TAMISEMI, Elimu, Afya, Maliasili na Utalii; Mambo ya Nje na Ushiriano wa Afrika Mashariki na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo

Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni mpya lakini iliyosheheni uzoefu mkubwa katika maendeleo ya nchi hii. Wizara hii iliundwa na Mhe. Rais tarehe 13 Septemba, 2021 kwa Tangazo la Serikali Na. 782 lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 22 Novemba, 2021 kufuatia kutenganishwa kwa iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuitoa Idara ya Habari na kuipeleka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki kifupi cha uwepo wake na kwa misingi iliyowekwa nyuma na Wizara mtangulizi wake, kati ya Julai, 2021 hadi Mei, 2022, Wizara hii imepata mafanikio mbalimbali na imeweka misingi muhimu ya mafanikio zaidi katika miaka ijayo, na kubwa linaloiangaza nchi na dunia ni kwa Wizara kujiimarisha na kuwa sehemu ya nguvu ya kujenga ushawishi *(Soft Power)* kwa Taifa Letu. Sekta hizi tatu zimesaidia kutengeneza ajira kwa vijana wengi na watu wa rika mbalimbali; zimewezesha kujenga afya ya akili na mwili kwa wananchi kupitia michezo. Aidha, ni sehemu ya kimkakati ya kuitangaza nchi yetu kupitia utamaduni, sanaa na michezo na hata utalii wetu ili mataifa mengine yaifahamu Tanzania na utamaduni wake.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nirudie kusisitiza, sekta hizi zina mchango mkubwa na wa kimkakati kwa Taifa letu na hapa nimshukuru tena Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa maono na uamuzi wake wa kuiunda

upya Wizara hii ili ipate nguvu ya kusimamia kwa karibu zaidi sekta hizi za ubunifu na burudani kwa Taifa. Umuhimu wa sekta hizi unadhihirishwa na maono na kauli ya zamani ya Mwasisi wa Taifa letu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akianzisha Wizara ya Utamaduni na Vijana, wakati akihutubia Bunge tarehe 10 Desemba, 1962 aliposema na ninukuu sehemu ya hotuba yake, *"Mabadiliko makubwa niliyofanya ni kuunda Wizara mpya; Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana. Nimefanya mabadiliko hayo kwa sababu ninaamini kuwa utamaduni ni kielelezo na roho ya Taifa lolote. Nchi isiyo kuwa na utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu pasipo kuwa na roho inayowafanya kuwa Taifa"*. Mwisho wa kunukuu.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021/22

## 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**30. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22 Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini (Sh.960,000,000). Baada ya Idara ya Habari ambayo awali ilikuwa imekadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja Sabini na Saba, Mia Saba Tisini na Nane Elfu (Sh.177,798,000) kuhamishiwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ilibaki na makadirio ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Saba Themanini na Mbili, Mia Mbili na Mbili Elfu

(Sh.782,202,000) zilizokadiriwa kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Michezo. Hadi kufika mwezi Mei, 2022 Shilingi Milioni Mia Tano Kumi na Tatu, Mia Mbili Kumi na Sita Elfu, Mia Nane Tisini na Tano (Sh.513,216,895) sawa na asilimia 65.6 ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nane Sitini na Sita, Mia Nne Arobaini na Nne Elfu (Sh.33,866,444,000) baada ya kuhama kwa Taasisi za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Taasisi zilizobaki wizarani zilibaki na makadirio ya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Mia Moja Ishirini na Moja Elfu (Sh.5,478,121,000), ambapo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Mia Saba Sitini na Sita Elfu, Mia Mbili na Sita (Sh.2,982,766,206) sawa na asilimia 54.4 ya lengo zilikuwa zimekusanywa hadi kufikia mwezi Mei, 2022.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22 iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa Shilingi Bilioni Hamsini na Nne, Milioni Mia Saba Arobaini na Moja, Mia Nane na Mbili Elfu (Sh.54,741,802,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ilikuwa Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Moja Arobaini na Sita, Mia Sita Hamsini na Tatu Elfu (Sh.19,146,653,000), Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Nane Themanini, Mia Moja Arobaini na Tisa Elfu (Sh.14,880,149,000) na Miradi ya

Maendeleo ni Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Saba Kumi na Tano (Sh.20,715,000,000).

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia kuundwa kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo bajeti iliyobaki ni Shilingi Bilioni Arobaini, na Milioni Tisini na Mbili, Mia Tano na Mbili Elfu, Mia Mbili Arobaini (Sh.40,092,502,240) ambapo Mishahara ni Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tano Tisini na Nane, Mia Tatu Hamsini na Tatu Elfu, Mia Mbili Arobaini (Sh.12,598,353,240); Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Saba Themanini, Mia Moja Arobaini na Tisa Elfu (Sh.12,780,149,000); na Miradi ya Maendeleo Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Saba Kumi na Nne (Sh.14,714,000,000).

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, kufikia mwezi Mei, 2022 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Nne na Nne, Mia Sita Arobaini na Tatu Elfu, Mia Mbili Thelathini na Saba (Sh.34,349,718,436) sawa na asilimia 85.6 ya bajeti yote, kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambapo kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tano Hamsini na Tatu, Mia Sita Sitini na Sita Mia Sita Tisini na Tisa (Sh.12,553,466,699); Mishahara Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Mia Moja Sabini na Tatu Elfu, Mia Tano na Tatu (Sh.11,973,173,503) na Miradi ya Maendeleo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane Ishirini na Tatu, na Sabini na Nane Elfu, Mia Mbili Thelathini na Nne (Sh.9,823,078,234). Fedha hizi zimekuwa chachu ya utendaji wizarani na katika Taasisi na msingi muhimu wa kufikiwa mafanikio mbalimbali ambayo tunayaeleza kwa kina katika hotuba hii.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

### 3.2.1 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

#### 3.2.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya utamaduni ina majukumu ya kuhifadhi na kuendeleza urithi na utamaduni, lugha na maadili ya Taifa; kuendeleza utambulisho wa Taifa letu; kuhimiza na kukuza utaifa kwa vijana wetu na wananchi kwa ujumla; kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA); kufanya tafiti katika uga wa sekta na kuratibu na kusimamia shughuli za Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuiwezesha Sekta ya Utamaduni kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutokea duniani kote, Wizara imeendelea kuhuisha Sera ya Taifa ya Utamaduni ya Mwaka 1997 ili iweze kukidhi mahitaji na kuendana na wakati kwa kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wasanii, maafisa utamaduni, na maafisa sanaa, Machifu na Viongozi wa Kimila. Kupitia vikao mbalimbali mathalani, kikao cha Machifu na viongozi wa kimila kilichofanyika tarehe 5 Oktoba, 2021 Jijini Dodoma, Rasimu ya Kwanza ya Sera hii sasa imekamilika na muelekeo katika mwaka ujao wa fedha ni kuiwasilisha katika Mkutano wa wadau wote na kuendelea na hatua zinazofuata za kuiidhinisha.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika katika kuhakikisha kuwa Wizara inakutana na kuweka mikakati madhubuti

na wadau wake, iliratibu Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo wa mikoa na Halmashauri za Wilaya zote nchini kilichofanyika tarehe 04 hadi 06 Aprili, 2022 Jijini Dodoma. Kikao hicho kililenga kuibua fursa zilizopo, changamoto na kupendekeza njia madhubuti za utatuzi wa changamoto hizo. Moja ya mafanikio ya vikao hivi ni kutambuliwa kwa Kada ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenye Muundo wa TAMISEMI ambapo sasa kimeanzishwa Kitengo kipya kinachojitegemea cha Utamaduni, Sanaa na Michezo badala ya kuwa chini ya Idara ya Elimu kama ilivyokuwa hapo awali. Muundo huo utakaochagiza mafanikio mengi kiutendaji tayari umesainiwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanza kutumika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na ni matarajio yangu kuwa huko tuendako sasa kutakuwa na utekelezaji wenye tija zaidi wa majukumu ya Wizara katika ngazi ya Halmashauri.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utamaduni, imeendelea kuratibu na kuandaa matamasha ya kiutamaduni kwa lengo la kudumisha urithi wa utamaduni. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, miongoni mwa matamasha yaliyoratibiwa ni pamoja na Tamasha la Utamaduni la lililohusisha jamii ya Wasukuma na Wanyamwezi lililofanyika katika Uwanja wa Red Cross, Kisesa Jijini Mwanza, tarehe 07 - 08 Septemba, 2021; Tamasha la Utamaduni Mkoa wa Kilimanjaro lililohusisha jamii za Wachaga, Wapare na Wamasai lililofanyika katika uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika katika Manispaa ya Moshi tarehe 22 Januari, 2022. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu Tamasha la Tambiko la

Kimila la Jamii ya Waluguru lililofanyika katika Himaya ya Chifu Kingalu Mwanabanzi wa XV, tarehe 16 - 17 Oktoba, 2021 katika Kijiji cha Kinole, Wilaya ya Morogoro Vijijini. Lengo la tambiko lilikuwa kuombea Taifa letu dhidi ya majanga mbalimbali ikiwemo homa inayosababishwa na virusi vya Korona (UVIKO-19), kukosekana kwa mvua na maradhi mengine.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Matamasha mengine yaliyoratibiwa ni pamoja na Tamasha la Kumbukizi ya Vita vya Maji Maji lililofanyika Mkoani Ruvuma tarehe 24 hadi 27 Februari, 2022; Tamasha la Siku ya Utamaduni lililofanyika tarehe 09 Oktoba, 2021 Jijini Dar es Salaam katika Shule ya Awali na Msingi ya Mt. Joseph na Tamasha la Mawasiliano, Utalii na Utamaduni lililofanyika Jijini Mwanza terehe 23 Novemba, 2021. Kutokana na uzoefu wa Matamasha haya kwa sasa, Wizara inaratibu Tamasha kubwa na la Kitaifa la Utamaduni litakalofanyika kuanzia tarehe 01 Julai, 2022 Jijini Dar es Salaam na kushirikisha mikoa yote;

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, kimataifa, Wizara ilishiriki katika Maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya ya Nchi zilizo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Rim Association - IORA)*. Maadhimisho hayo yalifanyika katika mji wa Mapou, Mauritius tarehe 7 Machi, 2022. Katika Maadhimisho hayo, Serikali ilipeleka kikundi cha utamaduni (*Tasting Corner and Cultural Perfomance*) kwa lengo la kutangaza utamaduni wetu, ambacho kilihusika pia na maandalizi ya chakula cha asili. Hii ilikuwa fursa adhimu ya kuutangaza utamaduni wetu nje ya nchi.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na suala la

mmomonyoko wa maadili nchini, Wizara imekamilisha Kitabu cha Mwongozo cha Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Mwongozo huo umejumuisha maoni ya wadau yaliyokusanywa kupitia vikao mbalimbali na unatarajiwa kuzinduliwa wakati wa Tamasha la Kitaifa la Kiutamaduni linalotarajia kufanyika mwanzoni mwa mwezi Julai, 2022.

### 3.2.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kuimarisha lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi; kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma; kuratibu utafiti wa Kiswahili kwa kushirikiana na wadau na kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Katika kipindi hiki mafanikio lukuki yamepatikana kama ifuatavyo:

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** naweza kujinasibu kuwa matumizi ya Kiswahili yanazidi kukubalika kitaifa, kikanda na kimataifa ambapo jitihada hizo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 zimezaa matunda kwa Kiswahili kuvishwa joho jipya kuwa lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika. Kiswahili kilipitishwa kuwa Lugha ya Kazi ya Umoja wa Afrika katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Jijini Addis Ababa, Ethiopia tarehe 5 - 6 Februari, 2022 ***Kiambatisho Na.1A*** *Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwasilisha hoja ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika.* Hatua hii ni fursa muhimu kwa Wataalamu wetu wa

Tafsiri na Ukalimani nchini ambao katika muda mfupi tu tayari Watanzania 65 wamesajiliwa kupata fursa za ajira za muda na za kudumu katika Umoja wa Afrika na Kamisheni zake. Aidha, nyaraka muhimu za Umoja wa Afrika ikiwa ni pamoja na Itifaki zitatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kutoa ajira zaidi kwa wataalamu wetu.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** tukirejelea fursa nyingine zilizoainishwa hapo juu, tayari Watanzania saba (7) wamepata nafasi ya kuhudumu katika mikutano mbalimbali ya Umoja wa Afrika na Kamisheni zake ambapo wakalimani wawili (2) walihudumu katika Mkutano wa Kawaida wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika  uliofanyika Februari, 2022 na wakalimani watatu (3)  pamoja na wafasiri wawili (2) walihudumu katika Mkutano wa 71 wa Kamisheni ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika uliomalizika tarehe 13 Mei, 2022.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, kutokana na nafasi ya Kiswahili kwa sasa, lugha hii inaendelea kushamiri, ambapo baadhi ya vyuo vikuu vya nje ya Tanzania ambavyo awali havikuwa na programu za Kiswahili vimeanza harakati za kuingiza Kiswahili katika programu zao ambapo tayari kuna makubaliano ya awali ya kushirikiana kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ethiopia, Chuo Kikuu cha Port Harcourt (Nigeria) na Chuo Kikuu cha Joachim Chisano (Msumbiji) katika kufundisha Kiswahili.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inafahamu, kunufaika zaidi kwa Watanzania katika fursa hizi za Kiswahili kutahitaji mikakati zaidi na nchi yetu kuwekeza katika kuieneza na utafiti wa lugha hii. Hivyo, moja ya

mafanikio muhimu katika kipindi hiki ni Serikali kupitia Wizara hii katika kulisukuma mbele zao jipya na diplomasia mpya ya Kiswahili, Wizara kupitia BAKITA imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili wa Miaka 10 (2022-2032) ambapo miongoni mwa maazimio yake makubwa unalenga kuwasajili wataalamu wa Kiswahili na kuimarisha stadi zao.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa lengo hili umeanza na tayari wakalimani 65 wamesajiliwa na Baraza na kupatiwa mafunzo ya kuwaimarisha katika uga huo. Vilevile, wataalamu 1,130 wamepatiwa mafunzo ya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambapo miongoni mwao kuna walimu 2 wamekwenda kufundisha nchini Uingereza, 1 Ujerumani, 1 Polandi, 5 Afrika Kusini na 1 Uganda. Aidha, miongoni mwa wahitimu hao wapo walioanzisha madarasa ya ana kwa ana ya kufundisha Kiswahili kwa wageni na wengine wanafundisha kwa njia ya mtandao. Kwa ujumla Kiswahili kwa sasa ni bidhaa na ni ajira.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BAKITA inaendelea kusajili wataalamu wa Kiswahili katika kanzidata ili Watanzania wengi zaidi watambulike utaalamu wao ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Baraza limesajili wataalamu 19 ambapo wanaume ni 13 na wanawake 6. Jumla ya wataalamu waliosajiliwa hadi sasa ni 1,325. Tunawaalika Watanzania wote wanaojiamini kuwa na utaalamu mahsusi katika Kiswahili kutumia dirisha hili la BAKITA kujisajili ili wapate vyeti vitakavyowapa ajira duniani.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ya kihistoria yaliyopatikana kwa juhudi za Serikali pamoja na wadau wa Kiswahili ni kupitishwa kwa tarehe 7 Julai ya kila mwaka, kuwa ya Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. ***Kiambatisho Na.1B,*** *ni nembo ya Kiswahili iliyotumika wakati wa Mkutano wa UNESCO kupitisha tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku ya kuadhimisha Kiswahili Kimataifa*. Tarehe hii ilipitishwa rasmi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) tarehe 23 Novemba 2021. Tarehe hii ilipendekezwa kutokana na ukweli kuwa tarehe 7 Julai, 1954 Mkutano Mkuu wa TANU chini ya Uenyekiti wa Baba wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere uliamua kwa kauli moja kutumia Kiswahili kwa lengo la kuleta umoja kwa Watanganyika wote katika harakati za ukombozi. Hivyo, si kujinasibu bali ni kueleza ukweli wa dhahiri shahiri kwamba msingi wa uamuzi huu ni kutokana na mchango mkubwa wa Tanzania katika kukiasisi na kukiendeleza Kiswahili.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimesema uamuzi huu ni wa kihistoria; kwani kwa mafanikio haya Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Kiafrika ambayo imepangiwa siku maalumu ya kusherehekewa na kuadhimishwa Kimataifa. "*Chanda chema huvishwa pete*". Licha ya kuwa lugha ya kwanza kutoka Bara la Afrika, pia ni lugha yenye wazungumzaji wengi, wanaozidi milioni 200 duniani kote.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni kwa kutambua umuhimu wa johari hii ya thamani na furaha yetu kwa mafanikio haya, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara hii inaendelea na mikakati ya kuiongoza Dunia kuadhimisha Siku hii kwa mara ya kwanza Julai 7, 2022. Tayari Kamati ya

Kitaifa ya Kuratibu Maadhimisho ya siku hii inaendelea na kazi. Kama wasemavyo Waswahili "*Hamadi ni ilio kibindoni, na silaha ni iliyo mkononi*" Kiswahili ndiyo silaha yetu.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kutambuliwa huku kwa Kiswahili kimataifa Baraza limeendelea kwa kasi kutangaza Kiswahili kupitia mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa njia ya mtandao kwa kuanzisha mfumo maalumu wa kufundisha Kiswahili kwa wageni (*Swahili Prime*), kutambua vituo vinavyofundisha Kiswahili nje ya nchi kikiwemo *Ethiopian Swahili Community* na *Kituo cha Utamaduni Tanzania Seoul* ambapo hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya vituo 17 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ndani na nje ya nchi vilitambuliwa rasmi na miongoni mwa vituo hivyo, vituo vinne (4) viko nje ya nchi. Vilevile, kwa kushirikiana na Balozi zetu nje ya nchi Serikali imeweza kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili ambapo hadi mwezi Aprili, 2022, Balozi zetu nchini Korea Kusini, Ufaransa na Nigeria zinafundisha lugha ya Kiswahili.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na jitihada hizi, Balozi nyingine zikiwemo Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe na Msumbiji zimeanza harakati za kufungua madarasa ya kufundishia Kiswahili. Pia, Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani unakusudia kufungua maktaba na Ubalozi wa Namibia unakusudia pia kufungua Klabu za Kiswahili nchini humo. Aidha, Serikali katika kuchagiza harakati hizi imesambaza vitabu vya Mwongozo wa Taifa wa Kufundisha Kiswahili kwa Wageni katika Balozi mbalimbali zikiwemo Ubalozi wa Uholanzi, Burundi, Namibia, Afrika Kusini, Zimbabwe, Ethiopia na Nigeria. Vilevile, ilipeleka vitabu 65 vya

kujifunza Kiswahili Hatua ya Kwanza katika maonesho ya *Dubai Expo 2022*, ambavyo viligawiwa bure kwa lengo la kuhamasisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika BAKITA imeendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili kwa jamii ndani na nje ya nchi kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari. Katika kutekeleza jukumu hili, jumla ya vipindi 679 vilirushwa hewani kupitia redio na televisheni. Vipindi hivi vililenga kuuelimisha umma kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili pamoja na isimu na fasihi ya lugha ya Kiswahili. Aidha, makala 32 zilichapishwa kupitia gazeti la HabariLeo; na Makala 4 katika magazeti mengine. Pia, gazeti la mtandaoni la Lugha Yetu lilitolewa mara 7. Baraza limekamilisha maandalizi ya Jarida la Lugha Yetu Toleo Na. 40 ambapo nakala 5,000 zimechapishwa na zitasambazwa kwa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha matumizi ya Kiswahili. Fauka ya hayo, elimu ya matumizi ya lugha ilitolewa kupitia mabango ya msamiati na misemo ya busara iliyotolewa kupitia akaunti za Baraza za mitandao ya kijamii za *Facebook*, *Twitter* na *YouTube*.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Baraza liliendesha mafunzo katika Mkoa wa Tanga kuimarisha ujenzi wa kada muhimu ya uandishi wa habari ambapo jumla ya waandishi na watangazaji wa vyombo vya habari 22 walipatiwa mafunzo ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Aidha, Baraza liliandaa Kongamano la Waandishi na Watangazaji wa Idhaa za Kiswahili Duniani tarehe 14 – 18 Machi, 2022 lililofanyika Jijini Arusha na kufunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor

Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kufungwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo washiriki takribani 250 kutoka redio na televisheni za ndani na nje ya nchi walishiriki. Kongamano hili litaendelea kila mwaka.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada hizohizo za nchi kujiimarisha kwa upande wa Kiswahili, tayari Sheria na Kanuni ishirini na sita (26) za Wizara na Taasisi mbalimbali zimetafsiriwa kwa Kiswahili kwa kushirikisha wataalamu wa Baraza. Fauka ya hayo, BAKITA lilitafsiri nyaraka mbalimbali 743 kutoka katika asasi, mashirika, taasisi za serikali na watu binafsi na kuthibitisha tafsiri 2,550 zilizofanywa na wakala wake.

### 3.2.1.3 PROGRAMU YA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu haitasahaulika kwa historia yake ya ushujaa na uthubutu; nguzo muhimu inayoendelea kutuongoza hadi sasa kwa jinsi tulivyoongoza huko nyuma mapambano ya ukombozi wa Bara la Afrika. Na kama unavyofahamu, kwa heshima hiyo Umoja wa Afrika (AU) uliipa Tanzania jukumu la kuwa Makao Makuu ya Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika, programu inayosimamiwa na Wizara hii.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama walivyojitoa wazee wetu, nasi pia katika kuendeleza historia hizo tumeendelea kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Programu, ambapo, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, tumeendelea kukamilisha ukarabati wa jengo

lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ambapo Makao Makuu yake yalikuwa Jijini Dar es Salaam kuanzia mwaka 1963 hadi 1994. Jengo hilo ambalo ni kielelezo cha Ukombozi wa Bara la Afrika lilikuwa kuukuu na wakati wowote lingebomoka na kufuta kumbukumbu hiyo muhimu.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara hii imekamilisha ukarabati huo kwa asilimia 85 kufikia Mei, 2022 na baada ya kukamilika eneo hilo litakuwa Makumbusho ya Afrika ya Historia ya Ukombozi ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2011. Aidha, katika kipindi hiki Programu hii pia imefanya utafiti na kukusanya taarifa za maeneo 15 yenye historia ya Ukombozi yaliyopo Dar es Salaam na Zanzibar; pamoja na kufanya mahojiano na mashuhuda 20 wa Harakati za Ukombozi wa Afrika ili kutunza historia hiyo.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yaliyotekelezwa na Programu ni pamoja na kutambua na kukusanya nyaraka za picha na magazeti yenye taarifa za harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika ambapo jumla ya nyaraka na magazeti 150 yamekusanywa; kufanya maonesho ya historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika; kuratibu ziara ya Mheshimiwa Monica Mutsvangwa (Mb.), Waziri wa Habari na Utangazaji kutoka Jamhuri ya Zimbabwe ya kutembelea maeneo ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika Novemba, 2021 katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Morogoro, na Pwani; na kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika yaliyofanyika Wilaya ya Kongwa Jijini Dodoma tarehe 23 Machi, 2022 ambapo takribani

washiriki 700 walihudhuria maadhimisho hayo wakiwemo wanafunzi.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu iliendelea kuweka mabango ya utambulisho wa maeneo yenye urithi wa Ukombozi wa Afrika katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Zanzibar kwa ajili ya kuyatambulisha na kuyalinda maeneo hayo; kuanzisha Maktaba ya Programu ya Ukombozi yenye vitabu 1,000 vyenye maudhui ya historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika; pamoja na kuandaa makala maalumu kuhusu mchango wa Tanzania katika Ukombozi wa Bara la Afrika. Nawaomba vijana wa Kitanzania kutembelea vituo vya Programu hii ili kujikumbusha na kujifunza uzalendo mkubwa waliouonesha wazee wetu katika kuipigania Afrika huru.

### 3.2.1.4 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Utamaduni na Sanaa imekuwa muhimu siyo tu katika kukuza na kuendeleza mila, desturi, lugha na sanaa zetu bali pia ni chanzo cha ajira na maendeleo ya uchumi kwa Taifa. Sekta hii imekuwa kimbilio la kundi kubwa la vijana kwa kuwapatia ajira kupitia shughuli za kiutamaduni na sanaa kama vile ususi, ufinyanzi, uchongaji, utengenezaji wa batiki, muziki na filamu. Hata hivyo, ili kuzalisha ajira, sekta hii imekuwa ikisuasua kutokana na kukosekana mitaji na utaalamu.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu huo, leo ninayo furaha kuliambia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imefanikiwa kufanya jambo jingine la kihistoria katika mageuzi ya kiutendaji kwa kuhuisha Mfuko wa

Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa uliokuwa umekwama kufanya kazi tangu mwaka 2013. Mfuko huu sasa utakuwa chachu ya ukuaji wa sekta za Utamaduni na Sanaa kupitia utoaji wa mikopo, ruzuku na kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo waandaaji wa kazi za Utamaduni na Sanaa. Hongera Mheshimiwa Samia Suluhu Hasaan kwa kufanikisha hili.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuanza mchakato wa utoaji mikopo, tayari Serikali imeshatoa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tano (Sh.500,000,000) kwa Mfuko huu kati ya bajeti ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano (Sh.1,500,000,000) ili kutimiza malengo yaliyotajwa hapo juu. Mikopo hiyo itaanza kutolewa kwa wadau wa utamaduni na sanaa mara Sekretarieti itakapokamilisha uundaji wa Kanuni za kutoa mikopo hiyo, ambapo kwa sasa ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Aidha, kutokana na umuhimu wa Mfuko huu, kwa mwaka 2022/23 Serikali imeongeza bajeti hadi Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne (Sh.2,400,000,000) kutoka Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano (Sh.1,500,000,000) kwa mwaka 2021/22. Niwaombe wabia wa maendeleo wengine kuunga mkono juhudi hizi za Mheshimiwa Rais katika kuchangia Mfuko huu.

## 3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

### 3.2.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Sanaa ni eneo jingine muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa).

***66. Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa moja ya majukumu ya sekta hii ni kuwapa vijana fursa za kuonesha vipaji vyao na pia kupata ajira, Wizara katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, imeendelea kuandaa matukio makubwa na ya kimkakati ikiwemo Tamasha kubwa la Kitaifa la Muziki la Serengeti *(Serengeti Music Festival)*. Tamasha hili lilifanyika kwa siku mbili mfululizo Jijini Dodoma tarehe 12 na 13 Machi, 2022 ambapo wasanii mbalimbali zaidi ya 250 walipata fursa ya kushiriki huku wananchi zaidi ya 12,000 wakihudhuria tamasha hili na wengine wakinufaika kiuchumi kupitia malipo ya malazi katika hoteli na nyumba za wageni, chakula, usafiri na huduma nyingine mbalimbali. Aidha, watu wengi zaidi walifuatilia mubashara kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, Tamasha hili ambalo tayari ni maarufu nchini kwa kushirikisha wasanii wengi zaidi litaendelea kufanyika kila mwaka kwa malengo yaliyoainishwa kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais wakati wa Tamasha la "Dream Concert" lililoandaliwa na Msanii Joseph Mbilinyi (Sugu) Dar es Salaam tarehe 31 Mei, 2022.

***67. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) la Zanzibar na Ofisi ya Waziri Mkuu iliratibu ushiriki wa vikundi vya burudani katika Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Ili kuhakikisha ujumbe katika Kaulimbiu ya Maadhimisho unawafikia wananchi wengi zaidi, kwaya 10 zilishindanishwa ambapo Kwaya ya Chuo cha Utumishi wa Umma Magogoni iliibuka kidedea na kutumbuiza

katika sherehe hizo. Aidha, Wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipya na vikundi 8 vya burudani kutoka Bagamoyo, Zanzibar na Dar es Salaam walishiriki. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni Mjumbe wa kudumu katika maadhimisho ya Kitaifa katika Kamati Ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ilifanya kwa ufanisi mkubwa maandalizi na ushiriki wa nchi katika maonesho ya Sanaa na Utamaduni duniani wakati wa maonesho ya *Dubai Expo2020* tarehe 21 hadi 27 Februari, 2022. Katika maonesho hayo, makundi ya kimkakati yaliiwakilisha nchi katika ngoma za asili na za kisasa, muziki wa Singeli, muziki wa Kizazi Kipya na Sanaa za Ufundi. Vilevile, kulikuwa na kikundi cha muziki wa Taarab kutoka Zanzibar. Vikundi vyote vilifanikiwa kuitangaza nchi katika majukwaa mbalimbali wakati wa maonesho hayo ambapo Msanii Mrisho Mpoto kupitia maonesho hayo amepata mwaliko katika maonesho ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika nchini Ufaransa tarehe 1 - 8 Julai, 2022.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuona umuhimu wa yeye binafsi kutumia Sanaa kuitangaza nchi yetu kimataifa, kikundi cha Sanaa kutoka TaSUBa kilipata fursa ya kufanya maonesho nchini Marekani katika Jiji la New York tarehe 18 Aprili, 2022 na Los Angeles tarehe 21 Aprili, 2022 wakati wa uzinduzi wa Filamu maarufu ya Tanzania: *"The Royal Tour*". Kutokana na mvuto mkubwa wa utamaduni na sanaa ya Tanzania kwa jamii ya kimataifa maonesho hayo ni kati ya matukio yaliyofuatiliwa sana na kusambazwa na watu wengi

kupitia mitandao ya kijamii ndani na nje ya Marekani wakati na baada ya uzinduzi wa "*Royal Tour*". Wizara itaendelea kutoa mchango wake wa kuwatafutia wasanii wengi zaidi fursa ya kwenda nje kuitangaza nchi yetu.

**70. *Mheshimiwa Spika***, katika ngazi ya Afrika, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania (KISUVITA) iliratibu kwa mafanikio makubwa mashindano ya urembo, utanashati na mitindo kwa Viziwi tarehe 14 Agosti 2021 Jijini Dar es Salaam ambapo jumla ya warembo, watanashati na wanamitindo 74 kutoka nchi 14 za Afrika walishiriki. Kati ya hao, Watanzania sita (6) wakiongozwa na Mtanzania mrembo kiziwi namba mbili Afrika walifuzu kushiriki mashindano kama hayo ngazi ya Dunia yaliyotarajiwa kufanyika nchini Brazil mwezi Aprili, 2022.

**71. *Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, ninayofuraha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na ufanisi uliooneshwa na Tanzania katika maandalizi ya mashindano hayo ngazi ya Afrika, Bodi ya Wakurugenzi ya mashindano hayo Duniani *(The Executive Board of Directors for Miss and Mr. Deaf Internaltional)* wameiteua rasmi Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano hayo na kukubaliana yafanyike Jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2022. Hii ni heshima nyingine kubwa kwa nchi yetu na katika mashindano hayo yanayotarajiwa kuwa na zaidi ya washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali duniani, tayari maandalizi yameanza na tutayaandaa kwa ubora wa Dunia. Pia Tanzania imevutia Taasisi mbalimbali  Duniani na sasa matukio makubwa yanaendelea kuletwa nchini, ambayo ni pamoja na MTV Africa Music Awards, Mkutano wa

wadau wa mziki Afrika na Mashindano ya AFCON yatakayofanyika mwaka 2027.

### 3.2.2.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Sanaa la Taifa ni pamoja na kukuza na kuendeleza sanaa nchini; kufanya tafiti za fursa za masoko na masuala mbalimbali yanayohusu sanaa; kuandaa Kanuni za kusimamia ubora wa kazi za sanaa, na kuandaa na kuendesha maonesho, mashindano, matamasha na biashara za sanaa.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kipindi kirefu tangu mwaka 2015 cha kutokuwa na Tuzo za Muziki nchini, Wizara kupitia BASATA pamoja na wadau wengine wa sekta ya Sanaa nchini tumezirejesha tuzo hizi. Serikali ya Awamu ya Sita imezisimamia na kuzigharamia tuzo hizi kwa lengo la kuhamasisha, kuchochea ushindani ili kuzalisha kazi bora na kuendeleza ubunifu kwenye tasnia ya Muziki nchini. Tuzo hizi zilizinduliwa tarehe 28 Januari, 2022 na kutolewa rasmi tarehe 02 Aprili, 2022 ambapo zilikuwa na jumla ya vipengele (categories) 19, na kwamba tuzo zilizoshindaniwa zilikuwa (47) na tuzo za heshima zilikuwa (4) na Tuzo Maalumu moja (1) kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais wakati wa Tamasha la "Dream Concert" tarehe 31 Mei, 2022. Tuzo hizi zimeamsha ari na kujituma kwa wasanii.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuonesha jinsi wasanii wetu walivyokuwa na ukame wa kupata Tuzo, na kwamba Serikali yao ilikuwa imefanya jambo jema kuzirejesha, jumla ya kazi za muziki zilizopokelewa

zilikuwa 1,360 kutoka kwa wasanii wapatao 536 waliojisajili na kuwasilisha kazi zao ili kushindania tuzo hizi. Aidha, katika kuhakikisha haki inatendeka mazoezi ya uwasilishaji wa kazi kutoka kwa wasanii pamoja na zoezi la wananchi kupiga kura vilifanyika kupitia mfumo maalumu `wa kielektroni na kusimamiwa na majaji na wakaguzi wabobezi wakiongozwa na mwanamuziki nguli nchini John Kitime. Tuzo hizi zitaendelea kutolewa kila mwaka na Serikali itapanua wigo kwa kuandaa tuzo katika Sanaa nyingine zikiwemo Sanaa za Maonesho na Ufundi. Aidha, Serikali kwa sasa inafanya tathmini na kukusanya maoni kutoka kwa wadau kuhusiana na tuzo hizi ili kuziboresha zaidi katika miaka inayofuata. "Pole pole ndio mwendo".

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** mageuzi mengine muhimu ni katika kuwaondolea adha wadau wa Sanaa kwani kwa mara ya kwanza imeanzishwa mifumo ya kielektroni ya usajili na utoaji wa vibali mtandaoni. Kwa sasa baada ya kero ya muda mrefu ya wasanii kutoka mikoa yote nchini kulazimika kusafiri kwenda ofisi za BASATA Dar es Salaam, kwa mifumo hii, wasanii wanaweza kujisajili mtandaoni na kupata vyeti na vibali vyao ambavyo vinatumika kuwatambulisha katika mamlaka na taasisi mbalimbali ili wapate huduma wanazohitaji. Mfumo huu unaojulikana kwa jina la *Artist Managenment Information System (AMIS)*, vibali vyote hutolewa bila ya wasanii kufika katika ofisi za BASATA na hivyo kuwapunguzia gharama. Mathalani, kutokana na matumizi ya mfumo huu muda wa msanii kupata huduma za usajili na vibali umepungua kutoka siku 3 hadi nusu saa tu. Pia, idadi ya wasanii binafsi wanaojisajili imeongezeka toka wasanii 65 kwa mwezi hadi wasanii 200 kwa mwezi. Mfumo huu unapatikana

kwenye mtandao kwa kiunganishi *(link)* cha https://sanaa.go.tz/login.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza pia limeimarisha utendaji wake kwa kuendeleza na kuimarisha utaratibu wa kukutana na kuwashirikisha wasanii na wadau wa Sanaa katika masuala mbalimbali ikiwemo utatuzi wa changamoto zilizopo. Baraza limefanikiwa kushirikiana na wasanii na wadau wa Sanaa katika zoezi la marekebisho ya Kanuni zake Na. 43 za mwaka 2018 pamoja na maandalizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili katika tasnia ya Muziki nchini. Wasanii na wadau wa sanaa zaidi ya 341 walishirikishwa kutoa maoni yao juu ya marekebisho ya Kanuni za BASATA pamoja na Mwongozo tajwa hapo juu.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Baraza limefanikiwa kuweka utaratibu wa kuwa na Mkutano Mkuu wa Sekta ya Sanaa wa mwaka *(Annual Art Sector Conference)* ambapo wasanii na wadau mbalimbali wa Sekta hii wanashiriki. Lengo la mikutano hii ni kujadili kwa pamoja masuala yanayohusu maendeleo ya Sekta ya Sanaa nchini kati ya Serikali, wasanii na wadau wa sekta hii. Katika mwaka 2021/22 mkutano huu ulifanyika katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa Jijini Dar es Salaam, tarehe 29 Septemba, 2021. Baraza litaendelea kuimarisha utendaji wake ili kuongeza tija na ufanisi katika kutoa huduma kwa wasanii na wadau wa sekta ya Sanaa nchini kwa kuendeleza mageuzi ya kulifanya lihamasishe zaidi maendeleo ya Sanaa kuliko kudhibiti zaidi kama zamani. Pamoja na nia hiyo Wizara kupitia Baraza itaendelea kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wakati wa Tamasha la "Dream Concert" tarehe 31 Mei, 2022 kuwakumbusha wasanii kuzingatia maadili.

## 3.2.2.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ni pamoja na kusimamia na kuratibu kazi za filamu ikiwemo kuhakiki na kuzipanga katika madaraja; kutoa vibali vya usambazaji, maonesho ya filamu, michezo ya kuigiza, kampuni za usambazaji wa filamu, kumbi za maonesho ya filamu, maktaba za picha za filamu, studio za uandaaji wa filamu; pamoja na kujenga uwezo wa wadau wa kazi za filamu.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyokuwa kwa suala la kihistoria la kurejesha Tuzo za Muziki, kwa upande wa filamu, Serikali ya Awamu ya Sita, imefanya mageuzi ya kukumbukwa kwa kuanzisha (haijapata kuwepo) kwa mara ya kwanza Tuzo za Kitaifa za Filamu. Tuzo hizi zilizotolewa Jijini Mbeya mwezi Desemba, 2021, zilishuhudia hamasa kubwa ambapo jumla ya filamu 638 ziliwasilishwa na kupatikana washindi 30 waliopata tuzo na fedha taslimu.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inapoziangalia tuzo hizi inaona maendeleo ya sekta tena ya kasi kwani tuzo hizi zimewajengea ujasiri na uthubutu wadau wa filamu kushiriki katika tuzo mbalimbali duniani na kupata ushindi. Mathalani, filamu ya Obambo na Safari ya Kifo zilizoibuka na ushindi katika tuzo hizi, zilishiriki na kushinda tuzo ya kimataifa nchini Marekani na Nigeria.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu Tanzania imeendelea kuwezesha matamasha mbalimbali yanayoanzishwa na wadau wa filamu ambapo katika kipindi hiki imesaidia kuratibu maandalizi na kufanyika kwa tamasha la tuzo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu (UNI

AWARDS) lililofanyika tarehe 3 Julai, 2021 katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (JINCC) Jijini Dar es Salaam. Kupitia tamasha hilo, tuzo 21 zilitolewa kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika fani mbalimbali ikiwemo za filamu zilizohusisha washiriki 187.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, Bodi ya Filamu inaratibu programu mbalimbali za mafunzo. Moja ya mafunzo yaliyoratibiwa ni mafunzo kwa njia ya Semina, ambapo Bodi kwa kushirikiana na Kamati Maalumu ya Rais, iliratibu mafunzo ambayo ni mafanikio ya awali kabisa ya Filamu ya Royal Tour. Aidha, mafunzo yaliyoratibiwa ni kuwakutanisha wadau wa filamu na Bw. John Feist, mtayarishaji wa Royal Tour, kutoka Hollywood, nchini Marekani, ambaye alitoa semina hiyo tarehe 29 Aprili, 2022 katika ukumbi wa JNICC Jijini Dar es Salaam kwa wadau takribani 300.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** semina hiyo imetoa fursa ya mafunzo mengine kwa wadau wa filamu, ambapo mapendekezo zaidi huko mbele yatahusu namna ya utengenezaji wa mawazo ya kibiashara katika uandaaji wa filamu *(Elevator Pitch)*, matumizi ya teknolojia ya utengenezaji wa filamu yakiwemo matumizi sahihi ya teknolojia ya simu mtelezo *(smart phone film)*, uandishi wa miswada na hadithi za filamu *(Script na Story Writing)* pamoja na kuwaunganisha waandaaji wa filamu kutoka Tanzania na Marekani (Hollywood). Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kushiriki *Royal Tour* kwani nasi katika sekta zetu tumeanza kuona mafanikio hayo.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kwa upande mwingine Wizara kwa maguezi yanayoendelea inazidi kuona umahiri wa wanatasnia ya filamu hapa nchini

ukiongezeka katika uzalishaji wa filamu bora zinazopata nafasi katika majukwaa ya kimataifa. Mathalani, filamu ya Vuta N'kuvute iliyoandaliwa mwaka 2021 na inayotoa uhalisia wa hadithi ya Vuta N'kuvute iliyoko kwenye riwaya ya Adam Shaffi, imepata nafasi ya kuzinduliwa katika Tamasha la *Toronto International Film Festival (TIFF)* nchini Kanada ambalo ni tamasha kubwa katika matamasha 5 makubwa Ulimwenguni, na ilishinda tuzo ya *FESPACO* ambayo inashindanishwa nchini Burkinafaso. Filamu hii imeendelea kuoneshwa kwenye matamasha mengi zaidi ya kimataifa na kuendelea kushinda tuzo kadhaa ulimwenguni. Aidha, filamu ya BINTI ambayo tarehe 7 Januari, 2022 iliingia katika moja ya majukwaa maarufu zaidi ya usambazaji wa filamu ulimwenguni lijulikanalo kama NETFLIX, inakuza ari ya wadau wa filamu kutengeneza filamu zilizo bora na zenye viwango vya Kimataifa, inatangaza utamaduni wa nchi ikiwemo lugha ya Kiswahili, inaongeza kipato cha wadau wa filamu na Serikali, na inafungua fursa ya washiriki wa filamu wa Kitanzania kwa kampuni za nje na kuwapatia ajira zaidi.

**85. *Mheshimiwa Spika,*** jitihada mbalimbali zimefanyika pia katika kutatua changamoto ya masoko na kuongeza fursa za ajira kwenye tasnia ya filamu nchini. Baadhi ya jitihada hizo ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wenye kampuni za utangazaji kama vile DSTV, Azam, Startimes na wengineo kuweka mazingira rafiki kwa wadau kuuza kazi zao. Kampuni hizo zimeendelea kuongeza uwekezaji, kuongeza idadi ya chaneli zinazoonesha filamu za Kitanzania kwa saa 24, siku 7 za wiki pamoja na kuboresha malipo ya filamu zinazonunuliwa kutoka kwa wadau wa filamu nchini.

**86. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea

kuvutia wadau wenye kampuni za usambazaji wa filamu kidijiti kupitia Programu Tumizi kama vile *Starmedia, VidoApp, Airtel, Swahiliflix, Kipaji App, Nilipe App, Mambo TV na Noela TV* inayotoka nchini Uholanzi. Katika hatua nyingine ya kuwaongezea masoko wadau wake, Bodi ya Filamu imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa kushirikiana na wadau kuhamasisha Watanzania kuangalia filamu kwenye kumbi za sinema zinazopatikana kwenye maeneo mbalimbali hapa Tanzania. Mageuzi na hamasa yote hii kwa ujumla, kwa upande wa sanaa ya filamu tu, katika kipindi hiki, tunakadiria kuwa takribani ajira 30,000 zimezalishwa kwenye tasnia ya filamu kupitia filamu 1,713 zilizowasilishwa Bodi ya Filamu kwa ajili ya uhakiki na kupangiwa madaraja.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ilitoa leseni 31 za uendeshaji wa shughuli na biashara za Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini. Leseni hizo zilitolewa ikiwa ni hatua za urasimishaji wa shughuli na biashara ya filamu nchini. Aidha, vitambulisho 125 vilitolewa kwa wadau wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza. Vilevile, kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022 filamu 1,751 zilipokelewa kwa ajili ya uhakiki na kupangiwa madaraja; na filamu zote zilihakikiwa na kupangiwa madaraja sawa na asilimia 194.5 ya lengo la filamu 900 zilizopangwa kuhakikiwa katika kipindi hicho. Kati ya filamu hizo, za ndani zilikuwa 1,713 na za nje ni 38. ***Kiambatisho Na.2***. Pia, katika kipindi hicho miswada na maombi ya vibali vya kutayarisha filamu 150 imechambuliwa ambapo kati yake, maombi 71 yalikuwa ya watayarishaji kutoka nje ya nchi na maombi 79 kutoka ndani ya nchi. Maombi ya utayarishaji wa filamu nchini hushughulikiwa na Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Vibali vya Filamu. Aidha, katika kipindi hiki maombi yote yalipatiwa

vibali. ***Kiambatisho Na.3***.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania imeendelea kulinda haki za wasanii kwa kushughulikia malalamiko ya wadau, kutatua migogoro kati yao na kukabiliana na watu wanaofanya shughuli za filamu bila kufuata Sheria hasa kwa upande wa usambazaji filamu. Wadau wa filamu nchini wameendelea kusaidiwa katika upatikanaji wa haki zao ambapo kupitia Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii inayoratibiwa na Bodi ya Filamu, malalamiko 12 yalipokelewa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko tisa (9) yalisuluhishwa na malalamiko matatu (3) yanaendelea katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na wasambazaji wasiofuata Sheria, Bodi imefanya operesheni 38 katika maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam na Mwanza ambapo hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa wahusika ikiwemo kuwafikisha mahakamani. Juhudi hizi za kulinda haki za wasanii dhidi ya maharamia wa kazi zao zitaendelea. Ni azma ya Serikali kuona sekta hii ndogo ya filamu katika sekta pana ya sanaa inaendelea kuimarika na hatimaye kufikia azma yetu mpya ya kuanzisha kiwanda kikubwa cha filamu yaani "*Swahiliwood.*"

### 3.2.2.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA).

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Taasisi ya COSOTA inayosimamia haki za kiuchumi za wasanii wetu ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, na wachapishaji, hususan kukusanya na

kugawa mirabaha au ujira unaotolewa kulingana na haki zao zilizofafanuliwa katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Aidha, COSOTA ina jukumu la kutunza rejesta za kazi, usanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha haki za wasanii zinapiganiwa, utendaji na usimamizi wa COSOTA uliimarishwa na kuweka rekodi ya ukusanyaji wa mirabaha ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2021 hadi 31 Desemba, 2021 jumla ya Shilingi 312,290,259 zilikusanywa na kugawanywa kwa wasanii wa muziki ambapo jumla ya wanufaika 1,123 wenye kazi 5,924 walipata mirabaha. Gawio hilo lililotangazwa tarehe 28 Januari, 2022 ni kubwa zaidi kuwahi kukusanywa tangu Taasisi hiyo ilipoanza kutoa mirabaha. Hii ni kutokana na agizo la Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuelekeza vyombo vya Habari (Televisheni na Redio) ambao ni wadau wakubwa wanaotumia kazi za muziki kulipia mirabaha. Mgao huo ni ongezeko la asilimia 58 ukilinganisha na gawio lililofanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2019 ambapo lilikuwa la jumla ya Shilingi 183,588,000 tu. Ongezeko hili limetokana na jitihada za Taasisi za kufikia maeneo mbalimbali yanayotakiwa kulipia, na kuongezeka kwa rasilimali fedha za usimamizi wa majukumu ya Taasisi. Kutokana na jitihada hizi, COSOTA katika kipindi hiki imeweza kugawa mirabaha mikubwa zaidi hadi kiasi cha Shilingi Milioni 8.7 kwa wasanii wa kwaya; na Shilingi Milioni 7.6 kwa msanii binafsi. Mgao kama huu utaendelea kutolewa kila baada ya miezi sita huku Serikali ikiendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na ugawaji sambamba na kutatua

changamoto zilizopo.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kusimamia haki za wabunifu, COSOTA imefanya mapitio ya Kanuni za leseni na utangazaji za mwaka 2003 zinazotumika kukusanya mirabaha na kuja na Kanuni mpya za Leseni na Haki ya Kunufaika na Mauzo Endelevu ya Mwaka 2022 zilizoanza kutumika kuanzia tarehe 18 Machi, 2022 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na.137 la mwaka 2022. Kanuni hiyo imeweka viwango rafiki vinavyolipika katika maeneo mbalimbali yanayotumia kazi za muziki na filamu ikiwemo Vyombo vya Usafiri, Redio na Televisheni pamoja na maeneo mengine yanayotumia kazi hizo. Kupitia Kanuni hii, kutakuwa na ongezeko la makusanyo ya mirabaha. Vilevile, itasaidia wasanii wa sanaa za ufundi kunufaika na haki ya mauzo endelevu.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia, imefanya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 Toleo la Mwaka 2002 kwa kuingiza vifungu vya Mkataba wa Marrakesh na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari, 2022. Hii imetoa fursa kwa Watu Wenye Ulemavu wa Macho au uoni hafifu kuchapisha machapisho mbalimbali katika maandishi yanayoshikika pasipo kuomba ridhaa ya mmiliki wa chapisho husika. Vilevile, Serikali kupitia COSOTA, imeanza mchakato wa kupitia Kanuni ya usajili wa wanachama na kazi zao kupitia *Tangazo la Serikali Na.* 18/2006 na tayari rasimu ya Kanuni hiyo imeandaliwa kwa lengo la kuwasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Fauka ya hayo, Taasisi imepitia na kuhuisha Kanuni zake za Utumishi ili kuongeza ufanisi katika Usimamizi wa Rasilimali Watu na kuongeza tija.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** COSOTA kama ilivyokuwa kwa BASATA na Taasisi nyingine, nayo imeboresha mfumo wa kuwahudumia wanachama wake kidigitali ambapo ilikamilisha uboreshaji wa mfumo wa usajili na utoaji wa Leseni kwa Watumiaji wa Kazi za Ubunifu kwa njia ya kielektroniki (AMIS) uliozinduliwa rasmi tarehe 22 Novemba, 2021. Mfumo huu unawezesha kutambua wabunifu na kazi zao lakini pia kutambua watumiaji wa kazi za sanaa bila ya wao kutembelea ofisi za COSOTA zilizopo Dar es Salaam au Dodoma. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 COSOTA imesajili jumla ya Wabunifu 444 na kazi zao 3,021.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kutoa elimu ya masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa Wabunifu ili kuelewa wajibu na haki zao, COSOTA imetoa elimu kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari ambapo zaidi ya vipindi 55 vimefanyika kupitia Redio na Televisheni. Aidha, kwa upande wa mitandao ya kijamii, zaidi ya taarifa 95 ziliwekwa kwenye mitandao ya *Instagram, Twitter, Facebook* na *Youtube*. Pia, Taasisi imetoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wadau kupitia Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF), Shirikisho la Muziki Tanzania, Shirikisho la Sanaa za Maonesho, Shirikisho la Sanaa za Ufundi, Watayarishaji wa Muziki, Chama cha *Tanzania Producers and Composers Association* (TPCA), Wasanii wa Muziki wa Injili kupitia Shirika la *Tanzania Music Foundation* (TAMUFO), Waandishi wa Vitabu, Wasanii wa Muziki wa Dansi, Wamiliki wa Vyombo vya Habari, Wahariri kwa kushirikiana na Kampuni ya Multichoice Tanzania na Mafunzo kwa Mahakimu kwa kushirikiana na Chuo cha Mahakama Lushoto na Mahakama ya Tanzania na Kampuni ya Azam Media.

**96. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kufahamu kwamba Sheria ya Hakimiliki ina mipaka na kazi za wasanii wetu zinatumika sehemu mbalimbali duniani COSOTA imeingia makubaliano na Taasisi mbalimbali duniani zinazofanya kazi kama za COSOTA. Makubaliano hayo yanawezesha usimamizi wa haki za wasanii wetu katika nchi hizo ambapo inawezesha pia wao kunufaika na mirabaha inayokusanywa na taasisi hizo. Taasisi ambazo tayari tuna makubaliano ni pamoja na CAPASSO *(Composers Authors and Publishers Association of South Africa)* ya Afrika Kusini ambayo husimamia matumizi ya kazi za wasanii kwenye mitandao ya kijamii. Aidha, kutokana na makubaliano haya mwezi Aprili, 2022 wataalamu kutoka nchini Afrika Kusini walikuja nchini kutoa elimu kwa wataalam wa COSOTA kuhusu matumizi ya mfumo wa *CAPASSO-Portal* unaowezesha wasanii wetu kujisajili pamoja na kazi zao ili wanufaike na mirabaha wanayoikusanya.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** pia, COSOTA ina makubaliano na mashirikisho mengine ya kimataifa kama vile The International Federation of Reproduction Rights Organizations, GHAMRO - Ghana, SAMPRO – Afrika Kusini, RSAU - Rwanda, COSOZA - Zanzibar, NASCAM - Namibia, COSOMA - Malawi, UPRS - Uganda, ZAMCOPS - Zambia, IPRS - India, TEOSTO - Finland, SPA - Ureno, MASA - Mauritania na AGADU - Uruguay. Halikadhalika, majadiliano yanaendelea ili kushirikiana na vyama na mashirikisho mengine. Ushirikiano huu ni mkakati mwingine muhimu wa kuhakikisha COSOTA inatoka kuwa na uwezo wa ndani tu wa kukusanya haki za wasanii hadi kujijengea wigo wa kufuatilia na kukusanya haki za wasanii wetu popote kazi zao zinakotumika nje ya nchi.

Huu ndio mwelekeo tunaokwenda kuuimarisha katika mwaka ujao wa fedha, sanaa ni ajira, sanaa ni biashara na hakika sanaa ni uchumi.

### 3.2.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatuwezi kuendeleza sanaa bila kuwekeza katika utaalamu na utafiti; TaSUBa ni Taasisi inayotoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya Sanaa na Utamaduni nchini. Mwaka 2012 TaSUBa iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa hivyo ni kituo chenye hadhi ya kimataifa.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu huo, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa chuo imeweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha na kuongeza udahili ambapo mwaka 2021/22 TaSUBa ilipanga kudahili wanafunzi 600 katika programu za Astashahada na Stashahada ambapo hadi mwezi Aprili, 2022 ilidahili jumla ya wanachuo 695 na walioendelea na masomo ni wanachuo 533 ukilinganisha na usajili wa Mwaka 2020/21 ambapo wanafunzi 300 pekee walisajiliwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 78. Sambamba na hilo, TaSUBa inafanya juhudi za ufundishaji wa kozi fupi ili kuwafikia vijana wengi zaidi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 TaSUBa iliendesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 275.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kupanua wigo wa mafunzo na kuongeza nafasi zaidi kwa vijana wa Kitanzania kujiunga na sekta ya ubunifu, Taasisi

imejipanga kuongeza mitaala mipya zaidi ya iliyopo sasa. Hatua hii itasaidia kutoa wigo mpana kwa wanafunzi kuwa na uchaguzi wa masomo. Mitaala mipya ni pamoja na Uongozi wa Sanaa na Masoko; Urithi wa Utamaduni na Utalii; na Muziki. Katika kutekeleza hilo, Taasisi inafanyia kazi marekebisho yaliyoagizwa na NACTE ili kukidhi vigezo vya kupatiwa ithibati.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendesha Tamasha la 40 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililofanyika tarehe 28-30 Oktoba, 2021 na kuhudhuriwa na watazamaji wapatao 75,000 kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tamasha hilo pia lilirushwa mubashara kupitia televisioni mbalimbali ndani na nje ya nchi. Jumla ya vikundi 79 vilishiriki kufanya maonesho ya sanaa za jukwaani ambapo vikundi 75 vilitoka nchini (Tanzania Bara na Zanzibar) na vikundi vinne (4) vilitoka nje ya Tanzania; Mayotte na India. Wakati wa maonesho hayo, Sanaa mbalimbali zilioneshwa zikiwemo ngoma, muziki, maigizo, sarakasi, vichekesho na mazingaombwe. Aidha, Vyombo vya Habari 25 vikiwemo redio, runinga, magazeti na blogu vilishiriki kutangaza shughuli mbalimbali za Tamasha. Matarajio ni kuongeza ushiriki wa vikundi kutoka nje katika tamasha lijalo.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni kuendeleza na kupima uwezo wa Taasisi kwa kuwatofautisha na vijana wengine wenye vipaji bila elimu, wanachuo wa Taasisi hii wamekuwa wakishiriki mashindano mbalimbali ya Sanaa ya Kitaifa ya kuibua vipaji mbalimbali kwa kufanya vizuri. Mashindano haya yanasadia kuhamasisha vijana katika kufanya kazi zao kwa weledi, bidii na maarifa na kutambua umuhimu wa elimu. Vijana kutoka TaSUBa wameendelea kufanya vizuri katika mashindano

mbalimbali kama inavyobainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Mashindano Yaliyoshirikisha Wanafunzi wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo Katika Mwaka 2021/22 na Hatua Waliyofikia**

| Na | Aina ya Shindano | Mwaka | Kundi (Category) | Hatua Waliyofikia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UN-Awards | 2021 | Kuimba | Nusu Fainali |
| 2 | UN-Talents | 2021 | Kuimba | Fainali |
| 3 | Taifa Cup | 2021 | Mziki wa Bongo Flava (Kuimba) | Nafasi ya Kwanza |
| 4 | UN-Talents | 2022 | Kuimba | Nafasi ya Kwanza |

***Chanzo:*** *Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, 2022*

### 3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO
### 3.2.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo ni mhimili mwingine muhimu wa ajira na siha za watu wetu hapa nchini na inahusisha Idara ya Maendeleo ya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka huu, kazi kubwa ya kupigiwa mfano iliyoanza kufanyika ni kuanza kushughulikia tatizo sugu la miundombinu ya michezo ambayo kwa muda mrefu imekuwa na changamoto au kuanzisha mipya inayoendana na matakwa ya sasa. Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuja na mtazamo mpya katika eneo hili na imetekeleza miradi kadhaa ya

kihistoria kama ifuatavyo:

**Mosi,** uamuzi wa kimkakati wa kujenga viwanja changamani vya michezo na sanaa *(Sports and Arts Arena)* katika mikoa ya Dodoma na Dar es salaam, umefikia hatua muhimu ambapo usanifu wa michoro (*Architectural Design)* umekamilika na sasa Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi lakini pia inazungumza na wadau wa sekta binafsi ili kutekeleza kwa pamoja ambapo sasa Tanzania inakwenda kuwa na Arena ya kwanza nchini zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua wastani wa watu 16,000 kwa wakati mmoja kila moja. ***Kiambatisho Na.4A*** *muonekano wa uwanja wa Sports and Arts Arena;*

**Pili,** Tumeanza hatua za ujenzi wa Viwanja vya mazoezi na mapumziko *(Recreational and Leisure Centres)* vitatu katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Geita ambapo hatua zote za usanifu zimekamilika na sasa ujenzi utaanza mara moja na tayari Wizara imeshapokea Shilingi Bilioni Tatu (Sh.3,000,000,000) kuanza ujenzi huo. ***Kiambatisho Na.4B*** *muonekano wa maeneo ya kupumzikia wananchi;*

**Tatu,** Ujenzi wa Kiwanja kikubwa cha michezo Jijini Dodoma nao umeendelea katika hatua za kutafuta mkandarasi baada ya upembuzi na hatua zote za maandalizi kukamilika. ***Kiambatisho Na.4C*** *muonekano wa uwanja wa mpira wa miguu utakaojengwa Dodoma;*

**Nne**, Mkakati mwingine ni ujenzi wa Kituo cha Umahiri katika michezo *(Center of Excellence)* katika Chuo cha maendeleo ya Michezo Malya na hosteli mpya ya wanafunzi ambapo kwa upande wa Kituo cha Umahiri,

hatua zote za usanifu zimekamilika huku ujenzi wa hosteli ukifikia asilimia 40. Vituo hivi vitakigeuza kilichokuwa chuo cha kawaida cha michezo Malya sasa kuwa na taswira mpya na kuwa Kituo cha Kimataifa kitakacholea watoto wenye vipaji kutoka mitaani huku kikiendelea kutoa mafunzo kwa vijana waliotoka mashuleni. Mwelekeo huu utasaidia kuzalisha wasomi wa michezo lakini pia na wanamichezo mbalimbali waliopikwa wakiwa wadogo.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine katika miundombinu ni pamoja na Serikali kutoa fedha za ukarabati na hatimaye kuurejesha uwanja wa michezo wa ndani wa Taifa uliokuwa umesitishwa kutumika kutokana na uchakavu na hii ilihusisha pia kuweka vifaa vya kisasa vya mazoezi (gym) kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es salaam. Mafanikio ya kuurejesha tu uwanja wa ndani wa michezo tayari yameamsha ari ya michezo ya ndani na pia nchi imekuwa mwenyeji wa mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo ya mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa kikapu na mashindano ya ngumi yaliyomalizika hivi karibuni na kuhusisha nchi zaidi ya tano za Afrika.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua hizi muhimu, lakini ni ukweli ulio wazi kuwa kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 na mantiki tu, suala la miundombinu haliwezi kubaki kwa Serikali peke yake bali linahusu wadau mbalimbali wa michezo kuwekeza katika maeneo mengine. Hapa niwapongeze wadau wote waliofanya jambo moja au jingine katika kuwekeza katika miundombinu ya kisasa na wanaoendelea kufanya hivyo. Mathalani, nakipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) na wadau wake kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na

ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM Taifa aliyoyatoa Jijini Mwanza mwaka jana, Chama hicho kimeendelea na mkakati wa kuboresha viwanja vyake hasa vya soka vinavyotumika kwenye ligi mbalimbali nchini na sasa vimeanza kuwa na sura mpya.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** siwezi pia kuishiwa wingi wa shukrani kwa baadhi ya Halmashauri kama Geita, Ruangwa; na majiji kama Arusha na Mwanza, Manispaa za Temeke na Kinondoni kwa viongozi wao kuona umuhimu wa michezo na kutumia fedha zao wenyewe kufanya ukarabati wa viwanja vyao au kuanza miradi ya ujenzi mpya wa viwanja huku wataalamu wa Wizara wakisaidia kutoa ushauri wa kiufundi. Hapa pia tutambue uwekezaji muhimu wa Jiji la Dodoma katika eneo la Chinangali lenye viwanja vingi vya michezo ikiwemo mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa mikono na michezo mingine. Nitumie fursa hii kuwaomba Wakurugenzi wengine nchini kufuata nyayo hizi kwani Sera ya Michezo inatupa hamasa hizo.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mashirikisho mbalimbali ya michezo nchini nayo yamewekeza katika ujenzi na ukarabati wa miradi ikiwemo Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa msaada wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) wanaojenga vituo viwili vya michezo katika miji ya Dar es salaam na Tanga ambavyo viko katika hatua za mwisho za ujenzi. Hatua hii itasaidia kuboresha timu zetu kwa kuwa na vituo maalumu vya kukuzia michezo, kambi maalum na zenye utulivu za timu za Taifa kama ilivyo kwa nchi nyingine zilizoendelea katika sekta ya michezo ili nasi tuendelee kushiriki kisayansi zaidi katika mashindano yenye ushindani.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuanza kuendeleza vipaji vya michezo katika hatua ya awali kwa kufuata misingi ya kisayansi ya uendelezaji na uibuaji wa vipaji, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tumekamilisha utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa hatua ya kwanza ya kuteua jumla ya shule 56 kuwa shule maalumu za Michezo nchini ikiwa ni shule mbili (2) za Sekondari kila Mkoa isipokuwa mikoa minne ya Iringa, Ruvuma, Morogoro na Mwanza ambayo itakuwa na shule tatu (3) ili kuwapokea watoto wenye mahitaji maalumu. Shule hizi zitakuwa kwenye uangalizi na mkakati kabambe ambapo zitakarabatiwa miundombinu yake na kupangiwa walimu na vifaa vya kufundishia. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga Shilingi Bilioni Mbili kuanza kazi hii.

***Kiambatisho Na.5*****:** *Shule 56 zilizoteuliwa kuwa shule maalumu za michezo nchini kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo uwepo wa viwanja kwa sasa, miundombinu mingine na jiografia***.**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mkakati huu utakaohitaji takribani Shilingi Bilioni 19 za kuanzia, tayari Wizara yangu kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI tumeanza ukarabati wa Shule za Tabora Wavulana na Wasichana mkoani Tabora zitakazotumika wakati wa mashindano ya Shule za Sekondari (UMISSETA) na Shule za Msingi (UMITASHUMTA) kitaifa mwezi Agosti, 2022.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** hapa pia nieleze kuwa tumeendelea kuboresha michezo ya UMISSETA na

UMITASHUMTA ambayo huko nyuma ilififia. Zoezi la uratibu mpya na wa pamoja chini ya Wizara tatu (3) za Utamaduni, Sanaa na Michezo; Elimu, Sayansi na Teknolojia; na OR-TAMISEMI lilifanyika vizuri katika michezo ya mwaka 2021 iliyofanyika mkoani Mtwara. Maandalizi ya vikao na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika shule hizo unaendelea vizuri. Michezo hii ni muhimu na imekuwa chachu kubwa ya kuibuwa wachezaji mbalimbali wanaocheza katika timu zetu za Taifa za vijana zinazofanya vizuri katika ukanda wetu wa Afrika. Wizara itaendelea kuisimamia michezo hii ili izidi kuwa chemchem ya kuzalisha vipaji.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufanikisha michezo hakuwezi kwenda bila kuwa na mikakati Madhubuti, katika kipindi hiki, Serikali imekamilisha Mkakati wa Maendeleo ya Michezo nchini wa mwaka 2022-2032. Mkakati huu umeandaliwa ili kuhakikisha Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 inatekelezwa kwa ufanisi ukilenga kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha miaka 27 ya utekelezaji wake. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Mkakati huo ni pamoja na kuongeza ushiriki wa wananchi katika michezo na mazoezi ya viungo; kuwa na miundombinu na vifaa vya michezo vinavyoendana na mahitaji; kuimarisha uteuzi na malezi ya timu za Taifa na kuwa na michezo ya kipaumbele Kitaifa.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** masuala mengine ni kuimarisha upatikanaji wa wataalamu wa michezo; ugharimiaji wa shughuli za michezo pamoja na kuimarisha utalii wa michezo. Aidha, Mkakati unabainisha mgawanyo wa majukumu kwa wadau mbalimbali ili kuwezesha malengo kufikiwa na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Mkakati

ulizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo kilichofanyika Jijini Dodoma tarehe 4 hadi 6 Aprili, 2022.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kulinda wanamichezo wetu na kutoruhusu matumizi ya dawa haramu michezoni, Serikali imeendelea na zoezi la kuandaa Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni inayolenga kuanzisha chombo cha kitaifa cha kuratibu na kusimamia masuala ya Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni *(National Anti-Doping Organization-NADO)*. Sheria hiyo inahitajika kwa ajili ya kudhibiti uzalishaji, usafirishaji, uagizaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa na mbinu haramu michezoni; kuweka utaratibu utakaowataka wazalishaji na wasambazaji wa virutubisho (*nutritional supplements)* kuwa na mfumo bora wa uuzaji na usambazaji wa bidhaa hizo; na kuhakikisha watendaji ikiwemo mameneja, madaktari, makocha, waamuzi na wachezaji hawajihusishi na vitendo vya matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa malezi ya timu zetu za Taifa ili kuziwezesha kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa, Serikali ilifanya uamuzi mwingine mgumu na muhimu katika miaka ya karibuni wa nayo kutobaki mtazamaji bali kurejea kutenga fedha kwa ajili ya walau, kwa kuanzia kusaidia timu za Taifa. Mathalani, kuanzia mwaka 2019/20 Serikali ilitenga jumla ya Shilingi 270,000,000; mwaka 2020/21 Shilingi 431,000,000 lakini ikaongeza kiasi hicho hadi Shilingi 1,320,000,000 mwaka 2021/22. Usaidizi wa Timu za Taifa kutoka Serikalini na wadau mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitatu

mfululizo umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa ambapo mwaka 2022/23 Serikali imeongeza bajeti kutoka Sh.1,320,000,000 za mwaka 2021/22 hadi Sh.1,446,900,000 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 9.6.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni juhudi za kuimarisha ushirikiano na wadau, Serikali kupitia Wizara ninayoisimamia, iliratibu Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo nchini kilichofanyika katika ukumbi wa Mtakatifu Gasper Jijini Dodoma tarehe 04 - 06 Aprili, 2022. Katika kikao hicho mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na Programu maalumu ya michezo Mtaa kwa Mtaa ambayo itazinduliwa hivi karibuni ikiwa ni mashindano yanayolenga kuhamasisha umma kushiriki katika michezo tangu ngazi za awali; kuibua vipaji vya michezo katika ngazi ya mitaa, vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na mikoa na hatimaye Taifa (Taifa Cup). Pia, Mashindano haya yanalenga kuunganisha na kujenga mshikamano katika jamii kwa kupitia michezo na kuifanya jamii kuelewa umuhimu wa Michezo katika ujenzi wa uchumi binafsi na nchi kwa ujumla.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na programu ya michezo ya mtaa kwa mtaa inatarajiwa vijana kati ya 50-100 kutoka mikoani watapata nafasi ya kushiriki michezo ya kitaifa. Halikadhalika, inatarajiwa jumla ya washiriki 724,370 watashiriki/watapata ajira katika michezo kwa mchanganuo ufuatao: mpira wa miguu (255,780); netibali (42,630); riadha (127,810); mpira wa wavu (127,810); mpira wa kikapu (127,710); na ngumi (42,630).

**118.** ***Mheshimiwa Spika;*** uwekezaji wa serikali na wadau wengine katika michezo, ikiwemo Serikali kuendelea kuimarisha bajeti za michezo, vimeleta mwanga mpya

wa matumaini, huku pia siri nyingine kubwa ikiwa ni umoja na ushirikiano kati ya wadau na Serikali na vyombo vyake kama BMT. Tumeona na sasa tumejifunza, pale ambapo kuna ushirikiano wa dhati na mikakati ya pamoja timu zetu zinapata morali na zinafanya vyema. Hapa naomba kulishirikisha Bunge lako tukufu katika baadhi ya mafanikio kwa baadhi ya michezo katika kipindi hiki kama ifuatavyo:

Kwa upande wa mchezo wa ngumi; Tanzania imeendelea kufanya vizuri kimataifa, mabondia mbalimbali wamefanikiwa kushinda mataji kadhaa ya kimataifa ikiwemo:

a) Bondia Twaha Kiduku alimchapa Alex Kabangu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika pambano lililofanyika tarehe 26 Machi, 2022, Tanzanite Hall, Morogoro na kutwaa ubingwa wa UBO Africa katika uzito wa kilogramu. 76;

b) Bondia Tony Rashid alimtwanga Bongani Mahlangu kutoka nchini Afrika ya Kusini katika pambano lililofanyika tarehe 25 Februari, 2022, Kilimanjaro Hall, Ubungo Plaza na kutwaa ubingwa wa ABU uzito wa kilogramu 55; na

c) Bondia Hassan Mwakinyo alimtandika Julius Indongo kutoka Namibia kwa Kock Out (KO), katika pambano lililofanyika tarehe 3 Septemba, 2021, Kilimanjaro Hall, Ubungo Plaza na kutwaa ubingwa wa ABU Superwelter uzito wa kilogramu 69; Aidha, Bondia Hassan Mwakinyo anashikilia nafasi ya 8/2144 kwa mabondia wa Afrika kwa uzito tofauti tofauti. Aidha, anashikilia nafasi ya 1/172 kwa mabondia wa Afrika kwa uzito wake; na anashikilia nafasi ya 15/1898 kwa mabondia wa duniani wa uzito wake.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Timu yetu ya Taifa ya Soka la Walemavu *(Tembo Warriors)*, ilitutoa kimasomaso baada ya mwezi Novemba, 2021 kufuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia nchini Uturuki Oktoba, 2022 kufuatia Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano yaliyoshirikisha zaidi ya nchi 13 za Afrika na kufanyika Dar es Salaam, Tanzania. Itakumbukwa ili kuchagiza ushindi huo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimtuma Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda kambini na kutoa kiasi cha Shilingi milioni 150 zilizosaidia kuitunza timu yetu ya Taifa na maandalizi mengine. Haikuwa kazi rahisi kwa Tembo Warriors kwani ili kupata nafasi hiyo walifanya yafuatayo:

a) Waliichabanga timu ya Morocco mabao 2-1;

b) Waliicharaza timu Sierra Leone mabao 1-0; pia,

c) Waliibugiza timu ya Cameroon kwa mabao 5-0.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** timu hiyo kwa sasa ipo kambini tangu mwezi Februari, 2022 kwa maandalizi ya mashindano ya Kombe la Dunia ambapo Serikali ndio inagharimia kambi hiyo kwa matumizi yote ikiwemo malazi, chakula, ufundi, usafiri wa ndani na nje pamoja na posho za wachezaji na benchi lao la ufundi.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine makubwa ni kwa Timu zetu za Taifa za wanawake ambazo nazo zimeendelea kufanya vyema kimataifa ikiwemo Twiga Stars iliyotwaa Kombe la COSAFA mara tatu mfululizo na Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake ya U17 ya Serengeti Girls ambayo inafanya vizuri katika mashindano ya kufuzu

kushiriki Kombe la Dunia kwa Wanawake. Hadi kufikia tarehe 03 Juni, 2022, Serengeti Girls ilifanikiwa kuzifunga timu zifuatazo:

a) Iliibugiza Timu ya Taifa ya Botswana kwa jumla ya magoli 11-0;

b) Ikaibamiza timu ya Burundi kwa jumla ya magoli 5-2 na

c) Iliichabanga timu ya Cameroon kwa magoli 4-1 ugenini kabla ya kurudiana hapa nyumbani.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) itahakikisha kuwa timu hiyo inapatiwa malezi na mafunzo yanayostahili ili iweze kuendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali Duniani. Aidha, nazipongeza sana timu zetu zote kwa hatua kubwa zilizofikia.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania pia katika kipindi hiki imefanya vyema katika mchezo wa Kabaddi Afrika mashindano yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam, ambapo nchi za Misri, Cameroon, Kenya na Tanzania zilishiriki, katika mashindano hayo Tanzania ilishika nafasi ya pili kwa timu ya wanawake na wanaume na wachezaji wawili (2) walipata ajira ya kucheza mchezo wa kulipwa nchini India. Kwa upande wa mchezo wa Karate timu ya Taifa ya mchezo wa Shotokhan karate ilitwaa medali 27 (7 za dhahabu, 8 za fedha na 12 za shaba) katika mshindano yaliyofanyika nchini Congo (Congo DRC). Kati ya medali hizo 27, medali 13 zilitwaliwa na wachezaji wanawake na zilizobaki 14 zilitwaliwa na wanaume.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** jambo jingine la kihistoria katika mageuzi kwenye michezo ni maandalizi ya kimkakati ya Timu za Taifa ambapo kwa mara ya kwanza Serikali imeweza kugharimia maandalizi ya timu za Taifa zinazojiandaa na mashindano ya Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika nchini Uingereza katika jiji la Birmigham na maandalizi ya Tembo Warriors kwenda Kombe la Dunia Uturuki Oktoba mwaka huu. Timu hizo za michezo ya Ridhaa, Ngumi, Judo, Mchezo wa kuogelea pamoja na kunyanyua vitu vizito *(Powerlifting*) kwa watu wenye ulemavu ambapo timu zote kama ilivyoelezwa hapo awali zipo kambini tangu mwezi Februari, 2022 na zinaendelea na mechi au mapambano ya kirafiki.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imegharimia kambi hizo kwa kulipa malazi, chakula, mavazi, huduma za afya na wachezaji wamelipiwa bima za afya, posho za kujikimu na kulipa benchi la ufundi kwa kambi zote. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa timu zetu zinapata malezi bora ili wachezaji watimize majukumu yao kimichezo na kuliletea ushindi Taifa letu kimataifa. Huu ndio utakuwa mwelekeo wetu mpya kama Serikali kuhakikisha Timu za Taifa hazibaki tu mikononi mwa vyama na mashirikisho, Serikali nayo inashiriki kuweka mchango wake na kwa pamoja si tu, tutashinda, bali uzoefu wa miaka miwili hii unaonesha kabisa umoja huu ni ushindi.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 si kambi ya Jumuiya ya Madola tu na ushiriki wa Tembo Warriors Uturuki, bali pia, Timu mbalimbali za Taifa zilizofuzu kuiwakilisha Tanzania katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa zilipatiwa usaidizi. Miongoni mwa timu hizo ni pamoja na timu ya wachezaji watatu (3) wa riadha walioshiriki michezo ya Tokyo-Japan

mwaka 2021 iliyofanyika mwezi Julai – Agosti, 2021 ambapo Mtanzania Alphonce Felix Simbu alishika Nafasi ya saba (7), Failuna Abdi Matanga Nafasi ya 22 na Gabriel Gerald Geay alishindwa kumaliza baada ya kupata ajali akiwa katika mashindano hayo. Aidha, mwezi Mei, 2022 mwanariadha Emanuel Giniki Gisamoda alishika nafasi ya kwanza katika mashindano ya Generali Geneve Marathon yaliyofanyika nchini Uswisi na katika mashindano ya Generali Milan Marathon yaliyofanyika mwezi Machi, 2022 katika Jiji la Milan Italia, mwanariadha Alphonce Felix Simbu alishika nafasi ya tatu (3). Pamoja na wanariadha hao, Timu 12 za Taifa ziliwezeshwa kushiriki mashindano ya Kimataifa. Mafanikio mengine nitayaeleza kwa kina katika eneo la Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

**127.** ***Mheshimiwa Spika*** katika kuhakikisha kuwa sekta ya michezo kwa kutumia Utalii wa michezo inalitangaza Taifa letu, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya Coca-Cola walishirikiana kuleta Kombe la Dunia litakaloshindaniwa Nchini Qatar mwezi Novemba, 2022 katika mashindano ya Kombe la Dunia kwa mchezo wa mpira wa miguu. Kombe hili liliwasili nchini tarehe 31 Mei, 2022 na kupokelewa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ikulu ya Dar es Salaam na baadae wananchi kupata fursa ya kuliona kombe hilo tarehe 01 Juni, 2022 katika uwanja wa Benjamin Mkapa.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ipo kwenye maandalizi ya kuwa wenyeji wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) utakaofanyika katika Jiji la Arusha mwezi Agosti, 2022. Kikao hicho

kitahudhuriwa na wawakilishi kutoka katika nchi 54 za Bara la Afrika pamoja na viongozi wa juu wa Shirikisho la Mpira Duniani (FIFA) wakiongozwa na Rais wa Shirikisho hilo Gianni Infantino. Inakadiriwa kuwa zaidi ya washiriki 300 watahudhuria. Hii itakuwa ni fursa muhimu kwa nchi yetu kuendelea kujitangaza duniani kiutalii, kiuchumi na kiutamaduni.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na jitihada hizo, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya vivutio mbalimbali vilivyopo nchini kwa kutumia michezo, sanaa na utamaduni ili kuvutia uwekezaji zaidi nchini pamoja na kuitangaza Tanzania kimataifa. Katika kufanikisha hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa maonesho ya mechi ya fainali ya Kombe la UEFA kati ya Timu ya Real Madrid na Liverpool iliyofanyika tarehe 28 Mei, 2022 juu ya Daraja la Tanzanite Jijini Dar es Salaam.

### 3.2.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kusimamia aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo; kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Michezo; kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho au Vyama vya Michezo na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha shughuli za michezo zinafanyika kwa ufanisi mkubwa Serikali katika kipindi hiki kwa mara ya kwanza imeridhia kutoa asilimia tano (5) ya kodi ya michezo ya kubashiri matokeo kupitia

BMT kama chanzo cha mapato katika Mfuko wa Maendeleo ya Michezo nchini ikiwa ni juhudi za kimkakati za kusaidia maendeleo ya michezo nchini. Serikali imetekeleza hilo na hadi sasa tayari kiasi cha Sh. 2,049,614,866.20 zimepokelewa.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika kutokana na fedha hizo ni pamoja na kuandaa mashindano ya Taifa Cup Desemba, 2021, kwa lengo la kuinua vipaji vya vijana wa kitanzania ambapo mashindano haya yalihusisha mikoa 30 ya Tanzania Bara na Zanzibar na yalirejea baada ya miaka mingi ya kutofanyika; kuratibu mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu Barani Afrika (CANAF) ambapo nchi 13 zilishiriki ikiwemo mwenyeji Tanzania, Uganda, Kenya, Angola, Nigeria, Cameroon, Misri, Morocco, Liberia, Sierra-Leone, Zanzibar, Ghana na Gambia. Aidha, mashindano hayo kama nilivyoeleza awali Tanzania sasa itashiriki Kombe la Dunia nchini Uturuki mwezi Septemba - Oktoba, 2022.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizo pia zimetumika kugharamia timu mbalimbali za taifa ambazo zimeshiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa kama ifuatavyo:

a) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanaume (Taifa Stars);

b) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake (Twiga Stars);

c) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake chini ya Umri wa miaka 20 (Tanzanite);

d) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wasichana chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Girls);

e) Timu za Taifa ya Mchezo wa Netiboli;

f) Timu ya Taifa ya Riadha;

g) Timu ya Taifa ya Judo;

h) Timu ya Taifa ya Shotokan Karate;

i) Timu ya Taifa ya Baseball;

j) Timu ya Taifa ya mchezo wa Ngumi;

k) Timu ya Taifa ya Riadha kwa watu wenye Ulemavu;

l) Timu ya Taifa ya mchezo wa Kuogelea; na

m) Timu ya Taifa mpira wa miguu kwa Watu wenye ulemavu *(Tembo Warriors*).

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika fedha hizi zinatumika kusaidia uwezo wa Taasisi ya BMT kuvihudumia vyama vyote vya michezo nchini ikiwemo kununua vitendea kazi ikiwemo gari maalumu aina ya "*Coaster*" ambalo litatumiwa na Timu za Taifa zinapokuwa katika mashindano mbalimbali ikiwa ni pamoja na safari za kimichezo ndani ya nchi na nchi za jirani. Katika mwaka ujao wa fedha, mapato haya yataendelea kusaidia maeneo ya kimkakati zaidi ikiwemo miundombinu ya michezo na mafunzo kwa wataalamu wetu.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, uwezeshaji huo na

namna ulivyosaidia timu zetu za taifa kushiriki mashindano mengi, umesaidia vijana wa Kitanzania kupata fursa za ajira nje ya nchi katika michezo ya kulipwa ikiwemo wachezaji wanne (4) wa timu ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu Frank Ngairro, Ramadhan Chomelo, Alfan Kiyanga na Shadrack Hebron waliopata nafasi katika timu mbalimbali nchini Uturuki. Kwa upande wa Mpira wa Miguu kwa Wanawake wachezaji waliopata fursa za ajira nje ya nchi ni Aisha Masaka - Sweden, Mwanahamisi Omari – Morocco, Enekia Kasongo - Morocco, Opa Clement – Uturuki na Diana Lucas – Morocco.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali, Sekta ya michezo imeendelea kukua katika eneo la michezo ya kulipwa ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/22 idadi ya wachezaji wa kulipwa imeongezeka kwa wachezaji wa Tanzania kupata nafasi ya kucheza katika Ligi za nchi mbalimbali. Jumla ya wachezaji 11 wa kiume wa mpira wa miguu walijiunga na vilabu mbalimbali wakiwemo David Uromi (Al Hilal - Sudan), Kelvin Pius John (KRC Genk- Belgium), Mourice Abraham (FK Spartak- Serbia), Abdul Yusuph Haule (FK Atmosfer-Lithunia), Alphonce Mabula (FK Spartak- Serbia), Omary Marungu (Hapoel Kfar- Israel), Shabani Mrope (Hahaya Fc- Comoros), Adam Salamba (JS Soura-Algeria), Shabani Ningazi (MFK-Czech), Dulla Hilka (Port Darwin- Australia), na Julius Hamis (Hahaya Fc- Comoros).

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika Michezo na kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa katika Bunge hili wakati wa hotuba yake ya kwanza, Wizara iliandaa Tamasha la

michezo kwa wanawake (Tanzanite) ambapo jumla ya wanamichezo 350 walishiriki katika tamasha hilo lililohusisha shughuli mbalimbali ikiwemo mashindano ya michezo ya Netiboli, Mpira wa Miguu, Riadha, Ngumi, Karate na Michezo ya jadi. Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na Kongamano la Elimu kuhusu fursa za Michezo kwa wanawake na maonesho ya shughuli za ujasiriamali zinazofanywa na wanawake. Lengo la Tamasha hilo lilikuwa kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo na kuonesha vipaji vya Michezo kwa wanawake na kuwaelimisha wanawake kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo katika michezo, hasa ikizingatiwa kuwa Timu za Wanawake ndiyo zinazofanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa. Kama alivyoelekeza Mhe. Rais, Tamasha hili litaendelea kila mwaka.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha dhana ya utawala bora inasimamiwa, BMT kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo kwa mujibu wa Katiba zao limehakikisha uratibu wa uchaguzi wa viongozi wa Vyama na Mashirikisho kumi (10) unafanyika ikiwemo Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma Tanzania (SHIMMUTA), Chama cha Mchezo wa Judo Tanzania (JATA), Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania (TAVA), Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Chama cha Makocha, Waamuzi, Wakuzaji, Mawakala na Mabondia wa Ngumi za Kulipwa Tanzania. Aidha, Baraza linaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kuwa vyama vya michezo vyote ambavyo havijafanya chaguzi zao vinafanya chaguzi haraka iwezekanavyo ikiwemo Chama cha Mpira wa Miguu kwa Wanawake Tanzania (TWFA). Chaguzi hizi ni muhimu kwa vyama ili kujiongoza

kwa kufuata dhana ya utawala bora kwani inapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya kiuongozi ndani ya vyama na mashirikisho ya Michezo nchini.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika michezo kwa kusajili vyama, vilabu, vituo, wakuzaji na Taasisi za michezo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Baraza lilisajili Vyama 16, Vilabu 150, Taasisi 13 za Michezo, Wakuzaji Vipaji vya Michezo 20, Vituo vya Michezo 9 na Mawakala wa Michezo 23. Rejea ***Kiambatisho Na.6.*** Aidha, marekebisho ya Katiba za Vyama 12, Vilabu saba (7) na Akademia za michezo tatu (3) yamefanyika na kuidhinishwa na Msajili wa Vyama na Vilabu vya Michezo nchini. Katiba za Vyama vilivyofanyiwa marekebisho hayo ni pamoja na Shirikisho la Michezo la SHIMIWI, *Tanzania Professional Golfers Association*, *Katavi Regional Football Association* na *Mwanga District Football Association*.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha michezo katika jamii na kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu wa michezo, mafunzo kwa walimu na makocha wa michezo 64 yalitolewa katika Mkoa wa Mara. Mafunzo hayo yalihusu uratibu wa matukio ya kimichezo, sheria za mchezo wa netiboli, mpira wa Wavu, mchezo wa riadha na namna ya uendeshaji wa mazoezi ya viungo vya mwili (aerobics). Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu na makocha wa Shule za Msingi na Sekondari ili kuwawezesha kufundisha masuala hayo kwa wanafunzi, jamii na wadau wengine. Mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 22 Februari, hadi tarehe 04 Machi, 2022.

### 3.2.3.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu kuu la Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni kufundisha taaluma ya michezo, kutafiti na kutoa ushauri kuhusu masuala ya maendeleo ya michezo.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na upanuzi wa miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambapo inajengwa Hosteli mpya na ya kisasa kwa ajili ya makazi ya wanachuo, ujenzi huu kwa sasa umefikia asilimia 40. Hosteli inayojengwa itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 192 hivyo, itasaidia katika kuongeza udahili wa wanachuo. Aidha, Wizara imekamilisha taratibu za awali za ujenzi wa shule maalumu ya michezo (Sports *Academy*) ambazo ni kupatikana kwa mshauri mwelekezi ambaye ni Chuo Kikuu cha Ardhi, na ameshakamilisha michoro inayopaswa kujengwa, hatua inayofuata ni kuanza kumtafuta mjenzi (Mkandarasi). Miundombinu hii itakifanya chuo kuwa kituo mahiri kilichotukuka katika utoaji wa mafunzo ya michezo nchini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22 chuo kimeendelea na jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo 221 katika kozi za Uongozi na Utawala katika Michezo, Elimu ya Ufundishaji Michezo na Elimu ya Viungo vya Mwili katika Michezo. Kati ya wanachuo hao, wanachuo waliosajiliwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 walikuwa 130. ***Kiambatisho Na.7.*** Chuo kinatarajia kuongeza idadi ya usajili wa wanachuo kufikia 210 kwa mwaka 2022/23. Kutokana na malengo hayo, juhudi zinazofanywa kuongeza udahili ni pamoja na kuzishawishi Halmashauri na Sekretarieti za mikoa kupeleka watumishi hususan

walimu kupata mafunzo katika chuo hiki, ambapo hadi kufikia Mei, 2022 Chuo kimefanikiwa kupangiwa wanafunzi 79 wa moja kwa moja kutoka OR - TAMISEMI ambao wanatarajiwa kuanza masomo mwezi Septemba, 2022.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi katika Halmashauri na Sekretarieti za mikoa mbalimbali nchini zikiwemo Halmashauri za Kalambo (Rukwa), Ngara (Kagera) na Handeni (Tanga) ambapo jumla ya washiriki 236 walinufaika na mafunzo hayo. Aidha, mafunzo yameendelea kufanyika katika Kituo kipya cha kampasi ya Chuo Dar es Salaam ambapo jumla ya washiriki 116 walipatiwa mafunzo hayo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Aprili 2022. Vilevile, Chuo kinaendelea kutoa mafunzo katika mikoa ya Mbeya na Tabora. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 jumla ya washiriki 352 wamepatiwa mafunzo hayo ikilinganishwa na lengo la kuwafikia washiriki 300 kwa mwaka ikiwa ni sawa na asilimia 117.

### 3.2.4 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mazingira bora ya utendaji kazi kwa watumishi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo magari mapya; kuanza ujenzi wa majengo ya kudumu ya ofisi za Wizara katika eneo la Mtumba, Dodoma; kupandisha watumishi vyeo ambapo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 watumishi 87 walipandishwa vyeo; kutoa mafunzo kwa watumishi ambapo jumla ya watumishi 11 walishiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi 9

walishiriki mafunzo ya muda mfupi. Aidha, katika kuimarisha ushiriki wa watumishi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Wizara, jumla ya mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi ilifanyika. Pia, Wizara iliendelea kushiriki katika mikutano, matamasha, mashindano na matukio mbalimbali ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Sherehe za Siku ya Wanawake Duniani zilizofanyika kimkoa katika Wilaya ya Kondoa; Michezo ya SHIMIWI Kitaifa iliyofanyika mkoani Morogoro na michezo na Sherehe za Wafanyakazi (Mei Mosi). Vilevile, katika kuhakikisha watumishi wanakuwa na afya na ari ya kazi hushiriki mazoezi ya jioni mara mbili kwa wiki na asubuhi kwa siku za mwisho wa wiki.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2021/22, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:

a) Ufinyu wa Bajeti ya kutekeleza majukumu ya Wizara na Taasisi zake ikiwemo ya kugharamia maandalizi na ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa na ununuzi wa vitendea kazi muhimu vya kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwemo magari; kompyuta; na printa. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeendelea kujadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili bajeti yake iweze kuimarishwa kila mwaka pamoja na kushirikisha wadau katika utekelezaji wa majukumu. Sambamba na jitihada hizo ambapo nyongeza kadhaa zimepatikana kupitia bajeti ijayo, Wizara imeendelea kufanya mazungumzo na Balozi mbalimbali nchini zikiwemo za China, Qatar, Falme za

Kiarabu (UAE), Morocco na Uturuki ili kushirikiana katika maeneo mahsusi. Tayari mkataba wa ushirikiano na China umetiwa saini Mei 26, 2022 ambao utasaidia mafunzo na ujenzi wa miundombinu ya michezo.

b) Athari za Ugonjwa wa Virusi vya Corona (UVIKO-19) katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo hususan sanaa ambapo watayarishaji wa picha za filamu na wasanii kutoka nje ya nchi walizuiliwa kusafiri kuja nchini kwa ajili ya shughuli za sanaa na hivyo kuathiri mapato. Aidha, wasanii wetu walikosa fursa ya kufanya matamasha katika nchi mbalimbali kutokana na nchi hizo kutoruhusu watu kuingia na pia kuzuia mikusanyiko kutokana na ugonjwa huo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali iliruhusu matamasha ndani ya nchi ili kuwapa wasanii fursa za kujiendeleza na kuwatia moyo. Aidha, Serikali inaendelea na juhudi za kuwahamasisha wananchi na wasanii kuzipenda kazi zinazozalishwa na wasanii wa ndani.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2022/23 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-25; ahadi na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 - 2025/26; na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, utekelezaji wa majukumu utazingatia pia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 katika maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua na Wizara.

## 5.1 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

### 5.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya Mwaka 1997 pamoja na kuandaa mkakati wa utekelezaji; kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani; kuratibu vikao viwili (2) vya Machifu na Viongozi wa Kimila kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili nchini; kuratibu na Kuendesha Matamasha sita (6) ya Utamaduni katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na Tamasha moja (1) la Kitaifa ili kusherehekea uanuwai wa Kiutamaduni na kukuza utalii wa Kiutamaduni; kuratibu ukuzaji na uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa; kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa nchini; kuratibu Kikao kazi cha Mwaka cha Maafisa Utamaduni nchini; kuratibu na Kushiriki katika Matamasha matano (5) ya Utamaduni ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayoandaliwa na wadau wengine; kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na kufanya utafiti na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za Urithi wa Utamaduni Usioshikika na kuandaa kanzidata ya maeneo ya kihistoria na kiutamaduni nchini.

### 5.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA litaratibu maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kiswahili Duniani; kuimarisha Kiswahili nchini na kukitangaza kimataifa; kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa

kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 650 kupitia redio na televisheni. Pia, makala 30 zitachapishwa katika magazeti na maudhui mbalimbali kuhusu Kiswahili yatatolewa kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni YouTube, Facebook na Twitter; kukamilisha kupitia Sheria ya BAKITA ya Mwaka 1967; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wataalamu 50 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania; na kutoa semina kuhusu matumizi bora ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji kutoka vyombo vya habari vya Mkoa wa Dar es Salaam.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA pia itaendelea kutoa ithibati kwa miswada 100 ya vitabu vya kiada na ziada; kuendesha mafunzo kwa wakalimani 50; kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka 200 na kuthibitisha tafsiri 3,000 zinazofanywa na wakala wake; kutambua na kusajili jumla ya wataalamu 40 katika kanzidata ya wataalamu wa Kiswahili; kutambua na kutoa ithibati ya vituo 2 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni; na kutoa mafunzo na kutahini kiwango cha ujuzi wa lugha ya Kiswahili kwa wageni 10 kupitia Kituo kilichopo Makao Makuu.

## 5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Tanzania imepanga kushirikiana na Asasi ya *Viacom CBS Network Africa and Peer Lead BET International* katika maandalizi ya Tuzo maarufu za Muziki Barani Afrika zinazojulikana kama *MTV Africa Music Awards* kwa mwaka 2023 kwa muda utakaokubalika. Tuzo hizi kawaida huvutia watu zaidi ya 10,000 mashuhuri duniani katika Sekta ya Sanaa na hufuatiliwa na watu

zaidi ya 1,000,000,000 kwenye televisheni zinazopewa haki ya kuonesha tukio hili mubashara. Tafiti zinabainisha kuwa nchi wenyeji wa Tuzo hizi hunufaika kiuchumi hadi kufikia thamani ya Dola za Marekani (US$ 25,000,000) sambamba na manufaa mengine ya kiutamaduni, kiutalii na Sanaa.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Asasi ya *Music in Africa Conference for Collaborations, Exchange, and Showcases (ACCES)* yenye Makao Makuu yake nchini Afrika Kusini inaandaa Mkutano wa Wadau wa Muziki Afrika utakaofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Novemba, 2022. Uzoefu wa Mkutano huo katika nchi nyingine unaonesha kuwa watu kati ya 600 - 1,000 kutoka zaidi ya nchi 40 duniani hushiriki, na watu milioni 72 watafikiwa kupitia Mkutano huo. Kupitia Mkutano huo, pamoja na manufaa mengine ajira 247 za moja kwa moja zitapatikana kwa watanzania wakati wa maandalizi na uendeshaji wa kikao. Aidha, wadau wetu wa muziki watapatiwa mafunzo katika masuala ya tasnia ya muziki na Hakimiliki na Hakishiriki.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine ni kuratibu Vikundi nane (8) vya Burudani katika Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara na vikundi nane (8) katika maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano; kuratibu maandalizi ya mashindano ya urembo na Mitindo kwa Viziwi Duniani (Miss & Mr. Deaf International); kuratibu na kuandaa Tamasha la Muziki la Serengeti (Serengeti Music Festival), matamasha saba (7) ya Kitaifa na Kimataifa, kusimamia programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa; kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sanaa; kuratibu uanzishwaji wa kikundi cha Sanaa cha Taifa kwa kushirikiana na BASATA; kuratibu Ujenzi wa Sanamu ya

Mwalimu Nyerere katika Jiji la Addis Ababa nchini Ethiopia; kuratibu mashindano ya Sanaa kwa vijana kupitia UMISSETA, UMITASHUMTA, Taifa Cup Music Challenge na Vyuo mbalimbali; kuratibu Mafunzo ya maadili kwa wasanii na wadau wa Sanaa; kuratibu ushiriki wa nchi katika Tamasha la JAMAFEST; na kuunda Mfumo wa kupokea taarifa kutoka BASATA, BFT na COSOTA za usajili wa Wasanii, vibali vya kuendesha shughuli za Sanaa nchini, leseni za kutumia kazi za Sanaa pamoja na makusanyo na ugawaji wa mirabaha ili kuwa na kanzidata ya kisekta.

**5.2.2 BODI YA FILAMU TANZANIA**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na kufanya operesheni 48 ili kudhibiti uendeshaji wa shughuli za filamu usiozingatia Sheria na Taratibu; kutoa ithibati na leseni 60 za uendeshaji wa shughuli za filamu na kutoa vitambulisho 1,200 kwa wadau wa filamu; kuhakiki, kupanga katika madaraja na kutoa vibali 1,500 vya uoneshaji wa filamu kwa umma; kupitia na kuchambua maombi 1,500 ya utayarishaji wa filamu na Michezo ya Kuigiza pamoja na kutoa vibali; kuwajengea uwezo wadau kwa kuanzisha/kuendeleza programu za ukuzaji na uendelezaji wa tasnia ya filamu; kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa semina/vikao vinne (4) vya wadau, kongamano moja (1), na matamasha matano (5); kuratibu na kuandaa Tuzo za Filamu; kutangaza huduma na kazi za Bodi ili kuongeza uelewa na kuimarisha elimu kwa umma; na kubaini na kuyatangaza maeneo 15 ya upigaji picha za filamu.

**5.2.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakatelezwa ni

kukuza ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora; kuongeza ushiriki wa jamii katika shughuli za sanaa; kuimarisha shughuli za sanaa katika shule tano (5) za msingi na shule tano (5) za sekondari; kuhabarisha umma na wadau wa sanaa juu ya masuala ya sanaa nchini; kusimamia matumizi ya sanaa za jadi nchini; kuratibu na kushiriki matamasha ndani na nje ya nchi; kuweka misingi na miongozo ya maslahi ya wasanii yasiyo ya hakimiliki au hakishiriki; kuratibu na kuandaa Tuzo za muziki; kuongeza rasilimali za Baraza na kudhibiti matumizi yake; na kusimamia Utawala Bora na masuala ya maadili katika kutekeleza shughuli za Baraza na uendeshaji wa sekta ya sanaa.

**5.2.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kukusanya mirabaha yenye thamani ya Sh.1,350,000,000 na kuigawa kwa wabunifu na kutoa leseni 1,490; kufanya usajili wa kazi zisizopungua 2,500 na wabunifu 500; kusuluhisha migogoro ya hakimiliki; kutoa elimu ya masuala ya hakimiliki na hakishiriki kwa wabunifu na wadau mbalimbali wa Hakimiliki; kuboresha mazingira ya kazi na maslahi kwa watumishi 27 wa Taasisi; kuboresha kanzidata ya kazi za hakimiliki zilizosajiliwa kidijitali; na kuendelea kufanya operesheni moja kila robo mwaka za kupambana na uharamia wa miliki bunifu.

**5.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)**

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa itaendelea kudahili wanachuo wapatao 600 katika kozi ndefu na 150 kwa kozi fupi; kuendelea na ukarabati wa mabweni, ukumbi mkuu, ukumbi wa "flexible" na ujenzi wa uzio kuzunguka

chuo; kuendesha semina 6, warsha 8 na makongamano 3; kuandika mitaala mipya mitatu (3); kujenga studio ya kisasa ya kurekodi na kutengeneza filamu na kuandaa maandalizi ya Kituo cha Redio na TV; kufanya tathmini ya uwezekano wa kuanzisha kampasi moja ya mafunzo nje ya Bagamoyo; kuendesha Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo; kuimarisha mfumo wa TEHAMA; kupitia upya Mpango Mkakati wa Taasisi unaoisha muda wake katika mwaka 2022/23; na kuimarisha mtandao (Networks) kati ya Taasisi na wadau wa sanaa nje na ndani ya nchi.

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### 5.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Tanzania inakidhi vigezo vya kuandaa mashindano ya Kimataifa na Kikanda, Serikali katika mwaka 2022/23 imetenga kiasi cha Shilingi Billioni 10 kwa ajili ya Ukarabati wa viwanja. Kwa hatua ya kwanza vitaanza viwanja saba (7) vilivyopo katika Majiji, ambavyo ni Jamhuri – Dodoma, Sheikh Amri Abeid - Arusha, Sokoine - Mbeya, CCM Kirumba – Mwanza, na Mkwakwani - Tanga. Aidha, ukarabati huo utavihusisha viwanja vya Uhuru na Benjamina Mkapa Jijini Dar es Salaam. Hatua ya pili ni kukarabati viwanja vingine ikiwa ni pamoja na kuweka nyasi bandia na majukwaa katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mtwara, Iringa, Tabora na Shinyanga baada ya kujadiliana na wamiliki wa viwanja hivyo. Mkakati huu utaiwezesha Tanzania kufanikisha maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON ambayo tayari Tanzania imependekezwa kwa mwaka 2027 ambayo ni ndoto ya Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya kuandaa mashindano makubwa ya michezo.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara vilevile itashirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuratibu na kusimamia mashindano ya michezo ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA) na ya Sekondari (UMISSETA); kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Shule 56 maalumu za michezo nchini kwa kukarabati miundombinu ya michezo na upatikanaji wa vifaa vya michezo; kuongeza ushiriki wa wananchi katika mazoezi ya viungo na michezo kwa kuongeza usajili wa vikundi kutoka 290, mwezi Februari, 2022 hadi 305, mwezi Juni, 2023; kusimamia uendelezaji wa Michezo ya Kipaumbele ambayo ni Mpira wa Miguu, Netiboli, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Riadha na Mpira wa Mikono ili kufanya vyema katika mashindano ya kimataifa; kuongeza idadi ya wataalamu wa michezo wanaokidhi viwango na mahitaji; kuimarisha udhibiti wa matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni na dawa za kulevya katika michezo; kuimarisha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalumu katika michezo na mazoezi ya viungo vya mwili; kutumia fursa ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwa maendeleo ya michezo, wanamichezo na Taifa kwa ujumla; na kuzingatia masuala mtambuka (VVU na UKIMWI, utunzaji wa mazingira, utawala bora na jinsia) katika michezo.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatayotekelezwa ni kutoa elimu na kusambaza Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995; kuimarisha uteuzi, maandalizi na ugharamiaji wa Timu za Taifa kwa kuongeza bajeti na kushirikiana na wadau wa michezo; kuratibu maandalizi na ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano ya Kombe la Dunia Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu na ushiriki wa michezo ya

Jumuiya ya Madola; kusimamia ujenzi wa Miundombinu ya Michezo inayotarajiwa kujengwa ikiwa ni pamoja na Kituo maalumu cha Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; kujenga maeneo ya michezo na kupumzikia wananchi *(Recreational and Sports Centres)*; Viwanja vya Michezo na Maonesho ya Sanaa (Sports and Arts Arena); na Uwanja Changamani wa Michezo Dodoma.

### 5.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT itaendelea kusaidia vyama vya michezo 7 na kugharimia Timu za Taifa 34 katika mashindano ya Kimataifa; kutoa mafunzo ya utawala bora katika michezo kwa viongozi na makocha 100 kutoka Vyama vya Michezo 54; kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za michezo katika Mikoa 26, Wilaya 52, Vyama vya Michezo 54 na Taasisi za Michezo 15; kuandaa Tamasha la Wanawake kuhamasisha ushiriki wao katika michezo na maonesho ya wanawake (Women Tanzanite Festival); kutoa tuzo kwa wanamichezo Mahiri; na kuandaa na kuratibu Mashindano ya Taifa Cup; kusajili vyama vya Kitaifa vinne (4), Mkoa 40, Wilaya 100, Wakuzaji na Mawakala 20, vilabu 150 na Vituo na shule za michezo 70; kuendelea kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo kwa kuzingatia programu za mazoezi ya viungo kwa kila mwisho wa wiki; na kushirikiana na vyama/mashirikisho ya michezo katika kuratibu na kugharimia mafunzo ya wataalamu wa michezo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

### 5.4 MIRADI YA MAENDELEO

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya utambuzi,

ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa, masimulizi na nyaraka zinazohusu historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika; kukamilisha ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi Kusini mwa Afrika na kuanzisha makumbusho ya kisasa kuhusu historia ya Ukombozi wa Bara la Afrika katika jengo hilo; kuandaa filamu (*Documentary*) kuhusu mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Afrika; kukarabati nyumba za Viongozi Wakuu wa Vyama vya Ukombozi kutoka nchi za Afrika walizokaa wakati wa harakati za ukombozi ili zitumike kwa utalii na utafiti; kuandaa makongamano na maonesho kuhusu historia ya harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na kuhuisha Mkakati wa Kitaifa na Kikanda wa Miaka Mitano wa Utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kuratibu uendeshaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasanii 2,000 na vikundi 25; na kuimarisha mitaji kwa kutoa mikopo nafuu kwa wasanii 500 wa Utamaduni na Sanaa pamoja na kuanza taratibu za kujenga ofisi za Mfuko Jijini Dodoma;.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia; kukarabati miundombinu ambayo ni mabweni, ukumbi mkuu, "Flexible hall", Jengo la Utawala, maji safi na maji taka, umeme, na TEHAMA; kununua vifaa vya kuendeshea Tamasha; kuanza ujenzi wa uzio kuzunguka chuo; na kujenga studio ya kisasa za kurekodi filamu, na kituo cha redio na TV.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2022/23 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limejipanga kutoa mafunzo elekezi kwa diaspora wanaofundisha Kiswahili kwa wageni katika nchi za Namibia, Malaysia, Komoro na Sudani Kusini; kutoa mafunzo kwa Walimu wa Walimu wa Kiswahili kwa wageni namna ya kutumia mwongozo wa Taifa wa kufundisha Kiswahili kwa wageni; na kuandaa machapisho kwa ajili ya kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma, katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kumpata mkandarasi wa mradi; kusafisha eneo la mradi; kufanya maandalizi ya upatikanaji wa rasilimali na kuanza ujenzi wa uwanja mkubwa.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumnzika Wananchi katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kumpata mshauri mwelekezi wa mradi; kumpata mkandarasi wa mradi; kusafisha eneo la mradi na kuanza ujenzi wa vituo husika.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kuboresha kumbi za mikutano kwa kununua samani pamoja na kuweka miundombinu bora zikiwemo "projector" pamoja na vipaza sauti (spika); kukamilisha ukarabati eneo la kufanyia mazoezi ya viungo (Gym) na kumpata mzabuni wa kuendesha GYM hiyo; kukarabati

eneo la kukimbilia (Track) kwa kuweka zulia jipya (Tartan) la kisasa; na kukarabati eneo la Big screen.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka wa fedha 2022/23 shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kituo cha kukuza na kuendeleza vipaji (Sports Academy); na kuendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi.

## 5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwemo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi; kuratibu na kuwezesha mazoezi ya wafanyakazi wote wa Wizara kila wiki mara moja; kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo uhamisho, likizo, safari n.k.; kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi; kuratibu ushiriki wa Wizara katika sherehe za Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Michezo ya SHIMIWI; na kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia kuratibu uandaaji wa Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2023/24; kuratibu na kuandaa utafutaji wa rasilimali fedha nje ya bajeti ya Serikali; kuratibu vikao vinne (4) vya ushirikiano baina ya Wizara zenye dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; kufanya mazoezi ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera, Miradi na Programu mbalimbali za Wizara; kuratibu maandalizi ya taarifa

mbalimbali ikiwemo za utekelezaji wa Bajeti na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025; na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za kutangaza shughuli za Wizara, uzingatiwaji wa Sheria za fedha na ununuzi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, matumizi ya TEHAMA na ushauri wa kisheria.

## 6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### 6.1 MAPATO

**172.** ***Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2022/23 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa (Sh.900,000,000) kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na viingilio katika matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, kwa upande wa Taasisi sita (6) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Hamsini na Tano Elfu (Sh.5,396,455,000). Rejea ***Kiambatisho Na.8A na B*** ni mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2022/23.

### 6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2022/23 Wizara imetengewa bajeti ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Mia Tisa Tisini na Moja Elfu** (Sh.35,425,991,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili na Moja, Mia Nane Themanini na Mbili Elfu** (Sh.8,201,882,000), Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tatu Tisini na Mbili, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu** (Sh.11,392,949,000) na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Thelatini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Sh.15,831,160,000). ***Kiambatisho Na.10A, B*** na ***C*** kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2022/2023

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2022/23 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2022/23 yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Mia Tisa Tisini na Moja Elfu** (Sh.35,425,991,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili na Moja, Mia Nane Themanini na Mbili Elfu** (Sh.8,201,882,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi **Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Tatu Tisini na Mbili, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu** (Sh. 11,392,949,000) na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu** (Sh.15,831,160,000).

## 8.0 MWISHO NA SHUKRANI

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Wizara yangu inakusudia kufanya mageuzi makubwa katika kuendeleza Sekta zake na kuimarisha mchango wake katika Pato la Taifa, kuongeza ajira hususan kwa vijana na kuimarisha michezo nchini. Aidha, kama nilivyobainisha hapo awali, Wizara itawajengea uwezo wasanii wetu kimitaji na mafunzo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, hatua ambayo itaongeza tija, ubora na ushindani wa kazi za sanaa na wabunifu wetu kitaifa na kimataifa. Pia, Wizara itaboresha matumizi ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya kuwahudumia wasanii na wadau wengine wa sanaa ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma, kurahisisha urasimishaji wa Sekta ya Sanaa na shughuli za ubunifu na kubwa zaidi, kuongeza mapato ya wasanii na Serikali kupitia ukusanyaji wa mirabaha. Mifumo hiyo ni pamoja na ya kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa hususani muziki na filamu katika vyombo vya habari, mfumo wa kusambaza kazi za wasanii kama ilivyo *Netflix* na mfumo wa usajili na usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mifumo hiyo inafanya kazi vizuri, Wizara itaweka mazingira bora ya Kisheria ikiwa ni pamoja na kukamilisha marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999, Sheria Na. 27 ya Mwaka 1967 iliyoanzisha BAKITA pamoja na Kutunga Sheria ya Kusimamia Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu katika Michezo.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2021/22 yamechangiwa pia na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Shukrani zangu za

dhati kama nilivyodokeza katika utangulizi wa hotuba yangu ziende kwa Viongozi Wakuu wa Nchi yetu yaani Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Viongozi wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa nje, nazishukuru nchi za China, Japan, Korea Kusini, Uswisi na Ujerumani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA).

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa wadau wa ndani, naomba nianze na mashirikisho na vyama vyote vya kisekta katika utamaduni, sanaa na michezo, vyombo vyote vya habari, wasambazaji wa kazi za sanaa, filamu na michezo ya kuigiza, kampuni za Azam TV, DSTV, Startimes, Mamlaka ya Bandari (TPA), TANAPA, HEINEKEN Tanzania limited, Coca Cola, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, na Shirika la Ndege Tanzania (ATC). Nawapongeza na kuwashukuru wadau wote wakiwemo wachezaji, wasanii mbalimbali na wanautamaduni. Hakika katika mwaka huu tumeweza, tuweze na kutekeleza zaidi katika mwaka ujao.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** nafahamu Bunge lako Tukufu linajua kwamba kauli ya "*Anaupiga Mwingi*" inatokana na lugha ya kimichezo. Nihitimishe kwa kuthibitisha kauli hiyo kwa mambo haya kumi (10):

a) Mheshimiwa Rais ndani ya mwaka mmoja karejesha Tuzo za Filamu;

b) Ndani ya mwaka mmoja karejesha Tuzo za Muziki;

c) Ndani ya mwaka mmoja karejesha mirabaha;

d) Ndani ya mwaka mmoja Tembo Worriors imeshiriki Kombe la Dunia;

e) Ndani ya mwaka mmoja Serengeti Girls wanafika hatua ya juu Kimpira;

f) Ndani ya mwaka mmoja Twiga Stars mabigwa COSAFA;

g) Ndani ya mwaka mmoja amekamilisha usanifu wa "Sports and Arts Arena";

h) Ndani ya mwaka mmoja ameanzisha shule 56 maalumu za michezo;

i) Ndani ya mwaka mmoja ametoka ofisini na kuigiza filamu ya "Royal Tour" na

j) Ndani ya mwaka mmoja ametoa asilimia 5 ya michezo ya kubahatisha kusaidia michezo.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** huku ni zaidi ya kuupiga mwingi.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.michezo.go.tz. na kupitia mitandao ya kijamii.

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri Mheshimiwa Waziri na suti yako inapendeza leo. Hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kabla ya yote kwanza nami nichukue fursa hii kuwapongeza sana *Serengeti Girls* kwa kufanikiwa kwenda kutuwakilisha katika mashindano ya Kombe la Dunia, wao pamoja na timu ya walemavu ya wanaume ambao nao watashiriki katika Kombe la Dunia. Kwa kweli wameupiga mwingi na hongera zao sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, natoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Naomba

taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(b) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Wizara kuwasilisha Bajeti yake ya Fungu 96 hapo tarehe 24 Machi, 2022, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo 18. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati inaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii likiwemo suala la matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato iliyoboreshwa ili kuvutia watumiaji lakini pia kuongeza mapato ya nchi pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Viwanja

na Maeneo ya kupumzikia *(sports recreational and leisure areas)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kuchambua ukusanyaji wa maduhuli na vilevile Kamati iliweza kuchambua jinsi ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Haya yote yako katika taarifa na ninaomba yaingie katika kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya taarifa yetu ni kwamba Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imejiwekea malengo mbalimbali kwa kuzingatia mipango na sera za Kitaifa na Kimataifa ambazo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo yaani mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano 2021/2022 na 2025/2026, pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Utamaduni ya Mwaka 1997, Kanuni za Maonesho kwa Umma na Utangazaji *(The Copyright Licensing of Public Performances and Broadcasting Regulations, 2003),* Kanuni za Mawasiliano ya Umma pamoja na Sheria nyingine zinazoongoza tasnia ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa na kupokea vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama inavyooneshwa kwenye taarifa kuu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza malengo haya pamoja na majukumu mbalimbali, Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati, Randama yake yenye kuonesha makadirio ya makusanyo ya maduhuli na matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati wakati inafanya kazi hiyo, na uchambuzi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliweza kuchambua makadirio na makusanyo ya maduhuli ya mwaka wa fedha 2022/2023. Vilevile tuliweza kufanya uchambuzi wa makadirio na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo na hii ilijikita katika sehemu: -

(a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara; tuliweza kuchambua na kulenga kufanya ulinganisho wa makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka 2021/2022 na makadirio ya bajeti katika mwaka 2022/2023 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika randama iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Shilingi 33,425,991,000/=. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yameombwa Shilingi bilioni 19.5 sawa na asilimia 59 na Shilingi bilioni 13.8 sawa na asilimia 41 zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba (6), Kamati inapongeza sana Serikali kwa kutenga makadirio ya asilimia 41 ya bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya

maendeleo. Hii inaonesha kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kuendeleza michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele (b) tulifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara Fungu namba 96 kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kamati katika hatua nyingine Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya Fungu 96 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huo, yaani Bajeti ya Taifa. Kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu namba 96. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Makadirio ya bajeti ya Fungu 96 ya mwaka 2022/2023 kwa ujumla wake ni Shilingi bilioni 33.4. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 0.08 ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022/2023 ambayo ni Shilingi trilioni 41.0. Aidha, bajeti hii imepungua kutoka asilimia 0.02 dhidi ya Shilingi trilioni 37.9 ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022;

(ii) Bajeti ya Mishahara ya Fungu 96 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2022/2023 ni asilimia 0.07. Bajeti hii imepungua kwa asilimia 0.2 dhidi ya asilimia 0.09 iliyotengwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(iii) Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 96 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa imepungua asilimia 0.01 kutoka asilimia 0.098 mwaka 2021/2022 hadi asilimia

0.08 Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kielelezo namba saba kinaonesha ulinganisho huo.

(iv) Uchambuzi wa Kamati vilevile umebaini kuwa wakati Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 ikiwa imeongezeka kwa asilimia 8.1 kutoka Shilingi trilioni 37.9 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi trilioni 41.06 mwaka 2022/2023. Bajeti ya Fungu 96 imepungua kwa asilimia 16.6 kutoka Shilingi bilioni 40.09 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi bilioni 33.4 kwa mwaka huu wa 2022/2023;

(v) Wakati bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 16.32 mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023, Bajeti ya Mishahara ya Fungu namba 96 imepungua kwa asilimia 34 katika kipindi hicho; na

(vi) Aidha, wakati Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 3.6, Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 96 imepungua kwa asilimia sita. Unaweza ukatazama vielelezo vimeonesha dhahiri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kwa mwaka 2022/2023 kuna ongezeko la Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hata hivyo ongezeko hilo haliakisi ongezeko la bajeti katika Fungu namba 96. Uchanganuzi wa Kamati unaonesha kuwa ongezeko la bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kuna upungufu wa bajeti ya Fungu hili namba 96. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya uchambuzi huu ni kwamba, wakati Bajeti Kuu ya Taifa ikiongezeka, hali inayoleta mtazamo chanya wa maendeleo ya nchi kwa ujumla, bajeti ya Fungu namba 96 inaendelea kupungua. Hali hii inaleta taswira hasi katika maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ni Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yetu. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake na kubaini mambo mbalimbali, inatoa ushauri, maoni na mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuibua vipaji vya michezo nchini. Michezo imekuwa ikiingiza Taifa au ikiliingizia Taifa mapato na kuifanya nchi ipate sifa Kimataifa. Hata hivyo uibuaji wa vipaji kwenye michezo mbalimbali imekuwa ya chini. Kutokana hali hiyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iweke mikakati ya kuibua vipaji katika michezo mbalimbali kuanzia ngazi za Mitaa, Vijiji kuweza kupata vipaji vingi na kuongeza wanamichezo wengi Kitaifa na Kimataifa

(ii) Serikali iweke mikakati ya kukuza na kuendeleza michezo shuleni katika shule za msingi pamoja na sekondari ili kuweza kubaini vipaji mbalimbali watakavyoonyesha watoto kupitia mashindano ya michezo shuleni;

(iii) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara zote zinazohusika na michezo shuleni ziweke mikakati ya kuhusisha wadau mbalimbali binafsi wa michezo ili kuwashawishi au kuwekeza katika

michezo shuleni yenye lengo la kukuza vipaji vya watoto;

(iv) Serikali iwekeze katika kufundisha wataalam maalum yaani walimu wa michezo na Maafisa Utamaduni katika kuwa wabobevu wa kuweza kuibua vipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili, ni uwekezaji katika wataalam wa michezo. Ili michezo iweze kuwa endelevu na yenye kuleta faida, ni muhimu kuwe na wataalam wabobevu wa michezo hiyo. Hata hivyo, kumekuwa na wataalam wachache sana wa michezo hapa nchini, kama vile mbio za *Marathon* na michezo mingine ya *Olympic*. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iwekeze kwa kuwasomesha wataalam wengi wa michezo ili kuiewezesha tasnia ya michezo mbalimbali kuwa ya kitaalam na bobevu;

(ii) Serikali iendelee na kuwekeza katika miundombinu ya kufundishia ili kuweze kufundisha hasa katika vyuo vya michezo na hasa katika kile chuo cha Malya;

(iii) Serikali iwahusishe na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika michezo kwenye shule, vyuo mbalimbali nchini ili kuongeza na kupanua tasnia ya michezo, utamaduni, na sanaa nchini itakayoongeza ajira kwa vijana wa wa Kitanzania; na

(iv) Kuhusu michezo ya *Olympic* Kamati inashauri kuwa Wizara itambue na kushirikana na Kamati ya *Olympic* ya Taifa ili kupata fursa mbalimbali zinazotolewa

na Kamati hiyo na kushirikiana mambo mbalimbali yanayotakiwa na Kamati hiyo kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu, ni kuimarisha utendaji katika Sekta ya Michezo. Tasnia ya Michezo, Utamaduni na Sanaa zinakua kwa kasi hapa nchini na zinagusa idadi kubwa sana ya wananchi na hivyo kuwa muhimu sana, na kuwa zinazalisha ajira binafsi nyingi. Vilevile Sekta hizi ni mtambuka maana zinagusa Wizara zaidi ya moja. Ili sekta hizi ziendelee kukua na kuleta tija stahiki kwa wananchi, inahitajika kuwe na utendaji wa pamoja kati ya Wizara zinahusika na mambo ya michezo kama vile Wizara ya Ardhi, Wizara ya *TAMISEMI* pamoja na Wizara mama ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hata hivyo, kumekuwa na utendaji hafifu hapa nchini katika tasnia za michezo mbalimbali ya kisanaa na utamaduni. Hivyo, Kamati inatoa ushauri:-

(i) Serikali iweke mkakati wa kuwianisha utendaji kazi wa Wizara zinazohusika moja kwa moja na utamaduni, sanaa na michezo ili kuleta utendaji bora wa tasnia hii hapa nchini;

(ii) Serikali iandae kanuni mbalimbali zitakazoongoza Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo zitakazotumika na Wizara zote zinazohusika na michezo pamoja na wadau mbalimbali wa michezo ili kuwa na utekelezaji wa pamoja wa majukumu ya utamaduni, sanaa na michezo kwa maendeleo ya tasnia hizo hapa nchini;

(iii) Serikali kuweka Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo rafiki kwa ajili ya sekta hii;

(iv) Serikali iweke mkakati wa kukutana mara kwa mara na vyama mbalimbali vya utamaduni, sanaa na michezo ili kuweza kuondoa changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara katika vyama, Mashirika Taasisi mbalimbali za michezo, utamaduni na sanaa hapa nchini, na hivyo kuendeleza tasnia kuhusika kwa wasanii au kwa maslahi ya Taifa;

(v) Kutokana na migongano inayojitokeza mara kwa mara kati ya Serikali na wasanii kuhusiana na vyama na mashirika ya kimichezo, sanaa na utamaduni, Serikali iwaachie wasanii na wanamichezo wenyewe kusimamia vyama na mashirikisho yao na Serikali kubaki kuwa msimamizi; na

(vi) Aidha, katika teuzi mbalimbali za wasimamizi wa vyombo vinavyosimamia utamaduni, sanaa na michezo Serikali iteue watendaji wenye uzoefu na ujuzi wa tasnia husika ili kuweza kuleta maendeleo sahihi katika tasnia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine wa nne ni kuimarisha miundombinu ya michezo nchini. Ili kukuza michezo, miundombinu ya michezo ni muhimu sana. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 imeweka bayana haja ya Serikali yake kuweka na kuimarisha miundombinu ya michezo, sanaa na utamaduni hapa nchini kwa nia ya kukuza tasnia hizo na kuleta ajira kwa Watanzania wengi. Vilevile kuliongezea Taifa mapato. Hata hivyo, miundombinu ya michezo hapa nchini bado ni dhaifu. Kutokana na hilo, Kamati inaishauri kama ifuatavyo: -

(i) Serikali iweke mikakati ya kujenga miundombinu mipya ya michezo na kuboresha iliyopo ili kuendeleza tasnia ya michezo, utamaduni na sanaa hapa nchini; na

(ii) Serikali ishirikishe sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu ya utamaduni, sanaa na michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tano, ni uimarishaji wa utoaji wa mafunzo mbalimbali ya utamaduni, sanaa na michezo nchini. Ili kukuza vipaji vya utamaduni, sanaa na michezo ni muhimu kuwepo na shule na vyuo vya kutosha vya tasnia hizo. Tanzania kuna vyuo vichache sana vya tasnia hiyo. Kutokana na hilo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iweke mkakati wa kuongeza idadi ya Vyuo vya Utamaduni, Sanaa na Michezo nchini ili kuweza kuongeza idadi ya wasanii na wanamichezo mbalimbali wabobevu; na

(ii) Serikali ihuishe mitaala ya ufundishaji wa mafunzo mbalimbali ya utamaduni, sanaa na michezo kwenye shule, vyuo mbalimbali vya michezo nchini kwa idadi ya kutosha ili kuwezesha kukuza vipaji mbalimbali vya utamaduni, sanaa na michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa sita, ni kuimarisha ligi ya mpira wa miguu hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha ligi ya mpira wa miguu ya Tanzania kuwa miongoni mwa ligi 10 bora katika Bara la Afrika. Hata hivyo, uwekezaji kwenye ligi hii bado ni hafifu. Kutokana na sababu hiyo, na kwa

kuzingatia umuhimu wa ligi hii kwa ajira nchini na mapato ya nchi Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Serikali kuweka mikakati ya kuvutia wawekezaji kwenye ligi hii ili kuweza kuendelea kuifanya kuwa bora zaidi katika Bara la Afrika;

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, kwa kuwa Serikali imeondoa kodi ya nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vyetu nchini, Serikali pia iangalie namna ya kuondoa kodi katika vifaa vinavyoendana na uwekaji wa nyasi bandia katika viwanja vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie, kwa kuwa Serikali imeondoa kodi ya nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vyetu nchini, Serikali pia iangalie namna ya kuondoa kodi katika vifaa vinavyoendana na uwekaji wa nyasi bandia katika viwanja vyetu hivyo. *(Makofi)*

Tatu, Kamati inapongeza na kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia timu za mpira wa miguu nchini. Kamati inashauri Wizara kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuleta tija kama ilivyokusudiwa na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kusema napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa

na zaidi kwa kushiriki vyema katika Kamati ikiwemo uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Naomba orodha yote ya Wajumbe hawa iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe, nimshukuru Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu, hakika ninyi ni viongozi wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge; Naibu Waziri wake ambaye ni Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge; Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Hassan Abbas; Naibu Katibu Mkuu ndugu yetu Mheshimiwa Saidi Yakubu, pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushirikiana vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa katika Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati kiufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kipekee tunawashukuru

sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Francisca Haule, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Emmanuel Mdidi na Ndugu Chacha Nyakega kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Fungu Namba 96 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi 33,425,991,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA, KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza maeneo yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(b) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Wizara kuwasilisha Bajeti yake ya fungu 96 hapo tarehe 24 Machi, 2022, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

### 2.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara kwa

Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kumi na nane (18). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato iliyoboreshwa ili kuvutia watumiaji lakini pia kuongeza mapato ya nchi pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Viwanja na Maeneo ya kupumzikia *(sports recreational and leisure areas)*.

### 2.2 UCHAMBUZI WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Fungu 96 k**atika mwaka wa fedha 2021/2022 kabla ya kuondolewa kwa Idara ya Habari-MAELEZO iliyohamishwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 34,826,444,000, a**mbapo **Shilingi** 960,000,000 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Ofisi Kuu ya Wizara na Idara zake na **Shilingi** 33,866,444,000 kutoka Taasisi zilizokuwa chini ya Wizara. Aidha, baada ya kuhamishwa kwa Idara ya Habari-MAELEZO Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,260,323,000,** sawa na **asilimia 17.97** ya fedha za maduhuli zilizokadiriwa kabla ya Idara ya Habari-MAELEZO kuhamishwa. Kati ya hizo **Shilingi** 782,202,000 ziliidhinishwa kukusanywa kutoka vyanzo vya Makao Makuu ya Wizara na Idara zake na **Shilingi** 5,478,121,000kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara ilikusanya jumla ya **Shilingi bilioni** 2,623,180,576 sawa na **asilimia 41.9**; ambapo kutoka Makao Makuu ya Wizara na Idara zake yalikusanywa maduhuli ya S**hilingi** 436,255,667, sawa na **asilimia 55.7** ya fedha za maduhuli yaliyoidhinishwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara na Idara zake na **Shilingi bilioni** 2,186,924,909 sawa na **asilimia 39.9** ya fedha za maduhuli zilizokadiriwa kukusanywa kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara, kama inavyooneshwa katika kielelezo Namba 1(a) na (b).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa makusanyo ya juu kwa Wizara hii yalifikia **Shilingi** 377,555,519ambazo zilikusanywa kutoka Baraza la Michezo la Taifa (BMT), sawa na **asilimia 126** ya **Shilingi** 300,000,000 ya makadirio yaliyoidhinishwa. Kamati ilitaka kufahamu sababu za makusanyo hayo kuwa makubwa kwa kiwango hicho. Na ilielezwa kuwa ni kutokana na usimamizi na utaratibu mzuri wa makusanyo uliowekwa na Serikali kupitia BMT. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa makusanyo haya.**

**Mheshimiwa Spika,** aidha, uchambuzi wa Kamati uliendelea kubaini kuwa makusanyo yaliyokuwa ya chini yalikuwa ni **asilimia 23** ambayo ni **Shilingi** 236,953,000ya **Shilingi bilioni** 1,025,000,000 ya maduhuli yaliyokadiriwa kukusanywa kutoka Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA). Kamati vilevile ilitaka kufahamu sababu za makusanyo haya kuwa ya chini kwa asilimia zisizofikia hata robo ya makadirio. Wizara iliieleza Kamati kuwa makusanyo madogo hayo yalitokana na kutokamilika kwa wakati kwa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa *-Art*

*Management Information System (AMIS)* pamoja na uelewa mdogo wa wadau kuhusu masuala ya Hakimiliki. **Kamati inasisitiza kuwa Wizara iweke mkakati wa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na Hati Miliki kwa wadau wote wanaohusika ili kuwezesha kuwainua wasanii na pia kuongeza Pato la Taifa. Kamati pia inashauri kutenga makusanyo ya maduhuli yenye uhalisia na yenye kutekelezeka.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilitarajiwa kukusanya jumla ya maduhuli kufikia **asilimia 66.6.** Hata hivyo, hadi kipindi hicho Wizara ilikusanya maduhuli kwa **asilimia 41.9**. Kamati pia ilihoji sababu za makusanyo ya jumla ya Wizara kuwa chini ya **asilimia ya 66.6**. Wizara ilieleza sababu za jumla kuwa ni;

i) Kupungua kwa kazi za tafsiri za wachina baada ya mkataba wao kumalizika na kutokana na mlipuko wa UVIKO-19 kumesababisha kupungua kwa wageni wanaohitaji kujifunza Kiswahili wakiwa nchini;

ii) Sehemu kubwa ya makusanyo ya TasuBa na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya inatokana na malipo ya ada ambayo inalipwa kwa muhula, kwa hiyo malipo yote ya muhula wa pili yatakusanywa kuanzia katikati ya mwezi Machi, 2022. Hivyo makusanyo yaliyoripotiwa ni ya muhula wa kwanza;

iii) Kupungua kwa waombaji wa vibali vya utayarishaji wa filamu hususani kutoka nje ya nchi inayotokana na janga la UVIKO-19. Janga la UVIKO-19 limesababisha kasi ya uombaji vibali vya nje kupungua kwa kiasi kikubwa, chanzo hicho huchangia **asilimia 60** ya

mapato yanayokusanywa na Bodi ya Filamu; pamoja na,

iv) Kutokamilika kwa wakati kwa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa -*Art Management Information System* (AMIS) ambao ulitegemewa kuongeza makusanyo ya Baraza la Sanaa kwa kiasi kikubwa;

Mheshimiwa Spika, **Kamati inasisitiza kuwa Wizara ifanyie kazi changamoto zote zilizojitokeza wakati wa makusanyo ya maduhuli kwa Wizara hii ili kuifanya Wizara kuongeza mapato yake.**

**Kielelezo Na. 1(a): Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli ya Mwaka 2021/2022 hadi Februari 2022**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Maendeleo ya Michezo | 782,202,000 | 436,255,667 | 55.7 |
| Taasisi zilizo chini ya Wizara | 5,478,121,000 | 2,186,924,909 | 39.9 |
| JUMLA | 6,260,323,000 | 2,623,180,576 | 41.9 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati

**Kielelezo Na.1 (b): Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli ya Mwaka 2021/2022 Hadi Februari, 2022**







**Chanzo**: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati

## 2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA MWAKA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, kabla ya Idara ya Habari-MAELEZO kuhamishwa kwenda Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo pamoja na Taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 54,741,802,000.** Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 19,146,653,000,** Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 14,880,149,000** na **Shilingi 20,715,000,000** kwaajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa mnamo tarehe 13 Septemba, 2021 Idara ya Habari-MAELEZO ilihamishwa kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kupelekwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kutokana na uhamisho huo taasisi zilizo chini yake ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) pia zilihamishwa. Hivyo, uhamisho huo uliambatana na kuondoka kwa Bajeti ya Matumizi Mengineyo (OC), Miradi ya Maendeleo na Mishahara ya Watumishi yenye jumla ya **Shilingi 14,649,299,760 ambapo**, Mishahara ni **Shilingi 6,548,299,760;** Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 2,100,000,000;** na Miradi ya Maendeleo **Shilingi 6,001,000,000.** Hivyo kufanya Wizara mpya ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kubaki na jumla ya Bajeti ya **Shilingi 40,092,502,240** ambapo Mishahara ni **Shilingi 12,598,353,240,** Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 12,780,149,000** na Miradi ya Maendeleo **Shilingi 14,714,000,000,** kama inavyoonekana kwenye kielelezo Namba 2.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, baada ya kuondolewa kwa Idara ya Habari-MAELEZO, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilipokea kutoka Wizara ya Fedha na Mipango **Shilingi 20,162,993,692** sawa na **asilimia 50.2** ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,400,397,160** sawa na **asilimia 65.7** ya fedha zilizopokewa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), **Shilingi 8,926,685,106,** sawa na **asilimia 70.8** ni kwaajili ya mishahara na **Shilingi 2,835,911,426** sawa na **asilimia 19.2** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kamati ilitaka kufahamu sababu zilizosababisha Wizara kupokea kiasi kidogo hicha fedha, na ikiwa kipindi kilichobaki fedha zitakazotolewa zitaweza


kukamilisha miradi kwa wakati kama ilivyopangwa. Aidha Wizara ilieleza kuwa ni kutokana na kupokea kiasi kidogo kutoka Hazina. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za maksudi na za dhati ili kupeleka fedha za maendeleo katika Wizara hii kutokana na umuhimu wake kwenye ajira za vijana wetu walio wengi. Hivyo uwekezaji kwenye Wizara hii ni nyeti na ni wa muhimu sana.

**Kielelezo Na. 2 (a): Ulinganisho wa upokeaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Februari, 2022**

| MAELEZO | | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA |
|---|---|---|---|
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 2,900,399,000 | 1,614,554,350 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 9,697,954,240 | 7,312,130,756 |
| **Jumla Ndogo** | | **12,598,353,240** | **8,926,685,106** |
| Matumizi Mengineyo (OC) | Wizara | 8,078,779,000 | 4,697,914,762 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 4,701,370,000 | 3,702,482,398 |
| **Jumla Ndogo** | | **12,780,149,000** | **8,400,397,160** |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 14,464,000,000 | 2,835,911,426 |
| | Taasisi chini ya Wizara | 250,000,000 | - |
| **Jumla Ndogo** | | **14,714,000,000** | **2,835,911,426** |
| **JUMLA KUU** | | **40,092,502,240** | **20,162,993,692** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati

**Kielelezo Na. 2 (b) Upokeaji wa Fedha kwa mwaka 2021/2022 hadi Februari, 2022**




**Chanzo**: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imejiwekea Malengo mbalimbali kwa kuzingatia Mipango na Sera za Kitaifa na Kimataifa ambazo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020). Vilevile Wizara imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Utamaduni ya Mwaka 1997, Kanuni za Maonesho kwa Umma na Utangazaji *(The Copyright (Licensing of Public Performances and Broadcasting) Regulations, 2003,* Kanuni za Mawasiliano ya Umma (*The Copyright and*

*Neighbouring Rights (Copyrighted Works - Communication to the Public) Regulations, 2015 pamoja na* Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka, 1995, Sheria ya BMT Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya mwaka 1971 pamoja na sheria nyingine zinazoongoza tasnia ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni vifuatavyo**:-**

i) Kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiwemo viwanja na kumbi;

ii) Kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Utamaduni, Sanaa na Michezo;

iii) Kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa katika michezo na michuano mbalimbali sambamba na kuhamasisha wadau kusaidia ushiriki wa timu, vilabu na wawakilishi mbalimbali wa kitaifa katika michezo na michuano ya kimataifa;

iv) Kukamilisha mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali za kisera na kisheria katika kuimarisha usimamizi na utekelezji katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo;

v) Kujenga, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kitaasisi katika usimamizi na utekelezaji wa masuala ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo;

vi) Kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususani zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, TAMISEMI, Afya, Maliasili na Utalii; na

vii) Kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi katika maendeleo ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutekeleza malengo haya pamoja na majukumu mbalimbali, Wizara iliwasilisha mbele ya Kamati, Randama yake yenye kuonesha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Kamati ilifanya kazi hiyo na uchambuzi ni kama ifuatavyo: -


### 3.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Fungu 96 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,296,455,000.** Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya Wizara pamoja na taasisi zake. Kati ya hizo **Shilingi 900,000,000** zinatarajia kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 5,396,455,000** kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara. (Kama inavyoonekana kwenye kielelezo Namba 3 na Namba 4.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya Uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo Wizara ilikadiria kukusanya **Shilingi 6,260,323,000** dhidi ya yale ya mwaka 2022/2023 ambapo **Shilingi 6,296,455,000** ya maduhuli yanatarajiwa kukusanywa. Baada ya uchambuzi huo Kamati imebaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha

2022/2023 yamepungua kwa **Shilingi 36,132,000** sawa na pungufu kwa **asilimia 0.6 Kamati ilihoji sababu ya kuwa na makadirio madogo licha ya kuwa sasa dunia imefunguliwa hata baada ya mlipuko wa ugonjwa wa Korona. Wizara iliieleza Kamati kuwa kuwekwa kwa makadirio hayo kunatokana uhalisia wa makusanyo na vyanzo vya Wizara hasa baada ya kuhamishwa kwa Idara ya Habari–MAELEZO kutoka Wizara ha Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.**

**Kielelezo Na. 3 (a): Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023 (Fungu 96)**




**Chanzo**: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati

**Kielelezo Na. 3 (b):Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Mwaka 2021/22 na 2022/2023 Makao Makuu ya Wizara (Idara ya Maendeleo ya Michezo)**

| Maelezo | Makadirio ya Maduhuli 2021/22 | Makadirio ya Maduhuli 2022/23 |
|---|---|---|
| Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa) | 470,200,000 | 640,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| Ada za Mafunzo | 312,000,000 | 259,998,000 |
| Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | 1,000 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | 1,000 |
| **Jumla** | **782,202,000** | **900,000,000** |


Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati.

**Kielelezo Na.4(a) :Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Taasisi Zilizo chini ya Wizara (Fungu 96) katika Mwaka 2021/2022 na 2022/23**

| Na | Jina la Taasisi | Makadirio ya Maduhuli 2021/22 | Makadirio ya Maduhuli 2022/23 |
|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 558,630,000 | 416,750,000 |
| 2. | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 700,000,000 | 720,000,000 |
| 3. | Bodi ya Filamu Tanzania | 1,413,572,000 | 1,359,642,000 |
| 4. | Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 1,480,919,000 | 865,063,000 |
| 5. | Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 300,000,000 | 685,000,000 |
| 6. | Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,025,000,000 | 1,350,000,000 |
| **Jumla** | | **5,478,121,000** | **5,396,455,000** |

Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 96) na Usanifu wa Kamati.

**Kielelezo Na. 4 9b): Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara (Fungu 96) katika Mwaka 2021/2022 na 2022/23**




## 3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika, Katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo: -**

**a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 96)**


**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unalenga kufanya ulinganisho wa makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka 2021/2022 na makadirio ya bajeti katika mwaka 2022/2023 [Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020] kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Randama iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia Fungu 96 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya

**Shilingi 33,425,991,000.** Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa **Shilingi 19,594,831,000.00** sawa na **asilimia 59** na **Shilingi 13,831,160,000** sawa na **asilimia 41** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 6. **Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kutenga makadirio ya asilimia 41 ya bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya maendeleo. Hii inaonesha kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kuendeleza michezo nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa bajeti ya mwaka 2022/2023 imepungua kwa **Shilingi 6,666,511,240** sawa na **asilimia 16.6** ya bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo ilikuwa na jumla ya **Shilingi 40,092,502,240;** (Kielelezo Na 6 (b) kinatoa ufafanuzi zaidi.

**Kielelezo Na. 5: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo (Fungu 96) mwaka 2022/2023**





Kamati iliihoji Wizara sababu za kushuka kwa bajeti hiyo na kuelezwa kuwa ni kutokana na kuhama kwa Idara ya Habari Maelezo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni,

Sanaa na Michezo kwenda Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa katika mwaka 2022/2023 makadirio ya mishahara yamepungua kwa **Shilingi 4,396,471,240,** kutoka **Shilingi 12,598,353,240** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 8,201,882,000** mwaka 2022/2023; sawa na upungufu wa **asilimia 34.** Vilevile makadirio ya Matumizi mengoneyo (OC) yaliongezeka kwa **Shilingi 2,992,551,840,** kutoka **Shilingi 8,400,397,160** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 11,392,949,000** mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la **asilimia 35.6**. uchambuzi pia ulibaini kuwa Makadirio ya bajeti ya matumizi ya maendeleo yameshuka kwa **Shilingi 882,840,000,** sawa na **asilimia sita (6**) kutoka **Shilingi 14,714,000,000** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi 13,831,160,000** mwaka 2022/2023 Kamati inavyoonekana kwenye kielelezo Namba 6(b)]. Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba Wizara inapunguza uwekezaji ukilinganisha na uwekezaji wa mwaka 2021/2022. Hali hii itapunguza kwa kiasi fulani maendeleo ya sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo**. Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwekezaji kwenye Wizara hii kutokana na umuhimu wake kwa ajira za Watanzania wengi pamoja na kuongeza Pato la Taifa.**

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi (Fungu 96) kwa mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023**




**b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 96) kwa Kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika hatua nyingine ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya Fungu 96 dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya Bajeti ya Wizara katika Mpango huo (Bajeti ya Taifa) kati ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani mwenendo wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri bajeti ya Fungu 96.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Makadirio ya bajeti ya Fungu 96 kwa mwaka 2022/2023 kwa ujumla wake ni **Shilingi 33,425,991,000.** Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 0.08** ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 ambayo ni **Shilingi**

**41,063,915,000,000.** Aidha, bajeti hii imepungua kutoka **asilimia 0.02** dhidi ya shilingi **37,980,601,000,000** ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2021/2022;

ii) Bajeti ya Mishahara ya **Fungu 96** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 ni **asilimia 0.07.** Bajeti hii imepungua kwa asilimia 0.2 dhidi ya asilimia 0.09 iliyotengwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka Fedha 2021/2022;

iii) Bajeti ya Maendeleo ya **Fungu 96** dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imepungua kwa **asilimia 0.01** kutoka **asilimia 0.098 mwaka 2021/2022** hadi **asilimia 0.08** Mwaka wa Fedha 2022/2023**.**
**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo Na. 7 kinaonyesha ulinganisho huo.

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti Fungu 96 Dhidi ya bajeti ya Taifa 2021/2022 na 2022/2023 (kwa milioni)**

| | ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 52 DHIDI YABAJETI YA TAIFA 2021/2022 NA 2022/2023 (KWA MILIONI) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BAJETI KUU YA TAIFA | | | | | BAJETI YA WIZARA 2022/2023 | | |
| MAELEZO | 2021/2022 | 2022/2023 | TOFAUTI YA ASILIMIA | 2021/2022 | Asilimia | 2022/2023 | ASILIMIA |
| BAJETI KUU | 37,411,370 | 41,063,915 | 8.1 | 40,092.5 | 0.1 | 33,425.9 | 0.08 |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 23,002,986 | 25,542,600 | 11 | 20,998.7 | 0.091 | 19,540.8 | 0.07 |
| MATUMIZI YA MAENDELEO | 14,977,615 | 15,521,300 | 3.6 | 14,714 | 0.098 | 13,831.1 | 0.08 |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Randama Fungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati.

iv) Uchambuzi wa Kamati vilevile umebaini kuwa wakati Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 8.1** kutoka **Shilingi Trilioni 37.9** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi Trilioni 41.06** mwaka 2022/2023; Bajeti ya Fungu 96 imepungua kwa **asilimia 16.6** kutoka **shilingi 40,092,525,240** mwaka 2021/2022 hadi **shilingi 33,425,991,000** mwaka 2022/2023;


v) Wakati Bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 16.32** mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023, Bajeti ya mishahara ya **Fungu 96** imepungua kwa **asilimia** 34 katika kipindi hicho hicho**;** na,

vi) Aidha, wakati Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.6,** Bajeti ya Maendeleo ya Fungu 96 imepungua kwa **asilimia 6.** (Tazama uchanganuzi kielelezo Na. 8)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla kwa mwaka 2022/2023 kuna ongezeko la Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hata hivyo ongezeko hilo haliaakisi ongezeko la bajeti katika Fungu 96. Uchanganuzi wa Kamati unaonesha kuwa, pamoja ongezeko la bajeti ya ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kuna upungufu wa bajeti ya Fungu 96.

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri ya uchambuzi huu ni kwamba, wakati Bajeti Kuu ya Taifa ikiongezeka, hali inayoleta mtazamo chanya wa maendeleo ya nchi kwa ujumla bajeti ya Fungu 96 inaendelea kupungua, hali inayoleta taswira hasi katika maendeleo ya Wizara hii.

**Kielelezo Na. 8: Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 96 Dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka 2022/2023 (kwa milioni)**




**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Randama Fungu 53 (Machi 2022) na Usanifu wa Kamati.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake na kubaini mambo mbalimbali inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

## 4.1 KUIBUA VIPAJI VYA MICHEZO NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Michezo imekuwa ikiliingizia Taifa mapato na kuifanya nchi ipate sifa kimataifa. Hata hivyo uibuaji wa vipaji kwenye michezo mbalimbali umekuwa wa chini. Kutokana hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

i. Serikali iweke mikakati ya kuibua vipaji katika michezo mbalimbali kuanzia ngazi za mitaa/vijiji ili

kuweza kupata vipaji vingi na kuongeza wanamichezo wengi kitaifa na kimataifa

ii. Serikali iweke mikakati ya kukuza na kuendeleza michezo shuleni katika shule za msingi pamoja na sekondari ili kuweza kubaini vipaji mbalimbali watakavyoonesha watoto kupitia mashindano ya michezo shuleni;

iii. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na wizara zote zinazohusika na michezo shuleni ziweke mkakati wa kuhusisha wadau mbalimbali binafsi wa michezo ili kuwashawishi kuwekeza katika michezo shuleni yenye lengo la kukuza vipaji vya watoto;

iv. Serikali iwekeze katika kufundisha wataalam maalum (walimu wa michezo na Maafisa Utamaduni) katika kuwa na ubobevu wa kuibua vipaji.

## 4.2 UWEKEZAJI KATIKA WATAALAM WA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,** ili michezo iweze kuwa endelevu na yenye kuleta faida ni muhimu kuwe na wataalam wabobevu wa michezo hiyo. Hata hivyo, kumekuwa na wataalam wachache sana wa michezo hapa nchini, kama vile mbio za marathon na michezo mingine ya Olympic. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ifuatavyo:-

i. Serikali iwekeze kwa kuwasomesha wataalam wengi wa michezo ili kuiewezesha tasnia ya michezo mbalimbali kuwa ya kitaalam na kibobevu;

ii. Serikali iendele na kuwekeza katika miundombinu ya kufundishia ili kuwezesha ufundishaji hasa katika chuo cha michezo cha Malya;

iii. Serikali iwahusishe na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika michezo kwenye shule na vyuo mbalimbali nchini ili kuongeza na kupanua tasnia ya michezo, utamaduni, na sanaa nchini itakayoongeza ajira kwa Watanzania.

iv. Kuhusu michezo ya Olympic Kamati inashauri kuwa Wizara iwatambue na kushirikana na Kamati ya Olympic Taifa ili kupata fursa mbalimbali zinazotolewa na Kamati hiyo na kushirikishana mambo mbalimbali yanayotakiwa na Kamati hiyo kwa manufaa ya Watanzania.

## 4.3 KUIMARISHA UTENDAJI KATIKA SEKTA YA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,** Tasnia za michezo, utamaduni na sanaa zinakua kwa kasi hapa nchini na zinawagusa idadi kubwa sana ya wananchi na hivyo kuwa muhimu sana kwa kuwa zinazalisha ajira binafsi nyingi. Na vilevile Sekta hizi ni mtambuka zinazogusa Wizara zaidi ya moja. Ili sekta hizi ziendelee kukua na kuleta tija stahiki kwa wananchi inahitajika kuwe na utendaji wa pamoja kati ya Wizara zinahusika na mambo ya michezo kama vile Wizara ya Ardhi, Wizara ya Tamisemi pamoja na Wizara mama ya Utamaduni Sanaa na michezo. Hata hivyo, kumekuwa na utendaji hafifu hapa nchini katika tasnia za michezo mbalimbali ya kisanaa na utamaduni. Hivyo, Kamati inashauri kuwa:-

i. Serikali iweke mkakati wa kuwianisha utendaji kazi wa Wizara zinazohusika moja kwa moja na utamaduni, sanaa na michezo ili kuleta utendaji bora wa tasnia hii hapa nchini;

ii. Serikali iandae kanuni mbalimbali zitakazoongoza Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo zitakazotumika na Wizara zote zinazohusika na michezo pamoja na wadau mbalimbali wa michezo ili kuwa na utekelezaji wa pamoja wa majukumu ya utamaduni, sanaa na michezo kwa maendeleo ya tasnia hizo hapa nchini;

iii. Serikali kuweka sera, sheria, kanuni na miongozo rafiki kwa ajili ya sekta hii.

iv. Serikali iweke mkakati wa kukutana mara kwa mara na vyama mbalimbali vya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kuweza kuondoa changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara katika vyama, mashirika taasisi mbalimbali za michezo, utamaduni na sanaa nchini, na hivyo kuendeleza tasnia husika kwa maslahi ya taifa.

v. Kutokana na migongano inayojitokeza mara kwa mara kati ya Serikali na wasanii kuhusiana na vyama na mashirika ya kimichezo, sanaa na utamaduni; Serikali iwaachie wasanii na wanamichezo wenyewe kusimamia vyama na mashirikisho yao na Serikali kubaki kuwa wasimamizi tu.

vi. Aidha, katika teuzi mbalimbali za wasimamizi vya vyombo vinavyosimamia Utamaduni, Sanaa na Michezo Serikali iteue watendaji wenye uzoefu na

ujuzi wa tasnia husika ili kuweza kuleta maendeleo sahihi katika tasnia hizo.

## 4.4 KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MICHEZO NCHINI

Ili kukuza michezo miundombinu ya michezo ni muhimu sana. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 imeweka bayana haja ya Serikali yake kuweka na kuimarisha miundombinu ya michezo, sanaa na utamaduni hapa nchini kwa nia ya kukuza tasnia hizo na kuleta ajira kwa Watanzania wengi. Vilevile kuliongezea taifa mapato. Hata hivyo miundombinu ya michezo hapa nchini bado ni dhaifu. Kutokana na hilo Kamati inaishauri kama ifuatavyo:-

i. Serikali iweke mikakati ya kujenga miundombinu mipya ya michezo na kuboresha iliyopo ili kuendeleza tasnia ya michezo, utamaduni na sanaa nchini;

ii. Serikali ishirikishe sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu ya utamaduni, sanaa na michezo nchini.

## 4.5 UIMARISHAJI WA UTOAJI WA MAFUNZO MBALIMBALI YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** ili kukuza vipaji vya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni muhimu kuwepo na shule na vyuo vya kutosha vya tasnia hizo. Tanzania kuna vyuo vichache sana vya tasnia hiyo. Kutokana na hilo Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali iweke mkakati wa kuongeza idadi ya vyuo vya utamaduni, sanaa na michezo nchini ili kuweza kuongeza idadi ya wasanii na wanamichezo mbalimbali walio wabobevu;

ii. Serikali ihuishe mitaala ya ufundishaji wa mafunzo mbalimbali ya utamaduni, sanaa na michezo kwenye shule na vyuo mbalimbali vya michezo nchini kwa idadi ya kutosha ili kuwezesha kukuza vipaji mbalimbali vya utamaduni, sanaa na michezo nchini.

**4.6 KUIMARISHA LIGI YA MPIRA WA MIGUU NCHINI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha ligi ya mpira wa miguu ya Tanzania kuwa miongoni mwa ligi kumi bora katika Bara la Afrika. Hata hivyo, uwekezaji kwenye ligi hii bado ni hafifu. Kutokana na sababu hiyo, na kwa kuzingatia umuhimu wa ligi hii kwa ajira nchini na mapato ya nchi Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

i. Serikali kuweka mikakati ya kuvutia wawekezaji kwenye ligi hii ili kuweza kuendelea kuifanya kuwa bora zaidi katika Bara la Afrika.

ii. Kwa kuwa Serikali imeondoa kodi za nyasi bandia kwaajili ya viwanja vyetu nchini, Serikali pia iangalie namna ya kuondoa kodi katika vifaa vinavyoendana na uwekaji wa nyasi bandia katika viwanja vyetu;

iii. Kamati inampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia timu za mpira wa miguu nchini. Kamati inaishauri

Wizara kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuleta tija ya kweli kama alivyokusudia Mheshimiwa Rais.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti - Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi kwa kushiriki vyema katika vikao vya Kamati ikiwemo cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samweli Hhayuma Xaday Mb - Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe

9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - MJumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
17. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe

26. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo – Mhe. Muhammed Mchengerwa (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndg. Dkt. Hassan Abass, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Said Yakub pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu ya Kamati Kiufanisi. Pamoja naye, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Francisca Haule, Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Emmanuel Mdidi na Ndg. Chacha Nyakega kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Utamaduni, Sanaa na Michezo - **Fungu 96** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 jumla ya **Shilingi 33,425,991,000.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

06 JUNI, 2022

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao wameingia sasa hivi; wageni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wachezaji wa *Serengeti Girls* ambao wamefuzu kwenda kucheza Fainali Kombe la Dunia Wanawake nchini India. Hongereni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni wengini ni wachezaji wa timu mbalimbali wakiongozwa na *Tembo Warriors. (Makofi)*

Wapo washiriki wa tuzo mbalimbali ambazo ni filamu, muziki na *Miss Tanzania* yuko ndani humu karibuni. *(Makofi)*

Wapo wawakilishi wamepata mirabaha mikubwa, wadau wote wa sekta ya utamaduni, wadau wa sekta ya sanaa. *(Makofi)*

Tunao vilevile washindi wa mbio ndefu za *marathon,* Ndugu Alphonce Nsimbu, Gabriel Geay na Emmanuel Giniki; hawa wameshinda *Boston Marathon* huko Marekani, hongereni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge wasimame kwa pamoja, wageni wa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wachezaji 26 wa Mpira wa Kikapu chini ya umri wa miaka 18 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania, wakiongozwa na Rais wa Shirikisho la Kikapu Tanzania ambaye ni Ndugu Michael Kadebe na hawa wanakwenda kushiriki mchezo wa vijana Kampala, Uganda tarehe 13 – 18 Juni, 2022. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge labda hamjui mimi nilikuwa mchezaji wa timu ya Taifa ya Kikapu. Tulicheza na wakina Majura, Zonga na Mollel. Sasa Wizara, Waziri uko hapa na Naibu wala hamtambui wala hamjui inaweza bajeti isipite hii. *(Makofi/Kicheko)*

Tuna wanafunzi 24 wa Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa *(MS TCDC)* kutoka *Usa River,* Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia moja kwa moja kwenye mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Ravia

Idarus Faina, ajiandae Mheshimiwa Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Riziki, ajiandae Mheshimiwa Festo Sanga. *(Makofi)*

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kunijalia kuchangia katika Wizara hii na mimi najielekeza katika mpira wa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFF* ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania ambalo limejipa madaraka ya kuongoza mpira Tanzania kama ilivyo katika Katiba yake Ibara ya Kwanza. Lakini katika Ibara ya 12 imeorodhesha wanachama wake, la kusikitisha Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar halijaorodheshwa katika orodha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akija Naibu Waziri nataka anielezee kwa nini *TFF* inavunja Katiba yake na Baraza la Michezo halichukui hatua yoyote. Kwa nini hadi leo Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake hawajafanya uchaguzi? Wakati Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake ni mwanachama halali kama alivyoorodheshwa katika Katiba Ibara ya 12. Hapa nisipopata maelezo ya kuridhisha nakusudia kuchukua shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi wa Machi, 2017 Chama cha Mpira wa Miguu cha Zanzibar kilipata uanachama wa *CAF,* lakini mwezi Julai, 2017 kiliondoshewa uanachama wake baada ya kukosa sifa za kuwa mwanachama wa *FIFA*. Mnamo mwezi Machi, 2021 *CAF* ilifanya mabadiliko yake ya Katiba Ibara ya 4(1) na Ibara ya 4(4); kwa mantiki hiyo Shirikisho la Mpira wa

Miguu Zanzibar haliwezi tena kuwa mwanachama wa *CAF*. Sasa naomba niishauri Wizara ikae na Baraza la Michezo (BMT) na Baraza la Michezo la Zanzibar (BMZ)... *(Makofi)*

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba nimpe taarifa mzungumzaji, wakati umefika sasa kurejeshwa kwa Ligi Kuu ya Muungano ili tupate wawakilishi halali wa vilabu Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ravia taarifa umeipokea?

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa naipokea na ninaiunga mkono kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naishauri Wizara ikae na Baraza la Michezo (BMT) na Baraza la Michezo la Zanzibar (BMZ); washauriane namna ya kubadilisha Katiba ya *TFF* na Katiba ya *ZFF* ili ziendane na uhalisia uliokuwepo kwenye Katiba ya *CAF* na Katiba ya *FIFA* ikiwezekana waangalie Katiba ya TOC. Iwapo hili halikufanyika Mwenyezi Mungu akitujaalia mwakani nitalizungumza tena na kuwaomba Wizara waruhusu kuwaeleza *CAF* na *FIFA* kwamba *TFF* na *ZFF* hawashirikiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nimepunguza naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Bulaya, sjiandae Mheshimiwa Riziki, sjiandae Mheshimiwa Festo, sjiandae Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi niwapongeze watoto wetu *Serengeti Girls* kwa kutufanya tutembee kifua mbele, tunakwenda kushiriki michuano ya dunia. Lakini pia nimpongeze Waziri na Naibu wake mmeanza vizuri tuna matarajio na ninyi, tupeni raha watanzania wanapenda michezo wanapenda wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mrefu sana tumekuwa tukitamani kwenye mpira wa miguu kusomeka kwenye ramani ya dunia, timu ya *Serengeti Girls* wametuonesha, kama Taifa Serikali inapaswa kuandaa bajeti stahiki ya kwenda kuwawezesha timu yetu kufanya vizuri, isiwe sasa utashi wa Rais peke yake, iwe *commitment* ya Serikali kwa ujumla. Hawa watoto wamejiwezesha sasa twende tuka-*invest* tuchukue Kombe la Dunia lije nyumbani. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitamani kwa wanaume wamefanya yao kwa kiwango chao, hawa mabinti tuwekeze, tumeona *commitment* ya timu za wanawake, dada zao kwa Afrika tuliona walivyofanya vizuri *COSAFA* kama sikosei wamefanya vizuri, hawa na wenyewe wanafanya vizuri. Hii inatukumbusha twende tuka-*invest* soka la wanawake kuanzia *level* za wilaya, kuanzia mashuleni na Mheshimiwa Waziri tumerudisha michezo

mashuleni kuna timu za wanawake za mpira wa miguu? Mpaka tulalamike wanawake ndio tuanze kusaidiwa, tuanze kupewa fursa kwenye maeneo mbalimbali. Sasa hawa wameonesha uwezo, wakati tunarudisha michezo mashuleni tusiangalie mpira wa miguu kwa wanaume peke yake, tuanze ku-*invest* kwenye mpira wa miguu kwa wanawake kwenye *level* za mashule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumeona *commitment* ya mtoto wa kike, sisemi kama wanaume hawafanyi vizuri, lakini hawa wamepewa nafasi na wameonesha. Leo tunatamba tutawaona timu yetu ya *Serengeti Girls* kwenye ulingo wa kidunia, sio jambo dogo, tumetamani hiyo nafasi. Sasa isiwe utashi wa Rais iwe *commitment* ya nchi. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wanafanya nchi zingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nami nampa taarifa Mheshimiwa Bulaya kwamba ni kweli anavyochangia kwamba Serikali lazima itenge bajeti sio utashi wa Rais. Mathalani tumeona wenzetu wenye ulemavu *Tembo Warriors* wanakwenda

kushiriki *World Cup,* lakini wana bajeti *constrained*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tuliona Rais aliwaita Ikulu wakati wameshiriki katika ile *level* ya Afrika, sasa wanakwenda *World Cup* lakini wana bajeti *constrained,* kwamba wangewatengea *specifically* kwa kuwa kuna bajeti kwa sababu ya kusaidia makundi haya inakuwa inasaidia sana. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kumpa hiyo taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko nilikuwa nasikia mipasho, mipasho ulikuwa unamaanisha nini? Mipasho ya nani? Umesema mipasho ya Rais sijakuelewa maana yako ni nini?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa Rais, lakini tuwe na bajeti kabisa imetengwa kwa haya makundi ambayo unakuta wamefikia *level* ya kwenda kwenye *World Cup* na kadhalika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya unaipokea taarifa?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipokea maana leo wanaweza wakawa na Rais ambaye ameona kuna jambo jema kwenye timu zetu, kesho akaja Rais mwingine ambaye sio kipaumbele, lakini tukiwa tuna mpango mkakati kama nchi itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie *netball* (mpira wa pete); hivi kama Serikali mpira wa pete tunauchukuliaje? Na ninashukuru leo viongozi wa CHANETA wako hapa, wamechaguliwa na niwapongeze, wameanza kujitambulisha. Lakini bado hatujawa na

mkakati wa kufufua *netball* kwenye nchi yetu, tuwawezeshe CHANETA, ni chama kidogo hiki hatuwezi kulinganisha na *TFF*. Hawana wadhamini, hawana fedha, watawezaje kwenda kuangalia vipaji mikoani na wilayani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaona je, na kwa sababu unahusu wanawake; tuanze kuuliza ni kwa sababu na wenyewe unahusu wanawake?

Mheshimiwa Waziri tuna wachezaji wazuri sana wa *netball* wako maeneo mbalimbali, hawapati fursa unakuta mpaka Wabunge waandae mashindano. Kuna muda mwingine mashindano yanakwama hawana fedha, tuiwezeshe CHANETA, tuanze sasa kuhamasisha na kuandaa mashindano mbalimbali *level* za wilaya ya *netball*. Tukarabati viwanja vya *netball* na kwenye mashindano yaliyopita hivi hivi kimkandamkanda tumepata wachezaji watatu kwenye timu ya Afrika. Je, tukiandaa, je, tukijipanga tutafika wapi? Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nadhani mmenisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye hotuba yako umezungumzia kiwanja cha mpira wa miguu hapa Dodoma. Nilikuwa nataka kujua hiki kiwanja kinahusiana na ule Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao zile fedha za huduma kwa jamii? Ndio nilitaka nijue na kama sio hiyo kwa nini? Kwa sababu na wenyewe upo na miongoni mwa fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 262 ukiwepo na ujenzi wa uwanja wa mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sio hizo je, huyu mkandarasi kagoma kutoa hizi fedha na kama Serikali tunasemaje? Nataka kujua hilo yaani kama sio na wakati

wameshaingia makubaliano na mradi unakamilika Juni 13 na hawajajenga uwanja, tunataka kujua je, huo uwanja utajengwa lini na makubaliano yanasema hivyo kuwa wajenge kiwanja cha michezo. Tumeamua kumuacha tu atuchezee tu kama nchi na tumeingia makubaliano, hilo pia nataka kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haraka haraka Baraza la Sanaa liko *dhooful-hali*, halina fedha. Ukiangalia mali tu za muda mfupi walizonazo milioni 116, madeni waliyonayo tofauti na mali milioni 350, mtaji wa kujiendesha milioni 234. Hawa ndio wanashughulikia tasnia nzima hii ya Sanaa, hawana Bodi hawa. Je, tumeweka hii sanaa yetu rehani na tunaona vipaji mbalimbali vya vijana wetu. Chombo chao kipo *dhooful-hali* kiasi hiki? Haya mlipanga kuwapa shilingi bilioni 1.1 mkawapa shilingi milioni 700 tu wajiendesheje? Sanaa imekua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama chombo chao tu hatukipi pesa, tuanze kulia kwenye timu za wanawake, tuanze kulia kwenye *netball,* tuanze kulia kwenye *football,* mpaka kwa wasanii ambao na wenyewe wanaliwakilisha vema Taifa letu? Hili suala la Bodi liko kwenye mikono yako, hawana Bodi huu mwezi wa nne, wako dhofuli hali, pesa hawana na ipo kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka huu, wapeni pesa Baraza la Sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Unga mkono hoja. Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Profesa Kitila.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA.** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetujalia kuwa na afya njema na kuwepo hapa. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuitangaza Tanzania duniani na *Royal Tour* imetua ndani ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, na Naibu wake Mheshimiwa Pauline Gekul kwa kazi kubwa wanayoifanya, Katibu Mkuu Ndugu Hassan Abbas na Naibu wake Ndugu Saidi Yakubu Majembe, vilevile niwashukuru BMT ikiongozwa na Ndugu Singo, anajua kabisa humu ndani anae Mama yake anaitwa *Double* Riziki, yeye ni *Single* mimi ni *Double*. Ninamshukuru Ndugu Neema Msita nae vilevile yuko BMT anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuwa hii Wizara ni Wizara nyeti ambayo ikiwekeza vizuri italeta ajira kubwa sana kwa vijana. Ninaipongeza timu yangu ya Tembo *Warriors,* hii timu ni ya vijana shupavu, wenye ulemavu, ambao walipambana mpaka sasa hivi na wamesaidiwa na Serikali katika uwekezaji wao mpaka sasa hivi Tembo *Warriors* wanakwenda katika *World Cup*. Ninamshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, akishirikiana na Mheshimiwa Rais walikuja kuwachangia uwanjani Shilingi Milioni 150. Ilileta chachu na hamasa kubwa kwa hawa vijana na ushindi wao sasa hivi tunaona unawapeleka katika *World Cup*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza *Serengeti Girls*. Haya yote ni makundi maalum, mkiyaacha makundi maalum mngefanya makosa makubwa sana, kumbe

makundi maalum yana uwezo mkubwa sana katika michezo. Leo nchi inapata faraja, inapata heshima kwa ajili ya makundi maalum ya walemavu na wanawake. Tujiulize, wanaume wako wapi, mimi naweka *question mark,* mtajitambua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, klabu zote sasa hivi Tanzania ziwashirikishe makundi maalum ikiwemo klabu kubwa kama Simba *Sports Club,* nasema tena, kama Simba *Sports Club.* Wawe na kundi maalum la walemavu na wanawake, na timu kama ile ya Yanga *Sports Club,* nao vilevile wawaweke wanawake na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninaposema ni ajira nataka niseme ni ajira kweli. Tembo *Warriors* sasa hivi nina vijana wanne wamepata u-*professional player,* wameajiriwa huko Uturuki. Tayari tumefanya wapate ajira na wajitegemee wenyewe, ninataka kuwataja kwa majina na tuwapongeze. Ndugu Khalfani Kihanga, ni kijana mlemavu kutoka Tabora lakini sasa hivi yuko Uturuki. Ndugu Ramadhani Chomelo, huyu kijana anatoka Kisarawe sasa hivi ni mchezaji Uturuki. Ndugu Frank Ngairo, anatoka Iringa, sasa hivi ni mchezaji Uturuki, Ndugu Shadrack Hebron kutoka Mbeya. Jamani kazi ya vijana ni kubwa sana kuwasaidia hawa, tukiwekeza zaidi hapa ina maana tutawatoa vijana wengi watakwenda katika *professional soccer,* watakuwa wanajitegemea wenyewe, hawategemei tena kusaidiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilichukuliwa watu wenye ulemavu ni watu wa kusaidiwa, Hapana! Watu wenye

ulemavu wanajiweza wenyewe. Twendeni pamoja tuka-*invest* kwa watu wenye ulemavu ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sanaa; kwanza niwapongeze wasanii, katika sanaa vijana wameonesha kazi kubwa sana, sasa hivi wanaitangaza Tanzania duniani katika *Royal Tour*. Maana yake katika kutangaza utalii, unatangaza katika maeneo mbalimbali, utalii katika utamaduni, michezo, mila na *culture* mbalimbali yote yanaingia katika *Royal Tour* na *Royal Tour* nyumbani kwake ndiyo hapa michezo na utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwataje vijana ambao sasa hivi unaona wanawika na kuitangaza Tanzania duniani. Namba moja ni Diamond Platinumz; Harmonize *(Konde Boy);* Ali Kiba, Zuchu, Ray Vanny na wasanii wengine ambao wanaendelea kuonesha nchi katika maendeleo makubwa. Hawa watoto wanaonesha usanii na wameajiri watu na kuajiri watu ina maana na wao wenyewe wanajitegemea katika kuipatia mapato makubwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini yangu ni kuwa tusimamame na hawa watu na haya makundi ili tuweze kuitengeneza Tanzania yenye kujitegemea kwa kupitia usanii pamoja na michezo inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Royal Tour;* mimi nakwenda kuitangaza nikiwa mmoja kati ya mabalozi wa utalii. Katika mabalozi wa utalii tunataka kuunganisha michezo na utaliii. Maana yake ni nini? Tunataka kuanzisha ndani ya mbuga zetu za wanyama waje wacheze mpira ndani ya Serengeti. Maana yangu ni kuwa ndani ya Serengeti na Ngorongoro kuna viwanja

vya mpira, tukalete timu kubwa ziingie pale. Zitakapoingia pale baadae tutakuwa tunajiuza wenyewe na soko letu liko pale, kuwa leo timu ya *Arsenal* wanashindana na Manchester ndani ya Serengeti. Hapo tutakuwa tumemuunga mkono na hii itakuwa na shughuli ambayo ni *very sustainable* na itatuingizia mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yale tutakubaliana kabisa, fungu maalum litakwenda kwa ajili ya makundi maalum ili baadaye wasihangaike na mambo ya kutafuta chakula, mavazi, hata nguo za kuvaa iwe ishu, kuombaomba. Hakuna kuombaomba, wenyewe hawa wanajiweza, tukiwatengenezea mfumo mzuri watakuwa wanaweza kujipatia mapato yao bila kutegemea kuombaomba na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi sana ya kuongea, kwa siku ya leo ninaomba na kuwaunga mkono kwa asilimia kubwa sana kuwasimamia hawa vijana. Vijana wanakwenda katika mapambano makubwa ya *World Cup* na tusibweteke sasa hivi ndiyo kipindi cha kusimama nao. Nashukuru Tembo *Warriors* wanaondoka kwenda *Poland,* wamepata nafasi maalum kwenda kujiimarisha kwa muda wa siku kumi. Ninaomba tufanye kila njia tuwasaidie hawa watoto katika kwenda kwao huko wasipate taabu ya chakula au ya matumizi, na Wabunge tuna jambo letu, tunasema hapa tunanyamaza lakini Wabunge kwa pamoja tumeungana kuwapenda watu wenye ulemavu na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeze vilevile Mheshimiwa Keisha, amekuwa ni *mentor wangu*, nae ameanzisha timu ya watu wenye ualbino nao

wanakwenda Kenya. Kutokana na mfumo huu, tukienda katika mazingira hayo Tanzania yenye maendeleo ya michezo na utalii na kuingiza kipato katika sanaa ya vijana inawezekana. Nawashukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao ni mabondia watatu, wageni wa Mheshimiwa Waziri, Ndugu Twaha Kiduku, karibu sana Bungeni. Ndugu Ibrahim Class na Ndugu Tony Rashid, karibuni. Mtawaona *Canteen. (Makofi)*

Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Profesa Kitila.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Michezo. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri inayoonesha mwelekeo mzuri kwenye sekta yetu ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa, niweze kuwapongeza Serengeti *Girls* kwa mafanikio makubwa ambayo wameyapata jana. Nimpongeze sana paka mweusi Bakari Shime pamoja na Edna Lyimo, kocha msaidizi, kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya. Kwa sababu ni muda mrefu hizi timu zimeandaliwa lakini leo Mungu ameamua kutupa nafasi ya kwenda kushiriki Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie kwenye mambo kama matatu hivi, jambo la kwanza ni suala la mfumo wa mchezo nchini kwetu na suala la maendeleo ya viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, jambo la kwanza ambalo ninajisifia kwamba Wizara imepata mwanamichezo hilo ni la kwanza. Wakati mimi nahangaika na Singida *United* wewe ulikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu, Haki na Hadhi za Wachezaji *TFF,* changamoto za wachezaji, changamoto za mpira, vyote unavifahamu. Kwa hiyo, ninafurahi kwamba tunakwenda kufanya kazi na mtu ambaye hii ni sehemu yake na ninafurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, mpira wetu una safari. Safari ndefu inaanzia kwenye mfumo wa soka letu la Tanzania, nitajikita sana kwenye soka. Mfumo wetu wa mpira wa Tanzania ambao tunaenda nao ni mfumo ambao wakati mwingine ni kama wa zimamoto, kwa sababu tunatamani sana tuwe na matokeo mazuri lakini hatujatengeneza *grassroots* nzuri za kuzalisha wachezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili leo tunaona Serengeti *Girls* wanakwenda huko, lakini mfumo wetu je, unawaandaa wengine kama hawa? Unakuta hauwaandai. Tunao majirani zetu ambao ni Watanzania wenzetu, Zanzibar. Zanzibar ndiyo watu ambao wana *the best model* ya mpira Afrika na Afrika Mashariki. Zanzibar wamechukuliwa *model* yao ya *soccer development* imekwenda kuwa *applied* Cameroon, Ghana na nchi nyingi, *model* ya *soccer* la Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa nini nazungumzia *soccer.* Katika Taifa lolote lile duniani lazima nchi ijipambanue nini inataka kwenda nacho. Leo nikiitaja Marekani ninataja *basketball,* nikiitaja Brazili

ninataja *samba, soccer,* nikizungumzia Afrika Mashariki nikiitaja Kenya ninaitaja riadha. Leo nikiitaja Burudi ninataja makocha. Makocha wa timu zetu za Ligi Kuu karibu zote ni Warundi. Wenzetu waliamua wawekeze kwenye makocha. Nikiizungumzia Rwanda ninazungumzia *basketball.* Leo hii ndiyo wana-*host basketball* kwenye Afrika nzima. Sisi Tanzania tunajiangalia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, tuna kitu cha kufanya kwa ajili ya Taifa letu. Sheria Na. 1 ya *FIFA* inazungumzia Taifa lolote lazima liwe na viwanja ndipo mpira uchezeke. Taifa letu kwenye suala la viwanja bado umekuwa ni mgogoro. Siku ile niliongea, mwaka jana, nikaomba hapa kwenye bajeti kwamba Mheshimiwa Rais atuondolee kodi kwenye nyasi bandia, akaondoa. Wakati ambao Taifa letu limepata *political will* ya Rais ni kipindi hiki. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mchangiaji ameongelea viwanja. Hapa Dodoma tuna uwanja wa kawaida sana, Uwanja wa Jamhuri, lakini ninapoongea hapa muda mwingi uwanja unatumika kwa maonesho na kufungiwa. Kwa hiyo, hata viwanja tulivyonavyo havitumiki kwa matumizi stahiki. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninapokea mchango wa Dada yangu ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, suala la viwanja limekuwa ni changamoto. *I ask myself, was it the intention* ya Mwalimu Nyerere kujenga viwanja nchi nzima, leo vigeuke magofu, vigeuke sehemu ambazo hazitumiki kwa ajili ya kuchezea, vimegeuka mazizi ya ng'ombe viwanja hivi, *was that the intention of* Mwalimu Julius Kambarage Nyerere? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama changu kina kazi ya kufanya. Nyerere alijenga viwanja kwa ajili ya michezo. *Political will* aliyonayo Mheshimiwa Samia kwa sasa kwenye michezo hadi akasema Mwanza kwamba nakielekeza Chama changu cha Mapinduzi kiweke nyasi bandia kwenye viwanja hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye ukurasa wako wa 62, unasema tunatenga bilioni 10. Bilioni 10 unatenga kwa ajili ya ukarabati, hatua ya kwanza, hatua ya pili kwa ajili ya ukarabati, hatua ya tatu kuweka nyasi bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nikuombe Ligi Kuu ya Tanzania haihitaji ukarabati viwanja, inahitaji kuwekwa nyasi bandia. Mwalimu Nyerere alitujengea viwanja akiwa na Watanzania milioni 20 tu, leo tupo milioni 64 tunashindwa kuweka nyasi bandia kwenye Taifa hili? Mheshimiwa Waziri, nikuombe, hizo Bilioni 10 fanya kazi ya kuweka nyasi bandia kwenye viwanja vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2027 tunakwenda ku-*host AFCON,* tuta-*host* vipi *AFCON* kwa nyasi hizi? Kwa sababu hawa watu ambao tunakwenda ku-host *AFCON* wataenda kuangalia viwanja vyetu miundombinu yake ikoje. Nikwambie mbinu ambayo wametumia Zambia, waliamua *CSR* kwenye migodi ndiyo itumike kuweka nyasi bandia kwenye viwanja vya Zambia. Tanzania tunayo makampuni mangapi nchi hii yanayochimba madini? Tuna makampuni mangapi nchi hii yanayowinda wanyama wetu? Tuna makampuni mangapi nchi hii wanatengeneza bidhaa zao na wanauza? *CSR* ingetumika kuweka nyasi bandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, *you'll be the game changer.* Nikuombe Kaka yangu, viwanja, viwanja viwanja. Viwekwe nyasi bandia. Hiyo Bilioni 10 ninajua huna, unakwenda kumuomba Mama. Nitumie nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Rais, Bilioni 10, achukue hata – kuna hizi fedha huwa mnarudisha mnaziita gawio – achukue hata gawio la *Vodacom* au Tigo au kampuni yoyote aweke kwenye viwanja, hapo tutakuwa tumemaliza tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, umezungumza hapa kwamba unakwenda kutengeneza ajira za vijana karibia 72,000 kupitia mtaa kwa mtaa. Hawa vijana utakwenda kuwapeleka wapi hatuna viwanja, hatuna *academy*. Mimi ninatoka Makete na hata hizi shule 56 za *academy* unakwenda kujenga, *my suggestion is* jenga kwa *zones. For instance,* kuna timu za Taifa zinakwenda kucheza maeneo ya baridi. Sisi tuna maeneo ya baridi ambayo ni Njombe, Makete na Mbeya, ungeweza kwenda kujenga kule shule moja kwa ajili ya kuwekea *camp* ili wanapokwenda kwenye mechi

huko wakatumia hapa nchini. Kuliko hela za kambi, hela nyingi, tunakwenda kutumia nje wakati tungeweza kuja kuweka maeneo haya. Hizi 56 ni nyingi, hata chache tu anza nazo kwa sababu safari ni hatua. Ninakuomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, wewe ulikuwa *TFF,* unajua wachezaji wetu walivyo na changamoto ya maslahi, *it's the time now. It's high time now* kwenye Taifa letu, lazima tuweke *salary scale,* lazima mishahara ya wachezaji wetu wa Ligi Kuu, wachezaji wetu wa Ligi Daraja la Kwanza, wachezaji wetu wa Timu za Taifa wawekewe kiwango cha mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, vijana wetu wanacheza kwa jasho na damu, wanalipwa laki mbili kwenye ligi kuu, wanalipwa laki tatu. Hawa vijana wanapata magonjwa wanalazwa mahospitalini tunaanza kuchangishana, lazima tuweke *salary scale* ya kwamba mchezaji wa ligi kuu lazima alipwe Milioni Moja *minimum. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna fedha nyingi sana kwenye mpira zinapotea, tungewasaidia vijana hawa ambao leo hii hapa kila mtu anawapigia makofi wakiwa wamekaa pale juu, lakini *do you know how much they get,* wanapata shilingi ngapi? Inawezekana hata laki mbili mfukoni hawana leo. Lazima kama Taifa tufanye mabadiliko ya sera zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, umeweka Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Soka 2022 - 2032 miaka kumi hapa, moja ya vitu ambavyo unatakiwa uingize ni maslahi ya wachezaji wetu.

Tutamshambulia Ndugu Karia lakini Ndugu Karia *is the best president,* amefanya kazi vizuri, anafanya kazi vizuri ndiyo maana leo wote tunajivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ninakuomba fanya mabadiliko…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sanga, kengele ya pili.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mwanamichezo, tuendelee kum-*support* ndugu yangu na Kaka yangu, *all the best. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu nyasi za bandia, Mheshimiwa *Chief Whip* na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI mko hapa; Mkurugenzi na Meya wa Jiji la Dar es Salaam waliahidi mbele ya Rais Samia kuwa watajenga uwanja wa nyasi bandia Sekondari ya Benjamin William Mkapa kwenye Jimbo la Ilala. Huu sasa ni mwezi wa tatu na nusu, hakuna kinachoendelea, hakuna tunachokiona na ahadi imetolewa na Meya na Mkurugenzi mbele ya Rais wetu Mama Samia. *(Makofi)*

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Michezo na *Chief Whip* uko hapa, hili suala lifuatiliwe kwa sababu michezo… na Ilala ndiyo kuna timu, mnazijua timu za Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, jiandae Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nataka nichangie pointi tatu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza sana, pale Jimbo la Ubungo kama unavyojua, tumejaliwa, tuna kila aina ya *talent* pale. Nataka nitumie nafasi hii niwapongeze vijana wetu, tuna timu pale za mpira wa miguu 25, karibu timu tatu kwa kila Kata, wanacheza na zimesajiliwa na *TFF*. Tunazo timu tisa za netiboli, wanacheza, pia pale tuna *champions,* wanamichezo wa ngumi, kila Kata, wako wengi. Tunao *champions* ambao wameshakuwa na majina Kitaifa, nataka niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza *champion* Selemani Kidunda wa kutoka *Jeshi Camp* kutoka Kata ya Mburahati. *Champion* Mfaume Mfaume wote mnamfahamu hapa, si mumpigie makofi, kutoka Kata ya Mabibo. Tunaye *Champion* Baiza Mazola kutoka Kata ya Mabibo. *Champion* Nasib Ramadhan kutoka Kata ya Mabibo. *Champion* Iddi Pialali wote tunamfahamu huyu kutoka Kata ya Manzese. Tunaye *Champion* Pengo kutoka Kata ya Manzese. Hawa ni vijana ambao wanatupa furaha sana kwa sababu Wizara hii moja ya jukumu lake ni kuleta furaha katika nchi na hawa vijana wanatupa furaha sana Dar-es-Salaam na katika kata yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wanamuziki wakubwa, wazito katika Jimbo la Ubungo, nikianza na Dulla Makabila, anafanya vizuri sana. Shoko Mwamba anafanya vizuri sana. Madee Ali, kijana yule, Ney wa Mitego, Tundaman, Segu Segumbo, Dogo Dulla, Amigo, Bayo Fundi Ubungo na Mariam wote kutoka Ubungo. Wanaleta furaha katika Mkoa wa Dar-es-Salaam.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Wewe uliomba ruhusa kwenda hospitali, nenda hospitali. Hakuna taarifa, endelea. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hoja yangu ya pili.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester kaa chini wewe ni mgonjwa. Sasa usije ukazungumza vitu hapa. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni ombi. Nataka nichukue nafasi hii, Mheshimiwa Ester ugua pole, nataka nitumie nafasi hii nilete ombi. Pale Jimbo la Ubungo na hususan Kata ya Manzese na Sinza tuna uwanja wa kihistoria, uwanja unaoitwa *TP*. Huu ni uwanja ambao upo mpakani mwa Kata ya Manzese na Kata ya Sinza, Mtaa wa Chakula Bora upande wa Manzese na Mtaa wa Sinza E upande wa Sinza, ni uwanja muhimu sana na umuhimu wake pia ni wa kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Yanga haijaanza mwaka 1935, mwaka 1920 mpaka 1926 ilikuwa inaitwa *Young Boys* na ilianzia Manzese kabla ya kwenda Kariakoo, walikuwa wanachezea uwanja huu wa *TP*. Baada ya kwenda Kariakoo ndio wakaanza kuitwa *Young Africans* na badaye mwaka 36 baada ya mambo kuwa mabaya walikuwa wanashindwa sana ndio wale

jamaa wakajitoa wakaondolewa wakaenda wakaanzisha Simba. Kwa hiyo, Simba *basically* ni timu ambayo inatokana na Yanga, walikuwa ni waasi baada ya kufukuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana maana haka kahistoria watu hawakaelewi, lakini ilianzia Manzese, ikaenda Kariakoo, *1935* ikawa ni *Young Africans, 1936* wakaenguliwa baadhi wakaanzisha Simba, wakabaki Yanga kupigania uhuru, kwa hiyo, hili ni jambo la msingi. Sasa ule uwanja wa *TP* ni muhimu na tunahitaji kwa kweli kwa ajili ya…

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kitila Mkumbo, Kiti kikikuomba ushahidi wa haya mambo unayo?

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio ninao, nitaleta. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, endelea.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaleta na *paper* zipo zimeandikwa, nitaleta. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aniangalie katika jambo hili. Kwa historia hii naomba anipe nguvu uwanja wa *TP* tuutengeneze, iweze kufanyika michezo. Sisi pale ni maarufu kwa suala la *Ndondo Cup* analifahamu, atatusaidia sana kwa *Ndondo Cup*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, kama nilivyosema awali, sisi maisha kisaikolojia, maisha ni nini?

Ni mchakato wa kutafuta furaha, ndio maana ya maisha. Kwa hiyo, jambo lolote ambalo linaleta furaha ni muhimu likaungwa mkono. Sasa juzi nilikutana na, pia suala la furaha Mheshimiwa Waziri ni kazi yake, moja ya kazi ya msingi ya Wizara hii ni furaha. Nimeona hata kwenye *speech* yake ameiweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekaa na Daktari mmoja anafanya kazi katika moja ya hospitali za Serikali Dar-es-Salaam, yeye anakaa Kata ya Makuburi, amekuja kunilalamikia anasema karibu kila siku mara tatu kwa wiki anakamatwa. Kwa sababu gani? Yeye anafanya kazi *mortuary,* usiku anaondoka asubuhi. Kabla hajaenda nyumbani, ananiambia, yeye hunywa bia sita asubuhi, lakini kila akienda kunywa bia sita pale karibu na nyumbani kwake kwenye baa anakamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikakutana pia na wafanyabiashara, nilikuwa na kikao nao Dar-es-Salaam. Wakaniambia kwamba, Dar-es-Salaam moja ya lalamiko lao ni kwamba, hawaruhusiwi kufungua baa asubuhi na mwisho saa sita, kwa hiyo, inamaanisha kwamba, nikasema tatizo ni nini? Nikagundua kuna sheria ya *The Intoxicating Liquors 1968,* kile Kifungu cha 14, kimepangia watu muda wa kufurahi kwamba, hakuna kufurahi mpaka saa 6.00 mchana na mwisho wa kufurahi saa 6.00 usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wewe unafahamu majiji yote duniani hufanya kazi saa 24. Hii habari kwamba, watu asubuhi wasifungue biashara, wasifungue baa, wasifurahi mpaka saa 6.00 mchana ni sheria ya kizamani na hii sheria ilitungwa *1968* mwaka mmoja baada ya Azimio la Arusha ili watu na wakati huo nchi

ilikuwa ni nchi ya wakulima na wafanyakazi, ilikuwa wanatakiwa wakalime mashambani, wakafanye kazi maofisini. Sasa huko tulishaondoka, hii ni nchi ya wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara, wanamichezo, wanaburudani, wote kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, hii sheria inazuia furaha ya nchi. Aiangalie tuibadilishe ili watu wawe na uhuru wa kufurahi wakati wowote maadam wanazingatia sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi...

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa. Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kumpa Taarifa tu rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Kitila kwamba, furaha haiko aina moja, ziko aina nyingi sana za furaha. Kama hawawezi wakaipata furaha inayotokana na kunywa pombe, basi wapate furaha inayotokana na vitu vingine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitila.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimtaarifu Mheshimiwa Askofu kwamba, kabla hajaziponya hizo roho, lazima tuponye miili ili apate roho. Kwa hiyo na kwa sababu hiyo, naomba kwa heshima na taadhima nisipokee Taarifa yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *so,* namalizia kwamba, *on a serious note* na hii baadaye Wizara ya Fedha itamhusu kwenye bajeti yake, Dar-es-Salaam Jiji la biashara, hawawezi kupanga muda wa kufanya biashara. Dar-es-Salaam watu watafanya kazi *24 Hours,* mtu anafanya kazi usiku ana haki ya kwenda kufanya burudani asubuhi. Hii tuiangalie sheria hii ibadilishwe ili tufanye biashara *24 Hours* tukusanye kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nichukue nafasi hii kabisa kwa dhati nimpongeze sana Mheshimiwa Mchengerwa. Nampongeza kwa jambo moja tu, hii Wizara ameipa hadhi sana, ameipa heshima, yaani ni Waziri ambaye yuko *very proud* kuwa Waziri wa Michezo, *this is very good.* Ameifanya kwamba, kumbe kila mtu anaweza akatamani kuwa Waziri wa Michezo, nampongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, wajiandae Mheshimiwa Khamis Taletale na Mheshimiwa Khadija Shaban Taya.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Timu yetu ya *Serengeti Girls* kwa ushindi waliopata kwa kuwakilisha kwenye Kombe la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza sana Wizara hii ya utamaduni kwa kazi kubwa wanazofanya katika kuhakikisha sanaa, utamaduni,

michezo vinaleta tija katika Taifa hili, lakini pia vinaleta tija kwa wanamichezo na wasanii wenyewe. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhati kabisa kwa kupenda na kukuza michezo na vipaji vya wanamichezo mbalimbali, kuvithamini na kutaka vipaji hivyo viendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza na mchango wangu katika eneo la lugha ya Kiswahili. Napongeza kwanza taasisi zote zinazojihusisha na uendelezaji na ukuzaji wa Kiswahili, zikiwemo BAKITA, BAKIZA, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza Kiswahili ambapo kwa mchango wao huo umefanikisha leo Kiswahili kuwa lugha inayotumika kwa kazi kwa Afrika, lakini pia ni lugha ambayo inatumika kikanda na kimataifa. Nawapongeza sana. Kiswahili ni bidhaa, Kiswahili ni ajira, lakini Kiswahili ni utambulisho wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya Kiswahili imesheheni maneno mengi ambayo tumetohoa na mengine tumeazima kutoka lugha mbalimbali. Kiswahili chetu hiki kimeunganishwa na kutohoa maneno mbalimbali ikiwemo Kiingereza, Kijerumani, Kiarabu, Kiajemi, Kichina, Kijapani, Kigiriki, Kihindu ambapo Kihindu kuna Kihindu, kuna Punjab, kuna Hindu kuna Ghujrat yote haya yapo katika Kiswahili, tumetohoa na kuazima haya maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutohoa na kuazima huko Kiswahili hiki kimetohoa kwenye vyakula, wanyama na kwenye mambo mbalimbali. Kwa mfano, nataka kutoa mifano michache tu, kwenye lugha ya

Kihindi tumetoghoa chapati, fenesi, bagia, kachori, achari, karakana, madhubuti, tamasha, kitabu, pesa, meza, bangili, gari na mengineyo. Kiarabu tumetohoa ghali, amiri, dhambi, ridhaa, kasi, dhaifu, nafsi, kalamu, hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kwenye Kijerumani tumetohoa neno soli. Kwenye Kigiriki tumetohoa neno lami, kwenye Kireno tumetohoa neno gereza, dama, lakini kwenye Kiajemi tumetohoa bahati, bahati nasibu, jambazi, balungi, hili balungi ni tunda. Kijapani tumetohoa judo, kichinchiri, kichinchiri maana yake ni kitoto kidogodogo kinachokuakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno tumetohoa ambayo yanaingiliana na lugha nyingine. Mfano, soko Kiswahili lakini Kihindi ni *sok* na Kiarabu ni *suuq*. Kiswahili dua, kiarabu dua, kihindi dua. shukurani Kiswahili, shukria Kihindi, lakini shukra Kiarabu na mengi mengineyo kama madarasa, madras na madrasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kujenga hoja, kwenye Kingereza tumetohoa penseli, *pencil,* baskeli, *bicycle,* ringi, *ring* na mengi mengineyo, hayo ni machache tu. Ninachotaka kusema tunataka kutumia Kiswahili kwa kuunganisha na kuongeza utalii nchini. Utalii nchini kwa kutumia Kiswahili, wanaotaka kujifunza Kiswahili wanakuja nchini na wengine wanataka Walimu wapelekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja yangu ni hapa, kilio huanza mfiwa ndipo na wa mbali akalia, lakini pia, kibaya chako si chema cha mwenzako, tutukuze Kiswahili chetu. Kiswahili ni hazina, Kiswahili ni rasilimali ya nchi,

tukikitumia vizuri, tukikiendeleza vizuri tutapata tija kubwa kupitia lugha yetu ya Kiswahili duniani na kuitangaza nchi yetu ya Tanzania tukiunganisha na kutangaza utalii wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninachotaka kusema katika kukiendeleza Kiswahili, tujitahidi basi tutumie lugha nyepesi, lugha ambayo inaweza kusomeka, kuandikika na kujifunza. Nimetoa mifano kwamba, hapa tumetohoa, mfano neno *television* linatumika karibu ulimwenguni kote *television;* Sudan *television,* Comoro *television,* Kifaransa *télévision*. Sasa maneno kama haya, tujaribu ndio tunataka tutumie maneno yetu ya kibantu, maneno yetu ya asili, lakini tutumie maneno mepesi kwa sababu kuna maneno tunayatumia sasa hivi hata mimi Mswahili nafikiri vile kitu gani vile? Nafikiri, nikishindwa natumia lile la Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lugha isiwe ngumu. Zamani lugha yetu inasema lugha nyepesi, mwananchi au wageni wanaifahamu kwa urahisi zaidi. Kwa hivyo, tuendeleze, tutohoe pia maneno yetu ya kibantu, lakini mengine ambayo ni magumu sana tumeyasahau, sitaki kuyataja hayo maneno yanajulikana, magumu. Unakifikiri kitu mara tatu, vile nini, vile nini? Hata ukilipata. Sasa hapa tuboreshe Kiswahili kiwe chepesi lugha inayoweza kuzungumzika ili kujenga ule uimara na watu kuja kujifunza kwa wingi Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kiswahili tunataka kiwe kama ajira, nashauri vijana wetu wajifunze lugha zaidi ya mbili kwa maana ya Kiswahili, achanganye Kiingereza na Kifaransa au Kiswahili, Kingereza na

Kihispania, ili lile soko la ajira la ukalimani, soko la ajira la kusomesha, liwe linapatikana kwa urahisi kwa vijana wetu kujua lugha zaidi ya mbili au tatu. Hiyo itasaidia zaidi kukitangaza Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu napongeza sana wasanii hapa nchini kwa kazi kubwa mbalimbali wanazofanya kuhakikisha sanaa inakua. Nashauri Serikali iendelee kuinua na kuibua vipaji vipya na kuviendeleza, lakini katika kuinua vipaji vipya hivyo tuangalie na sheria hasa kule kwenye halmashauri kuna sheria nyingi zinakandamiza wasanii wasije juu kwa sababu ya kodi na ushuru mkubwa au malipo makubwa ya vibali kwenye halmashauri. Msanii ndio kwanza anataka kuanza anaambiwa lipa 70,000, ndio kwanza, atajitangaza vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke muda maalum, kikundi kimeshakua, baadaye tuwatoze hizo kodi au tuwatoze hizo tozo, ili tuibue vikundi, kuwe na motisha fulani ya kuibua vile vipaji tuviendeleze. Vinaibuliwa vingi, lakini vinaishia hukohuko chini, wakati mwingine ni sheria tu kandamizi ambazo hazitaki kuinua vipaji vya wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea hapo sekta ya utamaduni. Utamaduni ni mpana sana, ni mpana kwa maana binadamu anapozaliwa anazaliwa kwenye utamaduni, analelewa kwenye utamaduni, anakuwa kwenye utamaduni, harusi ni utamaduni, mpaka anazikwa binadamu anazikwa kwenye utamaduni kutokana na eneo husika na nchi husika. Kwa hivyo, suala la utamaduni ni utambulisho mkubwa wa nchi,

tunataka kuliendeleza ili liendelee kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kuwapongeza wasanii, kuna suala moja linajitokeza, haki miliki. Wasanii wetu haki miliki zao bado zinadhulumiwa, kwa maana kuna nchi au mataifa wanatumia nyimbo zao wanazibadilisha lugha, lakini mdundo, muziki ni uleule, wimbo ni uleule na wanapata fedha nyingi kupitia hizo nyimbo zetu za Watanzania wetu wakiwemo akina *Diamond* na wenzake, tulinde haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kuna wasanii wa zamani wa nyuma wameimba nyimbo nyingi, lakini zinaimbwa na sasa hivi, anaonekana mmiliki ni yule wa sasa hivi, lakini kumbe ile nyimbo ni ya zamani na imetungwa zamani. Tuweke kumbukumbu wimbo huu umetungwa lini? Muimbaji alikuwa nani? Aliyetia sauti ni nani? Aliyetunga shairi ni nani ili kizazi na kizazi kiweze kujua wimbo huu ulikuwa ni wa nani? Hata kama utaimbwa tena mara ya tatu, mara ya nne, basi mmiliki awe na haki zake kwa uhalisi wake anapata zile kutokana na jasho lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa tunaipenda. Tunasikia wasanii mara wanafungiwa, hivi, nataka niongee kidogo tu; mimi niliwahi kutumikia chombo cha sanaa, niliwahi kuwa Naibu Mkurugenzi Idara ya Sanaa Zanzibar, tulikuwa na chombo kinaitwa *Sensor Board,* muziki, shairi lolote kabla halijatoka linakwenda kwenye *Sensor Board* kwanza. Hii inaifanya taasisi ya muziki ule wasipate hasara baadaye ya kuja kufungiwa muziki wao, lakini inataka mashirikiano ya pamoja kati ya wasanii na hivi vyombo. Wawe wakweli na wa wazi kupeleka

mashairi yao, maudhui yao, ili wasije wakafungiwa na kupata hasara isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yanaepukika. Tujitahidi kuwaonesha sanaa zenye kupendeza, lakini …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili. Mheshimiwa Khamis Taletale.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, wajiandae Mheshimiwa Khadija Shabani na Mheshimiwa Getere.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa dua, "*Rabbi shrahli swadri, wayassrli amri, wahlul-uqdata min-lisaani yaf-qahu qawli*".

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kuomba hii dua ni kumwomba Mwenyezi Mungu ausimamie ulimi wangu kwa yale ambayo naenda kuyaongea leo. Sababu ya kuomba hii dua kumwomba Mwenyezi Mungu aisimamie hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi leo ya kuongea, lakini nitaanza na hoja zangu tatu. Kabla ya kuanza kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Nampongeza kwa kile

ambacho anakifanya Morogoro Kusini Mashariki, ndio maana nimekuwa siwezi kuchangia Wizara yoyote naona mambo yanakuja, mambo yanakwenda kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na BASATA. Ninaposema nianze na BASATA, naanza na BASATA. BASATA ni chombo cha kusaidia wasanii, lakini bahati mbaya BASATA imekuwa Polisi wa Wasanii. Nampongezae Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, amekuwa kila siku akizungumza nami. Nina miaka 20 kwenye *music industry,* najua nini kinaenda vizuri, na nini kinaenda vibaya. Leo hii tuongee ukweli, BASATA hawana utaratibu wa kuwapa elimu wasanii, hawana utaratibu wa kutoa semina kwa wasanii, lakini BASATA wana utaratibu wa kufungia nyimbo za wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sanaa; watu wanatulia ku-*create* kitu asubuhi, mchana, halafu wewe jioni unaziba, unazuia eti kwa sababu ya sheria ambayo msanii haijui. Niseme leo, sijui kama sheria yako itaniruhusu kuimba. Nitaimba hapa Waheshimiwa Wabunge waitikie! Mamaa Amiinaa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiimba hii nyimbo kama mtu akiitikia vile inavyopaswa, basi BASATA walikuwa wanatakiwa waitazame hii nyimbo na waifungie. Hawawezi kufanya hivyo kwa sababu hajaimba msanii ambaye kwao hawana maslahi naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Mheshimiwa Waziri roho yake ni nzuri, naweza kutafsiri baadhi ya wafanyakazi wake, watumishi wake wana roho mbaya. Hawa vijana wanahangaika ku-*create* vitu, kama

tunakubali kuipeleka *Tanzania* katika *international level*, hatusemi kwamba tunavunja utaratibu wa sheria, hatusemi kwamba tunakwenda kuvunja utamaduni wetu, lakini wewe uko *busy* kuwaza huyu kakoseaje umfungie; mpe elimu, umeshindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Ummy nikampa hii nyimbo na kiitikio chake, alisikitika sana, lakini leo hii tuko na BASATA ambao wako *busy* tu kuangalia kafanyaje? Tumfungie! Kafanyaje? Tumfungie! Tuangalie hiki kitu, kama tuna nia ya kukuza *industry* ya Sanaa, tuangalie tunawezaje kuwapa elimu wasanii. Hakuna aliye juu ya sheria, hakuna ambaye anayetaka kufanya jambo kwa ajili ya kujifurahisha yeye.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda tu kumpa taarifa mtoa hoja kwamba, BASATA imekuwa ikiwashika mashati vijana wa Kitanzania na kuwavuta nyuma. Nikitolea mfano msanii kama *Gigi Money,* ni kijana ambaye alianza kusimama, lakini hawatoi elimu ya kuwasaidia wasanii bali kuwavuta nyuma. Angalia sasa hivi *Gigi Money* badala ya kwenda mbele tunamwona tayari ame-*drop*. Tunategemea BASATA iweze kuwasaidia wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake naipokea kwa mikono miwili kabisa, maana nilikuwa namwangalia nani anatoa taarifa? Maana leo nimesema atakeyetoa taarifa awe na *experience* ya muziki kama niliyonayo mimi humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiizungumzia BASATA unazungumzia vitu ambavyo… Aah, *Alhamdulillah!*

Mheshimiwa Naibu Spika, niachane na BASATA, nahamia *COSOTA,* maana naweza nikaongea kuhusu BASATA halafu nikaumia roho vile vile. Hii taasisi ya *COSOTA* kama siku utaipelekea TAKUKURU pale unafunga wote wale. Natoa mfano, nina msanii wangu hamna asiyemjua hapa anaitwa Kassim Mganga, anatokea Tanga, hakuna asiyeimba nyimbo zake kwenye msimu wa harusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kassim Mganga unamwita, unaenda kumpa shilingi 50,000 halafu unaenda kumwita Lulu Diva unampa shilingi 550,000 halafu umetumia vigezo gani? Kuna utaratibu gani ambao unatumika *COSOTA* kwenye kugawa mirabaha? Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, ametoa gari bovu uwani, kaliweka barabarani. Hii *COSOTA* ni gari bovu liko barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naondoka na Shillingi ya Mheshimiwa Waziri, nashika mshahara wake, atafuata Shilingi Kusini Mashariki namuahidi *brother* wangu. Kama hajaja na hoja ya kubadilisha utaratibu wa *COSOTA,* wasanii wale wanaimba; kuna msanii kama Mzee Yusufu? Nimemwona pale juu, ni mwanamuziki anaimba,

anaandika, anapata haki yake vizuri. Huwezi ukamkusanyia Mzee Yusufu Shilingi milioni tano! Ana *worth* ya Shilingi milioni tano? Tuongee ukweli! Hakuna utaratibu wa kugawa fedha kwa wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie wanatumia utaratibu gani kwenye kuwapa pesa wasanii? Nimeona kuna baadhi ya wasanii wanawapa pesa kwa sababu ya ukubwa wao wa *Instagram* na makelele tu. Sitaki kuongea mengi, mimi ni Kiongozi wa Taasisi ya Wasafi, hakuna msanii mmoja aliyepewa hata Shilingi kumi anakwenda kusimama pale Kiongozi wa *COSOTA* eti ooh, hawajakusanya nyimbo, hawajasaini kwa sababu ya redio fulani. Kama unapewa kitu, taasisi ambayo inasimamiwa na Serikali, usiegemee upande mmoja, ongoza kama kiongozi. Kuna redio zipo huko Morogoro Vijijini na wapi, zinapiga nyimbo za Wasafi, upo kwenda kuchukua hela? Leo hii eti unakwenda kumpa msanii pesa, Madii unampa shilingi 250,000. Mwaka 2021 watu kibao walikufa na Corona, hakuna nyimbo iliyoimbwa kama *"Kazi Yake Mola",* tuwe wa wazi. Unakwenda kumpa Madii shilingi 250,000 kwa vigezo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, nitaendelea kuishika Shilingi ya Mheshimiwa Waziri mpaka nijue utaratibu gani unakwenda kuufanya kwenye hii *COSOTA*? Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye hili tulisimamie kwa sababu *copyright* haisimami kwenye muziki tu. Mimi ni *publisher,* leo hii nasimamia *music,* kesho na keshokutwa watoto wangu watakula nini? Si ndiyo *copyright* inasimama kwenye kila eneo. Hakuna utaratibu mzuri! Mheshimiwa Naibu Waziri ukijiona huna jibu kwenye hili, ujue huna Shilingi ya Hamis Shaban Taletale kutoka Kusini Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kitu kizuri kama msanii anapofanya jambo akasifiwa. Hawa vijana wanahangaika kwenye kutengeneza vitu vyao mimi nimpongeze sana kuna dada mmoja anaitwa Lamata *movie* ilikufa nchini, tuwe wawazi. Yule dada amepambana; kuna kipindi kinaitwa Juakali, kinakwenda vizuri sana, lakini nikwambie, yule binti kama atataka kwenda kuigiza Polisi, haitawezekana. Kama atataka kwenda kuigiza Jeshini, haitawezekana kwa sababu ya utaratibu wa Wizara tulioufanya. Kama tunataka kuwasaidia hawa wasanii, tuwasaidie tusione hii ni sehemu ya wahuni. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Taletale, hii ni kengele ya pili.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Maneno yako ni muhimu, na juzi nimesema hapa kwenye kiti kwamba tunasema Rais anaupiga sana, ninyi mnaupiga wapi? Haya ndiyo mambo ya kuyafanya. Siyo kila kitu Rais, mtamsumbua, ana mambo makubwa ya kufanya. Hata haya ya wasanii aingilie yeye jamani! Naibu Waziri na uwezo wako na uzuri wako, yafuatilie haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, jiandae Mheshimiwa Getere.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** *Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa leo afya njema ya kusimama katika Bunge lako tukufu kuzungumza masuala ambayo yanaenda kustawisha maisha ya vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais sana na siyo kinafiki. Tuzungumze ukweli, *Royal Tour* siyo kitu ambacho kinaenda kunufaisha utalii peke yake, *Royal Tour* inaenda kunufaisha wasanii wa Tanzania hii. Mama alipoenda Marekani, alitembelea *Paramount Studio.* Katika hii studio amezungumza na watu masuala ya kuwekeza Tanzania kupitia hiyo hiyo *Royal Tour*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama alipoenda *Los Angeles* amekutana na wadau zaidi ya 15. Hawa wadau wamejadili mambo tofauti tofauti, wanakuja hapa Tanzania na amezungumza nao kabisa kuhusu fursa zinazopatikana hapa nchini. Leo hii mama anatuletea wasanii wakubwa ambao wanaweza kutuletea maendeleo katika hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachana na hayo, mama pia katika mtu ambaye ametengeneza hii *Royal Tour* anaitwa John, yule jamaa *Producer,* amekuja Tanzania, amezungumza na wasanii, amefanya kikao na wasanii tarehe 29 Aprili, ameona changamoto gani ambazo wanapitia na kadhalika ili waboreshe kazi zao katika maeneo tofauti tofauti. Mama anaupiga mwingi

sana. Jiulizeni sisi tunaupiga wapi? Umeuliza swali zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza timu ya *Serengeti Girls* na pia niipongeze timu ya *Tembo Warriors*. Pia naomba niwaambie kwamba tunahitaji timu za makundi maalum ziendelezwe vizuri. Tunahitaji timu hizi za makundi maalum waanze kuwa na maslahi mazuri, kwa sababu katika upeo wangu sasa hivi naanza kuona hizi timu ndiyo zinazotutangazia nchi yetu vizuri, na sasa hivi tumesaini mkataba wa masuala ya usawa wa kijinsia. Tunaomba maslahi ya hawa wanatimu ambao wanaenda kwenye kutuwakilisha katika nchi nyingine huko, maslahi yawe sawa na hizi timu za wanaume ili tuweze kutimiza masuala ya usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakienda kwenye *hotels,* wasifikie huko uchochoroni, Hapana. Waende kwenye hoteli, kama ni *Four Stars* au *Serengeti Boys* au *Taifa Stars* nao pia waende huko. Kuwe na bajeti nzuri ambayo itasaidia hawa vijana, kwani watajitoa sana na wanaumia sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala hili sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna timu hizi za watu wenye ulemavu, tunazisaidia vipi? Naomba nimwambie leo Waziri, kuna timu imekuja hapa *Tembo Warriors* tayari wanaenda kuwakilisha Kombe la Dunia, lakini kuna timu ya *Albinism Sports Club* ambao nao wanaenda Kenya keshokutwa hapa kwa ajili ya kuwakilisha nchi.  Sasa tunazisaidiaje hizi timu? Tutafute namna yoyote ile ambayo Wizara na Bunge lako Tukufu zisaidie hizi timu ili ziweze kwenda kuwakilisha michezo hii ili tuweze kukuza hii nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuhusu masuala ya muziki pia leo. Kaka yangu hapa Mheshimiwa Babu Tale amezungumza sana kuhusu BASATA na *COSOTA*. Naomba niwaambie jambo moja, msanii mpaka mnamwona amefika pale, amepitia mambo mengi sana; anapitia changamoto nyingi sana. Ukizingatia kwamba huyu msanii hana pesa, hana *capital* ambayo inamwezesha kufanya hizi kazi zake. Kwa hiyo, wanapitia kwenye changamoto nyingi hapa katikati kiasi kwamba zinaondoa yale maadili ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii msanii ameshakuwa hivyo: Je, Serikali mnafanya nini? Kazi yenu kubwa ni kutoa elimu siku hadi siku ili hawa watu tuweze kuwa-*shape,* wajue sasa kwamba wanaenda kuwakilisha nchi. Tuwa-*shape* wawe wasanii wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukisema tu msanii amekosea, amevaa vibaya, hujamtengeneza au hujamkuza vizuri au hujamlea vizuri, hujampa elimu vizuri, unamfungia kazi yake. Hivi mnafahamu tunatumia gharama kiasi gani kutengeneza hizi video? Hivi mnafahamu tunatumia muda kiasi gani ku-*invest* kwenye hizi *videos*? Hivi mnafahamu vyote hivi? Hamfahamu! Sisi ndio tunafahamu ndiyo maana leo hii tulipambana kuja humu Bungeni tuwazungumzie wananchi wetu waliotuleta humu Bungeni, lakini tuzungumze juu ya masuala ya sanaa ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii umemsikia pale Mheshimiwa Riziki Lulida hajaniita Mheshimiwa Khadija, ameniita Mheshimiwa Keisha. Hilo ndiyo jina ambalo

linatambulika katika nchi hii. Hili jina halikuja hivi hivi tu, limekuja kwa juhudi.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwa mwongeaji kwamba mambo yote yanayotokea, kwa kweli wanatakiwa Wizara hii pamoja na yote waelezee kwamba wameshawatafutia masoko ya kazi zao wasanii hawa katika maeneo au nchi ngapi? Watupe idadi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taarifa hiyo.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Sijaielewa taarifa. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba wasanii tunatumia muda mwingi sana kutengeneza majina yetu ili tufike pale tunapopataka. Tunatumia *investment* ambazo hatujui hata namna ya kuzipata lakini tunazipata. Sijui mnanielewa! Hatujui hata namna tunavyozipata, lakini tunazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kutumia hizi changamoto tunazopitia, *sometimes* tunakuwa *frustrated,* tunahitaji elimu, tunahitaji semina nyingi, nyingi. Kwa hiyo,

naomba hii Wizara ikiwezekana, mwakani mwongeze bajeti ya kuwaelimisha wasanii, na sio wasanii kubwa peke yake, mwende Tanzania nzima kutoa elimu kwa wasanii ili wajue namna gani wanazifanya kazi zao vizuri katika maadili ya Kitanzania ili tuweze kutangaza nchi yetu Kimataifa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo hii kuna wasanii jamani wanafanya kazi. Hii ni kazi kama kazi nyingine. Mfahamu hilo, hizi ni kazi kama kazi nyingine. Kuna wasanii wamesoma katika hii nchi. Kuna wasanii wamesoma; Nanji amesoma, Billnass amesoma, Zuchu amesoma *India Advance Diploma* ya *Business*, Saraphina amesoma *Petroleum Chemistry* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na leo hii ni msanii pale amesimama, Mwana FA ana *Masters* ya Uingereza, ana *Degree* ya pale *IFM,* mimi nina *degree* ya pale *CBE*. Tumesoma, msitudharau. Msione kama vile katika hii nchi hatuna mchango wowote. Tuna mchango mkubwa sana, na leo hii tunazungumzia kila siku hapa masuala ya ajira, sijui ajira ndogo, ajira nini! Tukiweza kutengeneza vijana vizuri vijana humu ndani, nawambieni suala la ajira litakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kila nyumba kuna msanii mmoja, katika kila nyumba, kuna wanamichezo, tunataka nini tena? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuna wageni maarufu kutoka kwa ndugu zetu, majirani zetu wa Msumbiji ambao wako kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika. Kuna wageni 11 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kutoka Bunge la Msumbiji, nao ni Hon. Saide Fidel *Vice President of the Assembly and Head of Delegation, will you please stand*, *muito obrigado;* Hon. Lucinda Bela Da Dores Malema, *Deputy Head of the FRELIMO Parliamentary Bench*, Muito; Hon. Antonio *Jose Amelia Member of the Standing Committee of the Assembly Republic of Mozambique*, muito; Hon. Alberto Jocinto Nankuta Matukutuko *Member of the Standing Committee of the Assembly of the Republic of Mozambique; muito obrigado*. *(Makofi)*

Mr. Numido Fanuel Arrone Manhique *Counsellor of the High Commission of Republic of Mozambique and United Republic of Tanzania*. Karibu; Mr. Momed Salim Khan *for Secretary of the High Commission of Republic of Mozambique the United Public of Tanzania;* Mr. Benjamin Pequeniono, *Advisor of Hon. Vice President of the Assembly of the Republic of Mozambique*. *(Makofi)*

Mr. Traquinho da Conceicao Traquinho, *Assistant of the Standing Committee of the Assembly of Republic of Mozambique;* Mrs. Rosane Cassamo *Giva Secretary of Hon*. *Second Vice President of the Assembly of the Republic of Mozambique;* Mrs. Carlota Duce, *Interpreter;* Mr. Filbert Mwampashe, *Interpreter*. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa, *Vice President* kwa *Mozambique* ni Naibu Spika kama mimi. Kwa hiyo, baadaye tutakutana nao kwenda kwa mwenye nyumba ya Mheshimiwa Spika na pale kama kutakuwa na matatizo ya kutafsiri au nini, nipo mimi naweza nikawasaidia, sababu tulishiriki kwenye ukombozi Msumbiji, kwa hiyo tunayajua haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, jiandae Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Wizara ya Michezo; mimi leo yangu ni ya ushauri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwateua watendaji wazuri katika Wizara hii Mheshimiwa Mchengerwa na mwenzake Naibu, Katibu Mkuu na watendaji wote wanafanya kazi nzuri kwa kweli, kwa mara ya kwanza na mara nyingi tumeona sasa michezo hii inaenda na watu wanahangaika kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nimshukuru kwakweli Mheshimiwa Rais kwa sababu Wizara nyingi amechagua watu sasa wenye mtazamo mpana, vijana walikuwa wanalia mara nyingi kwamba tunaambiwa sisi ni vijana Taifa la kesho, kumbe wanasema Taifa la leo, wamepata nafasi tunataka waitendee haki Wizara zote walizochaguliwa vijana, Mheshimiwa Mchengerwa nakushukuru sana kwa uchapakazi wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kushauri mambo machache tu; ushauri wa kwanza alikuja hapa Mfalme

wa Morocco tukaoneshwa uwanja hapa Dodoma na magreda yakaenda pale yakatengeneza uwanja ule na tukaahidiwa kwamba uwanja huu utakuwa upo tayari sijajua ni mwaka gani lakini maana yake ulikuwa upo *busy* kwenye huo uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka kujua tu kwamba je, hilo wazo la kujenga uwanja wa Dodoma pale limekufa au linaendelea? Maana sasa sioni kwa mfano kwa Tanzania kama kweli tunapata msaada hivi hata kuweka uzio ni kiasi gani hicho, kuonesha kwamba sisi tuna uwanja na tumeuwekea uzio. Uwanja huu wa Dodoma ambao ndio uwanja wa kitaifa tungeweza kuwa nao kwa sababu tulipata msaada na tungeendelea kuona uwanja kwamba uwanja huu unapendeza kwa Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ninaotaka kutoa, sasa tukubaliane Wizara hii ya Michezo na Serikali kwa ujumla watupe *shortlist* hivi tuna mikoa 26, mikoa mingine ina viwanja hivi kuweka nyasi za bandia kwenye hivyo viwanja kuna shida gani? Ni fedha kiasi gani zinahitajika kwenye hivyo viwanja?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Wizara kwenye bajeti ijayo mtuambie kwamba katika viwanja tulivyonavyo 26 vya mikoa ni vingapi vimewekwa nyasi bandia. Lakini hili niseme mimi niombe *TFF* kama sio *TFF* Wizara ya Michezo nendeni mkatoe tuzo maalum kwa Bakhresa *(Azam Tv)* muwape tuzo maalum wapeni tuzo maalum Bakhresa *(Azam Tv)* wametufanyia kazi nzuri sana kwenye nchi hii vijana wetu wengi walikuwa sasa wamelewa Ulaya wanatazama ligi za Ulaya, leo kila mtu yupo kwenye *tv* ya Azam wapeni tuzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri wewe ni kijana, angalia na Serikali yako mkae vizuri na Mawaziri na wetu wengine na Waziri Mkuu nendeni mkamwite Bakhresa na timu yake na makampuni yake yote, kampuni ya Bakhresa inafanya kazi nchi karibu 55 karibu 60 mwambieni tutengenezee nyasi za bandia, mpunguzieni bei zote za vifaa vya michezo, viwanja vyetu vyote vitakuwa na nyasi za bandia kwa kupitia Bakhresa kwa sababu biashara hii anaiweza. Kwa hiyo niwaombe kwamba sisi tusihangike mambo mengi, tuna mtu ambaye ni msamaria na mzalendo wa kweli kweli katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpeni viwanja vyote 26 vya mikoa na vile vya Zanzibar vilivyopo Zanzibar atengeneze mpunguzieni bei ya baadhi ya vifaa vinavyohusika mimi nadhani hilo linaweza kuwa wazo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine michezo ni ajira, nilikuwa naomba sasa kwanza demokrasia *TFF,* kila tukifanya uchaguzi wa *TFF* wa Rais kila mara kunakuwepo na watu mara wanakamatwa, mara karatasi zimepungua, mara watu wamefungiwa, mara sijui kuna nini, kuna nini *TTF*, kuna nini humo ndani kila uchaguzi ukija wa *TFF* hadi watu wafungwe, wengine waende *lock up* wengine wafanywe nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri uchungulie humo ndani hii ni kazi ya utendaji; wekeni demokrasia ndani ya *TFF,* anayegombea kama anastahili apewe fomu, ajaze fomu vizuri na ashinde, kwa hiyo nafikiri kwamba hili nalo tulitazame na tuone linavyokwenda kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *academy,* tujitahidi sasa tuna kanda sijui ngapi ikiwemo Kanda ya Ziwa, lakini kanda zipo nyingi kuna Kaskazini, kuna Kusini, kuna Kanda ya Ziwa tukajenga *academy* kwa hizo kanda tukubaliane kwamba sasa *academy* ziwepo kwenye hizo kanda, lakini tuhakikishe kwamba kwa kila timu ya ligi kuu inakuwa na timu ndogo inakuwepo *academy* zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhakikishe kwamba hilo linakuwepo, tupate wachezaji bora kwenye maeneo yote, lakini pamoja na hayo niwapongeze sana *Tembo Warriors* ambao walikuwepo, ile timu ambayo inakwenda kuchezo Kombe la Dunia, mimi naomba hata Wabunge tuwachangie, kwani kuna shida gani mbona watu wengine tunawachangia. Hebu kaeni vizuri tuangalie hayo mambo, tuangalie hawa watu ndio neema tunaipata hivi mtu anahangaika kwenyewe na fimbo yake na nini hadi anashinda anakwenda Ulaya tunashindwa nini kuwachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali ikae vizuri wachange na sisi Wabunge tuwachangie, mimi nafikiri kwamba hili ni jambo zuri na timu zote zinazoshiriki tuone nafasi gani tunawachangia ili na wenyewe waweze kucheza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimefurahi waliokuwa wanazungumzia wanamuziki, jamani wanamuziki wetu wa Tanzania wanahangaika sana, nilikuwa nasoma historia ya Diamond alivyoshinda kwenda kuwa mtu maarufu, wanahangaika wanakwenda kwenye ukumbi wanafukuzwa, wanahangaika sana hakuna chombo cha kuwashika, wakipata wenyewe wakishakuwa maarufu ndio tunaanza

kuimba, wamezunguza watu wengi hapa tutafute namna ya kuwashika mkono, vijana wapo wengi hata Jimbo la Bunda tunao vijana wengi sana wanaimba vizuri, lakini namna ya kufika huku inakuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafute mfuko maalum ambao utakuwepo wa kuwasaidia wasanii, tuweke mfuko maalum uwe chini ya Waziri Mkuu ambao utawasaidia wasanii wetu waweze kufanya vizuri kwa sababu ni ajira. Lakini mfuko huo pia uwepo wa kusaidia timu za Taifa. Sasa timu kama ya Biashara ya Mara leo wamenyong'onyea inafanya vibaya watu wanaiona kama timu imefanya vibaya, lakini ile timu imeshindwa kwenda kucheza michezo ya nje, imekosa nauli ya kwenda huko, sasa leo wanacheza kwenda wapi, wanasikitika Mungu wangu, sasa wanajiuliza tukicheza tukishinda tunakwenda wapi, hakuna fedha ya kutupeleka kucheza michezo ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuundeni mfuko wa kusaidia vilabu ili viweze kufanya vizuri tunakokwenda nakushukuru kwa yote hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgungusi hayupo, anachangia Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu, kwanza nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya katika Wizara hii, lakini sambama na naye nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Pauline Gekul kwa kazi nzuri sana unaifanya mama endelea tupo nyuma yako tunaunga mkono, lakini

kipekee niwapongeze watendaji wa Wizara hii ndugu yangu Dkt. Abbas lakini pia Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu utajikita sana katika mambo ya soka, lakini nikiangalia zaidi eneo la mapato. Nilikuwa ninamuuliza Mheshimiwa Mwijage hapa kwamba kuna wakati wa Yesu, kuna yule Zakayo ambaye alikuwa ni mtoza ushuru, sasa kwa bahati leo tupo na Mkurugenzi wa *Singida Big Star*s ambaye pia ndio mtoza ushuru wetu hapa Tanzania na kwa babati nzuri na yeye ana timu inacheza ligi kuu katika msimu huo unaokuja, sasa nikakumbuka ile methali ya mwenda tezi na omo marejeo ngamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilabu vya Simba na Yanga vimeanishwa muda mrefu sana, lakini vilabu havijiendeshi kibiashara, bado ni vilabu ambavyo vinategemea ruzuku za wanachama, lakini michango mbalimbali na kwa bahati mbaya sana huko nyuma walikuwa na mfumo ambao sio mzuri sana wa usajili kiasi kwamba walikuwa wanasajili wachezaji, hasa wachezaji wa nje…

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba vilabu ambavyo havijiendeshwi kibiashara sio vyote, *Young*

*Africans* sasa hivi ipo kwenye kumalizia kujiendesha kibiashara na muda mfupi tu watakamilisha mpango huo na itakuwa inajiendesha kibiashara sawa sawa. Kwa hiyo nampa taarifa na aipokee, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi sidhani kama ni taarifa, lakini ni …

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sio taarifa, kwanza angetega sikio asikie nazungumza nini ndio ataelewa kwamba kuna biashara inafanyika au hakuna biashara. Simba na Yanga peke yake hadi sasa hivi zinadaiwa na Mamlaka ya Kodi Tanzania bilioni kumi na hizi ni fedha ambazo zinatokana na…

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mbili mzungumzaji; moja sikuwa najua…

**NAIBU SPIKA:** Taarifa moja tu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji sikuwa najuwa anavyoongea Zakayo anamaanisha mimi, lakini nilitaka nimpe taarifa kwamba mimi similiki timu ni mdau tu wa michezo ya hapa Tanzania, kwa hiyo… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** ahsante lakini sidhani kama ulitajwa. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliona anaongelea Zakayo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Naona unajishuku, haukutajwa popote hapa yametajwa mambo ya Yanga na madeni ya *TRA* nilifikiri unasimama kuhusu unasamehe madeni ya *TRA* ya vilabu vikubwa. Haya Mheshimiwa Shangazi endelea.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naona mambo yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Simba na Yanga kwa umoja wao wanadaiwa takribani shilingi bilioni kumi na Mamlaka ya Kodi Tanzania na fedha hizi zinatokana na *pays as you earn,* lakini *skills development levy* ambazo hawakukusanya tangu wakati ule ambapo walikuwa wanaendesha katika mfumo ambao sio rasmi sana kama ambavyo sasa hivi angalau wanaelekea kwenye mfumo ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunawomba sana Wizara ya Fedha hivi vilabu kwasababu havijiendeshi kibiashara, havina mahali popote vinaweza kuja ku-*retire* hivi *amount,* basi wasamehe hizi kodi ili sasa virudi katika mfumo wa kuweza kuwa na *compliance* wakati huu ambapo sasa vimeanza kujiendesha katika mfumo ambao ni rasmi. Lakini bila kusamehe hili deni ipo siku Mamlaka ya Mapato ikiamua kuvifungia hivi vilabu hatutakuwa na kitu kinachoitwa Simba wala Yanga kwa sababu wana deni kubwa ambalo haliwezi kulipika. Kwa hiyo, nikuombe sana Waziri wa Fedha lakini nikuomba

Waziri wa Michezo ufuatilie hili jambo ili vilabu vyetu viweze kupata hiyo nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ambalo nilitaka kulichangia pia ni kwenye eneo ambalo sasa linawahusu hata wale wamiliki wa *Singida Big Stars,* lakini wengine ni wa Namungo, Simba, Azam na kadhalika. Hili ni eneo ambalo lina kodi ya zuio *(withholding tax); TFF* wameingia mkataba na Kampuni ya Azam ya kuonesha matangazo ya mpira, lakini kulikuwa kuna kipengele cha *withholding tax* ambacho vilabu vilikuwa havikuambiwa, kwa hiyo wakati sasa vilabu vinapewa fedha na Azam inabidi sasa wa-*retire* ile *amount* ya *withholding tax* kitu ambacho kimepunguza kile kiwango ambacho tumetangaziwa pale awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inavifanya vilabu sasa vikose fedha za kutosha za kuweza kujikimu kama ambavyo mdhamini alikusudia kwa hiyo tunaiomba Wizara ya Fedha, lakini pia Wizara ya Michezo ikae ikae katikati iangalie, kwa sababu vilabu vyote tunavyozungumza hapa havina mahali ambapo mwisho wa mwaka wanaweza wakaonesha hesabu ili waweze kurudishiwa hizi fedha, kwa sababu vilabu vyetu bado vipo katika mfumo wa ridhaa, kwa hiyo namna pekee ya kuwasaidia ni kuwasamehe hii kodi ya zuio katika hii biashara ya matangazo kupitia *Azam Tv*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la kwenye michezo ya kubahatisha *(betting)*. Ningeomba sana kwanza nawapongeza sana *SportPesa* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya, wameweza kudhamini Simba na Yanga takribani miaka mitano na wametoa zaidi ya shilingi bilioni

6.6. Lakini pia walikuwa wanadhamini vilabu vingine kama *Singida United*, wamedhamini Namungo tumeona wakiwa na msaada mkubwa. Lakini nitoe rai sasa kwa Wizara ya Michezo iweze kuongea na kampuni nyingine za michezo ya kubahatisha kwa maana ya *betting* sasa hivi tunazo kampuni zaidi ya 20 twende kuwaeleza kwamba ili aweze kupata leseni ni lazima angalau adhamini pia japo timu moja, kama ambavyo tumeona kuna *10Bet* wanadhamini timu ya Dodoma Jiji hapa, basi na hizi kampuni nyingine za *betting* zichukue japo timu moja ya ligi kuu au kama sio ya ligi kuu basi hata ya ligi daraja la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kwa sababu maudhui wanayokwenda kushindania yanatokana na mpira, kwa hiyo ni lazima wawekeze pia katika kuendeleza tasnia nzima ya mchezo ili waweze pia kupata malighafi ya kuzalisha kwa ajli ya hizo kampuni zao za ku-*bet*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa nilisemee ni eneo la kwa ujumla kuwapongeza wale ambao wanafanya vizuri katika udhamini kwa maana ya Azam kupitia *Azam Sports* wanafanya kazi nzuri sana. Lakini wadhamini wengine kama *Sport*Pesa wadhamini wengine kama Mohamed Dewji kupitia kampuni yake ya *MO*29 wanafanya vizuri kiasi kwamba sasa tumeona namna ambavyo Simba inaendelea kufanya vizuri katika Taifa hili, takribani kipindi cha miaka mitano tumeingia katika hatua ya robo fainali na tumeliwakilisha vyema Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hata katika hii *Royal Tour,* Simba ndio tumeanza kwa sababu katika

kuweka jezi ya Simba ile ya *Visit Tanzania* hao watalii ambao tunawaona kuna mchango mkubwa sana wa *Simba Sports Club.* Kwa hiyo ninakubaliana na wewe sasa kwamba na michezo nayo iingie hapa i-*chip in* kwenye hii *Royal Tour* kwenye *sports* ili tuweze kufanya michezo yetu iweze kuwa na msaada mzuri kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu na jioni mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Chumi, atafuatia Mheshimiwa Francis Kumba, Mheshimiwa Khamis Mohamed, *Engineer* Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Dennis Londo na Mheshimiwa Asia Halamga, hawa watachangia jioni kwenye kipindi chetu wakati *winding-up* ya bajeti itakapofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukiri kiukweli Mheshimiwa Waziri pongezi unazopewa wewe na Naibu wako, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kweli imekuwa ni *game changer* mmeiondoa hii Wizara kwenye unyonge na mmeiweka sasa hivi kwenye Wizara ambayo ina matamanio. Hawa *Serengeti Girls* ambao wanakwenda kwenye *World Cup* hii ndiyo *Post Royal Tour,* mkaitangaze Tanzania sasa upya kwa njia hii ya sanaa na michezo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya tunasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(06:55 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

**6 JUNI, 2022**

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Cosato David Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Hamis Mohamed ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii, sauti yangu haipo vizuri sana kwasababu ya furaha tuliyokuwa nayo kule tulikotoka, furaha ya kupata miradi ile ya maji kama tulivyosema kule leo Waheshimiwa Wabunge tumetoka kusaini ile Miji 28 tumeisemea sana. Kwa hiyo, tumekuwa na furaha sana tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Bunge kwa ujumla kwa sababu limesukuma sana ajenda hii, na kwakuwa maji ni kila kitu tunaamini sasa hata kama viwanja vilikuwa vikavu sasa vitakuwa vinamwagiliwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nipongeze Wizara kwa kazi nzuri inayofanya, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza mabinti zetu ambao wamefuzu kwenda *World Cup,* pia niweze kupongeza Simba *Sports Club* kwa kuendelea kutubeba katika michezo ya Afrika mwakani tena msimu ujao tutakuwa na timu nne, tutakuwa na timu nne kutokana na *performance* ambayo Simba imekuwa ikiifanya kwenye michuano ya Kimataifa na ninaona kuna dalili wenzetu pia wanaweza mwakani tukawa nao sasa waje kujifunza kutokana na uzoefu ambao Simba tumekuwa tukiupata mpaka kuwezesha kupata nafasi nne. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Cosato Chumi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, wanasema wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, nakubaliana na *performance* yao lakini unapozungumzia timu iliyojiandaa kuiwakilisha vema Taifa letu ni Dar *Young African* kwa kuanza kuchukua ubingwa mapema kwa *gap* kubwa zaidi ya *point* 10 mpaka sasa hivi, hamna namna na hii haijaja tu ni maandalizi mazuri ambayo tumejipanga wanayanga kuhakikisha tunaenda kuipeperusha bendera yetu vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Cosato Chumi unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, mimi nataka nijielekeze kwenye mambo ya msingi na kwa sababu hiyo siipokei. Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kweli.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, ninataka nitoe ushauri wa muhimu sana, mwakani tutakuwa na timu nne, tulishakuwa na timu nne lakini yaliyowakuta wale tunawaita wanajeshi wa mpakani biashara wakaishia njiani kutokana pengine na kukosa uzoefu wa namna gani unatakiwa ujipange unapokwenda Kimataifa. Pamoja na kucheza na kadhalika nikufahamishe kwamba kushiriki Kimataifa kuna mambo mengi na hapa niwaombe *TFF* watusaidie sana zile timu ambazo zitakuwa zimepata nafasi kwenda kushiriki Kimataifa ikiwezekana wawape hata *rehearsal*. Kwa mfano; nakumbuka Biashara walienda Djibouti siku hiyo hiyo wakashindwa kwenda Libya kwa sababu unapoenda nje lazima ujue je, ile nchi unayoenda je, unahitaji *visa*? Je, kama unahitaji *visa* ni ile *refereed visa* ambayo inabidi uombe *in advance* au unahitaji *visa* ambayo ni *visa on arrival,* haya mambo yote ya *logistics* haya lazima uwe na weledi nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana natoa wito kwa *TFF* hizo timu nne zitakazoshiriki michuano hiyo ya Kimataifa wawape hayo mafunzo, hapa natoa wito kwa vilabu vyetu kama ambavyo tunao wasemaji katika vilabu vyetu, kama ambavyo tunao Madaktari katika timu zetu ifike wakati sasa tuwe na ma-*protocol officer* kwenye vilabu vyetu. Mimi nimefanyakazi *Foreign Affairs*, nimefanyakazi Idara ya *Protocol* mtu wa itifaki ni muhimu

sana kwa sababu ndiyo anashughulika na *logistic* zote. Je, timu ina *passport,* wachezaji wana *passport,* masuala ya *visa,* mambo ya *Airline* kwamba je, hii *route* tunayoenda tuunganishe wapi au tufanye vipi iwe *route* fupi timu isifike imechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana naendelea kutoa wito kwa *TFF* na Serikali maana tunaweza tukawa tunapata timu nne, nafasi nne kila mwaka, Simba wanatoka jasho wanatubeba tunakuwa na timu nne lakini zikifika kule zinaishia njiani. Naomba hilo Waheshimiwa Wabunge tulichukulie kwa uzito sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili mchezo wa riadha. Huu ni mchezo ambao unaweza kusaidia sana kututangaza tena si kwa gharama kubwa sana. Kwa mfano, katika *marathon* kubwa duniani *New York Marathon, Tokyo Marathon, Boston Marathon, London Marathon, Chicago Marathon*. Kwa mfano, *New York Marathon* tu wakati wale wakimbiaji wanakimbia kuna zaidi ya watu milioni mbili *along the road* wanafuatilia. Sasa kama pale una wanariadha wa Tanzania watatu, wanne wamevaa ile nguo ya kukimbilia imeandikwa Tanzania unakuwa umetangaza Taifa kwa gharama bure kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya watu milioni 300 wanafuatilia kwenye *tv* hizi *marathon,* sasa sioni sababu gani sisi watushinde Wahabesh, watushinde Eritrea, watushinde Kenya ambao mazingira tunafanana. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali hebu tuwekeze pia katika mchezo huu tuwe *very serious* ili kusudi tuweze kuitangaza nchi yetu kupitia mchezo wa riadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajipanga sana kwenda Kombe la Dunia, tunaenda na hii timu ya mabinti zetu, je, tumejiandaaje? Mheshimiwa Waziri lazima tujue kama Taifa tunao makocha wangapi wa leseni gani na wako wapi, je, tunao matabibu wa michezo, tunao *sports psychologist* wangapi, wale watoto wameenda Cameroon kuna mazongezonge wamekutana nayo nani kulikuwa na *psychologist* ambaye anakuwa *sports psychologist* wa kuwaandaa hawa watoto kukabiliana na kwenda ugenini? Waamuzi ni mambo ambayo kama tunakataka tuwe *serious,* ndugu zangu kitu kama mpira wa miguu hakina muujiza *it needs serious preparation*. *Preparation* kubwa kwa watanzania hamasa jamani tumeshafika mbali, hamasa ya mpira ipo juu tunashida ya mambo mawili, miundombinu ya viwanja na suala la waamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kama unataka uache *legacy* jielekeze kwenye hayo mambo mawili. Viwanja Mheshimiwa Waziri bahati nzuri tunaweza kushirikiana na Chama cha Mapinduzi vile viwanja tayari miundombinu ya msingi ipo, lakini pia viwanja hivi tukivitengeneza viwe kwa ajili ya mchezo wa mpira wa miguu labda na riadha. Siyo sahihi sana kiwanja hicho hicho leo ikija sijui tamasha la muziki humo humo, tamasha la muziki wa injili humohumo, tamasha sijui la nini humohumo haiwezekani. Ndiyo maana tunaendelea kushauri kujenga *Sports Arena* na kujenga *facilities* kwa ajili ya mambo ya *entertainment* na burudani kwa sababu ni kitu ambacho kinapeleka sana Taifa mbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho; mchezo wa *netball*; nashukuru sana umerudi mikononi mwa watu wenye

mpira wao, kina Shyrose Banji nakumbuka miaka mitatu iliyopita tumeshinda kwenye South Africa kushiriki wakati nafasi tumeipata. Tunaomba nao tuupe *support*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri Chama cha Mpira wa Miguu wanawake, kwa kweli kwenye *soccer* kimataifa sasa hivi wanawake wanatubeba. Uchaguzi Mheshimiwa Waziri unajua ulisitishwa kimazongezonge na mimi huwa ni mtu *honest* niwaombe *TFF, TFW* muilee, msiiletee mazongezonge acheni wafanye uchaguzi wao. Figisu kwenye kile kitu si vizuri kama ningepata nafasi kwenye Maendeleo ya Jamii ningechangia hebu tuwanyanyue na wenyewe wanawake kwa sababu Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Mpira wa Wanawake pia ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya *TFF,* lakini saa hizi karibia mwaka wanakosa kule uwakilishi na sisi tunasema tuwawezeshe wanawake tutawawezesha nini kama hatutengenezi hiyo *platform? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itoshe kusema kwamba michezo ni zaidi ya burudani, nikazi, ni ajira *but we have to be very serious* Mama ametusaidia *Royal Tour* imetangaza nchi yetu na kupitia michezo, kupitia riadha, kupitia hawa watoto juzi, kupitia hawa watakaokwenda timu nne kimataifa tutaendelea kulitangaza Taifa letu lakini lazima tusaidie katika kutengeneza *logistic,* mambo ya *protocol,* mambo ya viwanja na mambo ya waamuzi na haya yote tukidhamiria inawezekana. Mungu Ibariki Tanzania, Mungi Ibariki Nchi yetu, Mungu wabariki viongozi wetu. Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mhandisi Samweli Hhayuma Xaday, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi siku ya leo kuwa mchangiaji wa pili jioni ya leo katika Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza nakumtakia kila la heri Mheshimiwa wetu Waziri, jirani yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa pamoja na Naibu Waziri wetu Mheshimiwa Pauline Gekul, Katibu Mkuu Hassan Abbas pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Saidi Yakubu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu kuna mambo mengi tangu wameingia katika Wizara hii kwa pamoja wameweza kuyafanikisha wakishirikiana na watumishi waliopo katika Wizara hii. Tumeshuhudia sinema ya *Royal Tour* waliisimamia vizuri na leo inaitangaza nchi yetu ya Tanzania katika medani ya utalii pia wamesimamia timu yetu ya michezo ya Tembo *Warriors,* Timu ya Taifa ya walemavu ambayo iliweza kufuzu katika mashindano ya Kombe la Dunia ya Timu za Walemavu.

Mheshimiwa Spika, juzi tu hapa tumeshuhudia Timu yetu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 17 ikifuzu kwa kucheza Kombe la Dunia kule nchini India jambo ambalo halijawahi tokea. Timu zetu za mpira wa miguu hazijawahi tokea wakati wowote ule ukiondoa ile ya walemavu kufuzu kwa ajili ya mashindano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitaipongeza Klabu ya *Young Africans* kwa kuwa na mafanikio makubwa sana katika msimu huu. Mafanikio ambayo yalikuwa adimu katika klabu yao kwa miaka mfululizo minne iliyopita. Nawapongeza lakini nawapongeza pia katika hata zile *point* ambazo tulipata za kutuwezesha kuendelea kuwa na washiriki wanne katika mashindano ya vilabu barani Afrika wao wamechangia alama 0.5 kati ya alama 30.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza klabu ya Namungo kwa kuendelea kuchangia katika timu ambazo zinakwenda kucheza msimu ujao wa mashindano ya vilabu Barani Afrika kwa kuwekeza *point* mbili pale. Hongera sana naona Mwenyekiti yupo hapa wa Namungo, hongera sana Mheshimiwa Hassan. Sana sana niipongeze Klabu ya Simba, Klabu ya Simba imetutangaza vilivyo katika medani ya Kimataifa hasa katika mashindano ya vilabu Barani Afrika, kuweza kushiriki mashindano ya Kimataifa ya vilabu Barani Afrika mara nne, ukaweza kupata nafasi ya kucheza robo fainali mara tatu, si jambo la mchezo ni jambo ambalo linatakiwa kuigwa, ni jambo la mfano ambalo limeiweka nchi yetu katika *level* ya juu kabisa ya mashindano ya vilabu Barani Afrika. Simba kutokana na mafanikio ya miaka minne wamechangia alama 28 kati ya 30.5 ambazo zimetufanya tuendelee kuwa na vilabu vinne. Alama za klabu ya Simba peke yake zimezizidi alama za nchi maarufu hapa Barani Afrika kama Libya na Nigeria *overall* kwa timu zao zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba tujifunze kutokana na Simba, haikuwa rahisi sana kwa klabu ya Simba kuweza kupata mafanikio katika medani za Kimataifa

haya ambayo wameyapata. Mimi ni mdau wa mpira wa miguu katika mpira wa miguu kuna mambo matatu huwa tunayazungumza ambayo ndiyo msingi wa kuboresha mpira mahala popote unapochezwa. Jambo la kwanza ni utawala bora katika klabu, jambo la pili ni kuwekeza katika wachezaji bora, jambo la tatu ni kuwekeza katika benchi la ufundi. Kwa hiyo, hayo ni mambo matatu ambayo ni ya msingi sana ambayo Simba yote walifanikiwa kuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Simba walijiongeza kwa kuongeza *factors* zingine, *factor* iliyoongezeka ya nne ilikuwa ni kuwekeza rasilimali fedha ya kutosha kwenye klabu. Kama huna fedha huwezi kucheza mpira lakini pia walikuwa na washabiki bora wa mfano Barani Afrika, pia walitumia vyombo vya habari vizuri … *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na umaarufu wa Simba lakini anadaiwa na *TRA* bilioni sita, Yanga anadaiwa bilioni tatu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, futa usemi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Unajua mimi humu ndani napima tu mashabiki gani ni wavumilivu, wapi uvumilivu hamna. Mheshimiwa Ndulane unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante nimeipokea taarifa yake lakini ni imani yangu kwamba klabu ya Simba haina shida ya kulipa deni kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la sita; ni kwamba Simba waliboresha miundombinu ya uendeshaji wa klabu yao ikiwemo kiwanja cha mazoezi pamoja na *program* nzima za mazoezi na ushiriki wa timu kwenye mashindano mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini nichotaka kusema, sifikiri kwamba Simba wamefika mahali ambapo wanatakiwa kufika, lakini wamejitengenezea *brand* ambayo inapaswa kuigwa na vilabu vingine. Vilabu vingine vinapaswa kujifunza kutokana na Simba ili tuweze kwenda mbele. Nina imani kama vilabu vingine vitajifunza kutokana na Simba sitashangaa kwa *speed* hii ambayo wanakuja nayo Yanga na vilabu vingine, mwakani sitashangaa kuona vilabu vyetu vinne vyote vikishiriki angalau hatua ya robo fainali Barani Afrika pia sitashangaa pia kuona vilabu vyetu nchini Tanzania vikifikia angalau viwili vikifikia hatua ya nusu fainali kwenye mashindano ya vilabu Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niviombe vilabu vingine viendeshe mpira kisayansi kama ambavyo wanafanya Simba, ingawa niseme tu hapa katikati Mheshimiwa Rais wetu Mstaafu aliwahi kusema wakati

fulani tatizo la nchi yetu kuna baadhi ya vilabu vinaendesha mpira, wanawekeza kwenye Kamati za ufundi badala ya benchi ya ufundi, hilo ningeomba lizingatiwe lakini pia tuweze kuona namna ambavyo timu zitasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Simba nao nafikiri hawajafika pale ambapo tunatarajia, haiwezekani miaka minne tunaishia robo fainali, nilifikiri wanapaswa sasa kupiga hatua kwenda mbele zaidi. Ninafikiri hilo linawezekana kwa sababu wametoka mbali, wamefika mbali. Kwa hiyo, niwaombe Viongozi wa Klabu ya Simba wakishirikiana na Serikali yetu kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo waweze kuboresha mazingira ya klabu zetu ili hatimae ziweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma atafuatiwa na Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma na Mheshimiwa Dennis Londo Lazaro ajiandae.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuweka senti 50 zangu kwenye bajeti ya Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ndugu yangu Sharifu wa Kipumbwi kule Pangani Jumaa Hamidu Aweso anasema asiyeshukuru kwa kidogo, hawezi kushukuru kwa

kikubwa. Nitambue mchango mkubwa na kazi nzito inayofanywa na wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwenye Wizara hii; ndugu yangu Waziri, Mohamed Mchengerwa; Naibu Waziri, dada yangu Pauline Gekul; Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbas; na ndugu yangu Said Yakubu, Naibu Katibu Mkuu ya kuitafsiri dira na maono na huruma za Mheshimiwa Rais kwa wanamichezo, wanasanaa na wanautamaduni wa nchi hii. Kazi nzuri wanaifanya na kusema kweli tunaiona na tunawashukuru sana na ushirikiano wanaotupa ni Mungu tu anayeweza kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo kadhaa ambayo napenda kuchangia, kwa hiyo, muda usipotosha mengine nitayaweka kwenye maandishi. La kwanza kabisa ambalo sitaki kuliweka mwisho, usije muda ukaniishia na sijalisema ni hili suala la mirabaha. Kusema ukweli kazi nzuri imefanyika, kazi nzuri imefanyika na hasa kwenye uthubutu. Mirabaha hii siyo mara ya kwanza kugawiwa, lakini mara ya mwisho iligaiwa mirabaha ya mwaka 2018 na kabla ya hapo ilikuwa ya 2014. Kusema ukweli kuna mazingira mengi ambayo yalikuwepo, yalikuwa yanafanya mirabaha ishindikane kugaiwa, lakini pia yalikuwa hayawezi kurekebishwa kama hatutaanza kuigawa, yaani ile lazima mvua inyeshe ndio tujue wapi panapovuja. Sasa hivi mvua imenyesha, tumejua wapi panapovuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na kuwa na *complain, complain,* kutoridhika kwetu kuhusiana na ugawaji wa mirabaha ile, nani kapata kiasi gani, kwa nini na vitu vya namna hiyo, lakini niwapongeze kwa uthubutu ule. Shida yangu kwenye mirabaha ni namna

ambavyo tunaifanya tokea mwanzo, ukusanyaji na ugawaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze mwanzoni kabisa, mirabaha iko kwa mujibu wa sheria. Sheria ya Hati Miliki na Hati Shiriki, Sheria Na.7 ya mwaka 1999 na marekebisho yake ya mwaka 2003. Moja ya vitu inachosema ni kwamba maeneo yote ambapo yanatumia kazi za sanaa, yanatakiwa kulipa mirabaha. Maeneo ambayo kusema kweli yanatumia kazi za sanaa yako mengi, hoteli, *buses*, *hair saloons* na *barbershops, restaurant*, *cafe, bars and social clubs, radio* na *televisions*, *shopping malls, medium size shops, night clubs, telecommunication companies* na *music festival*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa safari hii *COSOTA* wamegawa Shilingi milioni 321 na mirabaha ilikuwa haijagaiwa toka mwaka 2018. Kwa hiyo, hiyo milioni 321 hii ni ya miaka minne, ndio tafsiri yangu. Nikajaribu kuchukua *effort* kupiga simu kwa watu wetu *TRA* watusaidie kujua sehemu ambazo *COSOTA* wanatakiwa kuchukua mirabaha. Kusema ukweli tumeshindwa ku-*capture* kila kitu, lakini *beverage servicing activities* ziko 3,009 nchi hii. *Passenger land and transport* ziko 66,738, *restaurants mobile food activities* ziko 30,957, *urban and sub-urban passenger land transport* ziko 1,347. Jumla ni biashara ambazo zimesajiliwa *TRA* ambazo zinatakiwa kulipa mirabaha 102,051. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii milioni 321 ambayo tunasema ni mirabaha ya miaka minne kwa biashara 102,051 inamaanisha biashara hizi zote zimelipa shilingi elfu tatu tatu kwa miaka minne kutumia kazi za sanaa. Yaani nafikiri hii ni sahani ya chipsi mayai kwa Edo pale.

Watu wamelipia kupiga muziki, kutumia kazi za sanaa kwa miaka minne bila kipingamizi, anapiga mtu yoyote, saa yoyote 24 *hours a day* kwa siku 365. Sasa unaweza kuona jinsi ambavyo *COSOTA* haijaanza kufanya kazi yake. Ninachojaribu kufanya, ni kulinganisha ile *scope* ambayo *COSOTA* wanakusanya na ile *potential* ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara hizi kama ambavyo zingelipa Sh.30,000 tu ambayo ni Sh.2,500 tu kwa mwezi ambayo hamna mtu yoyote anayeweza kukataa kati ya hawa kulipa, bado tungekuwa na mara 10 ya kiwango ambacho COSOTA wamekikusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli sheria inasema waziwazi kwenye marekebisho ya mwaka 2003 na nikisoma kipengele cha tatu inasema: *"No person shall hold a public performance or a broadcasting of a work in which a copyright subsists except under a license issued by the society." By the society* wanamaanisha *COSOTA*.

Mheshimiwa Spika, sasa swali la kwanza kuwauliza ni kama *COSOTA* wametoa leseni za sehemu hizi 102,000 ambazo ni wazi zinatumia kazi za mziki. Kama hawajatoa kwa miaka 23 toka sheria hii ilipotengenezwa, ni wazi *COSOTA* hawajaanza kufanya kazi yao. Kiwango tunachokusanya hakijafika hata asilimia tano ya hasa ambacho tulitakiwa tuwe tunakikusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria iko wazi haijamumunya maneno, *you pay to play as you want* na hicho ndio ambacho kinatakiwa kufanyika. Kwa hiyo, kazi za muziki, kazi za sanaa zinatumika na hakuna anayelipa. Maeneo haya yote ya biashara ninayokwambia, *OSHA*

wanakusanya chao, *NEMC* wanakusanya chao, *TRA* wanakusanya chao. Watu pekee ambao hawalipwi kutokana na shughuli hizi za kibiashara zinazofanyika ni wasanii wa nchi hii. Sasa unaweza kuona na sheria iko wazi, yaani siyo kitu ambacho tunaenda kuifanya sheria tukae tena tutengeneze sheria upya ama nini. Sheria iko wazi inasema, kwa hiyo, kuna mtu tu hafanyi kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu ni kwamba, kwa mujibu wa maelekezo ya sheria, kiwango tunachokusanya ni kidogo sana na tumejaribu kuongea na *COSOTA* miaka nenda, miaka rudi kujaribu kuwaelekeza hili kuhusiana na uwezekano wa ku-*outsource* shughuli hii ili watu wengine waifanye. Hata kama ikibidi ku-*privatize* moja kwa moja, halafu *COSOTA* ikawa inalipwa kutokana na makusanyo kwa kiwango wanachokiweka, ingekuwa sawa. Serikali inapoteza pesa nyingi na wasanii wanapoteza pesa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama Serikali haitaki kukusanya hela yake, wasanii wanataka kukusanya hela zao. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, akae chini upya na *COSOTA*, waseme maeneo yote ambayo yanatakiwa kukusanywa mirabaha, wana mpango nayo gani na kama kwa miaka 23 wameshindwa kufanya shughuli hii, wanatuambia nini sababu ambayo itafanya shughuli hii isiwe *outsourced* na maeneo haya yakaanza kukusanywa na watu binafsi wengine kwa sababu wao shughuli hii imewashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hili ndiyo eneo ambalo lina pesa nyingi kwenye Wizara yake kuliko maeneo yote. Tulijaribu kupiga hesabu

maeneo yote kwa ka-*research* kadogo ambacho siyo rasmi sana, tulipata tunaweza kukusanya takribani bilioni 56 kwa mwaka. Bilioni 56 kwa mwaka Waziri anajua ni kodi ya kiasi gani ya Serikali, anafahamu ni hela ngapi kwa wasanii. Uzuri wa *royalties* ni kwamba hata wasanii kama wameacha kufanya muziki, familia zao zinaweza kufaidika hata kama wao hawapo duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii familia ya Mzee wangu Waziri Ally, familia ya Remmy Ongala, Marijani Rajabu zingekuwa zinalipwa kwa pesa hizi, lakini baadae unapata malalamiko kuna mtu *royalties* amepata Sh.50,000 kwa sababu tu *COSOTA* wameshindwa kufanya kazi yao. Hii siyo ramli, hizi ni hesabu na hiki kitu kiko wazi kabisa kwa mujibu wa sheria, hatuhitaji kupita kokote ili kukifanya kitokee. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 mwezi uliopita, Mheshimiwa Rais alihudhuria *concert* ya *hip hop* pale Dar es Salaam na moja ya vitu alivyosema ni kuhusiana na umuhimu wa kuanza kukusanya *blank tape levy* na aliisema hii kwa nia njema kabisa. *Blank tape levy* ni ile tozo ambayo inatakiwa kuchajiwa kwenye vifaa vyote ambavyo vinaweza kubeba kazi za sanaa kama *flash disks, memory cards* na *CDs* wakati vinaingia tu. Tukichukulia kwamba asilimia 90 ya vifaa hivi vinakwenda kutumia kuhamisha shughuli za sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hatuna teknolojia, hatuna *human resources* ya kutosha ya kuanza kupita sehemu moja moja kuhakikisha kila ambaye anahamisha muziki, anahamisha shughuli ya sanaa tunamchaji. Kwa hiyo, namna pekee ambayo tunaweza kufanya ni wakati vifaa vile vinapoingizwa kwenye nchi hii tunaongeza

katozo kidogo ili wasanii wa nchi hii nao wakafaidika kwa kazi zile zinazokwenda kuhamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja nimalize.

**SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa hivyo, Mheshimiwa Rais ameliweka wazi hili. Pamoja na ile kazi ya *COSOTA* ambayo tunamwomba Mheshimiwa Waziri akahakikishe inafanyika ya makusanyo, lakini kwenye *blank tape levy* kwa sababu maelekezo ya Rais ni maagizo tayari, imeshakuwa sheria. Nategemea hili kuliona linaaanza *as soon as* mwezi Julai na ndugu yangu Mheshimiwa Mchengwerwa asipolifanya hili tunarudi kumsemea kwa Mheshimiwa Rais kwamba amepuuza maelekezo yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine nitauweka kwenye maandishi kwa sababu nina mengi ya kusema na muda haunitoshi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo na Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa; Mheshimiwa Naibu Waziri, dada yangu Pauline; Katibu Mkuu, ndugu yangu Abbas; lakini Naibu Katibu Mkuu, ndugu Yakubu pamoja na watumishi wote ndani ya Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ukiona *Serengeti*

*Girls* wanafanya vizuri na wanaenda *World Cup,* ukiona Tembo *Warriors* wanafanya vizuri, wanaenda *world cup* na maeneo mengi wasanii wanafanya vizuri hiyo ni kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyotangulia kusema kwamba angalau uhai wa Wizara tumeuona, baada ya Waziri kuchakarika, tumekuwa naye kwenye Kamati, ametuambia sasa anaenda mtaa kwa mtaa, anaenda kijiji kwa kijiji hatimaye kata kwa kata, wilaya kwa wilaya kupeleka salamu za Mama kwenye michezo. Tunamsubiri, hiyo salamu njema ya Mama itufikie.

Mheshimiwa Spika, kipekee nizipongeze sana timu zetu hizi zinazofanya vizuri. Jana nilikuwa miongoni mwa waliokuwa Amani kushuhudia Serengeti *Girls* wakiicharaza *Cameroon*, siyo kazi ndogo *Cameroon* ni timu kubwa, jina lake ni kubwa kwenye mpira lakini vijana wetu wamefanya vizuri sana, nawapongeza sana. Hata hivyo, siku za karibuni pia tumeanza kufanya vizuri hata kwenye riadha. Nalisema hili mahususi, nchi hii ukitafuta medali nyingi, zipo Hanang. Tunayo kumbukumbu nzuri ya mzee wetu Gidamis Shahanga ameleta medali mbili za dhahabu za *Commonwealth, lakini* kijana wetu mahiri Emmanuel Giniki amevunja rekodi iliyodumu kwa miaka nane ya *Warsaw Peace Half Marathon,* ni kazi kubwa inafanyika.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia eneo hili, ninachoomba Hanang iangaliwe kipekee kwenye eneo la riadha. Nimeona orodha ya michezo ya kipaumbele, mpira wa miguu, *netball,* mpira wa kikapu, mpira wa wavu, riadha, mpira wa mikono. Sisi tuanze na riadha kwa

Hanang kwa sababu tunayo *record* ukitafuta medali Tanzania hii Hanang tunaongoza, tunaomba tupewe kipaumbele cha kuangaliwa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, michezo hii yote ya vipaumbele ambayo imewekwa, ili ifanikiwe naishauri sana Wizara washirikiane na TAMISEMI kuboresha eneo la michezo mashuleni, UMITASHUMTA na UMISSETA. Kazi inafanyika lakini ukienda kwenye shule zetu hakuna vifaa vya michezo. Bila vifaa vya michezo itakuwa ni hadithi kuimba, kwamba tutaibua vipaji, ukienda kwenye shule zetu mipira bado wana matambara shule nyingi. Tusaidiane kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la wataalam wa michezo, wenzangu wamelisema sana hili. Ukiangalia hakuna motisha yoyote wanayopewa Walimu ambayo wanajihusisha na michezo. Tuwatambue, tuwape motisha, lakini tuwape mafunzo mahusus ili wawafundishe vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekuja na mpango mzuri wa shule 56 mahususi kwa ajili ya michezo. Mambo ambayo nimeeleza kwa ajili ya Hanang naomba shule ya kwanza ikajengwe Hanang. Wakashirikiane vizuri lakini bila kutatua changamoto ya upatikanaji wa wataalam, upatikanaji wa vifaa, bado changamoto ni kubwa. Wizara waanze na suala la kutatua changamoto ya vifaa na wataalam ili hizo shule sasa zitakapokuja ziweze kuwasaidia na tutengeneze vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia michezo yetu ukitoa kwenye mfumo huu wa shuleni, UMITASHUMTA na UMISSETA. Baada ya hapo, vijana wakienda vijijini

wanazagaa tu. Kwa sisi wakulima na wafugaji kuanzia mwezi Aprili mpaka mwezi Desemba hatuna shughuli mahususi, kwa hiyo, vijana wengi wanakaa vijiweni. Lazima tuje na mkakati mahususi wa kuwapelekea michezo kwenye mitaa ni mkakati muhimu sana naomba ukatekelezwe. Waziri aje ili tuwaokoe vijana na changamoto za kukaa vijiweni. Vijana wengi wakienda vijiweni wanafundishana mambo ya ajabu. Ndio unakuta watoto wadogo wamejifunza kunywa pombe utotoni tunapoteza nguvu kazi ya Taifa kwa sababu hatuna shughuli za kuwaweka na kuwatoa kwenye vijiwe. Kwenye vijiwe kuna mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa viwanja; kwenye bajeti ya Wizara wana viwanja saba ambavyo wanavikarabati, lakini mahitaji ya viwanja nchi hii ni makubwa sana. Tunachoomba kwenye eneo hili hatusemi Wizara wajenge viwanja kila sehemu, kwa sababu wanao uzoefu kwenye eneo la michezo, watutengenezee mpango ambao halmashauri zetu zitafuata wa *PPP* ili tuwekeze na viwanja hivyo viweze kujengwa, tuweze kuwaendeleza vijana wetu na tuwe na *facilities* za kufanya mazoezi, lakini ni sehemu ya kutambua vipaji vya vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kutohoa kutoka kwenye Wizara ya TAMISEMI, wao walielekeza kila halmashauri inayokusanya zaidi ya bilioni tatu ijenge kituo cha afya cha milioni 400. Kwa sababu tunapoenda kwenye kituo cha afya tunaenda kutibu watu, lakini ukiwa na maeneo ya michezo unawakinga watu na maradhi. Sasa tuangalie namna ambavyo tunaweza kutohoa na namna ambavyo tunaweza kutekeleza, tukajaribu kuwekeza kwenye eneo la kuwakinga

Watanzania na maradhi wakati huo huo tukiendeleza utaratibu wa kupelekea huduma kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana wakiunganisha na mpango mahususi wa *PPP* na halmashauri zetu ili kuondoa *burden* kubwa na uhaba wa viwanja tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la utamaduni; ukiangalia sasa Watanzania kama wengi tunaanza kusahau asili zetu. Niombe Wizara ianzishe siku mahususi ambako watu watarudi kwenye tamaduni zao, kutakuwa na michezo mbalimbali, wasukuma watakuwa na mambo yao ya kiutamaduni, lakini Wairaki watakuwa na mambo yao ya kiutamaduni, Wakurya watakuwa na mambo yao ya kiutamaduni pia ndugu zangu Wanyaturu watakuwa na mambo yao ya kiutamaduni. Tuchague siku mahususi ili tuweze kuhamasisha tamaduni zetu. Hiyo itatusaidia sana ili angalau watu tusisahau na tamaduni zetu zisipotee.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa pongezi kwenye makampuni ambayo yanaweka au wanafadhili kwenye michezo.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi? Mheshimiwa Nicodemas Maganga. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa tu Mheshimiwa mchangiaji, mchango wake ni mzuri sana, naomba Wizara iuzingatie. Kwa kweli kwenye utamaduni hapo kama kweli Wizara ikipashika vizuri, Wasukuma tunacheza ngoma vizuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Hhayuma. *(Kicheko)*

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nafikiri anaongezea kwenye yale ambayo nimesema, ni mambo ya msingi sana ambayo Mheshimiwa Maganga ameyagusia.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema, wale ambao wanawekeza kwenye michezo, wanaofadhili michezo mbalimbali, wanaofadhili sanaa, tutambue mchango wao. Nasema tu kwa wachache tu, nitaje Azam, *Mohamed Enterprises, Sports Pesa*, juhudi zao tumeziona. Huko nyuma Serengeti waliwekeza kwenye michezo, lakini Tanzania *Breweries* pia wamewahi kuwekeza kwenye michezo na wengine ambao wanagusa maeneo hayo. Hao wadau tutambue mchango wao, utatuhamaisha wengi zaidi kwenye eneo la michezo kwa sababu inagusa zaidi upande wa sekta binafsi. Tuweze kuhamasisha wengi ili kwenye sekta ya michezo kuwe na fedha ya kutosha na tuweze kuendeleza vipaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Utamaduni. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, hasa kutuzindua na kutuonesha umuhimu wa sisi Watanzania kuhamasisha ama kujali utamaduni wetu. Ziara aliyoifanya kule Mwanza, Magu katika tamasha la machifu na ngoma za utamaduni ni kiashiria ambacho kinaonesha *commitment* yake kwa utamaduni wa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipee pia nakupongeza wewe Spika wetu Tulia Ackson kwa jinsi ambavyo unaendesha tamasha la utamaduni kule Mbeya. Tamasha hili tunalifuatilia kwa ukaribu, lakini pia ni *model* ambayo inapaswa kuigwa Tanzania nzima. Kwa kweli kama tunaweza kumnukuu Mwalimu Nyerere, alisema kwamba utamaduni ni kiini ama roho ya Taifa lolote lile. Taifa ambalo halina utamaduni, ni mkusanyiko wa watu ambao hawana roho. Kwa hiyo, jitihada hizi ambazo mnazifanya, zinaonesha jinsi gani viongozi wetu mnatuonesha njia ya kupambania utamaduni wetu ambao ndiyo roho ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo, wakati nachangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje, nilizungumzia umuhimu wa *economic diplomacy,* nikaeleza kwamba wakati umefika sasa wa ku-*adapt* kitu kinachoitwa *innovative diplomacy*. Alichokifanya Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kupitia *Royal Tour,*

ni hicho ambacho tunakiita *innovative diplomacy*. Kupitia *Royal Tour* tumeweza kuuza utamaduni wetu, tumeweza kuwafikia wananchi ndani ya nchi na tumeweza kuifikia dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia sasa hivi, hasa huko tunakoelekea, Taifa kama Tanzania hatuwezi kwenda ku-*influence* wenzetu ama kutafuta ama kupigania nafasi yetu kwenye dunia hii kwa kutumia mizinga ama bunduki, lakini kuna kitu kinaitwa *soft power approach* ambayo pia ni sehemu ya *innovative diplomacy* ambapo tunaweza tukafikia dunia kupitia sanaa utamaduni na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili hatujalifanyia kazi vya kutosha, lakini nilikuwa naomba kusema kwamba tunaona jitihada ambazo Serikali inazifanya. Kwa mfano, kama jana tumeona timu yetu ya Taifa imeweza kufuzu Kombe la Dunia. Hizi ni jitihada ambazo zinaashiria kwamba tuna *commitment* ya kutangaza jina la Tanzania nje ya mipaka ya Tanzania na *inshallah* tunatumaini kwamba timu yetu itaenda kufanya vizuri na kuliuza jina letu huko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna mengi ambayo yamefanywa katika tasnia ya utamaduni, utamaduni wa utalii bado hatujautendea haki. Huko tunakoenda hatutaendelea tena kuuza milima, misitu na bahari. Utamaduni unaenda kuwa bidhaa ambayo bado hatujaitumia kikamilifu kama chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa kwa Rais wetu na pia nina matumaini makubwa kwa timu ambayo ipo Wizara ya Utamaduni ikiongozwa na ndugu

yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Naibu wake, dada yangu Mheshimiwa Pauline Gekul, Hassan Abbas na ndugu yetu Hassan Yakubu, wanafanya kazi kubwa ya kuiamsha Wizara na kutuonesha kwamba Wizara ya Utamaduni imepata wadau ambao wanaweza kuipambania na sisi tukaitumia kama *tool* ya kufikia dunia kupitia sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, wanasema kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Michezo ni kitu muhimu sana katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza. Kwa mujibu wa tafiti za Muhimbili *Costech* na hata *NIMR,* wanazungumza kwamba asilimia 41 ya vifo, vinatokana na maradhi yasiyoambukizwa. Vifo hivi ni mara mbili ya vifo ambavyo vilikuwa vinatokea miaka 25 iliyopita. Taifa kama letu ambalo linapambana ku-*transform* uchumi wetu, tunatumia zaidi ya dola milioni 700 kwa ajili ya kutibu, hatujajikita kwenye kuzuia. Ila kuzuia magonjwa kama ya moyo shinikizo la damu na kisukari, ni michezo.

Mheshimiwa Spika, michezo inaweza ikasaidia ku-*save* kiasi kikubwa cha fedha, lakini kwenye hili, kwa nini Watanzania wengi hawajihusishi na michezo? Wengine wanashindwa kujihusisha kwa sababu tu ya gharama kubwa ya vifaa. Kama wanapata *access* ya vifaa wanaweza wakaweza kushiriki michezo.

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba Wizara yetu ya Fedha inapoenda kutoa hotuba yake, ituambie ni kwa jinsi gani imejipanga kupunguza kodi ama kutoa nafuu ya kodi kwenye vifaa vya michezo ili ku- *encourage* Watanzania wengi zaidi kushiriki michezo kwa ajili ya ku-*preven*t afya zao ili ikoe fedha nyingi za nchi kwenye kutibu maradhi badala ya kukinga maradhi. Katika hili,

matumizi ya kodi ambazo zinapitishwa na Bunge hili, naomba sana ndugu zetu wa *TRA,* Hazina wasizitumie vibaya kuumiza shughuli ama jitihada za michezo.

Mheshimiwa Spika, kuna vitu ambavyo vimezungumzwa kuhusiana na madeni ya Simba na Yanga, lakini ndugu zetu wa *TFF* wanadaiwa zaidi ya Shilingi bilioni 10, sasa hivi wamelipa Shilingi bilioni tano na haya ni malimbikizo ya madeni ya nyuma. Sasa kwa taasisi ama chama cha michezo kama hiki ambacho kinajikokota kwenye kukuza michezo, kinadaiwa kodi ya Shilingi bilioni 10; na sasa hivi kinajiandaa kuleta *AFCON* nchini, chama ambacho kina madeni lukuki; hivi kama kuna moja ya *criteria* ambazo zitatumika na *CUF* kuleta mashindano hapa ni madeni kwa chama, tutafanikiwa kweli!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye majumuhisho, naomba tuone namna bora ya kusaidia vyama vyetu vya michezo na hasa timu zetu. Azam wamejitolea kudhamini ligi, wanatoa shilingi milioni 40 kwa kila timu, lakini katika shilingi milioni 40 hizo, shilingi milioni sita zinarudi *TRA*. Sasa haya ni maeneo ambayo yanakuza ajira na kupanua fursa kwa vijana wetu. Shilingi milioni 40 ni kitu gani ambacho unakata kama *withholding tax?* na mbaya zaidi, shilingi milioni sita ni hela nyingi sana kwa timu zetu ambazo zinachechemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba tuangalie kwa jicho la huruma kama fursa kwa watoto masikini, tuone namna bora ya kupeleka ujumbe kwao kwa kukuza vibaji vyao na pia kwa kuangalia kodi ambazo zinaweza zikawa-*encourage* na siyo kuwa-*discourage.*

Mheshimiwa Spika, pia kuna umuhimu wa kusamehe kwenye vifaa vya michezo hasa kwa watoto wadogo. Inaumiza sana unapoona timu ya watoto 22 wanacheza, watano wana viatu, 15 hawana viatu, inaumiza sana na ni kwa sababu tu ni gharama, wazazi hawewezi ku-*afford*. Kama tunataka ku-*train* vijana wetu, kujenga haiba na utamaduni wa kuheshimu sheria na taratibu, kuthaminiana, kupendana, lazima tu-*invest* kwenye michezo na kwa kuanzia tuweze kusamehe vifaa vya michezo, kodi hasa vifaa vya watoto wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza ndugu zetu au wadau wetu wakubwa wa michezo; kuna Dkt. Singo, ndugu yangu Askalia na dada yetu Neema Msita, wamefanya jitihada kubwa za kuboresha utawala bora kwenye michezo, lakini tunahitaji wapatiwe bajeti ya kutosha ili waendeleze michezo.

Mheshimiwa Spika, kwenye tasnia ya filamu tumeona imekua kwa kasi, kuna zaidi ya filamu 1,500 kwa mwaka ukilinganisha na 200 mwaka 2011. Wastani wa filamu 116 kila mwezi, 29 kila wiki, na nne kwa siku. Sekta hii imeajiri zaidi ya vijana 30,000. Sekta ya filamu ambazo zinatengenezwa ndani ya nchi ni kubwa sana kwa idadi katika Bara la Afrika. Kwa idadi ya filamu 1,500 kwa mwaka, Tanzania ni ya pili kwa wingi wa filamu ambazo ni *local produced* ikifuata Nigeria. Kwa hiyo, sekta hii ni muhimu sana na inakua kwa asilimia 14, tunahitaji kui-*support*.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia umuhimu wa Kiswahili kama roho ya Taifa. Kuna vijana ambao wamejitahidi kutengeneza *movie documentaries* ambazo Kimataifa zimeweza kuuza jina la Tanzania. Filamu kama

ya Vuta Nikuvute ambayo imetengenezwa na Mtanzania Amil Shivji, imesadifu riwaya mashuhuri ya mwandishi Shafi Adam Shafi na imetayarishwa na Watanzania. Filamu hii imewezwa kuchezwa kule Toronto, Seto, Ottawa na maeneo mengine mbalimbali kama Burkina Faso na hata Zanzibar inaenda kutumika kwenye tamasha la filamu**.**

Mheshimiwa Spika, filamu kama "Binti" ambayo imewezwa kutengenezwa na dada yangu Seko Shamte, filamu kama "Jua Kali" imetengezwa na dada yetu Lea Mwendamseke; ni filamu ambazo zinaibeba nchi yetu, zinabeba lugha yetu na utamaduni wetu. Serikali inafanya nini sasa kuzalisha akina Shivji wengine, akina Mwenda Mseke wengine na akina Shamte wengine? *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, mwisho naomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja tu, namalizia.

**SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na ombi moja, fedha ni changamoto kukuza tasnia ya Sanaa na michezo. Naomba 4% ya *Skills Development* iende kukuza vipaji na ujuzi mbalimbali hasa michezo na utamaduni na 5% ya mapato yote ambayo yanatokana

na michezo ya kubahatisha iende kwenye mifuko ya kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, na ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Muharami Mkenge Shabani, ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Sanaa, Utamaduni na Michezo. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi za dhani kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Moja ya kazi kubwa ni pamoja na kutangaza lugha yetu ya Kiswahili katika Tamasha la *Dubai Expo* kule nchini Dubai. Tunawapongeza sana, lakini hata katika bajeti yenu mmeonyesha namna gani mtaendelea kununua vifaa vya kutafsiri lugha ili kuendelea kukuza lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutenga Shilingi bilioni moja ya kuongeza katika Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa. Hii iwe rai kwa Watanzania na wadau wengine mbalimbali kuweza kuchangia mfuko huu ili uweze kuwasaidia vijana wengi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee katika Wizara hii Shirikisho la Maonesho ya Sanaa na Ufundi Tanzania. Kwenye bajeti ya Wizara hatuoni sehemu ambapo

shirikisho hili limepangiwa bajeti, lakini tukiangalia shirikisho hili limebeba ajira kubwa za Watanzania, kwa marika tofauti tofauti; vijana akina mama, wazee na makundi mengine mbalimbali. Shirika hili la Maonesho ya Sanaa wapo wachongaji, wachoraji, wabunifu wa mavazi, wabunifu wa mapishi, watu wa sarakasi na ma-*MC*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, pale ambapo wageni mbalimbali wanakuja kwenye nchi yetu, kitu cha kwanza cha utamaduni tunachokwenda kutambulika nacho ni hivi vikundi vya ngoma, vinakwenda kupokea misafara mbalimbali lakini vinashiriki katika matukio mbalimbali, ndani ya nchi yetu. Itapendeza tukiona watu hawa wanawekwa kwenye bajeti wanatambulika kwa sababu wana mchango mkubwa katika nchi yetu ya Tanzania lakini wamebeba ajira nyingi za kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe**.**

**T A A R I F A**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika ahsante. Nilitaka kumpa taarifa kwamba BASATA nchini Tanzania imesajili mashirikisho manne, lakini haya mengine yanasemwa sana isipokuwa Shirikisho la Sanaa za Maonesho Tanzania, humo ndani kuma ma-*MC, ma-DJ*, halafu kuna shirikisho sasa la ufundi. Kwa hiyo, nilikuwa

nampa taarifa pia kwamba hivi ni vyombo muhimu sana na visaidiwe na bahati nzuri wana uongozi wao unaongozwa na Mama Henjewele.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa wewe ulikuwa umeshaota kuwa hayo hana kwenye mchango wake? Maana alikuwa hajamaliza bado. Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru ndugu yangu Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kuliona hili na yeye, hakika lina mchango mkubwa sana kwa Taifa letu. Hili nisiendelee kuchukua muda kwa sababu ameliongelea pia kwa mapana yake, niombe tu sasa Wizara, lile jengo la Maonesho la *BASATA* lililopo pale Ilala, basi vikundi hivi vikikusanywa na wakawa wamepewa eneo lile, itasaidia sana hata wageni wanapotoka maeneo mbalimbali ikatambulika kwamba jengo fulani ukifika utakutana na vinyago vinavyochongwa na vijana wa Kitanzania na akina mama wa Kitanzania; vitu kama shanga, bangili, nguo za kiasili, iko *center* moja ambapo tunaweza tukavipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia mchango wangu katika eneo hilo, naomba niende kwenye suala la riadha. Nianze kwa kutambua kwanza mchango mkubwa wa watangulizi wetu ambao wamefanya vizuri sana katika mchezo wa riadha. Napenda kumtambua Mzee Filbert Bayi, Gidamis Shahanga, Selemani Nyambui, Juma Ikangaa, Mwinga Mwanjala na Simon Robert. Tunatambua mchango mkubwa sana wa wazee na waasisi hawa katika mchezo wa riadha. Naomba Wizara

isiache, iendelee kuwatumia kwa sababu waliwahi kuwa na mchango mkubwa katika Taifa, lakini hata sasa bado wana ushauri mkubwa katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza kijana Emanuel Giniki anayetokea Wilaya ya Hanan'g katika Mkoa wa Manyara kwa kufanya kazi kubwa na nzuri na kuweza kushinda mashindano ya riadha kule nchini Geneva tarehe 15 /5/2022. Hivi karibuni vijana wawili wa Kitanzania akiwemo Emanuel Giniki wanatarajia kwenda nchini *USA* kwa ajili ya mashindano ya kidunia.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iweze kuwaweka vijana hawa kambini. Changamoto inayowakuta wanariadha wengi ni mazingira na maandalizi ya kwenda kushinda kwao kwa sababu hawana makambi rasmi ya kuweza kujiandaa kwa ajili ya kwenda kupambana huko duniani. Wote tumeshuhudia na tumefurahia alivyokuja hapa amepeperusha bendera ya Kitanzania vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuweze kuwatumia vijana hawa kwa kuhakikisha kwamba viwanja wanavyotumia vinakuwa na mazingira bora na pia vifaa vya michezo mbalimbali ya riadha wanaweza kupatiwa na wanaendelea kupeperusha bendera ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza *CHANETA* kwa kufanya kazi kubwa na nzuri sana. Tunaamini sasa watarudisha heshima ya mpira wa pete na kama ambavyo *Serengeti Girls* kwenye mipira mbalimbali hii ya kiume sasa wameanza kufanya vizuri, na

tunaona kwa namna ambavyo wanawake wote ambao wamefanya mashindano, wameweza kuiletea heshima nchi yetu. Tunaamini *CHANETA* ikipewa nguvu itafanya vizuri zaidi na kuendelea kuongeza nguvu ya kupeperusha bendera vyema na kuleta vikombe vingi katika nchi yetu ya Tanzania kupitia *CHANETA* na mipira mbalimbali ya miguu inayofanywa na wanawake wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuiomba Wizara, kuendelea kutoa semina mbalimbali kwa wasanii. Wasanii wengi saa nyingine wanaadhibiwa siyo kwa kupenda kwao. Wasanii wa Kitanzania ni vijana ambao wanahitaji semina za mara kwa mara, na ikimpendeza Mheshimiwa Waziri waweze kutoa elimu za ujasiriamali kwenye makundi haya, kwa sababu kile kidogo wanachokipata waweze kukihifadhi ili kiweze kuwa na maslahi bora na tija kwao kwa sababu bado ni vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, mchango wangu wa siku ya leo unatosha, niwe nimeishia hapo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Mkenge Shabani na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Nimesimama hapa, awali ya yote naomba nimshukuru Mungu kwa nafasi hii

kwa sababu kwa kweli leo ukumbi umekaa vizuri na kila mtu ana bashasha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Waziri kwa kuwakaribisha hata machifu, wako huko na niseme leo ni siku ya tofauti niliyoiyona, mpaka saa hizi *gallery* zako zimejaa na zimetulia. Mara nyingine ikifika saa 4.00, ikishasomwa hotuba, hakuna mtu huko juu. Namshukuru sana Waziri kwa kutupa hotuba nzuri. Nampongeza yeye, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa jambo moja; nimeipitia hii hotuba kwa makini, au labda nimepoteza, sikusikia mahali ambapo amepongeza Bunge hili kwa vikombe vilivyokuja mwaka huu vingi vilivyozidi. Nimerudia, nimerudia, sikuona, labda siyo mahali pake. Hatuombi sisi chochote kwenye hii bajeti, kwa sababu Spika tayari ana fungu lake, lakini nimeumia, nimekwazika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond hebu rudia hapo kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimechukua muda sana kuipitia hii ripoti ya Mheshimiwa Waziri na labda atanisahisha atakapokuja kutoa na taniambia ukurasa kwa sababu mimi namuamini, kwanza yeye ni msomi, ni Wakili Msomi na ninamwamini hata kama hajazishika hizo nyadhifa. Sikuona kwa nini hakulitamka Bunge hili kwa ushindi uliopatikana Uganda, Kenya, *East Africa* yote. Sasa mimi

nimesikitika nimeona itaniumiza, nashukuru, nimeona lisiniue kifuani niliachie tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kama nimemkosea atanisamehe, lakini atanionesha ushahidi, maana yake yeye ni muda wa *exhibit,* utanipa *exhibit* kwenye ukurasa.

Mheshimiwa Spika, nimesimama zaidi hapa kumuomba Mheshimiwa Waziri kama ataona ni muhimu basi Kilimanjaro nayo ipate uwanja wa mpira. Mikoa yote ina uwanja wa mipira kasoro mikoa michache sana mmojawapo ni Kilimanjaro. Endapo tunaweza tukakaa hapa Waziri wa TAMISEMI akatoa amri, Halmashauri shirikianeni jengeni vituo vya afya katika kila kata, shilingi milioni 400, milioni 400; inashindikana nini Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoa tamko, Kilimanjaro sasa kujengwe uwanja mkubwa wa michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna eneo linaitwa *memorial* ni kubwa sana pamoja na kwamba sehemu inafanyika ni soko la mitumba, lakini hilo linalobakia linatosha kabisa kujenga uwanja na uwanja huo una upako. Kwa sababu alipokuja Baba Mtakatifu Tanzania alikanyaga ardhi ile. Kwa hiyo, kama tutajenga huo uwanja tukiwa na mashindano na Kenya, na nchi nyingine, Uganda na wapi tutashinda tu, kwa sababu pale ni patakatifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Waziri kuliko tunavyofanya sasa kwenda kucheza kwenye uwanja wa *Cooperative University,* kwa nini tusiwe na uwanja wetu Kilimanjaro. Tunaomba sana na chonde chonde na ninaposema hapa na

Mheshimiwa Rais ananisikiliza, tunaomba na yeye pia akipata namna atuangalie watu wa Kilimanjaro tupate uwanja wa michezo. Eneo tunalo tayari lakini halijawahi kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi niseme kwamba nilitamani sana katika vipindi vya michezo vinavyooneshwa, wasanii wetu wawe wabunifu, vipindi vya watoto viwe vya mafunzo zaidi. Kuna filamu zinazooneshwa sasa hivi zimekwaza wazazi japo wazazi ndiyo wanaonunua kifurushi cha kuangalia *tv*. Lakini kila mtu unamsikia anasema aaah, ile filamu ya watoto ya *Azam Tv* hivi na hivi. Sasa kwa nini msifanye filamu za watoto au katuni za watoto ninyi wabunifu wazuri.

Mimi huwa naangalia sana Mizengwe na kweli mizengwe hainipiti, lakini leo sijamuona hata mmoja wao huko juu. Lakini hiyo nasema kwetu sisi watu wazima, nimetoa mfano Mizengwe inafundisha leo watakwambia jinsi gani mtu alikwenda kupangisha nyumba, labda hakulipa nakadhali. Lakini pia wasanii wetu wangeweza wakawa wabunifu wakawafikiria pia watoto, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba kwa vile wote wako hapo na wengi wao waangalie namna fulani au watakuja tu wanaweza kuigiza sauti kama kina Steve Nyerere na wengine, basi wanaweza kuja na ubunifu huo wakuweza kufanya hizi katuni za watoto zikawa *more interesting* yaani zenye elimu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo sikuwa na mengi ya kuzungumza zaidi ya kuomba huo uwanja wa *memorial* yaani Kilimanjaro tuwe na uwanja wa michezo.

Niwapongeze wageni wetu wote waliotufikia siku ya leo kwa kweli mmetupa joto na sisi tunawapenda sana, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, ajiandae Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii niweze kuchangi machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze ndugu yangu Waziri Mchengerwa kwa kazi kubwa anayoifanya, na Naibu Waziri dada yangu Pauline Gekul, Katibu Mkuu, Dkt. Abbas, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Saidi Yakubu na timu yote ya Wizara na pia sitamsahau Mkuu wa Chuo changu cha Bagamoyo *TaSUBa* kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi za pili ziende kwa mama yetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya *Royal Tour*. Jambo la *Royal Tour* Mheshimiwa Rais amelianzia pale Bagamoyo na jambo lolote likianza Bagamoyo basi mambo yake yatakuwa mazuri kabisa na mnaona kabisa idadi ya utalii imeongezeka sana katika nchi yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumzia suala la Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo au Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Chuo hiki cha siku nyingi sana lakini kazi kubwa sana chuo hiki imekifanya na viongozi waliyoko pale wanaendelea kudumisha na kuhakikisha kwamba kazi kubwa iliyokuwa inafanyika inaendelea kuwa nzuri. Mwaka 2021 kulikuwa na Tamasha la Sanaa Bagamoyo tarehe 28 mpaka 30 Oktoba, lilifanyika mwaka jana. Tamasha hili kwa kweli lilikusanya watu wengi sana; wa ndani na wa nje ya nchi, makadirio ya Wizara wanasema kama watu 75,000 lakini mimi ninasema zaidi ya 100,000; yalikuwa makadirio madogo sana. Kwa kweli chuo hiki kinafanya kazi kubwa na chuo hiki kinaitangaza nchi yetu, kwa mfano mwaka 2021 Chuo cha Sanaa Bagamayo wamechukua *Uni Award* ya mwaka 2020/2021 wameingia nusu fainali. Mwaka huo huo 2021 katika *Uni Talent* katika suala la kuimba wameingia fainali, katika *Taifa Cup*, katika masuala ya *bongo fleva* wameshika nafasi ya kwanza, katika *Uni Talens* ya 2022 katika suala la kuimba wameshika nafasi ya kwanza na vilevile wameiwakilisha nchi katika suala zima la kuhamasisha *Royal Tour* kule Marekani, wamefanya maonesho kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema Mheshimiwa Waziri hiki chuo kinatakiwa kiangaliwe kwa jicho la tatu, siyo macho mawili; maana yake ni chuo ambacho kinafanya kazi kubwa sana. Nimeona katika bajeti ya mwaka huu 2022/2023 chuo kimetengewa shilingi milioni 550 kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kufundisha, kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu, mabweni, ukumbi, jengo la maji safi, maji taka, kununua vifaa vya uzio, kununua vifaa vya *tv*, kununua vifaa vya redio na kuweka mtambo wa redio

pale. Kwa hiyo hivi vitu naomba Mheshimiwa Waziri, kama mmedhamiria kuvifanya mvifanye kweli kweli kwa sababu hiki chuo kinatembelewa na watu wengi na hiki chuo kimefundisha wageni wengi sana.

Mheshimiwa Spika, miaka iliyopita mpaka wazungu walikuwa wanacheza ngoma pale, wengi kabisa, kabisa, wanakuja wanajifunza. Mimi hiki chuo natamani kukiita Chuo cha Kimataifa cha Sanaa Bagamoyo kwa sababu ni chuo ambacho kinatambulika dunia nzima na kazi kubwa inafanyika na waliopo pale viongozi wangu wanafanya kazi kubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri hebu jaribu sana kuongeza bajeti hii ya hiki chuo ili kiweze kuwa bora kiweze kushindana kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia, Mheshimiwa Waziri siku moja ulinidodosea na tulizungumzia kuhusu *sports arena* na ukanihakikishia siku moja ungeweza kufanya mpango tukapata *sports arena* pale Bagamoyo. Kwa sababu kuna Chuo cha Sanaa pale, kuna utalii Bagamoyo, ni jambo la msingi lile wazo lako kwa sababu sijaliona katika bajeti yetu ya mwaka huu. Naomba liwepo Bagamoyo ipatiwe *sports arena* kwa sababu ni sehemu ambayo ina utalii wa hali ya juu sana ukichukia na Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo pale cha Utamaduni, ukichukua na vivutio vya kitalii basi mkiweka *sports arena* pale mambo yatakuwa mazuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, niipende sana kuipongeza timu yetu au timu zetu za Serengeti, timu za wanawake kwa kazi kubwa wanayoifanya, nizipongeze timu zote za mpira wa miguu Tanzania, niipongeze klabu ya Yanga kwa hatua nzuri ambayo wanaendelea nayo, wanafanya kazi

kubwa. Na nawaomba wakaze msuli kwamba baada ya kuchukua kombe mwaka huu lisitoke ndani ya miaka nane mpaka tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Wizara kwa maandalizi ya hotuba nzuri ya bajeti, Mawaziri wa Wizara hii wana bahati ya kuwa na watendaji wenye weledi, namfahamu Katibu Mkuu Dkt. Abbas toka tukiwa naye kwenye media, akiwa *newsroom* ya *Business Times*-Majira, kadhalika Ndugu Yakubu ambaye pia amekaa *newsroom* za kimataifa, Ndugu Singo Mkurugenzi wa Michezo ni mtu *open minded,* kwa hiyo Wizara ina kila sababu ya kuacha alama *(legacy)*.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *TFF* kwa kuwezesha na kufanikisha ushiriki wa timu zetu za Taifa zote kuanzia za vijana, wanawake na wakubwa. Tunajua ni mzigo mkubwa sana, lakini wanajitahidi sana,

Ushauri wangu kwanza ni kuhusu kufungia fungia, nashauri pamoja na kuwa ni kanuni ambazo vilabu vimejitungia kwa kushiriki katika kuzitunga, *TFF* wasaidieni ili tuwe na adhabu mbadala, kumfungia mtu miaka mitano ndugu zangu *put yourself in such a position!*

Mheshimiwa Spika, tulipitisha sheria kwamba 5% ya zawadi ya mshindi iende kuimarisha michezo, nashauri fedha hii kwa kuanza tuutupie jicho mchezo wa riadha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye mchango wangu wa kuzungumza, tuepuke kuingilia uchaguzi wa *TWF* na hapa kwa nia njema nawashauri *TFF,* waacheni wanawake wachaguane kwa huru na haki, hakuna asiyejua kuwa *TFF* kwa ujanja ujanja walivuruga uchaguzi wa *TWF,* matokeo yake mpaka sasa *TWF* haina mwakilishi katika Kamati ya Utendaji ya *TFF,* hili suala tukilitizama katika jicho la jinsia, linaleta tafsri ambayo sio nzuri. Wizara kama kiongozi na msimamizi mkuu naishauri suala hili liishe, hakuna jambo ambalo linasemwa lisiwafikie familia ya michezo. Baadhi ya viongozi wa *TFF* kauli zao katika suala hili sio jema, tujitafakari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa (Mb) pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Paulina Gekul (Mb). Nawapongeza pia Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, watumishi wote wa Wizara na wanasanaa na michezo wote.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza timu ya wanawake *Twiga Stars* na kwa namna ya pekee nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kujitoa kuhamasisha utalii na michezo ikiwemo kuwafadhili vijana wa *Twiga Stars* pamoja na kuwapatia

viwanja kwa ajili ya maisha yao ya mbele. Napongeza pia kwa kuwaenzi waasisi wetu kupitia sherehe na makongamano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu; kwanza Wilaya ya Nyasa katika kuimarisha michezo tumeamua kuanza kujenga uwanja wa michezo. Tunaomba *support* yenu ya hali na mali ikiwemo kusaidiwa nyasi za bandia na michango ya fedha kutoka kwa wadau mbalimbali na pili, tunaomba pia mtutembelee Nyasa ili kutuhamasisha.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia amani, upendo, afya, mshikamano na utashi wa kisiasa katika Taifa letu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi wao thabiti katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2022-2025.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote Serikalini, kwa kuzitumikia vizuri sana nafasi zao kikamilifu, hongereni.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge letu; tunaiomba Serikali itoe mpango kazi wa shughuli za michezo kwa Kamati za Wilaya na Mikoa ili kufanikisha

uibuaji wa vipaji vya michezo kwa vijana wetu kutoka ngazi za shule za msingi, sekondari na wilaya ili kuwalea na kuendeleza vijana wetu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iajiri maafisa michezo na utamaduni katika halmashauri zote nchini ili kufanikisha maendeleo ya michezo hapa nchini na pia tunaiomba Serikali ifanye utaratibu wa kuendeleza viwanja vya michezo kama vile uwanja wa michezo wa *Nyerere Stadium,* Mbulu kwa kuingia ubia na Chama cha Mapinduzi kwani hali ya hewa ya Mbulu ni nzuri sana kwa michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUSTUN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, kuna haya mashindano ambayo yanaandaliwa na Waheshimiwa Wabunge yaani mfano *Mchengerwa Cup, Bashungwa Cup* na mengine, hivi haiwezekani kutenga bajeti kidogo na kuchangia kama ambavyo Mfuko wa Jimbo upo? Jambo hili litakuza michezo majimboni na kuwapunguzia Wabunge mzigo mkubwa wa kununua mipira na jezi. Tunaweza kutumia fedha ya Mfuko wa Michezo kwa namna hiyo fedha hiyo itawanufaisha watu wa kipato cha chini vijijini kwetu. Hata kila jimbo likipata mipira 100 na seti kadhaa za jezi tu itasaidia sana kwa kuanzia

**MHE. ABEID R. IGHODO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo; kwanza kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya ya kuiheshimisha

nchi yetu katika sekta ya utamaduni, michezo na sanaa na kuwapongeza Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa ni kuhusu kufanyika kwa matamasha ya utamaduni; Wizara ione namna bora ya kuendelea kuenzi utamaduni wa Mtanzania. Kwa mfano leo tarehe 6 na 7 Juni, 2022 Mkoani Shinyanga linafanyika Tamasha la Utamaduni wa Msukuma pamoja na kuzindua Kijiji cha Makumbusho ambapo itakuwa sehemu ya kupata historia ya eneo hilo kuanzia utawala wa kimila na desturi za Wasukuma. Sasa ni vyema Wizara ikatambua jitihada za Mkoa wa Shinyanga kwa kuwa imetekeleza kwa vitendo agizo la Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan la kuandaa matamasha ya utamaduni lakini pia iwe ni chachu kwa Mikoa mingine kuweza kufuata mfano huo ili na maeneo mengine nayo yawe na vijiji vya makumbusho na itaweza kuwa kama sehemu ya utalii ambapo itasaidia kwa wananchi kujua asili ya makabila na historia zake, lakini pia itasaidia kuongeza vyanzo vya mapato kutoka kwa watu watakaotembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nashauri ili kuenzi utamaduni wa Mtanzania, itengwe siku au wiki ya utamaduni kwa nchi nzima ambapo mikoa yote itatumia vijiji ambavyo vitajengwa kwa kushirikiana na machifu ili Taifa liwe na siku ya kuenzi utamaduni wake. Lakini pia katika kukazia siku hiyo kuwe na sehemu ambayo itakuwa ya kitaifa ambapo kila mwaka mnaweza kufanya mzunguko *(rotation)* ili liwe na ladha tofauti.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuweke utaratibu wa kuandaa au kuchapisha vitabu vya kihistoria ambavyo vitaonesha asili ya kila sehemu kwa wakati huo na namna

utawala wa kimila ulivyokuwa ili kuongeza wigo wa utalii kupitia fasihi andishi kwa kuwa vitabu hivyo vitakuwa vikielezea utamaduni wa kila mikoa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa hotuba nzuri iliojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(nation competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inastahili pongezi kwa kuwezesha timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya

miaka 17 kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Dunia. Pia naipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mkakati katika kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa na vilabu katika michezo na michuano mbalimbali ya kimataifa na kikanda. Kama sehemu ya mkakati huo Wizara iweke msukumo zaidi wa kuhamasisha kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo hususani vya mpira wa miguu. Viwanja vingi vya mikoani vipo katika hali mbaya na kwa kiasi kikubwa ni sehemu ya changamoto katika maendeleo ya michezo nchini. Michezo na sanaa ni muhimu sana katika kujenga sura na sifa ya Taifa letu *(nation brand*). Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha inaweka umuhimu mkubwa wa ushiriki wa timu zetu za Taifa na kuwepo kwa mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha timu zetu za Taifa na vilabu zinafanya vizuri kwenye mashindano ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu katika michezo na sanaa ni nguzo muhimu katika kutekeleza Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Serikali itenge bajeti ya kutosha kuhakisha tija katika ushiriki wetu katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuboresha miundombinu ya viwanja, Wizara ijikite katika kuibua vipaji mbalimbali vya michezo na sanaa kwa kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine hususani Elimu na TAMISEMI. Pamoja na kutokuwepo kwa miundombinu rafiki, mikoa mingi imekuwa inatoa wachezaji wenye vipaji vikubwa katika mpira wa miguu, riadha na hata sanaa mbalimbali. Imefika muda sasa wa kuwepo kwa mkakati

wa kuibua na kuendeleza vipaji hivyo ambavyo vimekuwa vinaonekana kikanda zaidi kama vile riadha kwa Mikoa ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kati. Pia kwa upande wa mpira wa miguu kumekuwepo na mikoa kadhaa ya vipaji vikubwa na huko ndio Serikali iweke msukumo zaidi wa kuibua na kuendeleza hivyo vipaji. Hata kwa wasanii, kuna mikoa imekuwa inatoa idadi kubwa ya vipaji kwenye uigizaji, uimbaji ikiwemo nyimbo za injili ambazo zinapata umaarufu sana duniani. Kutokana na vipaji vingi vya michezo hususani mpira wa miguu na riadha, napendekeza Shule ya Sekondari Santilya ya Wilaya ya Mbeya iongezwe kwenye orodha ya shule teule za michezo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Kiswahili kuwa lugha rasmi kimataifa, napendekeza uwekezaji zaidi katika kuitangaza na pia kuwezesha ulimwengu kujua kuwa mizizi na ustawi wa Kiswahili ni Tanzania pekee na wengine wanaigiza kwetu. Serikali iendelee kuchukua hatua zaidi ya kukistawisha Kiswahili katika mataifa mengine Barani Afrika na kwingineko kwa kushirikisha vyuo vikuu hapa nchini na vyuo vikuu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Ndugu Mohamed Mchengerwa na Naibu wake Mheshimiwa Pauline Gekul pamoja na timu ya wataalamu Wizarani kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuipongeza timu yetu ya soka ya wasichana ya *Serengeti Girls* kwa hatua kubwa ya kuingia fainali ya kombe la dunia itakayofanyika huko India kuanzia tarehe 11.10.2022 hadi 30.10.2022.

Mheshimiwa Spika, soka la wanawake nchini Tanzania linakua kwa kasi ya ajabu na timu hizi zimeonesha mafanikio makubwa ukilinganisha na zile zinazotoka ukanda wa *CECAFA, COSAFA* na zile za Kanda za Afrika Magharibi.

Mheshimiwa Spika, timu hii imetupa heshima kubwa kwa hiki kilichotokea, soka hili la wanawake Tanzania limefanikiwa kuitangaza vyema nchi kupitia timu ya Taifa ya *Twiga Stars* na *Serengeti Girls* ambazo zimeweza kutwaa vikombe mbalimbali, kushinda katika mechi kubwa za kimataifa na kuipaisha nchi yetu katika viwango vya soka Barani Afrika na duniani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya kubeba makombe mbalimbali na kuingia fainali ya kombe la dunia kwa wasichana wenye umri wa chini ya miaka 17, soka la wanawake nchini linakabiliwa na changamoto kubwa za aina mbalimbali, na ninazitaja kama ifuatavyo; kwanza kuna wakati maandalizi ya timu za taifa za wanawake kushiriki katika mashindano huwa duni sana; pili, kumekuwa kuna tatizo la kuibua vipaji vya wachezaji kutoka ngazi za vijiji, kata, wilaya na mikoa na tatu, kuna tatizo la uhaba wa makocha na waamuzi wa kike hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nne, kuna tabia ya wasichana wanaocheza soka kuiga tabia za kiume na hivyo

kupoteza uhalisia wao kama wasichana. Tabia hiyo imehusisha uvaaji wa suruali, pensi, fulana na kofia za kiume. Vilevile wachezaji wengi wameiga kutembea kitemi kama watoto wa kiume. Kwa mawazo yangu, kitendo hiki kimesababisha wasichana wetu wakadhalilishwa huko Cameroon kwa kuhisiwa kuwa walikuwa wavulana.

Mheshimiwa Spika, tano, changamoto nyingine kubwa ya kukua kwa soka la wanawake ni kukosekana kwa wadhamini wengi wa kueleweka

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha changamoto hapo juu, ninaishauri Serikali ichukue hatua zifuatazo; kwanza Serikali itenge bajeti ya kutosha kuhudumia kambi ya Taifa ya timu za wanawake; pili, ili kuibua vipaji, soka la wasichana lianze kuchezwa katika ngazi za shule za msingi na sekondari. Hii ni pamoja na kuwa na mashindano ya aina mbalimbali kwa watoto hawa katika ngazi ya wilaya, mikoa, UMITASHUMTA na UMISETA.

Mheshimiwa Spika, Serikali iandae mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa walimu na waamuzi wa soka la wanawake na pia Serikali kupitia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* liwekeze kikamilifu katika soka la wanawake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihamasishe makampuni ya udhamini yawekeze kwenye soka na ligi za akina dada kwani wamefanya vizuri kimataifa ukilinganisha na zile soka na ligi za wanaume. Ushiriki wa wanawake katika soka utakuwa zaidi kama wadau zaidi watajitokeza na

kuwainua na kutoa sapoti kwa wanamama ambao wanajitoa kwa ajili ya maendeleo ya soka la wanawake.

Mheshimiwa Spika, ninashauri mamlaka husika ziwahimize wachezaji wa kike kuvaa mavazi ya kike na matendo yao yawe kama ya watoto wa kike kwani huko Ulaya na kwingineko, wanasoka wanawake huwa na kila sifa anayostahili kuwa naye mtoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hajaanza kuchangia Mheshimiwa Naibu Waziri, nimesimama hapa kwa ajili ya heshima ya wageni waliyoko humu Bungeni mchana huu wa leo ili niwatangaze; na hawa wengine naambiwa asubuhi walikuwepo lakini hawakupata nafasi ya kutangazwa.

Kwanza ni Ndugu Wallace Karia ambaye ni Rais wa *TFF,* haya naona alikuwepo asubuhi hajapata fursa ya kurejea, lakini naambiwa alikuwa ameongozana na Ndugu Almas Kasongo ambaye ni *CEO* Bodi ya Ligi, haya nadhani wote watapata salamu kwamba asubuhi nadhani kulikuwa kuna kupitiwa majina yao hayakuletwa hapa mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wako hapa ndani, wote wasimame kwa pamoja wageni wa Waheshimiwa Wabunge, haya karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine waliyoko hapa ndani ni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa

Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambao ni watoto wake, wako upande gani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo hapa ndani pia na hawa ndiyo wengi zaidi viongozi na vijana 320 kati ya vijana 1,276 wa UVCCM walioshiriki kwenye *Vijana Ngorogoro Green Tour* kwa ajili ya ku-*support Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Sasa ngoja nimalizie kuwasoma mkiwa msimama bado, hawa ni vijana 320 kati ya vijana 1,276 walioshirikia kwenye *Vijana Ngorongoro Green Tour* ku-*support Royal Tour* iliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na hawa wameongozwa na Katibu Mkuu UVCCM Ndugu Kenani Kihongosi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mussa Mwakitinya ambaye ni Naibu Katibu Mkuu UVCCM, na katika kundi hili wapo pia Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Chama cha Mapinduzi, karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine yatatangazwa baadaye, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, achangie, halafu mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Wizara yetu siku ya

leo. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujaalia afya njema sisi sote humu ndani kuweza kuiona siku hii lakini tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kuendelea kuniamini kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Mheshimiwa Rais nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia Wabunge wenzangu ambao wewe unatuongoza katika Bunge hili tukufu kuendelea kuwa washauri katika Wizara yetu, siyo washauri tu, lakini wewe binafsi wewe pia ni mwanamichezo mwenzetu, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao pia mmetukumbusha katika hotuba yetu kuwaweka pale ambapo tumesahau mtuwie radhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo imekuwa ikitusimamia na ikitushauri kwa niaba ya Bunge zima katika masuala mbalimbali kwa ajili ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru Waziri wetu, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, amekuwa kiungo kwetu sisi wasaidizi wake, lakini amekuwa akitushauri kwa upendo, amekuwa akitusisitiza tushikamane sisi kama Wizara na wasaidizi wake tumekuwa na amani sana kufanya naye kazi na ndiyo maana mambo yanakwenda, Mheshimiwa Waziri tunakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini ambao wameendelea kuniamini na kunifanya Mbunge wao, niwaahidi kwamba jambo letu la maendeleo liko palepale na tutafikia *Inshallah* Mwenyezi Mungu atutangulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru familia yangu kwa maombi yao lakini pia watanzania kwa maombi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache kwa shukrani naomba sasa nipitie kwa haraka haraka baadhi ya hoja za Kamati na hoja Waheshimiwa Wabunge wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja namba moja ambayo nilitaka kuzungumzia ambayo imetokana na Kamati ni hoja inayosema kuibua vipaji vya michezo, Serikali ina mkakati gani. Mikakati yetu tumeeleza pia katika hotuba Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri, lakini nitaje baadhi. Baadhi ya mikakati tuliyonayo ni pamoja na kuanzisha shule maalum kwa ajili ya michezo, hizi *academy* za michezo 56 kote nchini. Lakini mnakumbuka Mheshimiwa Rais pia alituelekeza kwamba turudishe *Taifa Cup* ambayo ilichezwa mwaka jana na mwaka huu pia tuko kwenye ratiba hiyo. Lakini pia kupitia Taifa *Cup* tumekwenda tena mwaka huu kwenda mtaa kwa mtaa ndiyo mpango wetu tumesema kwenye bajeti yetu, kuhakikisha kila mtaa, kila kata tunaenda kuibua vipaji na ndiyo maana tunaomba bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni uwekezaji katika wataalam ya michezo, Kamati imeshauri na imesisitiza jambo hili, sisi kama Wizara tumeona ni jambo la msingi

sana kwa sababu tukiibua vipaji toka kwenye ngazi za chini lazima tuwe na wataalam. Ndiyo maana katika mpango wetu huu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mmeona tumeweza kuweka fedha kwenye Chuo chetu cha Malya, kuhakikisha kwamba kozi pale zinatolewa. Lakini pia wanachuo wanaokwenda pale tunawajengea hosteli waweze kutulia, wapate mafunzo tukishirikiana na Wizara ya Elimu kwa upande wa mitaala. Kwa hiyo, Wizara imeshaona hili lakini pia tunashirikiana pamoja na mashirikisho, BMT tunashirikiana nao ili kuhakikisha kwamba wataalam hawa wanapatikana.

Kwa hiyo, sisi tushukuru Bunge lako tukufu limeendelea kututengea fedha kupitia Wizara hii kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo. Kazi mojawapo ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika vizuri ni pamoja na kuibua wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine la usimamizi wa vyama na mashirikisho liachwe kwa wadau wenyewe. Hili jambo sasa ndivyo lilivyo, sisi kupitia BMT, kupitia Msajili wa Vyama vya Michezo tunasimamia katiba zao na tunahakikisha kwamba wanachama wanatendewa haki na Mheshimiwa Waziri alishamteua Msajili, mwanzoni tulikuwa hatujampitisha lakini amepatikana, tunaamini Waheshimiwa Wabunge zile kero ambazo ziko kwenye vyama, ziko kwenye mashirikisho zinakwenda kusimamiwa kupitia BMT. Lakini Katiba za vyama zinasimamiwa ili wanachama watendewe haki.

Mheshimiwa Spika, lingine ilikuwa ni kwa nini mshahara umepungua katika Wizara hii ilikuwa ni hoja ya Kamati. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, fedha hizi

zimepungua kutoka kwenye Wizara yetu baada ya Mheshimiwa Rais kupunguza majukumu ya Wizara yetu ya Habari kuondolewa kwetu, zaidi ya bilioni sita zimeondoka na Idara ya Habari kwenda kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niende kwenye hoja za Wabunge baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Bulaya na Wabunge wenzangu tunapokea pongezi zetu zote ambazo mmetupatia kwa ujumla na tunazithamini. Mheshimiwa Bulaya ameshauri kwamba Serikali iandae fedha kwa ajili ya timu yetu ya *Serengeti Girls*.

Kwanza niwapongeze sana hawa mabinti zetu, niwapongeze kwa moyo wa dhati kwa sababu jana mwenyewe nimeshuhudia jinsi ambavyo ule mchezo ulikuwa mgumu sana dhidi ya Cameroon. Mheshimiwa Waziri nashukuru uliniamini nikuwakilishe kule, lakini wale watoto walipambana kuhakikisha bendera yetu inapeperushwa na tunashinda, pamoja na ngumi, pamoja na adha zote walizozipitia hawa vijana wametuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunawathamini, tunawapenda na Taifa linawapenda, lakini hatukuwa nyuma kuwawezesha, tumetumia zaidi ya milioni 140 kuwawezesha mpaka wamefika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru BMT, tunashukuru *TFF*, tunashukuru Chama cha Mpira wa Wanawake kuhakikisha vijana hawa wanapata stahiki zao, kwa kweli hawakupungukiwa. Pia mwaka unaofuata tumetenga

zaidi ya Milioni 985 kwa ajili ya kuhakikisha hizi timu zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilikuwa ni uwekezaji wa mpira wa wanawake mpaka ngazi za chini, nikuhakikishie kupitia Taifa Cup, kupitia viwanja tunavyovijenga tunazingatia viwanja vya *Netball*, pia kule mpira hautachezwa wa miguu tu ni pamoja na *Netball* tutahakikisha unachezwa na viwanja vinajengwa sambamba na viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu CHANETA iwezeshwe kifedha. Tunawapongeza BMT wamesimamia uchaguzi wa CHANETA umefanyika, wamekuja mpangokazi wao wa miaka kumi kuhakikisha kwamba wanafufua mpira wa Netball hapa nchini. Mheshimiwa Bulaya nikutoe wasiwasi kwamba jambo hili tunalifuatilia kwa karibu sana mimi kama Naibu Waziri, Waziri na timu nzima ya Wizara kuhakikisha CHANETA mpangokazi wao watakaotuletea tutawakutanisha na wadau mbalimbali na wao waweze kupata ufadhili. Tumeshawaambia watuletee *writeup* zao ili kuhakikisha kwamba na wao wanaweza kupata ufadhili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja za jumla. Mheshimiwa Profesa Mkumbo amezungumza jinsi ambavyo sheria inatakiwa irekebishwe kuhakikisha kwamba starehe hatuiwekei mipaka kama ni usiku, asubuhi kuna mtu anataka kustarehe, tuongee na Wizara zingine kuhakikisha kwamba sheria hii inarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la riadha nchini. Ninaliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yetu tumeamua kutenga

Mikoa kulingana na vipaji vyao. Kwa upande wa riadha tumeteua si chini ya Mikoa, Manyara, Arusha, Singida ambapo Kaka yangu Simbu anatoka, Mara na Mbeya. Tunawahikikishia Waheshimiwa Wabunge tutaibua vipaji vya riadha kuanzia ngazi za chini kabisa mpaka kuja juu tutapata vijana wazuri sana, huo mkakati tunao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la Kaka yangu Mheshimiwa Hamis Mwijuma kuhusu *COSOTA* naomba nilisemee kwa dakika kadhaa ambazo zimebaki. Kwanza tunakubali kwamba hoja zote ambazo Wasanii hawa wamekuwa wakizungumzia kuhusu *COSOTA* ni za kweli, pia niwapongeze kwa kuwa mmekuwa wakweli. Mheshimiwa Babu Tale amesema kama ni gari lipo barabarani linaanza kazi, tunashukuru kwa kulitambua hilo. Kuna mambo matatu kwenye suala la mirabaha.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni suala la mirabaha hii inapatikana wapi. Mheshimiwa Mwijuma ninakushukuru kwamba ilikuwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, nasi tumeyafanyia kazi, tumekaa na Wizara ya Fedha kuhusu *blank tape Levy* ianze kufanyiwa kazi. Tunashukuru Wizara ya Fedha wamepokea, naomba tusiwahishe shughuli tuwasubiri kwenye *Finance Bill* watuambie sasa wame-*adopt* mambo gani. Pamoja na nyasi bandia tumepeleka zile *accessories* kwa ajili ya kuweka nyasi kwenye uwanja, inahitajika kuna vitu vinahitajika vipunguzwe kodi vyote tumepeleka. Hili la kwenu mlihitaji kwamba tuwe na chanzo ambacho ni cha uhakika kwa ajili ya mirabaha, mkasema kwamba kule kwenye Halmashauri zetu tulikuwa na Maafisa Utamaduni wakusanye, washirikiane na Maafisa Biashara katika *Hotel*, *Restaurant* na maeneo mengine. Jambo hili COSOTA wamejaribu na ndiyo *failure* ambayo ninyi

mmekuwa mkiongelea, lakini *wewe* mwenyewe ulituletea swali ukihitaji kwamba *CMOs* zenu zikusanywe.

Mheshimiwa Spika, hayo yote tumepokea na ahadi yetu kama Wizara kwa tasnia hii ni kwamba tutakutana na wadau, tutapitia haya yote lakini pia *Finance Bill* itakapoletwa maana yake sasa kama kutakuwa na *adoption* ya *Blank Tape Levy source* itakuwa imepatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika hili la COSOTA ilikuwa ni suala zima la *distribution* ya mirabaha, tunapokuwa tumepata tunagawa vipi, mfumo uko wapi? Ninakiri kwamba ni lazima tuwe na mfumo ambao utawekwa kwenye redio zote, *television* zote, media zote ambazo zitakuwa zinacheza nyimbo hizi ili ijulikane ni wimbo upi ambao umechezwa wapi. Hii ya juzi siyo kwamba tuligawa tu kama zawadi hapana! Tulitumia mfumo ambao unatumika kidunia.

**SPIKA:** Malizia sentensi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Suala hili tulitumia mfumo unaitwa *WIPO* ambao wao wanaufahamu, ambao unakubalika *worldwide* na zile nyimbo nani kapata nini ilipatikana pale. Tatizo tulikuwa na pesa chache sana, tulikuwa na Milioni kama Mia Tatu ambazo ukizigawa mtu anaona amepungukiwa kidogo ndiyo maana tunasema sasa redio zote, kwa sababu ule mrabaha tulitoa ulitokana na redio kama tisa tu kati ya redio zaidi ya Mia Mbili. Ninaomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wenzangu hili jambo Wizara

tumelipokea na tunalifanyia kazi baada ya Bajeti hii tutakutana tuhakikishe kwamba tunakwenda vipi na tunawahakikishieni kwamba haki zenu mtapata.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamuita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakushukuru tena, asubuhi nilipata fursa ya kukupongeza na kukushukuru kwa bahati mbaya ulikuwa kwenye majukumu mengine mazito ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ninaishukuru sana Kamati ya Bunge ambayo imekuwa ni mshauri mzuri wa Wizara hii, tumepokea maelekezo, tumepokea maoni yote ya Kamati na yale maeneo yenye mapungufu mawili, matatu tayari Naibu Waziri amekwisha yatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, siku ya leo kumekuwepo na wachangiaji zaidi ya 20 na wachangiaji wengi toka asubuhi wamekuwa wakitupongeza Wizara, hivyo Wizara tunalichukua hilo kama deni ili tuende tukafanye vizuri zaidi. Ukiangalia maelezo yetu Wizara, hotuba yetu imejikita katika taarifa ambazo kwa kweli msingi wake ni Bunge, ndiyo maana tunaipongeza sana Bunge, tunawapongeza sana Wajumbe wa Kamati

wakiongozwa na Mwenyekiti mahiri kabisa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kwa kutushauri, kwa kutupa maoni na kimsingi naomba niwaambie Watanzania kwamba Wizara hii itaongozwa na ubunifu, Wizara hii itaongozwa na weledi pia Wizara hii itaongozwa na uchapakazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ya wananchi kwa msingi wake kwa sababu wananchi wanaitegemea izara hii katika kuleta furaha na faraja, kwa mantiki nyingine Wizara hii ni Wizara ya furaha na faraja kwa Watanzania. Jukumu letu kubwa tutaiponya mioyo ya Wasanii. Ninaahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tunakwenda kuponya mioyo ya wanamichezo pia tunakwenda kuimarisha utamaduni, hivyo haya naomba niweze kuyaweka vizuri kabisa katika Bunge lako Tukufu kwamba tutakwenda kuchapa kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba ile kazi ambayo tuliianza nayo tunakwenda nayo mbele ili Kwenda kuleta faraja kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja chache ambazo Naibu Waziri hakupata fursa ya kuzitolea ufafanuzi wa kina, hapa ninaomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja chache ambazo ninaamini Watanzania wanatamani kuzisikia. Imeibuka hoja hapa kuhusu suala la ZFF, FIFA, CAF na TFF. Eneo hili Wizara tunahitaji kuendelea kulifanyia kazi sana ili Watanzania waweze kuwa na furaha kwa pande zote mbili. Ninachukua fursa hii kulitangazia Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara ya kwanza kabisa katika historia, tumekuwa na ushirikiano wa karibu kabisa baina ya Wizata yetu ya Michezo, Utamaduni na Sanaa pamoja na Wizara ya Michezo ya Zanzibar, tumeshirikiana na karibu sana, nichukue fursa hii

kumpongeza Waziri wa Michezo Zanzibar, amefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba timu yetu ya Serengeti Girls iliweka kambi Zanzibar toka tunaanza mashindano ya kulekea Kombe la Dunia, kwa hiyo ninawapongeza sana Viongozi wa Zanzibar, leo nafikiri tulikuwa nae Rais wa ZFF hapa Bungeni. Kwa mara ya kwanza kabisa katika historia miongoni mwa Wajumbe ambao niliwateua kuingia katika Baraza la Michezo BMT, mmoja wa Wajumbe katika Baraza la Michezo anatoka Zanzibar. Pia tumewashirikisha wenzetu kutoka Zanzibar katika baadhi ya Kamati mbalimbali muhimu za nchi yetu katika kuendeleza michezo hapa nchini, hivyo Wizara tunashirikiana vizuri.

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kazi kubwa inayofanya na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, pia ni lazima tupongeze na tukiri kazi nzuri inayofanywa na Rais wa Awamu ya Nane wa Zanzibar, ni kazi kubwa na nzuri. Tunaliahidi Bunge lako Tukufu kwamba eneo hili tutakwenda kulifanyia kazi, msemo ambao napenda niutumie hapa ni kwamba hakuna mkate mgumu mbele ya chai, hivyo katika Wizara hii hakutakuwa na jambo gumu, kila jambo tutahakikisha tumelifanyia kazi na kulitatua kwa mustakabali wa Taifa letu. Hivyo naomba niwashauri Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwasi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo lilizungumzwa hapa ni kuhusu Chama cha Mpira wa Miguu wa Wanawake (*TWFA*) kwamba kifanye uchaguzi. Watanzania wanataka mabadiliko, wanataka mabadiliko

katika sekta ya michezo, eneo hili ninatambua Mheshimiwa Mbunge amelizungumza hapa, lakini kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa miongozo, utaratibu wangu ni kufuata utaratibu. Ninatambua Mheshimiwa Mbunge anaweza asiridhike na majibu haya lakini siwezi kuwa na majibu mazuri ya kumfurahisha zaidi ya haya ninayoyasema sasa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana huko nyuma wenzangu hawakufuata taratibu lakini mimi nitanyooka kwenye taratibu. Ninawathibitishia kabisa kwamba *TWFA* haina wanachama katika baadhi ya Wilaya, haina wanchama walisajiliwa katika baadhi ya Mikoa, tayari nimeshawaagiza wenzangu katika Mikoa na Wilaya kuhakikisha kwamba wanaharakisha michakato ya kupata wanachama wa *TWFA* ili tuweze kuwapata Viongozi ambao wamechaguliwa katika misingi ambayo wanachama wao wenyewe wamewachagua. Kwa hiyo, inawezekana nisiwe na majibu mazuri hapa, lakini ninawathibitishia Waheshimiwa Wabunge, inawezekana tulikuwa hatufanyi vizuri kwa sababu tulikuwa hatufuati utaratibu.

Mheshimiwa Spika, nyakati zangu hizi tutahakikisha tumejikita katika misingi ya kufuata taratibu ili tuweze kufanya vizuri. Ninakuomba Mheshimiwa Mbunge ninatambua majibu haya hayawezi kukufanya ushindwe Ubunge lakini sitakuwa na majibu mazuri zaidi ya haya ninayokuambia kwamba watu wafuate taratibu nami nitajikita katika misingi ya taratibu. Hayo ndiyo majibu yangu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Uwanja wa Dodoma, Serikali yetu ya Awamu ya Sita imedhamiria

hakika katika kuhakikisha kwamba uwanja wa Dodoma unajengwa. Ninaomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba dhamira na ndoto za Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba Tanzania tunaendesha mashindano ya Afrika ya mpira wa miguu ifikapo mwaka 2027, hizi ndizo ndoto za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Katika maeneo ambayo Wizara yetu imeyapa kipaumbele ni ujenzi wa uwanja wa Dodoma. Naomba niwathibitishie Wabunge kwamba Wizara hii itaongozwa na mikakati, itaongozwa na weledi na uchapakazi, hatutajikita katika sehemu ambayo tumefungwa na bajeti tu. Viongozi katika Wizara hii tumekubaliana kila mmojawepo kuhakikisha anachapa kazi, tunajiongeza tusifungwe na mipaka ya bajeti tuliyonayo, huu ndiyo msingi ambao nimeujenga katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika Wizara tayari tumeshafanya vikao kadhaa na wadau wa michezo. Naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba tayari tumepokea wadau mbalimbali wa michezo zaidi ya Saba ambao wako tayari kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa uwanja wa Dodoma na tayari tumekwishaonesha michoro ya uwanja wa Dodoma, mchakato wetu ni kuhakikisha kwamba uwanja huu umejengwa ndani ya miezi 17, pengine baada ya kuahirishwa kwa Bunge hili Tukufu tutaendelea na michakato ya kumpata mdau ambae atashirikiana na Serikali katika ujenzi wa uwanja huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwathibitishie Watanzania wote kwamba Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Nchi, tutahakikisha kwamba tunajenga uwanja wa kisasa, siyo uwanja tu wa kawaida, nimewaagiza wenzangu, tumepokea michoro ile ya awali lakini tumesema kwamba hatuwezi kuwa na uwanja ambao

unatumika tu kwa ajili ya mpira wa miguu, tunataka tupate uwanja ambao utakwenda kutumika katika kuendesha mikutano mbalimbali, kuwepo na *shopping mall* ndani, maduka mbalimbali pia kuwepo na ofisi. Dhamira yetu ni kujenga uwanja wa kisasa kabisa, hii ndiyo ndoto ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba uwanja wa Dodoma umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi kati ya timu ya Yanga na Simba ambalo limezungumzwa hapa, Wizara tayari tumekaa na Wizara ya Fedha nae neo hili ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wasiharakishe kwa sababu tayari Waziri wa Fedha amelichukua na pengine kwa kuwa tunae siku ya kesho hapa ataweza kulitolea ufafanuzi wa kina kabisa eneo hili la kodi kwa sababu linaangukia katika Wizara yake, lakini mimi Waziri mwenye dhamana kwenye eneo hili tutaendelea kushirikiana na Waziri wa Fedha kuona ni namna gani tunaleta nafuu kwa Watanzania ambao wamejitolea kuendesha michezo hapa nchini hasa timu hizi kubwa za Yanga na Simba. Tumelipokea suala hili na tutakwenda kulifanyia kazi, ninaamini kwamba kwa kuwa maandalizi ya *Finance Bill* yanaendelea Waziri wa Fedha atakuja kulitolea ufafanuzi wa kina kabisa eneo hili. Serikali tumelipokea na tutakwenda kulifanyia kazi kwa maslahi na maendeleo ya mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ujenzi wa *Arena*, viwanja vya sanaa, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba tayari Wizara imeshakaa na Wadau mbalimbali ambao wamejitokeza kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa viwanja vya Sanaa. Tunakwenda kujenga viwanja ambavyo pengine kwa mara ya kwanza

Afrika vitakuwa ni vizuri na bora kuliko viwanja vyote Afrika. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam tunategemea kujenga uwanja ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua na watu 16,000 mpaka 20,000 pia kwa Mkoa wa Dodoma tunakwenda kujenga uwanja utakaochukua watu takriban 15,000. Eneo hili michakato yote imekamilika, michakato ya maongezi na wadau imekamilika, hatua ambayo tumebakiza hivi sasa ni ya majadiliano baina yetu na wadau ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza Kwenda nalo na kulikamilisha eneo hili, lakini Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inayo dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tumejenga *Sports and Arts Arena.*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu kwa mara ya kwanza ifikapo mwaka 2023 pengine anategemea ku-*host* mashindano ya kutafuta wanasanaa bora hapa Afrika, *MTV Music Awards*. Kwa mara ya kwanza kabisa Afrika ni dhamira ya Mheshimiwa Rais anataka kuona pengine mashindano ya kuwatafuta wanamziki bora yamefanyika katika viwanja vyetu vya Sanaa. Hili tunaenda kulifanyiakazi Pamoja na wadau kuhakikisha kwamba Serikali imetekeleza eneo hili.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa eneo la *COSOTA* kuhusu mirabaha. Wizara ni lazima tukiri mapungufu ambayo tumeyaona kwenye eneo hili la mirabaha. Tumeshauriwa na Kamati pia Waheshimiwa Wabunge hapa wamelizungumza suala hili kwa kina kabisa wakibeba maono na maoni ya Wasanii nchini. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kama ambavyo nimesema awali, yapo mambo makubwa ambayo tumekwishaanza kuyafanya, katika eneo hili naomba niwaambie wenzangu akiwemo Mheshimiwa Babu Tale, kwamba mkate mgumu utawezekana mbele ya chai.

Eneo hili ni dogo sana, tutakwenda kulifanyia kazi. Mimi kama Waziri nimepata fursa ya kukaa na kuzungumza na Mameneja wa wanaoendesha kampuni ya Wazafi, nimezungumza nao. Nimezungumza na viongozi wao, Babu Tale mwenyewe, nimezungumza na Meneja Mkuu anayemsimamia Diamond Platnumz, pia nimezungumza na Diamond mwenyewe ili tuweze kwa pamoja kushikamana, tuzungumzie kero zetu na tuweze kuzitatua. Nimefanya mazungumzo hayo ili kwa pamoja tuweze kuleta manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto hizi na tayari Mheshimiwa Rais amekwishatupa maelekezo tarehe 31 Mei, kwamba tuhakikishe tunakwenda kuzimaliza changamoto hizi. Nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba tayari nilikwishatoa maelekezo kwa *COSOTA* kuhakikisha inashirikiana na wadau mbalimbali kutafuta mfumo mzuri ambao utatoa haki ili kila msanii mwenye haki aweze kupatiwa haki yake. Kwa hiyo hili tumelipokea na tutakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Sanga amelizungumzia hili eneo la ujenzi wa viwanja akitoa nukuu za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu, kwa mwaka huu wa fedha tunakwenda kukarabati uwekaji wa nyasi bandia na ujenzi wa viwanja vya kisasa kabisa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitangazie Bunge lako tukufu kuwa, tunakwenda kuweka nyasi bandia na kukarabati Uwanja wetu wa Jamhuri wa Dodoma. Kwa mwaka huu wa fedha tunakwenda kukarabati, ukarabati mkubwa ikiwa ni pamoja na kuweka nyasi bandia katika

Uwanja wetu wa Sokoine, Mbeya. Naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba tunakwenda kukarabati pamoja na kuweka nyasi bandia katika Uwanja wetu wa Sheikh Amri Abeid kule Arusha. Naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba tunakwenda kuweka nyasi bandia na kuboresha Uwanja wetu wa Mkwakwani uliopo kule Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba tunakwenda kuweka nyasi bandia na kukarabati Uwanja wetu wa Kirumba ulikoko kule Mwanza. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwa kiasi cha fedha ambacho Mheshimiwa Rais ametupatia kupitia Wizara ya Fedha tunakwenda kufanya ukarabati mkubwa katika Uwanja wetu wa Benjamin Mkapa pamoja na Uwanja wetu wa Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndoto za Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha kwamba Taifa letu linaendesha mashindano ya Afrika *(AFCON)* ifikapo mwaka 2027. Hii ndiyo sababu tumeanza kutenga kiasi cha bilioni kumi kwa ajili ya ukarabati mkubwa katika viwanja vyetu hivi. Tunakwenda kuweka nyasi bandia lakini pia tunakwenda kukarabati miundombinu ya ndani katika viwanja vyetu hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono; ahsante sana. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu; Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, ukurasa wa 488.

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 96 – Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.......................Sh. 5,692,247,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na hapa ninayo majina ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wanataka ufafanuzi juu ya jambo mahususi la kisera. Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, amezungumza vizuri sana, ametuahidi kama Kamati na

kama Bunge kwa ujumla, lakini nilisema na nilimuahidi Mheshimiwa Waziri nitaondoka na shilingi yake Morogoro Kusini Mashariki, lakini amesema kwamba mkate mgumu mwenzie chai, nataka tuione hiyo chai. Kwa kuwa ametamka kwamba mkate mgumu mwenzie chai, tunataka tuione hiyo chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Naibu Waziri ameongea kizungu, sisi watu wa Morogoro vijijini hatujui, kwenye utaratibu wa kugawa hizo pesa amesema huo utaratibu upo hata Ulaya; tuko Tanzania, atuelezee utaratibu upi, basi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumekiri upungufu uliojitokeza katika utaratibu wa ugawaji wa mirabaha. Hii ndiyo sababu mimi mwenyewe kama Waziri nimewaelekeza watendaji wa Wizara kuhakikisha kwamba wanakaa na wadau mbalimbali, hasa sekta binafsi ili tuweze kupata mfumo ambao utatusaidia Watanzania katika mgao wa mirabaha na kuondoa malalamiko yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimemwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara inawezekana utaratibu ambao tuliutumia huko nyuma haukuwa utaratibu rafiki. Nakiri kabisa kwamba pengine hata mimi nina wapenzi wasanii, nilitegemea na mimi baadhi ya wasanii wangu ningewaona mle kupata mirabaha lakini sikuwaona, kwa hiyo hata mimi nakiri

mapungufu. Hivyo, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka ujao huu upungufu hautajitokeza tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba nilipoteuliwa ni wiki kama mbili nadhani ndiyo mchakato wa ugawaji wa mirabaha ukaendelea, kwa hiyo taratibu tayari zilikwishaanza. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge yeye mwenyewe anatambua kwamba gari bovu linalotembea ni tofauti na gari bovu lililolala. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo hili tutakwenda kulifanyia kazi, asiwe na wasiwasi. Hili ni eneo dogo sana ambalo mimi pengine hata mkinipa mwezi mmoja nakwenda kulimaliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa hii misemo hii, sijaelewa gari bovu linalotembea tena, sisi tunajua ni gari zima, sasa ukisema tena gari bovu. Haya, Mheshimiwa Taletale amekaa kuashiria kwamba ameelewa maelezo yaliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Baraza la Michezo Tanzania katika kusimamia michezo kwenye ngazi ya wilaya limekasimu madaraka kwa Makatibu Tawala wa Wilaya, lakini hivi karibuni imeonekana michezo ikiendeshwa kiholela, haifuati taratibu, kanuni wala miongozo ya chama na kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua; ni ipi kauli ya Serikali kwa ajili ya kuondoa usumbufu huu unaojitokeza? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba katika nyakati tofauti Taifa letu limekuwa likiendesha michezo katika namna ambayo imetufanya kama Wizara tushindwe kuratibu michezo mbalimbali ambayo imekuwa ikiendelea. Kwa hiyo sisi kama Wizara tumekwishatoa maelekezo kwa wenzetu wa *TFF*. Pia tumekwishatoa maelekezo kwa viongozi wa michezo wa wilaya kuhakikisha kwamba michezo na mashindano yoyote yanayofanyika katika wilaya zao, basi ni lazima kwanza yapate vibali maalum katika wilaya husika, lakini pia yapate vibali maalum kupitia Shirikisho la Mpira wa Miguu *(TFF)*. Hii itatusaidia sisi kama Wizara kuweza kuratibu na kuwapata wale vijana wenye vipaji. Kwa hiyo naomba nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu tayari imekwishalifanyia kazi eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa ridhaa yako niwatangazie viongozi wote wa michezo katika Wizara na Shirikisho letu la Mpira wa Miguu kwamba Wizara haitegemei kuona mashindano yanaendeshwa katika wilaya zetu bila kibali au ridhaa ya Shirikisho la Mpira wa Miguu, lakini bila kibali au ridhaa ya wenzetu katika wilaya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo eneo hili tumelipokea na tunakwenda kulifanyia kazi ili tuweze kuleta tija katika uinuaji wa vipaji nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sima, naona umesimama.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa heshima kubwa sana ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa tamko lake hili. Naomba niambatane na barua rasmi kuhakikisha jambo hili linaisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umetoa ufafanuzi mzuri sana nikawa najiuliza; hilo katazo ni pamoja na, sijui, huwa naona watu wanaandika *Jimbo Cup*, sijui kitu gani, hilo katazo ni pamoja na *Jimbo Cup*, kwamba haziruhusiwi mpaka ziombe kibali *TFF*?

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwatangazia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini kwamba hakuna mtu yeyote anayepaswa kuendesha michezo katika jimbo lolote nchini, katika wilaya yoyote nchini bila kupata ridhaa ya Shirikisho la Mpira wa Miguu, bila kupata ridhaa ya Viongozi wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia sana sisi viongozi wa Wizara hii kuweza kuratibu michezo yote katika wilaya zetu. Itatusaidia kupata vijana wenye vipaji ambao tutawaratibu sisi wenyewe kama Wizara. Kwa hiyo niwaombe Viongozi wote wa Wilaya, wanaosimamia Wenyeviti wa Michezo katika Wilaya ni ma-*DAS,* kwa hiyo mategemeo yetu sisi kama Wizara, tunawaagiza ma-*DAS* (Makatibu Tawala wa Wilaya), wao ndio watoe ridhaa ya

kuendeshwa kwa mashindano yoyote yanayoendelea katika wilaya zetu nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana, nadhani tumeelewa.

Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niseme tu kwamba nisiporidhika nitashika shilingi. Tunajua kwamba ili tuweze kushinda na kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa tunahitaji maandalizi na maandalizi siyo tu kutengeneza viwanja, ni pamoja na kuandaa vipaji mbalimbali vitakavyoenda kushiriki kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rais alionesha dhamira ya kujenga *soccer academies* 56 zitakazogharimu takriban bilioni 19. Sasa hatuhitaji miaka mingine 10 kukamilisha ujenzi wa *soccer academies* kwa kushindwa kutenga bilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia *Volume IV,* Kitabu cha Maendeleo, wametenga bilioni mbili tu, halafu wanatenga bilioni 10 kukarabati viwanja vya Chama Cha Mapinduzi baada ya ku-*invest* kwenye kuandaa vijana wengine, *Serengeti Girls* wengine, *Serengeti Boys* na Timu ya Taifa nzuri kwenye michezo mbalimbali kwenda kushindana duniani na Afrika na kutuletea medali, wanatenga bilioni mbili? Bilioni mbili tunahitaji miaka tisa kukamilisha *soccer academies* 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu nashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Bulaya kwa sababu ni mdau wa michezo pia na pamoja na Wabunge wenzangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelifanyia mchakato wa muda mrefu na tulishirikisha ngazi za chini. Hizi *academies* 56 Mheshimiwa Bulaya, Mbunge mwenzetu, tulikwenda huko tukawaambia muangalie miundombinu kwanza. Kuna shule nyingi hapa zinahitaji kila moja tungeweza kujenga kwenye jimbo lake, lakini pia tumewashirikisha Maafisa Michezo na Maafisa Elimu kwenye ngazi za huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili sasa kama Serikali tunahitaji tuanze mwaka huu, ndiyo maana tumekuja mbele ya Bunge tuombe fedha. Bilioni mbili hizi ambazo tumeomba tunakwenda kuanza kujenga, tunaanza na chache, tunafahamu mahitaji ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata hivi viwanja ambavyo tunakarabati kwa shilingi bilioni 10 vyote havitumiki na wana CCM tu, vinatumika na Watanzania. Tunapokarabati hivi viwanja ni vya Watanzania wote. Kwa hiyo hizi bilioni 10 zisiangaliwe kwa jicho lingine, wala hizi bilioni mbili za *academies* 56, kote tunakwenda sambamba ili kuhakikisha tunaibua vipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo Mheshimiwa Bulaya, amesoma kwenye *Volume IV,* Kitabu cha

Maendeleo, ameona kiasi gani tumewekeza pia kwa ajili ya wataalam, katika Chuo cha Malya, *1.3 billion*. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Bulaya asichukue hii shilingi, tuanze, kuanza ni muhimu zaidi kuliko kutokuanza. Tunaomba watupitishie hizi bilioni mbili tuanze nazo. *(Makofi)*

**MWENYE:** Haya, Mheshimiwa Bulaya ameridhika, ahsante sana. *(Makofi)*

Haya, tatizo rafiki yangu leo kavaa nguo nyekundu, kwa hiyo anafanana na kiti, nikawa najua ameshakaa, kumbe kasimama; Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi, Wajumbe waniunge mkono tujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Watu kumi hawajafika Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Umeanza na hayo maneno kwa hiyo watu wanapaswa wasimame, hicho kitu huwa mnaambiwa siku zote.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, hebu kaeni kwanza halafu niwaelezee kidogo; angekuwa hajaanza na

maneno ya kwamba anatoa hoja Wajumbe wamuunge mkono maana yake angeyaweka mwishoni, kwa hiyo huwezi kusema alikuwa bado anaeleza wakati kashasema jambo la msingi na watu mnajivuta kusimama. *(Makofi)*

Waheshimiwa ngoja, makofi nitayadai, bado kidogo. Ngoja tuelewane vizuri, ni hivi; ukishasema natoa hoja watu hawatafutwi, huwa ni mara moja. Sasa Mheshimiwa Ester Bulaya ameanza kwa kusema hivi; natoa shilingi Wajumbe waniunge mkono. Maana yake kaanza na kutoa hoja ndiyo maana walisimama hapo wanne wengine mkawa bado mnashangaa, mnasubiria atoe hoja nyingine.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumzia bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Hapana, sasa huwezi kutoa mara mbili, si ndiyo utaratibu ulivyo, unatoaje hoja mara mbili? Ukishatoa mara moja ulishatoa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe utaratibu ndiyo huo, lazima twende nao, lazima twende na utaratibu tuliojiwekea wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo Wajumbe hoja inapaswa kuungwa mkono na Wajumbe kumi na waliokuwa wamesimama ni pungufu ya kumi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........................................Sh. 441,388,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*........Sh. 576,909,000

Kifungu 1004 – *Govt Communication Unit*....Sh. 271,877,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*..........................................Sh. 298,616,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*...................Sh.153,530,000
Kifungu 1007 – *Information & Communication Technology Unit*............................................ Sh. 347,534,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* ................Sh.117,902,000
Kifungu 6001 – *Culture Development Division* .................................Sh.1,694,748,000
Kifungu 6004 – *Sports Development*...........Sh.3,073,137,000

Kifungu 6005 – *Arts Development Division*..................................Sh. 6,935,943,000
Kifungu 7003 – *Information Services*..............................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 – Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*..........................................Sh. 0
Kifungu 6001 – *Culture Development* Division..................................Sh.3,215,000,000
Kifungu 6004 – *Sports* Development..........Sh.12,066,160,000
Kifungu 6005 – *Arts Development* Division.....Sh.550,000,000
Kifungu 7003 – *Information Services*...............................Sh. 0
*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2020, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kupitishiwa makadirio yao ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati yetu pia kama ambavyo Waziri na Naibu Waziri wamekiri kwamba wanafanya kazi nzuri ya kuwasimamia na kuwashauri katika maeneo mbalimbali nao wamekuwa wasikivu. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Wizara kwa ujumla kwa kushirikiana kwa karibu na Kamati yetu ya Huduma za Jamii katika kuhakikisha tunakuza utamaduni, Sanaa na michezo.

nitangaze hapa rasmi kwamba, Bunge siku ya leo limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. *(Makofi)*

Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale mliyoyaahidi kwenye haya ambayo mmeyasema mbele ya Bunge hili na hasa ukizingatia ninyi kama Wizara mmesema hakuna mkate mgumu mbele yenu, mkiashiria ninyi ndio chai. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba Mwenyezi Mungu atuweke, mwakani tutakapokuwa tukisikiliza changamoto nyingi zilizotajwa zinazohusu michezo, utamaduni, sanaa na wasanii pia tunaamini mtakuwa mmezimaliza. Kama hamkuzimaliza, basi mtakuwa mmezipunguza kwa asilimia kubwa. Tunawatakia kila la heri katika hilo, nasi tunaamini uwezo huo mnao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa mbele, halafu nina mambo machache ya kukumbushana. Tunalo tangazo ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kwamba, leo siku ya tarehe 06 Juni, 2022 mnaalikwa kwenda kuhudhuria na kujionea filamu ya "Vuta Nikuvute", iliyoandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Bodi ya Filamu na Shirikisho la Filamu Tanzania. Filamu hiyo itaoneshwa katika Ukumbi wa Sinema, yaani *Dodoma Century Cinemax,* uliopo ghorofa ya pili, jengo la *PSSSF* Kambarage, Dodoma, kuanzia Saa 2.00 usiku leo.

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana kwenda kutazama filamu hii ambayo imetengenezwa kwa kuangalia historia ya wakazi wa Zanzibar katika miaka ya 1950. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwenda, lakini sababu nyingine ya kwa nini twende? Ni kuwatia moyo wasanii wetu kwa sababu hii imeandaliwa na Mtanzania na imeongozwa na Mtanzania.

Sasa filamu ziko nyingi na watu watajiuliza mbona filamu nyingine hazijatajwa, imetajwa hiyo? Ziko sababu muhimu na za kipekee. Tutaendelea kufanya hivyo kwa filamu nyingine pia zitakazokuwa zinafanya vizuri maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ufupi tu ni kwamba, filamu hii pamoja na kwamba, ilitengenezwa tu mwaka jana, 2021, lakini imeshashinda tuzo mbalimbali. Mojawapo ya tuzo iliyoshinda ni *Oumarou Ganda Prize for Best Fiction FESPACO* nchini Burkina Faso mwaka 2021. Pia imeshinda *Best Long Fiction Film* katika Tamasha la Mashariki ambalo linaitwa *African Film Festival,* nchini Rwanda mwaka 2021; pia imeshinda *Seattle International*

*Film Festival Special Jury Award,* Mei, 2022 nchini Marekani na pia imeoneshwa katika matamasha mbalimbali duniani. Hapa wanasema hii ni filamu ya kwanza ya Kitanzania kuzinduliwa katika Tamasha la Kimataifa la Filamu la Toronto *(Toronto International Film Festival)* nchini Canada. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kwenda hapo kwanza kuitazama kwa sababu ina maudhui ya nchini kwetu hapa, lakini pia kuwatia moyo vijana wetu ambao wanajishughulisha kwenye sekta hii ili waweze kusonga mbele zaidi na watie bidii zaidi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mnaalikwa kwenda hapo na saa 2.00, hii filamu itaanza kuoneshwa.

Waheshimiwa Wabunge, michango yenu leo ilikuwa ni ya msingi sana na Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa kirefu hapa, hakuna haja ya kuyarejea hayo, lakini pengine kwa uchache tu ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri kama ulivyoahidi kuweka uzito kwenye mambo ambayo sisi tuko vizuri. Hatuwezi kuwa vizuri kwenye kila jambo. Tukishaona wenzetu wanatuzidi uzuri kwenye jambo fulani, tunaweza kutafuta eneo ambalo sisi tuko vizuri zaidi tukawekeza nguvu hapo ambapo sisi tunafanya vizuri kuliko kila siku tunakuwa tukivutana kama Simba na Yanga hivi, lakini tunaweza kufanya vizuri kwenye michezo ambayo tumeshaona mfano mpaka sasa. *(Makofi)*

*Twiga Stars* tumeona inafanya vizuri, inaleta ushindani mzuri Kimataifa. Kwa hivyo, ni vizuri tukiwekeza huko nguvu, na sasa tumeona *Serengeti Girls* wamefanya vizuri. Ni vizuri tukiwekeza nguvu huko kwa sababu, hawa wanaocheza kwenye *Serengeti Girls* maana yake ndio

watakaoendelea sasa kwenda kucheza kwenye *Twiga Stars*. Kwa hiyo, tukiweka mazingira mazuri kama ambavyo tunaweka mazingira mazuri huko ambako hatufanyi vizuri, naamini kama Taifa tutachagua eneo ambalo tunataka kutambuliwanalo. Hili tunaweza kuamua kabisa kwamba, sisi kama Taifa la Tanzania tumeamua kwamba, tuko vizuri kwenye eneo la mchezo wa watoto wa kike. Kwa hiyo, tuwekeze nguvu huko basi, halafu tuone mambo yataendaje? *(Makofi)*

Vivyo hivyo kwa timu nyingine pia. Tumeona *Serengeti Boys* wanafanya vizuri, tunaweza kuwekeza ngazi hiyo kwa sababu wakishakuwa wakubwa pengine kuna mambo fulani hivi yanawachelewesha, lakini tuwekeze nguvu. Sasa kuna *Tembo Worriors,* mambo kama hayo, tuone sehemu ambayo nasi tunafanya vizuri tujielekeze huko ili tusipoteze nguvu sana au tukazitawanya halafu kila mahali tunakuwa tunashika kidogo kidogo. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo hata wengine wanafanya vizuri, lakini nadhani eneo mojawapo ambalo Tanzania huko nyuma tulikuwa tunafanya vizuri na pengine tukiwekeza nguvu zaidi tutafanya vizuri, ni mbio fupi. Kama ndefu huwa tunaenda na tunajitahudi kufanya vizuri, lakini mbio fupi Tanzania kwenye historia tunaonekana kuna wakati tulikuwa tunafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, tujaribu kwenda kwenye yale maeneo ambayo kwa kweli, tunaweza kuonesha mfano mzuri.

Jambo lingine nimefurahi hapa kwamba umetoa maelekezo kwa Maafisa Utamaduni wa Wilaya na ma-*DAS*. Naamini utashirikiana pamoja na TAMISEMI, siyo kwa ajili tu ya mpira wa miguu kama ambavyo jambo hili

limezungumziwa hapo kwamba kuna michezo inaendelea kwenye Wilaya na Majimbo. Binafsi nisingefikiri kwamba ile michezo inapaswa kuzuiwa kwa sababu lengo la Wizara hapa mlivyoeleza, mmesema mnataka kuinua vipaji, sasa mtaviinuaje? Sijui ni kwa namna gani? Ila ningetamani kwamba yale maelekezo utayoyatoa kwa maandishi, yatolewe kwa namna ambayo maeneo hayo hao Maafisa walazimike basi kufanya hiyo michezo ama kuendesha hiyo michezo. Kwa sababu, kuna maeneo yatakaa tu kwa sababu mtu anaona uvivu kuanza kufuatilia hicho kibali na mchezo wake yeye anataka kuendesha kwenye kata au kwenye mtaa. Sasa ukimwambia asafiri mpaka kwenda wilayani akatafute kibali, inaweza ikawa kidogo mtihani. Kwa hiyo, tunaweza kuwa tunaenda mbele, tunarudi nyuma sisi wenyewe tena. Kwa hiyo, hili nalo mlitazame kwa mapana yake.

Kwa namna hiyo hiyo, ni muhimu sana kuendelea kutambua juhudi mbalimbali zinazoendelea. Namshukuru sana Mheshimiwa Shally Raymond, humu ndani pia kuna vipaji mbalimbali na ni muhimu kuendelea kuvitambua, kwa sababu vijana hata humu ndani wapo na wako vijana ambao wako vizuri kwenye vipaji vya aina mbalimbali. Kwa hiyo, hawa nao ni muhimu kuendelea kuwatambua.

Katika hayo maelekezo utakayotoa kwa hao Maafisa walioko huko ngazi za Wilaya ni pamoja na Wizara kufika mahali ambapo mtakuwa mkipata taarifa kuhusu shughuli za Wizara yenu kutoka kwenye hizo Wilaya. Kwa sababu, nimeona kama Mheshimiwa Shally alivyosema, kwenye hii hotuba mambo mengi mazuri yametajwa, lakini yako mazuri zaidi ya haya yaliyotajwa kwenye kitabu. Nataka kuamini kwa sababu Wizara

pengine haina taarifa au ni zile zile changamoto sasa kwamba chai, mikate ile migumu mnaendelea kuifuatilia ili mwendelee kuichovya kwenye chai. Basi mwendelee kufanya hivyo maeneo mengi zaidi ili hao watu ambao wanafanya hizo shughuli ambazo kimsingi zilipaswa ziwe shughuli zenu, basi mtafute namna ya kuwatia moyo badala ya wao tena kujikuta wamepata Polisi wa kusimama nyuma yao. Ninyi lazima muwe ni watu ambao mnawasaidia wafanye vizuri zaidi.

Hapa niwataje kipekee kabisa, siyo kwa namna yoyote ile jamani; Mwanza kuna Tamasha la Utamaduni, acha hili mlilofanya juzi, lakini kuna Tamasha ambalo liko kila mwaka mwezi Juni, linaitwa Bulabo. Sasa vitu kama hivyo ni vizuri kwa sababu lile lipo na watu wote wanalitegemea. Hata kama lingine lilikuwepo, lakini wao wataendelea na la kwao. Kwa hiyo, hizo juhudi ziko maeneo mengi, kwa hiyo, mngeweza kuzitazama. *(Makofi)*

Hapa nimefurahi kwamba Waziri anayeendesha Majimaji Serebuka ameinama, kwa hiyo, hajasikia vizuri. Hayo ni mambo ambayo lazima Wizara myatazame ili kama ziko fedha, basi mwekeze huko badala ya kuanzisha mambo mapya wakati yale yaliyotangulia yapo na mnaweza kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tunawatakia kila la heri kwa kweli na muanzie hapa ndani, vipaji vya *Bunge Sports Club.* Sasa hapo sitajiongelea mimi kwa sababu kidogo umri umesonga, lakini nawatakia kila la heri wale ambao vipaji vyao vitaibuliwa humu ndani na hii Wizara, naamini mtatuwakilisha vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge, mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku, Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jamanne, Tarehe 7 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*